

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 9 Februari, 2017**

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Sita, leo ni Kikao cha Tisa. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**SPIKA:** Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:-**

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha, Mapitio ya Nusu Mwaka 2016/2017 (Monetary Policy Statement The Mid-Year Review 2016/2017).

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha. Naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Anakuja Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016 (*The Annual Report of Energy and Water Utilities Regulatory Authority for the Financial Year ended 30th June, 2016*).

**SPIKA:** Ahsante sana Eng. Isack Kamwelwe, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Karibu sana Mheshimiwa. (Makofii)

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2016 hadi Januari 2017.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. (Makofii)

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kipindi cha kuanzia Januari 2016 hadi Januari 2017.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. RAMADHANI A. ISSA - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Swalii linaulizwa na Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Viti Maalum.

Na. 95

**Umuhimu wa Kuanzisha Benki ya Vijana**

**MHE. HALIMA A. BULEMBO** aliuliza:-

Serikali imeanzisha Benki ya Wanawake na Benki ya Kilimo na kwa sasa asilimia kubwa ya Watanzania ni vijana:-

(a) Je, ni lini Serikali itaona umuhimu na kuanzisha Benki ya Vijana?

(b) Je, kwa nini Serikali isianzishe dhamana kwa vijana kukopa?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga mfumo madhubuti wa Hifadhi ya Jamii ili vijana waweze kuiwekea akiba ya uzeeni, kupata Bima ya Afya na kupata mikopo ya kuendesha biashara zao?

## **NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a), (b na (c). kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inalipa umuhimu sana suala la kuanzisha Benki ya Vijana nchini ili kuwawezesha vijana kupata huduma za mikopo yenye masharti nafuu. Kwa hatua za awali, Serikali imeona ni muhimu kwanza kuwajengea vijana tabia ya kuweka akiba na kukopa kwa kuanzisha SACCOS za vijana katika kila Halmashauri ili baadaye ziweze kuwekeza hisa katika Benki itakayoanzishwa. Hatua hii itawezesha Benki ya Vijana itakapoanzishwa kumilikiwa na vijana wenyewe.

(b) Mheshimiwa Spika, suala la Serikali kuanzisha dhamana kwa vijana kwa ajili ya kukopa ni la msingi. Tunakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tutaufanyia kazi. Aidha, utaratibu utategemea uwezo wa kifedha wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na ubainishaji muhimu wa nani apewe dhamana ya Serikali kwa lengo la kuwanufaisha vijana wote.

(c) Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeweka utaratibu wa mwanachama kuijunga katika mfuko wa uchangiaji wa hiari pamoja na kuijunga na Bima ya Afya. Serikali kwa kushirikiana na mifuko hiyo imekuwa ikiwahamasisha vijana kupitia mafunzo, mikutano na makongamano mbalimbali ili waweze kutumia fursa hiyo kwa ajili ya ustawi wa maisha yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima, naona wamekosea jina hapa, naona hujabadilisha jina sawasawa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Halima, swali la nyongeza. (*Kicheko/Makofii*)

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba niulize swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, changamoto kubwa katika kuanzisha Benki za Maendeleo ni mtaji. Hivi sasa nchini kwetu tumejiwekea utaratibu kwamba kila Halmashauri hutenga 5% kwa ajili ya vijana. Bajeti ya mwaka huu katika Serikali za Mitaa imekusanya takriban shilingi bilioni 600 ambapo katika ile 5% ya vijana ni sawasawa na shilingi bilioni 30. Iwapo fedha hizi zitatumiwa vizuri, tunaweza kuanzisha Benki ya Vijana zenyet matalwi katika kila Halmashauri na tukiweza katika hili, tutaweza kutatua suala zima la mikopo kwa vijana.

Je, Serikali haioni ni vyema sasa, Halmashauri zote nchini kuwa wanahisa wa Benki za Vijana na kutumia fedha hizi kama mtaji wa kuanzisha benki hii? (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Anthony Mavunde, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Spika, nataka tu nianze kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwafuatilia vijana wa nchi hii na amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba vijana wengi wanapata fursa ya mitaji na mikopo.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la msingi, ni kweli kwamba umekuwepo utaratibu wa utengaji wa 5% za mapato ya ndani kwa kila Halmashauri ambao lengo lake kubwa ni fedha hizi kwenda kuwafikia vijana. Kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, lengo kubwa la uanzishwaji wa benki hii ni kutaka ije imilikiye baadaye na vijana kupitia SACCOS za kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatua ya kwanza ambayo Serikali tulianza ni kwamba mwaka 2014/2015 alitafutwa mtaalam kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na baadaye sasa Serikali tukaanza kuchukua hatua; mojawapo ni kuhakikisha kwamba kila Halmashauri nchi nzima inaanizisha SACCOS ya vijana ili baadaye SACCOS hizo za vijana ndiyo zije zimiliki hisa katika hii benki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimwondoe hofu tu Mheshimiwa Bulembo kwamba tukikamilisha uanzishwaji wa SACCOS katika Halmashauri, kazi itakayofuata sasa itakuwa ni namna ya kuutafuta huo mtaji na wazo alilolitoa ni wazo jema. Kama Serikali, tunalichukua, tutaona namna ya kuweza kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na swali linalofuata, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha. (Makofii)

Na. 96

### **Uhitaji wa Vifaa vya Maabara za Sekondari Serengeti**

**MHE. MARWA R. CHACHA** aliuliza:-

Ujenzi wa Maabara za Shule za Sekondari Wilaya ya Serengeti umeshakamilika kwa kiwango kikubwa lakini maabara hizo zimebaki kuwa makazi ya popo:-

Je, ni lini Serikali italeta vifaa vya maabara kama ilivyoahidi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ina mahitaji ya vyumba vya maabara 63. Zilizokamilika ni 22 na zinatumika; maabara 29 zimekamilika lakini hazina vifaa na vyumba vya maabara 12 viko katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga shilingi bilioni 16 kupitia mradi wa P4R kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara zote zilizokamilika nchi nzima. Vifaa hivyo vinatarajiwa kupatikana kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2016/2017.

**SPIKA:** Mheshimiwa marwa, swali la nyongeza, nilikuona.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Serengeti kwa kujitahidi kukamilisha vyumba vya maabara kwa asilimia 81.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wamekamilisha kwa asilimia 81, Mheshimiwa Naibu Waziri uko hapa na umekuja pale Jimbo la Serengeti na umeona hali ilivyo; kwa kuwa wananchi hawa wamejitatihidi kwa hali hii. Je, Serikali kupitia hizi fedha za P4R mko tayari kukamilisha hivi vyumba 12 ambayo ni sawa na asilimia 19? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa ujenzi wa maabara ulipaswa pia kuendana na upungufu wa vyumba vya madarasa: Je, kupitia hizi pesa za P4R, mko tayari kupeleka sehemu ya fedha hizi kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Selemani Said Jafo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niwapongeze kwa kazi kubwa

waliyoifanya; na kama kuna deficit ya vyumba 12, niseme kwamba Serikali tutashirikiana, siyo na watu wa Serengeti peke yake, isipokuwa jukumu letu kubwa ni kuhakikisha tunapata maabara katika kila sekondari zetu zilizokamilika. Ndiyo maana Mheshimiwa Mbunge nilikwambia hiyo juhudhi iendelee, lakini Serikali na sisi tutatia nguvu yetu kuhakikisha maeneo yote yale ya Serengeti yanapata maabara kama tulivyokusudia.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimezungumza hapa kwamba tumetenga karibu shilingi bilioni 16. Lengo ni kwamba zile maabara ambazo wananchi wamejitolea kwa nguvu kubwa kuzijenga, lazima ziwe na hivyo vifaa. Kuanzia mwezi Machi mpaka mwisho wa mwaka hapa tutajikuta tumekamilisha suala zima la maabara siyo Serengeti, lakini katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, suala zima la ujenzi wa vyumba vya madarasa, ni kweli. Tuna changamoto ya vyumba vya madarasa katika maeneo mbalimbali ikiwepo kwako Serengeti, nami nakupongeza sana, nilikuwa nawe siku ile. Tutajitahidi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu ukiangalia katika michakato mbalimbali, tulikuwa na madarasa ambayo yapo katika program ya P4R ambayo tumejenga kwa kiwango kikubwa katika nchi yetu, lakini tulikuwa na madarasa ambayo tulikuwa tunayajenga kwa mpango wa MES // lakini kuna mipango mingine mbalimbali ambayo takriban shilingi bilioni 29 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vingi vya madarasa, zaidi ya vyumba 3,000.

Mheshimiwa Spika, katika harakati hizi, tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo maeneo ya Serengeti, lakini nchi nzima kwa ujumla kwa hii mipango mipana ya Serikali ili tuondoe changamoto ya madarasa. Lengo kubwa ni wanafunzi wetu wapate maeneo mazuri ya kusomea.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli. Aah, Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Profesa, tafadhali, majibu ya nyongeza.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Jafo kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwalishwa Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali imeshanunua vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 16.9 kwa ajili ya maabara zote nchini zilizokamilika. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaanza zoezi la usambazaji wa vifaa hivyo. Kwa hiyo, natoa tu wito kwa Waheshimiwa Wabunge ambao katika maeneo

yao maabara hazijakamilika, waendelee kuzikamilisha kwa sababu utaratibu wa Serikali ni kwamba tutakuwa tunapeleka vifaa pale ambapo maabara zimekamilika. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu hayo ya kutia moyo sana. Mbunge wa Lupembe, Mheshimiwa Hongoli. Swali linaofuata.

Na. 97

### **Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Njombe**

**MHE. JORAM I. HONGOLI** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ilianzishwa mwaka 1982, lakini mpaka leo hii haina Hospitali ya Wilaya na ina Vituo vitatu vya Afya:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kuvizezesha Vituo hivi vya Afya kutoa huduma ndogo ya upasujji ili kupunguza vifo vya akinamama na watoto pamoja na wananchi wengine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli, Mbunge wa Lupembe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga shilingi milioni 82.0 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Njombe na itaanza kwa jengo la wagonjwa wa nje, yaani OPD. Fedha hizo bado hazijatolewa kutoka HAZINA.

(b) Mheshimiwa Spika, ukarabati wa chumba cha upasujji katika Kituo cha Afya cha Lupembe umekamilika kwa gharama ya shilingi milioni 21.0 kutohana na mapato ya ndani ya Halmashauri. Vile vile, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri imepanga kutumia shilingi milioni 36.0 kwa ajili ya kukarabati chumba cha upasujji katika Kituo cha Afya cha Kichiwa. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Hongoli, swali la nyongeza.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sasa tutakuwa na huduma ya upasuaji mdogo katika Kituo cha Afya Lupembe na hatimaye Kichiwa ili kuboresha huduma ya madawa kwa kuwa dawa ni tatizo: Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua duka la dawa kwa maana ya MSD katika Kituo cha Afya Lupembe na baadaye Kichiwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza lazima nikiri kwamba harakati za Mbunge huyu na watu wa Mkoa wa Njombe kwa ujumla wake tutajitahidi kuziunga mkono. Lengo kubwa ni Mkoa mpya wa Njombe uweze kupata huduma ya afya. Ndiyo maana hata Waziri wangu Mkuu juzi juzi alikuwepo kule kwa ajili ya mipango ya kimkakati katika Mkoa ule mpya.

Mheshimiwa Spika, suala zima la ujenzi wa duka la madawa katika vituo hivyo, siwezi kukiri kwamba katika hivyo Vituo vya Afya tutafanyaje, lakini kwa sababu pale tuna hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa ambayo inajengwa sasa hivi, tutafanya mpango mkakati tufanyeje katika eneo lile tupate duka maalum la MSD. Nia ya Serikali ni watu wa ukanda ule waweze kupata dawa kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba niwahimiza Waheshimiwa Wabunge wote, kwa sababu sasa hivi tunaelekeza fedha nyingi sana katika Halmashauri na nashukuru sana, juzi juzi karibu kila Mbunge hapa amepata orodha ya idadi ya fedha kwa ajili ya madawa katika eneo lake, sasa ni kuona jinsi gani twende tukazisimamie.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nilisema katika siku za nyuma kwamba, tumeelekeza fedha nyingi za *basket fund* ambazo fedha zile lengo lake ni kwamba one *third* nikwa ajili ya ununuzi wa madawa na vifaa tiba. Naomba tukazisimamie tutatue kero za madawa kwa wananchi wetu, kwa sababu tukifanya hivi, naamini Watanzania wote watafarijika kupata dawa bora katika maeneo yao kwa sababu Serikali sasa hivi imepeleka fedha nyingi sana katika Sekta ya Afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Doto Biteko, nilikuona.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa wepesi wake katika kutatua changamoto tulizonazo kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, chumba cha upasuaji cha Hospitali ya Wilaya ya Bukombe kilikuwa kimejengwa kwa ajili ya kutumika kwa muda baadaye ijengwe *theatre*. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya alikuja pale akaona hali halisi ilivyokuwa. Nataka tu kujuu *commitment* ya Serikali, ni lini wataisaidia Hospitali ya Wilaya ya Bukombe na yenyewe ipate chumba cha upasuaji cha kisasa kwa ajili ya kuwapatia huduma wananchi wa Bukombe? (Makofii)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo tafadhali, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri wazi kwamba nilifika Jimboni kwa Mheshimiwa Mbunge na ni kweli nimeenda kuitembelea hospitali yetu ya Wilaya angalau pale upasuaji unaendelea. Kwa kuwa eneo lile lina changamoto kubwa sana, ndiyo maana tuna mpango vile vile siyo kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ile peke yake, isipokuwa hata katika Kituo chako cha Afya cha Uyovu kama tulivyoongea.

Mheshimiwa Spika, tutaangalia jinsi gani tutafanya ili tupeleke huduma katika maeneo yale, tupate na back up strategy katika Kituo cha Afya cha Uyovu, tupunguze idadi kubwa ya wagonjwa ambao wataendelea katika Hospitali yetu ya Wilaya. (Makofii)

Kwa hiyo, amini Serikali yako kwa sababu tumekuja kule, tumefanya survey, tumetembelea, tumekutana na wananchi, tumebaini changamoto. Baada ya kubaini changamoto, Serikali tunapanga mkakati wa kuweza kuwasaidia wananchi wa Bukombe.

**SPIKA:** Tuendelee na Utumishi na Utawala Bora, swali la Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, Mbunge wa Siha.

Na. 98

**Matukio ya Ufisadi - Ushirika wa Wilaya ya Siha**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL** aliuliza:-

Ushirika katika Wilaya ya Siha umekumbwa na matukio ya ujisadi yakiwemo upotevu wa zaidi ya shilingi milioni 840 katika Ushirika wa Siha Kiyeyu, upotevu wa shilingi milioni 337 ya SACCOS ya Sanya Juu pamoja na matumizi mabaya ya ardhi, licha ya uchunguzi mzuri uliofanywa na TAKUKURU Mkoa:-

Je, ni kwa nini uchunguzi huo unaingiliwa na maslahi binafsi ya watu wachache na kusababisha matukio yanayodhalilisha Serikali?

## **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kujibu swali liloulizwa na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, Mbunge wa Jimbo la Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 5 (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007, TAKURURU imepewa mamlaka kuwa chombo huru cha kuzuia na kupambana na rushwa nchini; na inatekeleza majukumu yake muhimu kama yalivyofafanuliwa katika Kifungu cha (7) cha sheria hiyo ya kuzuia na kupambana na rushwa. Kutokana na mantiki hiyo ya kisheria, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa namna yoyote ile, Taasisi ya TAKUKURU haiwezi kuingiliwa na mtu yeyote.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba TAKUKURU ilipokea tuhuma za udanganyifu wa matumizi ya fedha za umma kutoka katika vyano vyake mbalimbali zilizokihusu Chama cha Ushirika cha Siha Kiyeyu na Sanya Juu SACCOS. Kutokana na tuhuma hizo, uchunguzi uliofanywa na TAKUKURU ulithibitisha pasipo shaka kwamba viongozi wa Chama cha Ushirika Siha Kiyeyu bila ridhaa ya wanachama wake, waligawa mashamba kwa watu wasio wanachama wapatao 13, shamba lenye ekari 16 ambazo zililimwa kati ya miaka miwili na mitano bila ya kulipiwa gharama yoyote. Kitendo hiki kiliukosesha ushirika Siha Kiyeyu mapato ya kiasi cha sh. 1,600,000/=.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi pia ulithibitisha pasipo shaka kwamba uongozi wa Chama cha Msingi cha Ushirika cha Siha Kiyeyu ulitoa maeleo ya uongo kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa William Olenasha kwa kumpatia stakabadhi za uongo juu ya matumizi ya sh.500,000/= za ushirika kwa ajili ya semina. Baada ya uchunguzi kukamilika uongozi huo ulikiri kutenda kosa hilo mbele ya wachunguzi.

Mheshimiwa Spika, tuhuma kuhusu ufisadi wa sh.337,000/= unaokihusu SACCOS ya Sanya Juu ni tuhuma mpya. Tuhuma za Sanya Juu SACCOS zilihusu kiasi cha sh.160,100,406, na tuhuma hizi zilichunguzwa na Jeshi la Polisi na kesi Na. CC 15/2016 imeshafunguliwa na ipo katika Mahakama ya Wilaya ya Siha.

Mheshimiwa Spika, tuhuma za upotevu wa shilingi milioni 840 unaokihusu Chama cha Ushirika cha Kiyeyu ni malalamiko ya wanachama juu ya tozo anazolipa mwekezaji katika shamba la maparachichi ambapo anadaiwa kulipa kiasi cha shilingi milioni 60 kwa mwaka. Tuhuma hizi ni mpya na Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro imezipokea kwa ajili ya uchunguzi zaidi. Uchunguzi utakapokamilika, taarifa itatolewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kushukuru Wizara ya Kilimo, vilevile kumshukuru Rais. Nimemweleza hili, nimeona cheche kidogo. Niseme, kwa kuwa tumeshamkamata aliyekuwa Mkurugenzi wa Siha na amewekwa ndani kwa muda kwa ajili ya tuhuma kama hizi za ufisadi, lakini sh. 1,600,000/= ambazo zimeshushwa siyo za kweli. Amesharudisha ambaye sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Mara, Charles Mlingwa na risiti tunazo. Tulinmafuta tukamkamate, lakini tukakuta amezungukwa na Jeshi la Tanzania. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa kuwa Mkuu Mkoa wa Kilimanjaro Meck Sadiq amemtishia Meneja wa TAKUKURU wa Mkoa wa Kilimanjaro, kwamba hizi tuhuma anazozichunguza ni za uongo, swali langu la kwanza ni kwamba. Je, Serikali inatoa *commitment* gani kuhakikisha watuhumiwa wote wa ufisadi ndani ya ushirika na KNCU Mkoa wa Kilimanjaro, wamefikishwa mbele ya sheria; na kutuhakikishia watamlindaje Mkuu wa TAKUKURU anayezuiliwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kufanya kazi zake? (Makofij)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali inatupa *commitment* gani kwamba Charles Mlingwa ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Mara, vilevile Meck Sadiq ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, bado wanastahili kupeperusha bendera ya Tanzania na vilevile kupigiwa saluti na majeshi yetu ya Tanzania kama Wakuu wa Mikoa na kumwakilisha Rais baada ya vitendo hivi? (Makofij)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusiana na swali lake la kwanza, kwamba Serikali inatoa *commitment* gani kuhakikisha kwamba watuhumiwa wanafikishwa Mahakamani au wanafunguliwa mashtaka? Nimhakikishie kwamba tunaendelea na chunguzi mbalimbali na pindi chunguzi hizo zitakapokamilika na itakapothibitika pasipo shaka kwamba wanayo hatia au wana hoja ya kujuu Mahakamani, basi kwa hakika watuhumiwa watafikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili kwamba Afisa wa TAKUKURU wa Mkoa anaingiliwa ama anazuiwa kufanya kazi zake na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, niseme kwamba siyo kweli. Ukiangalia kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, TAKUKURU kama chombo, kinao uhuru wa kufanya kazi zake bila kuingiliwa na imekuwa ikifanya hivyo. Hata katika jibu la msingi nilieleza, tayari kulikuwa kuna mkutano wa wanaushirika, tena Mheshimiwa Meck Sadiq huyo huyo aliiifisha na waliweza kusomewa taarifa ya TAKUKURU pale na aliweza kuridhika na ndiyo maana mpaka leo kunakuwa na utulivu na uhimilivu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, endapo ataona ana malalamiko dhidi ya Wakuu wa Mikoa hao, basi asisite kuwasilisha malalamiko stahiki na aweze kuchukuliwa hatua.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya...

Ooh, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Kumbe upo mzee! Karibu sana. (Kicheko/Makofi)

Swali la nyongeza Mheshimiwa Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza.

Kwa kuwa matatizo ya vyama vya msingi vya ushirika katika Wilaya ya Siha, yanafanana sana na matatizo ya Vyama vya Msingi vya Ushirika katika Wilaya ya Hai; na kwa sababu Vyama vya Msingi vya Ushirika katika Mkoa wa Kilimanjaro vimehodhi maeneo makubwa sana ya ardhi, ambayo kimsingi kwa Mkoa wa Kilimanjaro ndiyo backbone ya economy ya Mkoa ule kwenye upande wa kilimo; na kwa kuwa kumekuwa na shutuma nyngi za muda mrefu ambazo pengine zimelindwa kwa kiwango kikubwa na sheria yenewe ya ushirika, ambayo inatoa *limited power* kwa mtu mwingine ye yote kuingilia vitendo na kazi za ushirika:-

Je, Serikali haioni sasa kwa sababu ya matatizo haya ya muda mrefu yaliyokithiri, ni wakati muafaka wa ku-review Sheria ya Ushirika; na kabla ya kui-review Sheria ya Ushirika, kuangalia kwa kina matatizo ya Vyama vya Msingi vya Ushirika katika Mkoa wa Kilimanjaro ili kuweza sasa kuweka mapendekezo sahihi ya kurekebisha sheria ile? (Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kuhusiana na kufanya mapitio katika Sheria ya Ushirika, Wizara ya Kilimo bahati nzuri wapo. Niseme tu kama Serikali tumekuwa tukifanya hivyo kwa sheria mbalimbali siyo hii tu ya ushirika; na naamini Wizara husika itaweza kulichukua na nina uhakika watakuwa wameshaanza mapitio kwa sababu ni suala endelevu kila mara kungalia sheria inakidhi mahitaji ya wakati husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Serikali kuviangalia Vyama hivi vya Ushirika kama vina matatizo, napenda tu kusema kwamba katika Mkoa wa Kilimanjaro hata hivi sasa tunavyoongea tayari Vyama vya Ushirika vinne

vimefanyiwa uchunguzi na tayari vyama vitatu uchunguzi umeshakamilika, kimebakia kimoja. Naamini matokeo ya uchunguzi hayo yataweza kutangazwa huko baadaye ili kuona ni hatua gani iweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumeshafanya uchunguzi katika Chama Kikuu cha Ushirika cha KNCU na tumefanya uchunguzi katika Chama cha Tanganyika Coffee Curing Company Limited na siyo kwa Vyama hivi vya Ushirika peke yake. Tumefanya pia uchunguzi katika SACCOS nne na tayari mbili zimeshafikishwa Mahakamani na mbili zinaendelea na uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbewe, kwa kutambua umuhimu wa Vyama hivi vya Ushirika kwa wakulima, tutakapoona kuna harufu au chochote kinachoashiria vitendo vya rushwa au vitendo vingine vya ubadhirifu wa mali za umma, tutahakikisha kwamba hatua stahiki zinachukuliwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Swalii la Mbunge wa Tanga, Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, kwa niaba yake nyuma kabisa kule, Mheshimiwa Khatib.

Na. 99

### **Hitaji la Usafiri wa Uhakika Kati ya Tanga na Pemba**

**MHE. KHATIB SAID HAJI (K.n.y. MHE. MUSSA BAKARI MBAROUK)** aliuliza:-

Kwa muda mrefu hakuna usafiri wa uhakika kati ya Pemba na Tanga halii inayopelekea vyombo vya usafiri vya kienyeji kupata ajali mara kwa mara na kupoteza maisha ya watu na mali zao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua meli ya kisasa na ya uhakika ili kuokoa wasafiri wa Tanga – Pemba?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kuanzia tarehe 29 Januari, 2017 Kampuni ya Azam Marine imeanza kutoa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo kati ya Pemba na Tanga kwa kutumia meli ya Sealink 2 yenye uwezo wa kubeba abiria 1,650 na mizigo tani 717.

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 Januari 2017 Meli ya Sealink 2 ilizindua safari ya kutoka Tanga saa 3.00 asubuhi kwenda Mkoani Pemba hadi Unguja. Sealink 2 itafanya safari zake mara moja kwa wiki baina ya Pemba na Tanga hadi pale idadi ya abiria na mizigo itakapolazimu kuongeza safari nyingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu inapenda kutumia fursa hii kuipongeza kampuni ya Azam Marine kwa kuitikia wito wa kuanzisha huduma ya usafiri majini baina ya Tanga, unguja na Pemba na kuendelea kutoa wito kwa wawekezaji wengine kuleta vyombo vyaa usafiri majini vyaa kisasa ili kuongeza huduma ya usafiri katika maeneo yanayokabiliwa na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia tunaomba wananchi wanaosafiri kati ya Pemba na Tanga kutumia huduma za meli salama na kuachana na vyombo visivyo salama vinavyohatarisha maisha na mali zao. Aidha, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Tanga na Pemba kuendelea kuhamasisha wananchi kuachana na vyombo visivyo salama ili kulinda maisha na mali zao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khatibu, swali la nyongeza.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nachukua nafasi hii kuishukuru kampuni ya Azam kwa kuleta usafiri huu kati ya Pemba na Tanga. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, swali langu ni hili kwamba meli hii ya Sealink ni meli kubwa na uwezo wa abiria wa Pemba na Tanga siyo mkubwa sana. Viko vyombo vilivyojaribu kufanya safari za pale lakini vikashindwa kulingana na runningcost zilivyo kubwa sana. Je, ikitokea meli hii imekatisha safari kama zilizotangulia, Serikali itakuwa tayari kukubaliana na mimi kuipeleka meli ya MV Dar es Salaam, ambayo kwa sasa imekaa haifanyi kazi na ni ya Serikali, ikatoe huduma kati ya Pemba na Tanga? (Makofii)

Swali la pili, kwa kuwa ajali nyingi zinazotokana na vyombo vyaa baharini, moja ya sababu ni uzito unaopitiliza katika vyombo hivyo: Ni utaratibu gani unaotumika kujua uzito unaostahiki ili kuепusha ajali zinazotokea mara kwa mara katika vyombo vyaa baharini? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Eng. Ngonyani, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, Sealink 2 ya Azam Marine imefanya utafiti wa muda mrefu, ndio maana imeanza na safari moja kwa wiki na kama wateja wataongezeka wataongeza safari. Kama itatokea kwamba hiyo ikasimamisha, ina maana abiria hakuna wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuipeleka MV Dar es Salaam kufanya kazi hiyo, tatizo litakuwa lile lile, kwamba abiria hakuna wa kutosha. Sidhani kama nimemaanisha kwamba Serikali iendeshe meli hiyo ya MV Dar es Salaam kwa hasara, lakini kubwa ni kwamba MV Dar es Salaam haijakkabidhiwa rasmi kwa TEMESA. Nadhani tumekuwa tukijibu maswali mengi kuhusu MV Dar es Salaam na hivi tunavyoongea sasa hivi kuna kampuni ya South Africa imekuwa contracted na ile kampuni ya Holland kufanya marekebisho ya ile speed. Ni mpaka pale watakapolikamilisha hilo, ndiyo tutakabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, tutakapokabidhiwa tutajua nini cha kufanya, kwa sababu maombi yako mengi. Sasa tunaongelea Tanga, wenzetu wa Mafya wameomba, kwa hiyo, tutaangalia nini muafaka wa kufanya kwa MV Dar es Salaam itakapokabidhiwa rasmi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzito, tuna taasisi yetu ya SUMATRA ndiyo inayosajili vyombo vyote vya majini na vitu vinavyotumia criteria ya kusajili ni pamoja na uzito wa mizigo, kiwango cha abiria, hivi vyote vinaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, chombo chetu au taasisi yetu ya SUMATRA ndiyo yenye wajibu wa kuhakikisha kila chombo kinachoingia majini kinachukua kiwango cha abiria na uzito unaostahiki. Ndiyo maana kila mahali ambapo meli au boti imesajili, tuna wataalam wa SUMATRA katika maeneo hayo. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud nilikuona, swali fupi la nyongeza.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Nami naishukuru Kampuni ya Azam Marine kwa kurahisisha usafiri kutoka Tanga kwenda Pemba. Swali langu ni moja dogo lifuatalo:-

Kwa kuwa kuna malalamiko ya muda mrefu ya kutokupatikana kwa usafiri wa uhakika kutoka Dar es Salaam kuelekea Bandari ya Mtwara; na Serikali imekuwa ikiahidi mara kadhaa kwamba wako katika mkakati kabambe wa kuhakikisha kwamba usafiri kwa njia ya baharini kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara utapatikana kwa haraka; Serikali ituambie, ahadi hii ya muda wa miaka saba iliopita, ni lini Serikali itaandaa mikakati ya kurahisisha usafiri huu? Naomba majibu. (Makofii)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali, Mheshimiwa Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni tu humu Bungeni nilisema kwamba Serikali inaangalia uwezekano wa kutatua tatizo la usafiri kwenye Bahari ya Hindi, kwa sababu maamuzi yetu ya nyuma yalilenga kutoa fursa hii kwa wawekezaji binafsi. Ndiyo maana tulipotoa hizo fursa, wawekezaji kama Azam Marine walijitokeza na wengineo kuwekeza. Ni kwenye Maziwa Makuu tu ndiyo Serikali tulien��elea kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuhamasisha wawekezaji binafsi lakini pale itakapoonekana kwamba wawekezaji binafsi, hawawezi kabisa kutoa huduma hiyo, Serikali itaangalia uwezekano wa kurudisha TACOSHILI ya zamani ili iweze kutoa huduma katika Bahari ya Hindi. Nimhakikishie tu kwa sasa hivi watu wa Mtwara wanasafiri kwa raha sana kwa njia ya barabara.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Tabora Kaskazini, Mheshimiwa Almas Maige.

Na. 100

#### **Msajili wa Hati za Viwanja - Tabora**

**MHE. ALMAS A. MAIGE** aliuliza:-

Kufunguka kwa mawasiliano ya barabara za Tabora, Nzega, Tabora - Manyoni na Tabora - Kigoma kumeleta maendeleo ya kukua kwa Mji wa Tabora na kuongezeka shughuli za uwekezaji na ujenzi wa nyumba za makazi na biashara:-

Je, ni lini Serikali italeta Msajili wa Hati za Viwanja Tabora ili aweze kuidhinisha hati za viwanja kwa wakazi na wawekezaji kwa kuwa kwa sasa huduma hizo hazipo Mkoani Tabora?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Hati Msaidizi ameshateuliwa kwa kuzingatia Kifungu Na. 4 cha Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura Na. 334. Tangazo la utezi lilitolewa katika Gazeti la Serikali la tarehe 16, Desemba, 2016, Toleo Na. 52.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Msajili Msaidizi ameshawasili kituoni. Aidha, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu mpaka sasa Wizara imeshapeleka Wasajili wa Hati katika Ofisi zote za Kanda. Rai yangu kwa Halmashauri zote nchini ni kuongeza kasi ya upimaji, upangaji na umilikishaji wa ardhi ili wananchi waweze kupatiwa hati za umiliki wa maeneo yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maige swalii la nyongeza tafadhali.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pongezi zangu kwa niaba ya Wanauyui na Tabora wa ujumla kupeleka Msajili wa Hati, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa vile kuna upungufu mkubwa sana wa idara mbalimbali za ardhi pale ikiwemo ya upimaji na mipango: Je, Serikali iko tayari kupeleka tena wataalam hao ili wafanye kazi na Msajili huyu wa Hati?

Swali la pili; kwa vile kabla ya kupelekwa Msajili huyu wiki moja iliyopita, kwa miaka mingi iliyopita Hati za Tabora zimekuwa zinasajiliwa katika Ofisi nyingine za Kanda, Dodoma na Mwanza: Je, Serikali sasa iko tayari kurudisha kumbukumbu ya Hati zetu zote pale Tabora? Ahsante sana. (Makofii)

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza ameuliza kuhusu upungufu wa wataalam wa idara nyingine, ametaja mipango mijii, kama tuko tayari kupeleka.

Mheshimiwa Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako kwamba kwa sasa katika kipindi hiki ambacho pia tunatakiwa kama Wizara zote au Serikali kuhamia Dodoma, baadhi ya Wataalam ambao wako Makao Makuu tutawasambaza katika kanda ambazo zina upungufu, kwa sababu, maeneo mengi ni karibu yanao wataalam wa kutosha, lakini ni machache likiwepo la Tabora ambao hawana wataalam hao. Kwa hiyo, tutawapeleka katika Kanda ili kuendelea kuziimarisha kama tulivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, amesema Hati zilizoko Mwanza na maeneo mengine ambazo ni za Tabora; naomba nimhakikishie tutafanya utaratibu wa kuhakikisha hati hizo zinarudi katika ofisi husika kwa sababu tayari Msajili ameshapatikana, basi anao wajibu pia wa kuhakikisha anatunza Hati za Maeneo ambayo anayasimamia na yeye wa Kanda ya Tabora ana Mikoa zaidi ya minne. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga.

Na. 101

### **Mradi wa Maji wa Mwalushu**

**MHE. NJALU D. SILANGA** aliuliza:-

Mradi wa Maji wa Mwalushu ulianza kutekelezwa tarehe 19 Januari, 2014 na vituo vyote 28 vimejengwa, mabomba yamelazwa na matenki mawili yamekamilika, lakini mradi huo hautoi maji mpaka sasa kutokana na Mkandarasi kutolipwa fedha zake:-

Je, ni lini Serikali itatoa pesa ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata maji safi na salama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Jimbo la Itilima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, Mradi wa Maji wa Mwalushu ulianza kujengwa mwaka 2014 na kwa sasa umefikia asilimia 70 ya utekelezaji. Mradi huu unagharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.2 na umelenga kuwashumia jumla ya watu 2,051 kwa kutumia vituo 29 vya kuchotea maji. Kwa sasa kazi zilizobakia ni ufungaji wa umeme, ujenzi wa tenki la chini ya ardhi na ununuzi wa pampu.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Januari, 2017 Mkandarasi wa mradi huu tayari amekwishalipwa jumla ya shilingi milioni 701. Wizara itaendelea kumlipa Mkandarasi madai yake kadri atakavyowasilisha kuititia Halmashauri ya Wilaya ya Itilima. Aidha, Mkandarasi anatarajia kukamilisha kazi zilizobaki ifikapo mwezi Aprili, 2017.

**SPIKA:** Eeh! Hili swali hili, watu wengi kweli! Leo si tutajadili maji jamani! Mheshimiwa Njalu.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa, Halmashauri tayari ilishatoa certificate Wizarani: Ni lini sasa fedha hizo zitaenda ili kusudi wananchi wa Nkoma na Mwalushu, takriban 14,000 waweze kupata huduma iliyo sawa? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Itilima inayo mabwawa 17; mabwawa haya yana upungufu wa miundombinu: Serikali iko tayari sasa kukutana na Wataalam wa Halmashauri yangu ya Itilima ili watakapoleta maombi wawze kuyashughulikia hayo mabwawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Njalu na wengine mnaotaja vile vijiji, sijui kama Waheshimiwa Mawaziri watavifahamu. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Engineer Kamwele.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, tumeshaweka utaratibu kwamba tutatoa fedha kwa kuwasilisha certificate. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara tu certificate itakapofika, fedha tunazo na kutokana na Mfuko wa Maji, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekuwa anatupatia fedha kila wakati. Kwa hiyo, fedha ipo, ila wakati mwininge tunachelewa kwa sababu ya uhakiki; lazima tuhakikishe kwamba certificate hiyo ni ya kweli na kwamba ikienda iende ikalipe malipo ambayo ni ya halali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la mabwawa 17; sasa hivi tayari bwawa moja tumemaliza ukarabati Bwawa la Habia, ambalo ni fedha zilizotolewa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Wizara imeshaagiza kwamba ikiwezekana kila mwaka kila Halmashauri itenye fedha na kujenga bwawa moja. Pia tuko tayari kukaa pamoja na Halmashauri ya Itilima ili kuangalia ni jinsi gani tunaweza tukashirikiana katika utekelezaji wa hayo mabwawa 17. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Masele, nilikuona.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mwezi uliopita Mheshimiwa Rais alifanya ziara kwenye Manispaa ya Shinyanga, Jimboni kwangu na aliagiza Waziri wa Maji aje Shinyanga akiambatana na mimi tukae tujadiliane mgogoro wa bei ya maji baina ya KASHUWASA ambao ni Mradi wa Maji wa Kitaifa na SHUWASA ambayo ni Mamlaka ya Maji ya Manispaa ya Shinyanga na wananchi wa Shinyanga:-

Je, Waziri wa Maji yuko tayari kuambatana na mimi mara baada ya Vikao hivi vya Bunge ili tukakae na wadau wote hao husika tutatue mgogoro wa bei kati ya KASHUWASA, SHUWASA na wananchi wa Shinyanga? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa KASHUWASA ni Mradi wa Kitaifa, siwezi kukubali kama Mbunge, wananchi wa Shinyanga wabebeshwe adhabu ya kugharamia mradi wa Kitaifa kwa kubebeshwa bei kubwa ya maji. Nahitaji majibu leo, Waziri kama yuko tayari twende tukashughulikie mgogoro huu. (Makofii)

**SPIKA:** Kwa kuwa, Waziri wa Maji, Engineer Lwenge yupo, tafadhalii, majibu Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mhweshimiwa Spika, kwanza kabisa, kwenda Shinyanga siyo tatizo, tunaweza tukaenda, lakini tunapokwenda kule lazima tuelewane tunachokwenda kufanya. Tunakwenda kule kwanza tunarejea Sheria Namba 12 ya mwaka 2009 inayohusu uendeshaji na utoaji wa huduma ya maji. Ndani ya Sheria ile tuliweka Mamlaka ya Udhibiti inayoitwa EWURA, hii ndiyo imepewa mamlaka ya kupanga bei za maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alichokielekeza ni kwamba, ni lazima tufanye ulinganifu kuangalia, je, maeneo mengine watu wanachangia maji kwa kiasi gani? Kwa Shinyanga Mamlaka ile bado ni changa. Bei ya maji inaweza ikaonekana kwamba ni kubwa kwa sababu ya wachache amboa ndio wanaochangia. Kwa hiyo, Serikali tuna jukumu la kuongeza mtandao ili wananchi wengi waingie kwenye mtandao waweze kuchangia huduma ya maji ili iweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakwenda Shinyanga, lakini nataka twende huku wakijua kwamba, siyo kwamba tunakwenda kushusha bei. Tunakwenda kufanya ulinganifu wa kuona ni kipi kifanyike kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Silinde, nilikuona.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kutokana na ukubwa wa tatizo la maji, Bunge lako liliidhinisha Sheria hapa ya kuweka zuio la fedha ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri hapa amekiri kwamba fedha zipo, lakini maji hakuna. Sasa swali ambalo nataka watupatie majibu, tumewapa fedha, lakini kwenye miji na vijijini kwetu kule maji hakuna. Nini kinachowafanya wanakwamisha miradi ya maji mpaka sasa hivi inashindwa kukamilika? Ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Engineer Lwenge, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tulipitisha Sheria ya Mfuko wa Maji; na fedha hizi huwa zinatolewa kila mwezi; lakini ili fedha hizi zitumike tulipeleka mwongozo kwenye Halmashauri zetu za Wilaya. Pamoja na mwongozo, tumefanya semina nchi nzima na Wakurugenzi pamoja na Wahandisi wa Maji kwamba fedha hizi zitatolewa kwa mfumo wa certificate. Kwa sababu tulishakubaliana katika bajeti ya mwaka huu kwamba kwanza tukamilishe miradi inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, nimetembelea baadhi ya Halmashauri, unakuta fedha wanazo zilizo-carry forward kutoka mwaka uliopita, lakini hawajafanya jambo lolote, wanasubiri wapelekewe fedha. Mwongozo tumewapa na tumewaelekeza. Kwa hiyo, kuna baadhi ya Halmashauri ziko na ile hali ya ufanyaji kazi wa kimazoea, hawataki kwenda na kasi ya Awamu ya Tano tunavyotaka matokeo.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge, awe karibu sana na Halmashauri yake kuweza kuona kwa nini hiyo miradi haiendelei? Kwa sababu, wakileta certificate, hakuna certificates ambazo zimebaki, tumeshapeleka fedha. Sasa hivi tuna certificates chache sana. Kila mwezi zikija, tunapeleka fedha. Kwa hiyo, nashauri tukae tuweze kuona kwa Halmashauri yako hasa ni nini kinachoendelea?

**SPIKA:** Waheshimiwa, mjadala wa maji tuufanye baadaye hapo, natambua kwamba wengi sana mnaguswa na haya mambo ya maji na Mheshimiwa Waziri wa Maji yupo kuwasikiliza.

Tuendelee na swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy. Bado tuko kwenye Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Keissy.

Na. 102

### **Ukamilishaji wa Skimu ya Lwafi**

**MHE. ALLY K. MOHAMED** aliuliza:-

Serikali imekwishatumbia zaidi ya shilingi milioni 800 kwa ajili ya Mradi wa Skimu ya Lwafi, lakini mradi huo haujawanufaisha kabisa wakulima zaidi ya 4,000 kwa sababu haujakamilika:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha mradi huo na kuwa msaada kwa wakulima wa mpunga zaidi ya 4,000?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi wa Tarafa ya Kirando inaendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mto Lwafi. Hadi sasa eneo la Awamu ya Kwanza la hekta 300 linaweza

kumwagiliwa kati ya hekta 2,500 zilizokuwa zimetengwa. Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha eneo lote la hekta 2,500 zilizopimwa na kusanifiwa mwaka wa 2012/2013 zimejengewa miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha eneo lote la hekta 2,500 zilizopimwa na kusanifiwa zinajengwa miundombinu, Serikali ilifanya marudio ya usanifu uliokamilika mwezi Septemba, 2016. Usanifu huo wa mapitio ulifanyika kulingana na hali ya sasa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza awamu ya pili ya utekelezaji wa skimu hiyo kwa kupata fedha za mkopo kutoka Serikali ya Japan, ambapo jumla ya shilingi milioni 580 zimepelekwa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuchimba mifereji ya kati yenye urefu wa mita 16,000, kujenga kivushamaji chenye urefu wa mita 200 kwa kuvuka mto Lwafi na kujenga vigawa maji 28 katika mifereji ya kati.

Mheshimiwa Spika, kazi hizo zitakapokamilika, eneo litakalomwagiliwa litafika hekta 800 kati ya hekta 2,500 zilizosanifiwa. Serikali itaendelea kutafuta fedha kupitia vyanzo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba eneo lote la hekta 2,500 linajengewa miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za kuwapata Wakandarasi wa Ujenzi wa miundombinu iliyopangwa; na makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kuwapata Wakandarasi hao, yamekamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy ameridhika.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nimeridhika vizuri sana, lakini ninachoomba ni Wizara ya Maji na Umwagiliaji kufuatilia kwa ukaribu mradi huu. Maana karibu miradi yote ya maji ya Wilaya ya Nkasi inaibiwa pesa. Tukisema hapa Bungeni, hakuna kinachofanyika. Juzi juzi namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji mwenyewe, alikwenda mpaka Namanyere, akaangalia miradi ambayo iliibiwa pesa na mingine iko chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba, Serikali inatoa pesa kwa wingi, lakini Serikali za kule Wilayani ndiko kuna mambo mazito, kuna mchwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifuatilie miradi hii. Hizi ni kodi za wananchi, tena ule ujenzi ni kodi ya Wajapani. Kwa hiyo, naomba Serikali iwe karibu kwa mradi huu ili wananchi wa Tarafa ya Kirando wanufaik. Siyo wauza chupi chupi wale, wala maji barabarani; wale wanafanya kazi na kazi yao ni kilimo ili kuwalisha wananchi wa Tanzania. Ahsante. (Makofij)

**SPIKA:** Ulikuwa ni ushauri tu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri upokee. Ila wale wengine sijui wanauzwa nini sijui, hata sikusikia vizuri. (Kicheko)

Mheshimiwa Azza Hamad Hilal, nilikuona.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kijiji cha Ishololo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kilitengewa fedha kwa ajili ya Mradi wa Umwagiliaji, zaidi ya shilingi bilioni moja. Mradi huu haujaweza kukamilika na Mkandarasi kuweza kuondolewa na Serikali kwa sababu, mradi huu haukuisha kwa wakati. Je, Mheshimiwa Waziri, uko tayari sasa kuja katika Kijiji cha Ishololo na kuona mashimo tulioachiwa na mkandarasi yule na mradi huu kuwa hauna tija kwa wananchi wetu? (Makof)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, uko tayari kuja?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niko tayari kutembelea miradi yote ya kilimo cha umwagiliaji. Labda niseme tu, hii miradi ya kilimo cha umwagiliaji katika sehemu kubwa, mingi ina matatizo. Kwa sababu ya matatizo, kweli tumekwenda tumekuta miradi mingi haifanyi kazi jinsi inavyotegemewa.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kurekebisha hivi, ndiyo maana Serikali tulianzisha Tume ya Umwagiliaji. Kazi yake ya kwanza ilikuwa kurekebisha miradi yote iliyokuwa imeanzhishwa kwa ufadhili mbalimbali huko nyuma ikiwa chini ya Wizara ya Kilimo, tuweze kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimwahidi Mheshimiwa Azza, fedha hata zikipatikana katika bajeti ya mwaka huu, tutaweza kuona nini tufanye katika kurekebisha mradi huu ambaa Mheshimiwa Mbunge anauelezea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, tafadhalii, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa swali la nyongeza. Kwa kuwa, tatizo kubwa la miradi hii ya umwagiliaji ni ule upembusi yakinifu sijui na usanifu. Kwa sababu, katika Jimbo langu la Liwale kuna Mradi wa Umwagiliaji wa Ngongowele umetumia zaidi ya shilingi bilioni nne na mradi ule sasa hivi uko grounded, hautegemei tena kufufuka. Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya pesa zile zilizopotea pale na hatima ya mradi ule? (Makof)

**SPIKA:** Duh! Mradi wa kijijini shilingi bilioni nne! Shughuli pevu. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la Mbunge wa Liwale.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Mradi wa Ngongowele ni kweli Mheshimiwa Mbunge tumeshaongea naye. Mradi huu umeshakamilika na tulikuwa tunatarajia kwamba sasa wananchi wagawane na kuanza kuutumia.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoongea Mheshimiwa Waziri muda mfupi uliopita, miradi mingi hii ya umwagiliaji ilisanifiwa. Nimejaribu kuzungukia miradi ya umwagiliaji, unakuta mradi umekamilika, lakini umekumbwa na tatizo la chanzo cha maji; kimekauka. Sasa hivi tulikuwa tunafikiria kurudia usanifu kuhakikisha miradi yote ambayo imekamilika, basi tunajengea mabwawa ili muda wote iwe inafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine imekamilika, lakini unakuta inafanya kazi kipindi cha mvua tu. Baada ya mvua kunakuwa hakuna maji, miradi haifanyi kazi, jambo ambalo siyo lengo. Ni miradi michache tu kama miwili katika mzunguko niliozunguka ndiyo nimekuta kwamba ina vyanzo vya maji vya kudumu ambavyo vinafanya kazi muda wote, watu wanalima mara mbili mpaka mara tatu. Kwa hiyo, alichokizungumza Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba, huu mradi ulikamilika na umetumia fedha nyingi, lakini una shida kwamba haufanyi shughuli iliyokuwa inatarajiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwamoto, swali la mwisho katika eneo hili.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali langu dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, katika Wilaya ya Kilolo kilimo cha mvua ni kilimo ambacho hakitegemewi; sasa hivi kilimo cha uhakika ni umwagiliaji; na kwa kuwa, katika Wilaya ya Kilolo kuna maeneo ambayo tayari mabwawa yалишахимбва kwa muda mrefu, lakini yanashindwa kusaidia wananchi kwa sababu ya ongezeko la watu; sehemu za Nyanzwa, Ruaha Mbuyuni na Mahenge. Je, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa, ni ahadi ya muda mrefu ya kuboresha mabwawa hayo, atakuwa tayari kufika na kuona ili katika bajeti hii aweze kutenga fedha ili kuboresha mabwawa hayo ili yaweze kulisha wananchi wengi wa Tanzania tuondokane na njaa? (Makofij)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu kwa kifupi. Unaweza ukafika huko Kilolo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme niko tayari kwenda kuangalia hayo mabwawa. Katika orodha tuliyonayo kwa sasa ya mabwawa, tumeainisha pamoja na bwawa hili kulifanya usanifu upya ili kuyakarabati yaweze kutoa huduma iliyokuwa inatarajiwa.

**SPIKA:** Tunaendelea, ambapo bado tuko Wizara ya Maji, swalii la Mheshimiwa Mbunge wa Ngara, Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza. Mheshimiwa Gashaza!

Na. 103

### **Tatizo Kubwa la Maji Safi na Salama – Ngara**

**MHE. ALEX R. GASHAZA** aliuliza:-

Jimbo la Ngara ni mionganini mwa Majimbo tisa ya Mkoa wa Kagera yenye tatizo kubwa la maji safi na salama katika vijiji vyake vingi; na Jimbo hili lina utajiri mkubwa wa vyanzo vya maji vikiwemo Mto Kagera na Mto Ruvubu pamoja na mlima mrefu kuliko yote ya Mkoa wa Kagera (Mlima Shunga) ambaao kitako chake kinagusa hii mito yote miwili kiasi kwamba yakijengwa matenki makubwa kwenye kilele cha mlima huu, maji yanaweza kusambazwa kwa mtiririko Vijiji vyote vya Wilaya ya Ngara, Biharamulo, Karagwe, Kyelwa na Chato:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia mito hii miwili ili kumaliza kabisa tatizo la maji katika maeneo yote tajwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Jimbo la Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mji wa Ngara una uhaba wa maji kama ilivyokuwa miji mingine iliyoko ndani ya Mkoa wa Kagera. Serikali kuitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bukoba, imemwajiri Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni katika miji mitano iliyopo katika Mkoa wa Kagera na mji mmoja katika Mkoa wa Geita. Miji hiyo ni Ngara, Biharamulo, Kayanga/Omurashaka, Kyaka/Bunazi, Muleba katika Mkoa wa Kagera na Chato katika Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya upembuzi yakinifu uliofanywa na Mhandisi Mshauri huyo, Mto Kagera na Mto Rubuvu itakuwa ni mojawapo ya vyanzo vya maji vitakavyotumika katika Mji wa Ngara. Miji mingine itapata maji kutoka katika vyanzo vyenye uhakika vilivypo katika Wilaya hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mhandisi Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2017. Baada ya kukamilika kwa kazi hiyo, Serikali itatenga fedha za ujenzi kuititia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Pili ambayo imeanza kutekelezwa Julai, 2016.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gashaza, swali la nyongeza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ambayo yamejielekeza kwenye sehemu ndogo tu ya swali langu la msingi; kwa sababu ameelezea juu ya mpango wa maji kwenye miji sita ya Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba Wilaya yangu ya Ngara, takriban asilimia 50 ya maeneo ya vijiji kuna tatizo kubwa hili la maji; na bahati nzuri tarehe 30 mwezi Desemba mwaka jana, 2016, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo alifika akaona mito hiyo na mlima huo ninaousema; na kwa kutumia vyanzo hivi maana yake ni kwamba tutaondoa kabisa kero ya maji katika vijiji vyote vya Wilaya ya Ngara na hizi nyingine ambazo nimezitaja; na huu ndiyo utakuwa ni mwarobaini:-

Sasa swali langu namba moja: Je, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI wako tayari kutuma wataalam ili waweze kufika maeneo yale na kuweza kuweka mkakati wa kuandaa mradi mkubwa ambao unaweza ukaondoa kero hii ya maji kwenye Viji vya Wilaya ya Ngara, Karagwe, Kyerwa, Biharamulo na Chato kama ilivyoelezwa kwenye swali la msingi? (Makofij)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; mwaka 2016 mwezi wa Pili Halmashauri yangu ya Wilaya ya Ngara ilipeleka barua kwenye Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa ajili ya kuomba mitambo miwili ya kusukuma maji kwenye eneo la K9 ambapo kuna taasisi za Serikali na wananchi kwa maana Kambi ya Jeshi, Shule mbili za Sekondari na wananchi wa Kijiji cha Kasharazi; na pampu ya pili kwenye eneo la Mamlaka ya Mji wa Ngara Mjini, ambayo pamoja mamlaka kushugulikia usambazaji wa maji mjini, bado kulingana na umuhimu wa taasisi zilizopo pembezoni kama Shule ya Sekondari Ishunga walikuwa wakipeleka maji kule, lakini baada ya mtambo kuharibika uliokuwa unasukuma maji, imekuwa ni tatizo.

Je, Wizara kwa sababu tayari ilishaji-commit tangu tarehe 25 mwezi wa Pili kwamba itapeleka pampu hizi mbili mwaka jana...

**SPIKA:** Mheshimiwa Gashaza, sasa si uulize swali!

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Spika, swali langu je, ni lini sasa Wizara itapeleka fedha hizi ambazo ni takriban shilingi milioni 50 kwa ajili ya kununua pampu hizi za kusukuma maji katika maeneo haya? (Makofij)

**SPIKA:** Haya. Majibu Naibu Waziri, Mheshimiwa Engineer Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gashaza amezungumzia matatizo ya maji ya Ngara na Wilaya zote Mkoa wa Kagera akihusisha pia na vijiji vya wilaya hizo; na ameomba kwamba tupeleke wataalam.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa yupo mtaalam mshauri ambaye anaangalia uwezekano wa kutumia mito hiyo miwili ambayo ni mikubwa ili kuweza kupeleka maji kwa wananchi. Miradi hii ambayo itatekelezwa chini ya Wizara ya Maji, itahakikisha inapeleka maji kwenye miji mikuu ya hizo Wilaya na vijiji vinavyopitiwa na bomba kuu kuelekea kwenye hizo Wilaya.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Vijijini, katika bajeti ya mwaka huu tumehakikisha kwamba kila Wilaya imepewa bajeti ili waweze kushughulikia kupeleka maji kwenye Kata na Vijiji vinavyozunguka hizo Halmashauri. Mheshimiwa Waziri ametoka kuzungumza sasa hivi kwamba tayari baada ya kuona kwamba utekelezaji unasuasua tuliamua kuandika mwongozo kupeleka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maji kupitia bajeti ambayo imetengwa na Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, pia nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tupo tayari na tumekuwa tunafanya hivyo. Kama Halmashauri zinahitaji wataalam, basi tunaweza tukashirikiana kutoa wataalam ili kwenda kuangalia hilo tatizo kwa pamoja tuone jinsi ya kulishughulikia.

Mheshimiwa Spika, nikiri katika swali lake la pili, ni kweli na mimi mwenyewe waliniambia na aliniletea nakala ya barua kuhusiana na maombi ya pampu kwa ajili ya kufufua zile pampu ambazo zimeharibika.

Mheshimiwa Spika, nizungumze suala moja. Waheshimiwa Wabunge, ikishakuwa Mamlaka, maana yake, inajitegemea kwenye *running*. Serikali inasaidia katika uwekezaji. Sasa inawezekana barua hizo baada ya kwenda kule kwenye Wizara zilikutana na tatizo hilo. Mara nydingi kwenye uwekezaji ndiyo tunasaidia mamlaka, lakini kwenye yale matumizi ya kila siku huwa tuaachia wao wenyewe wafanye kazi hiyo kwa kutumia mapato yao. Inategemea sasa, Mamlaka kama ipo chini ya Wilaya, kama kuna matatizo inabidi waripoti kwenye Wilaya. Mamlaka zilizopo chini ya Mikoa, kama kuna tatizo, wanaripoti kwenye Mikoa.

Mheshimiwa Spika, namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hili suala kwa sababu nalifahamu, nitajaribu kuwasiliana na Wizara kuona limefikia wapi. (Makofii)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, masuala ya maji kwa kweli inaelekea ni tatizo kubwa. Waheshimiwa Wabunge mliosimama ni karibu robo ya Bunge zima.

Kwahiyo, Waziri wa Maji na Naibu, mvulimie kidogo. Nimechukua baadhi ya majina yenu, kwa hiyo, kaeni chini nitakuwa nawaita wale ambao watasisimama. Nimeshawaona wote, nyie kaeni tu. Tuanze na Mheshimiwa Joseph Mbllinyi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa wokovu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, wakati maeneo mengi tatizo ni miundombinu na vyanzo vya maji, Mbeya hatuna tatizo la kati ya hayo kwa maana ya vyanzo vya maji, hatuna au hatutakiwi kuwa na tatizo la vyanzo vya maji; lakini pia miundombinu Mbeya ilishakamilika mwaka 2013 ikazinduliwa na Rais Mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete mradi ambao ulifadhiliwa kwa mabilioni na EU. Leo hii pamoja na yote hayo, tuna wiki ya nne, takriban mwezi mzima Mbeya maji hayatoki kuanzia Uyole kwenda Mwakibete, Mama John na Sai, maji hayatoki kote.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Maji asimame hapa awaambie wana Mbeya anatusaidiaje kutuokoa kwa sababu tupo kwenye hatari ya kukutana hata na magonjwa ya milipuko ukizingatia hiki ni kifuku, mvua zinanyesha, halafu maji ya kufanya usafi hamna. Kwa kweli Mbeya ni disaster na inahitaji neno la haraka sana kutoka kwa Waziri Mheshimiwa Engineer Lwenge. (Makofii)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Engineer Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Sugu kuhusiana na matatizo ya maji katika Mji wa Mbeya; wiki iliyopita ilinyesha mvua kubwa sana Mbeya ya muda mfupi lakini ilikuwa mvua kubwa. Maji yalitiririka yakaenda mpaka kwenye chanzo cha Nzogwe sehemu ambayo ina pampu zinazosukuma maji katika Mji wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kutohana na hilo, kwa sababu zile pampu zinatumia umeme na kwa teknolojia, kukiwa na maji huwezi kuwasha umeme, kwa hiyo Mji wa Mbeya umekosa maji kwa muda wa siku nne. Taarifa hii kabla

Mheshimiwa Sugu hajasema, nilikuwa nimetaarifiwa tayari na Mheshimiwa Mwanjelwa kwamba Mji wa Mbeya una matatizo... (Makofii)

(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, hivyo, niseme kwamba...

(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Naomba mnisikilize...

**SPIKA:** Ongea na mimi Mheshimiwa Naibu Waziri. Endelea kuongea na mimi.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, jana tatizo hilo lilikamilika, baadhi ya mashine zikawashwa; na leo asubuhi mashine zilizobaki tayari zimeshawashwa. Kwa hiyo, nakuomba tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tukitoka Bungeni saa 7.00 naomba upige simu tena utakuta hali ya maji tayari imeshakaa vizuri. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilisema kaeni tu wote. Mheshimiwa Sofia Mwakagenda.

**MHE. SOFIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tuliku-miss hekima zako. Kwa kuwa tatizo la wana Ngara linafanana kabisa na tatizo la watu wa Rungwe. Rungwe kuna vyanzo vingi sana vya maji, lakini tuna shida ya maji katika Vijiji vya Mpandapanda, ikuti na sehemu nyinginezo. Je, Mheshimiwa Waziri anatusaidiaje tuweze kupata maji ukizingatia tunavyo vyanzo lakini watu bado wanahangaika kupata maji salama? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Eng. Lwenge.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa kutoa majibu ya ujumla kwa wale wengine ambao pengine watauliza swali linalofanana na la Mheshimiwa Sofia.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu, kama alivyosema Naibu Waziri kwamba kila Halmashauri tumepanga fedha kwa ajili ya kuendelea kutoa miradi ya maji. Sasa katika Halmashauri yako, ninyi ndio mlipanga vipaumbele kwamba kwa mwaka huu mtapeleka maji kwenye Vijiji vipi?

Mheshimiwa Spika, tumetoa mwongozo kwamba kama mmeshapanga vipaumbele, tangazeni tenda ili tupate Mkandarasi aweze kufanya. Waziri wa Maji anafanya kazi ya uratibu, mtekelezaji ni Mkurugenzi wa Halmashauri ambayo wewe unatoka kule. Naomba tusaidiane kusimamia hawa Wakurugenzi kwenye Sekta ya Maji ili waweze kufanya kazi inayotakiwa wananchi wetu wapate maji. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu. Mbulu Vijiji tuna tatizo linalofanana na Ngara.

Mheshimiwa Spika, tuna Bwawa la Dongobesh ambalo limejengwa zaidi ya shilingi bilioni mbili; na kwa kuwa limekaribia kukamilika na Naibu Waziri ameshafika; kilichobaki ni njia tu ya maji ya kwenda kuwafikia watumiaji. Je, Mheshimiwa Waziri atuambie lini anapeleka fedha kwa ajili ya kumalizia tu hilo bwawa ambalo kimsingi limekamilika bado tu njia ya kwenda kupeleka maji kwa watumiaji? (Makofii)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Engineer Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba Mheshimiwa Flatei Massay Jimbo lake nimelitembelea, Bwawa la Dongobesh nimeliona na limekamilika kwa zaidi ya asilimia 90. Kilichobaki ni spillway ambayo itakuwa inatoa maji yale yanayozidi ili yasije yakabomoa ule ukuta mkubwa uliojengwa kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Flatei kwamba fedha imeanza kutoka. Mwezi uliopita tumeputa shilingi bilioni moja na fedha zitakazotoka mwezi huu nitahakikisha napanga kwa sababu hela iliyobaki ni ndogo sana ili tulikamilishe hilo Bwawa la Dongobesh liweze kufanya kazi iliyotarajiwa. (Makofii)

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa Wizara hii kwa siku ya leo, Mheshimiwa Devota Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo la maji Ngara linafanana kabisa na tatizo la maji katika Mkoa wa Morogoro, licha ya Mkoa Morogoro kuwa na mito mingi, lakini wananchi wa Morogoro hawapati maji safi na salama. Je, Serikali haioni kama kuna haja sasa ya kujenga bwawa lingine liweze kusaidiana na Bwawa la Mindu ili kutosheleza maji kwa wakazi wa Morogoro? (Makofii)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Engineer Kamwele tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Devotha Ninja kuhusiana na kuongeza kiwango cha maji katika Bwawa la Mindu; kwa bahati nzuri pia nimeuzunguka Mkoa wote wa Morogoro, nimeenda Bwawa la Mindu.

Mheshimiwa Spika, nimpe taarifa Mheshimiwa Ninja kwamba tayari Benki ya Ufaransa imetupa Euro milioni 70 sawa na zaidi ya shilingi bilioni 170 kwa ajili ya kuongeza kiwango cha Bwawa la Mindu ili Bwawa la Mindu liweze kuwa na maji mengi. Wakati nafanya ziara kule, nilikuta uzalishaji wa maji ni lita milioni 25 badala ya lita milioni 45 zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa hivi makabrasha ya zabuni yamekamilika, tumeshasaini mkataba wa mhandisi mshauri ambaye atapitia nyaraka zilizopo kwa muda wa miezi sita na baada ya hapo tunatangaza tenda ya kuanza ujenzi ili tuweze kuongeza kiwango cha maji katika Mji wa Morogoro. Kwa hiyo, suala hilo la Mheshimiwa Ninja tunalifanyia kazi, lakini naomba Mheshimiwa Mbunge anisaidie. Wakati nafanya ziara pale tumekuta lile bwawa linachafuliwa sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa tunaimba kila siku kuhusu uchafuzi wa mazingira, naomba tusaidiane. Watu tayari wanafanya kilimo cha umwagiliaji juu ya mito ambayo inaingiza maji katika Bwawa la Mindu. Tusaidiane, tuwatengenezee utaratibu mwingine ili tuwe na uhakika wa maji katika Bwawa la Mindu. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Tunawashukuru na poleni kwa maswali mengi ya leo. Swali la mwisho kwa siku ya leo linaelekezwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Faida Bakar.

Na. 104

### **Wanafunzi wa SUZA Wanaofanya Internship – Tanzania Bara Kutolipwa Posho**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha SUZA wa Sayansi ya Afya na Mazingira (*Bachelor of Science in Environmental Health*) ambao wanafanya internship ya mwaka mmoja Tanzania Bara sambamba na wale wanaomaliza Vyuo vya Tanzania Bara, hawalipwi posho yoyote ya internship wakati wenzao wanaomaliza Tanzania Bara wanalipwa posho hizo:-

Je, ni kwa nini wanafunzi hao hawalipwi posho hizo kama ambavyo wenzao wa Tanzania Bara wanalipwa ili kuwaondolea maisha magumu walijonayo wakati wa *internship* ambayo yanaweza kusababisha kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**  
ali jibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Baraza la Kusajili Wataalam wa Afya ya Mazingira, huratibu zoezi la *internship* na hutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria ya Kusajili Wataalam wa Afya ya Mazingira ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii, inawataka wataalam wa Afya ya Mazingira wote wanaomaliza Shahada ya Afya ya Mazingira Tanzania Bara, washiriki mafunzo ya kazi kwa vitendo (*internship*) kwa kipindi cha miezi 12 kabla ya kuajiriwa. Hivyo basi, Serikali hulazimika kuwalipa posho ya kujikimu wakati wa mafunzo kwa vitendo ili kukidhi matakwa ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itashauriana na Wizara ya Afya Zanzibar ili nao waangalie uwezekano wa kuwalipa wahitimu kutoka Chuo Cha SUZA, waweze kutekeleza vyema mafunzo ya kazi kwa vitendo (*internship*) kwa kipindi cha miezi 12 kabla hawajasajiliwa ili kuwaondolea maisha magumu walijonayo wakati wa mafunzo haya, ambayo yanaweza kusababisha kushindwa kutekeleza wajibu yao kwa ufanisi. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Faida Bakar, swali la nyongeza.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri amenijibu majibu mazuri sana na ndiyo kawaida yake. Pamoja na majibu mazuri, naomba kuuliza swali moja na nikipata baadaye hata la pili naweza kuongezea. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Wizara ya Afya ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itashauriana na Wizara ya Afya ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kuona uwezekano wa kuwapatia posho wataalam hawa wanaotoka Chuo Kikuu cha SUZA ambao wanafanya kazi za vitendo katika maeneo mbalimbali ya hapa Tanzania Bara, nakubali atashauriana, lakini anaweza akasema kwamba atashauriana, lakini tukasubiri mwaka mzima umeisha; naomba kujua, ni lini hasa ushauri huu utanza, natamani uanze hata leo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri huyu ameonesha nia safi ya kusaidia suala hili na kwamba amesema atashauriana na Waziri mwenzake wa Zanzibar, naomba kushauri, akishauriana naye aweze kumweleza sheria kama hii ya huku iwekwe au mwongozo ili kuwaondoshea madhila wataalam wetu ambao wanafanya kazi kiuzalendo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofii)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar kwa kunipiga fagio zito kama alilonipa hapa siku ya leo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwamba ni lini tutashauriana na wenzetu wa upande wa Zanzibar, utaratibu tulionao kila baada ya miezi mitatu Wizara hizi mbili huwa zinakutana, kikao cha kwanza cha mwaka huu kimefanyika mwezi Januari na cha pili kitafanyika mwezi wa tatu kwa ajili ya mashauriano ya mambo mbalimbali na hili sasa litakuwa ajenda ya kikao cha Mawaziri kitakachofanyika mwezi wa Tatu.

Mheshimiwa Spika, ili kumtoa wasiwasi, na kuwatoa wasiwasi wahitimu wote wa kozi ya *Environmental Health Sciences* wanaotokea Zanzibar ambao wanapenda kufanya *internship* huku Tanzania Bara, ni kwamba kuna utaratibu ambao sio rasmi sana umewekwa ambao umekuwa ukiwasaidia kwa muda mrefu wahitimu wote ambao wanahitaji kufanya *internship* Tanzania Bara ambao wanaotokea upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu utaratibu huo umekuwepo na haukuwa rasmi ndiyo maana leo hii ninavyoongea hapa Wizara ya Kazi ya Jamhuri ya Muungano imeita wadau kwa ajili ya kutengeneza kitu kinachoitwa *National Framework on Internship Programme* ambapo ndani yake utawekwa utaratibu wa namna ya kuwashudumia wanafunzi wanaotoka Zanzibar ambao wanataka kufanya *internship* huku Tanzania Bara. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Najma Giga swali la nyongeza, kabla ya Najma, Mheshimiwa Waziri wa Afya tafadhali, majibu ya nyongeza.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nataka kujibu sehemu ya pili ya swali la Mheshimiwa Faida kwamba ni kwa nini sasa na yeye anatushauri na sisi tukashauri Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar walifanyie kazi suala hili. Tunao Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndani ya Bunge hili, kwa hiyo, napenda kuwashauri walibebi suala hili walieleze pia katika Baraza la Wawakilishi ili liweze kupata nguvu, kwa hiyo litatoka katika Wizara ya Afya ya Jamhuri ya Muungano lakini pia litoke kwenye Baraza la Wawakilishi la Zanzibar mwisho wa siku watoto wetu wataweza kufanya *internship* bila shida. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu. Mheshimiwa Giga nilishakutaja.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa vile suala la elimu ya juu ni suala la Muungano na kuna watu kama sisi yaani kama mimi, wazazi, hasa wa kike tulio majumbani, huwa hatuwezi kwenda *directly* kusoma kwenye vyuo vikuu kwa kuijendeleza. Kwa mfano kama mimi mwenyewe nimesoma *distance learning* kwenye Chuo cha ICM cha Uingereza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa hili si tatizo kwa upande wa Jamhuri ya Muungano, wenzetu hawa ambao wamesoma *distance learning* wanaajiriwa kwenye taasisi za muungano na Serikali kwa ujumla lakini tatizo lipo kwa upande wa Zanzibar; sisi ambao tumesoma *distance learning*, hasa wanawake tunaoishi majumbani tunakuwa hatuwezi kwenda vyuoni, tunaonekana kwamba vile vyeti vyetu vya *distance learning* si chochote isipokuwa wale ambao wamekwenda *direct* kusoma wanakubaliwa.

Sasa je, kwa nini Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hazikai pamoja zikakubaliana mfumo ulio bora ili na sisi wazazi hasa wa kike wa Zanzibar tuweze kuijendeleza kimasomo kuitia *distance learning*? (Makofij)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Sijui ni la Profesa Ndalichako naona, tafadhalii majibu Mheshimiwa Waziri wa Elimu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Niseme tu kwamba, ni kweli suala la elimu ya juu ni suala la muungano na taratibu za kujunga na vyuo na kuhakiki watu wanaosoma nje zinafanywa na TCU. Lakini pia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina taratibu zake za ajira na ndiyo maana kabla ya kuajiri wana taratibu zao za kuhakiki vyeti. Kwa hiyo, niseme kwamba na mimi nilipokee ili kama sehemu ya masuala ambayo ni ya muungano tunakaa tunayajadili na lenyewe tuangalie

kwa pamoja na Waziri mwenzangu wa Elimu wa Zanzibar ili tuangalie namna ya kulipatia ufumbuzi. Nashukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa kwa sababu ya muda naomba tukubaliane kwamba kwa leo tuishie hapa kwenye kipindi cha maswali, nawashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa mliotupa, tuendelee na matangazo.

Nimwombe radhi Mheshimiwa Engineer Kamwelwe, nilimtaja kimakosa hapa nikamtaja kama Mheshimiwa Ngonyani. Unajua Wangoni hawa wanatusumbua majina yao hawa, maana yake kuna Mheshimiwa Joseph Ngonyani, Mbunge wa Korogwe, kuna Edwin Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo, kwa msiofahamu kuna Mheshimiwa Jenista Ngonyani lakini pia humuhumu ndani kuna Mheshimiwa Jenista Mhagama, kuna Mheshimiwa Joseph Mhagama, basi hawa Wangoni ndiyo hivyo tena tuwazooee majina yao yanachanganyachanganya kidogo. (Kicheko)

Wageni tulionao siku ya leo, kama mtakavyoona galleries zimejaa kwelikweli zote ziko full:-

Tuanze na wageni 29 kutoka kule Kongwa, wanakwaya wa KTC, naomba msimame hapo mlipo, wakiongozwa na Dada Eliezer Balisidya na Amani Kasomo. Karibuni sana, bahati mbaya Bungeni hapa hatuimbi lakini mngeweka tune moja Waheshimiwa Wabunge wote hapa wangeshangaa jinsi ambavyo Kongwa kuna vipaji vya kila aina na kwa vile Mheshimiwa Nape yuko hapa basi angeona namna gani ya kuwa-promote. Karibuni sana Bungeni, karibuni, ahsanteni sana na mnaweza kukaa. (Makofi)

Tuna wageni wanne kutoka Jumuiya ya Ulaya (EU) hapa nchini, wakiongozwa na Balozi Van de Geer, karibuni sana wageni kutoka Ubalozi wa EU hapa nchini, karibuni sana pamoja na ndugu David Martin. (Makofi)

Tunaye Mkuu wa Wilaya ya Chunya, ndugu Rehema Madussa ambaye pia ameambatana na viongozi na watendaji kutoka kwenye Wilaya hiyo ya Chunya. Karibuni sana Mkuu wa Wilaya ya Chunya, karibuni sana na Mbunge wenu Mheshimiwa Mwambalaswa yuko hapa. (Makofi)

Tuna wageni kutoka kule Urambo, jimboni kwa Mheshimiwa mama Margaret Sitta, hawa ni Shule ya Santa Maria, naomba msimame pale mlipo Santa Maria. Wako wapi Santa Maria, eeh, baadhi yao wako pale juu, karibuni sana. (Makofi)

Hawa Santa Maria kwenye mtihani wa darasa la nne mwaka huu, Mheshimiwa Profesa Ndalichako, katika wanafunzi ambao idadi yao haizidi 40 walikuwa ndiyo wa kwanza Tanzania na kwenye mtihani wa kidato cha pili katika Shule hii ya Santa Maria wanafunzi wao wote walipata daraja la kwanza; halafu kuna Waheshimiwa Wabunge huwa wanasimama humu wanasema elimu imeshuka, haijashuka chini ya Mheshimiwa Profesa Ndalichako, ushahidi ni huo jamani. (Makofi/Kicheko)

Naomba nitambue uwepo wa vijana wetu wa Serengeti Boys. Ahsanteni sana Serengeti Boys, tunawakaribisha Bungeni, makofi hayo ni kuashiria furaha waliyonayo Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri ambayo mnaioneshaa. Hawa ndiyo wawakilishi wetu kwenye fainali za Afcon under 17 mwaka huu, tunawaaminia na tunawategemea na tutakuwa tunafuatilia kwa karibu sana, tunaomba sana safari hii mtuletee heshima kwa kutuletea kombe lile kutoka kwenye mashindano yale. Waziri wenu, Mheshimiwa Nape, ametuhakikishia kabisa kwamba atawapa kila aina ya support. Ahsante sana. (Makofi)

### **WABUNGE FULANI:** Kocha, Kocha!

**SPIKA:** Tunaendelea na matangazo mengine; tangazo la ofisi la semina, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba leo, Alhamisi, tarehe 9, Februari, kutakuwa na semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote kuhusu mpango wa kunusuru kaya maskini. Semina hiyo itaratibiwa na TASAF na itafanyika katika Ukumbi wa Bunge kuanzia saa saba mchana.

Tumeelewana Waheshimiwa Wabunge, eeh! Kule vijijini pakiwa na kikao cha TASAF hata kama mpaka saa 12.00 wawezeshaji hawajafika wananchi wanasubiri maana kikao cha TASAF huwa kina utaratibu wake mzuri, sasa leo TASAF iko Bungeni, kwa hiyo naomba saa saba... (Makofi/Kicheko)

Napenda niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Kampuni ya Simu ya TTCL wanafanya maonesho ya huduma za mtandao wa simu za mikononi za 4G LTE. Maonesho haya yanafanyika katika Viwanja vya Bunge nyuma ya jengo la Utawala leo, tarehe 9, Februari. Mgeni rasmi katika maonyesho haya ni Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kutembelea eneo hilo ili kujiona bidhaa na huduma zitolewazo na Kampuni ya TTCL na jinsi kampuni hiyo ilivyojiandaa katika kutoa huduma kwa Serikali hapa Dodoma na kwa Waheshimiwa Wabunge majimboni. Kwa hiyo, tunawaomba mfike pale nyuma ya jengo la Utawala kuna maonyesho maalum kwa ajili yenu Waheshimiwa Wabunge.

Tangazo la Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya CPA anawaomba kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo ya utendaji leo Februari, 9, katika ukumbi namba 229. Wajumbe mnajifahamu, tunaomba wote mhudhurie katika kikao hicho cha CPA cha Kamati ya utendaji.

Katibu tuendelee!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji na Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa Kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017**

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mwongozo!

**SPIKA:** Haya, Katibu nitajieni majina.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nimeomba mwongozo kwa sababu sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri na ukisikia timesema zimepotea shilingi milioni 840 halafu kuna watu wanakuja wanasesma sio 840 ni 500,000, ni 1,600,000, ni ukweli sisi Siha hatuwezi kumkimbiza mtu aliyeiba 500,000 wala 1,600,000. Hii sh. 1,600,000 ambayo naizungumzia hapa ni pesa ambayo tayari Charles Mlingwa amezikabidhi TAKUKURU, amezikabidhi na amepewa risiti ya TAKUKURU kwamba amerudisha hizi hela.

Mheshimiwa Spika, sasa nilitamani niambiwe mtu akirudisha hela alizoiba TAKUKURU kinachofuata ni nini? Vilevile nimeambiwa kwamba Mkuu wa Mkoa haingilii TAKUKURU lakini nina ushahidi wa kutosha, nilitegemea ningeambiwa nipeleke ushahidi na nikwambie ningesema hapa Wakuu wa Mikoa watatu wanaoingilia TAKUKURU lakini mmoja amekwepa kamera zangu na sikutaka nzungumze kitu nisicho na ushahidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukubaliane kwamba tunataka kukomesha ujisadi katika nchi hii, lakini tunataka kuokoa ushirika katika Mkoa wa Kilimanjaro na Wilaya ya Siha. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako ni nini inapofika mahali viongozi waandamizi wa Serikali wanashiriki kwenye mambo machafu. (Makofi)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, tuliku-miss. Naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7), sitaki kuisoma, kwa jambo ambalo limetokea hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, tunajua Taifa letu Watanzania wanapenda michezo, Waheshimiwa Wabunge wanapenda michezo na sisi kama Wabunge tumekuwa tukililia sana timu yetu kufuzu kushiriki katika Mataifa mbalimbali. Lakini tunajua kwamba kuiachia Serikali peke yake na wadau kuhakikisha timu hii inafanikiwa na kupata morale katika kuhakikisha inaliwakilisha Taifa letu najua kabisa ni kazi ngumu na bajeti ni kama bilioni moja, kama sikosei, ili kuhakikisha timu hii inafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba mwongozo wako na Waheshimiwa Wabunge kama watakubali wote kwa pamoja, kwa sababu mafanikio ya timu hii naamini kabisa yatakuwa mafanikio ya timu ya *Taifa Stars*. Sasa naomba mwongozo wako, na Waheshimiwa Wabunge mkiridhia, kwa nini tusitoe mchango wa posho ya siku moja tu kuunga mkono jitihada ya kutoa motisha... (Makofij)

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MBUNGE FULANI:** Hakuna hiyo, hakuna!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Ili timu yetu hii ya Taifa iende ikafanye vizuri...

**MBUNGE FULANI:** Hatutaki!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namlinda Mheshimiwa...

**WABUNGE FULANI:** Hatutaki!

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy nilikusikia, unasemaje!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, tutoe.

**MBUNGE FULANI:** Hakatwi mtu!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, Uganda timu yao ilipokuwa inakwenda michezo ya Afrika Wabunge walitoa posho, Wabunge hii namuunga mkono Mheshimiwa Ester. (Makofij)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, samahani, inawezekana ni mwongozo.

Mheshimiwa Spika... kanuni ileile...

**SPIKA:** Nimekuruhusu, endelea kuongea.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, pia naunga mkono kwamba timu hii kwa sababu ni ya kwetu na imetupa heshima kuja hapa Bungeni, naunga mkono tutoe mchango wetu kwa ajili ya timu hii. (Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, mwongozo, Mheshimiwa Spika mwongozo

**SPIKA:** Mheshimiwa Khatib haya twende huku.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, haya mambo ya mchango yanaenda na hiari ya mtu. Isitumike Bunge hili kila aliye na lake analeta mchango. Mchango atoe anayetaka, asiyetaka afanye anavyotaka, hatutoi.

**SPIKA:** Sasa naomba nilimalize jambo hili.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa huku.

**SPIKA:** Naomba nilimalize jambo hili kwa utaratibu wetu ule wa Kibunge kwa sababu ni jambo kubwa na ni jambo muhimu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa huku.

**SPIKA:** Timu hii imetuletea heshima kubwa sana katika Nchi yetu, na sisi tunawaomba Watanzania wote waiunge mkono timu hii. Nadhani ni vizuri tukawaomba Watanzania waiunge mkono timu hii kwa sisi kuwa mfano. Sasa naomba niwahoji, hoja ya Mheshimiwa Bulaya ya kuichangia timu ya Serengeti Boys shilingi 20,000. (Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**SPIKA:** Nilivyosikia waliounga mkono wameshinda.

**MBUNGE FULANI:** Wameshindaaaa!!

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Tuhesabu kura, tuhesabu kura.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, tupige kuraa.

**SPIKA:** waheshimiwa Wabunge, kuhusu suala la Mheshimiwa Mollel, Mheshimiwa Waziri wa Nchi Serikalini lichukueni mlifanyie kazi kwa wakati muafaka...

**MBUNGE FULANI:** Tuhesabu kura

**SPIKA:** Tutakapokuja kurudi tuone ni namna gani nini cha kufanya. Naomba hilo mlichukue.

**MBUNGE FULANI:** Tuhesabu kura

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge...

**MBUNGE FULANI:** Tazama anacheka cheka pale.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo sasa naomba nimwite Mheshimiwa Zungu muweze kuendelea na kikao.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MBUNGE FULANI:** Tupige kura

**MBUNGE FULANI:** Kuchanga ni hiari.

**MBUNGE FULANI:** Tuhesabu kura.

**MBUNGE FULANI:** Mie yangu isijekatwa!

**MBUNGE FULANI:** Hatutaki.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Elfu ishirini.

**MWENYEKITI:** Order please. Wabunge naomba utulivu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu.

**MBUNGE FULANI:** Madawati yetu...

**MWENYEKITI:** Katibu. Mwenyekiti, Wabunge naomba utulivu. Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu...

Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge. Namwita Katibu, Waheshimiwa Wabunge si jambo jema tuitane majina sasa hivi. Mwenyekiti, Kamati ya kudumu ya Bunge ya Kilimo (Makofii)

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA - MAKAMUMWENYEKITI, KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, naomba maelezo yote yaingie katika Hansard.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15), Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya shughuli zilizotekelawa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017, ili iweze kujadiliwa na kuungwa mkono na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017, Kamati imeweza kutekeleza shughuli mbalimbali zilizoainishwa kwenye taarifa ya Kamati iliyogawiwa kwa Wajumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Serikali kuhusu hali ya hewa na ukame nchini. Taarifa iliyowasilishwa iliashiria kujitokeza kwa upungufu wa chakula nchini. Hadi inapowasilishwa taarifa hii, tathmini ya Serikali imebainisha halmashauri 55 zina upungufu wa chakula. Aidha, maeneo mengi nchini bei ya vyakula imeendelea kupanda kutokana na athari za ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali ya ukame, upungufu wa chakula na kuendelea kupanda kwa bei ya mazao, Kamati inashauri Bunge liitake Serikali kuchukua hatua za dharura zifuatazo:-

(a) Sehemu ya akiba ya chakula kilichohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NRFA) kitolewe na kuuzwa kwa bei elekezi iliyowekwa na Serikali katika Halmashauri 55 zilizobainika kuwa na upungufu mkubwa wa chakula na maeneo mengine ambapo bei inapanda kwa mazao ya chakula.

(b) Serikali ihakikishe kuwa, mbegu bora zinazostahimili ukame na zenye kukomaa kwa muda mfupi zinapatikana na kuwafikia wakulima mapema kabla ya mvua za msimu wa mwezi Machi;

- (c) Serikali iongeze kasi ya kuhamasisha, kuratibu na kusimamia wakulima, kulima mazao ya muda mfupi na yanayostahimili ukame;
- (d) Serikali iratibu na kusimamia ipasavyo udhibiti wa usafirishaji wa mazao ya chakula nje ya nchi.
- (e) Wananchi wahimizwe kuweka akiba ya chakula cha kutosha hasa kwenye maeneo yaliyopata mvua chini ya wastani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Taarifa ya Serikali kuhusu hali ya ukame na athari zake na hatua ambazo Serikali imekuwa ikichukua, Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya maeneo kame katika Wilaya za Kiteto na Simanjiro mkoani Manyara kwa lengo la kubaini hali halisi ili iweze kuishauri vema Serikali kuhusiana na matokeo ya ziara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shabaha kubwa ya ziara hiyo ilikuwa ni kutambua athari za ukame, upatikanaji chakula, hali ya mifugo na maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa ukosefu wa mvua umeleta madhara yafuatayo:-

- (a) Uhaba mkubwa wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.
- (b) Kukauka kwa visima na mabwawa.
- (c) Upungufu wa uzalishaji wa mazao mbalimbali, hali iliyopelekea usalama wa chakula kutoridhisha.
- (d) Mabadiliko ya tabianchi na shughuli za binadamu kwa kiasi kikubwa vimeathiri vyanzo vya maji vya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha tangu mwaka 2013/2014, kumekuwepo na ongezeko kubwa la uzalishaji wa mazao ya bustani. Ongezeko hili limechangiwa na juhudi za Serikali katika kuhamasisha kilimo cha mazao ya bustani kwa kutumia skimu ya umwagiliaji na kuimarike kwa ushiriki wa sekta binafsi na hivyo kutoa ajira kwa wananchi na hasa vijana na akinamama. Hata hivyo, mazao ya bustani yanakabiliwa na changamoto mbalimbali, changamoto hizo ni pamoja na:-

- (a) Upotevu wa mazao tangu yanapovunwa hadi kumfikia mlaji;
- (b) Ubora duni wa mazao;
- (c) Ukosefu wa mikopo kwa wakulima wa mazao ya bustani.
- (d) Upatikanaji wa nishati ya umeme isiyoaminika;

(e) Ukosefu wa usafiri mbadala na vifaa vyatuhifadhi na au vifungashio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilianzishwa ili kuwasaidia wakulima kupata mikopo yenye riba ndogo kwa urahisi ili kuchagiza mapinduzi ya kilimo kutoka kilimo cha kujikimu kuwa kilimo cha biashara na kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuanzishwa kwa Benki hiyo, kilimo cha Tanzania bado kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kiwango kidogo cha uzalishaji, kutokana na ukosefu wa mbinu na teknolojia za kisasa, ukosefu wa mitaji na upatikanaji wa mikopo kwa wakulima, ukosefu wa masoko ya uhakika wa mazao pamoja na kutokuwepo kwa ongezeko la thamani kwa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba, pamoja na sababu nyingine, changamoto za sekta ya kilimo kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo kukosa mtaji wa kutosha kuwezesha benki hiyo kuketeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi pamoja na sababu nyingine migogoro hii huchangiwa kwa kiasi kikubwa na kutotekelizwa ipasavyo mpango wa matumizi bora ya ardhi na hivyo kusababisha mwngiliano wa shughuli za kilimo na ufugaji pamoja na hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na migogoro hiyo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ambazo hazijaweza kumaliza tatizo la migogoro ya wakulima na wafugaji. Aidha, Kamati ina taarifa kuwa Tume iliyoundwa na Serikali kushughulikia migogoro baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi haishirikishi ipasavyo wadau muhimu kama wafugaji. Kamati inashauri Bunge liitaki Serikali kushirikisha ipasavyo makundi yote yanayohusika na migogoro ya ardhi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuongeza kasi ya kutekeleza kwa vitendo mpango wa matumizi Bora ya Ardhi kwa kupima na kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za kilimo, mifugo, uhifadhi na shughuli nyingine. Lakini pia kupata uzoefu wa namna nchi zenye mifugo mingi zilivyoweza kuondokana na migogoro. Nchi hizo ni pamoja na Ethiopia na Sudan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango iliyopo katika kuendeleza mazao ya biashara kwa mfano, korosho, pamba, tumbaku na kahawa. Mazao ya

korosho, pamba, tumbaku na kahawa ni mazao ya biashara ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakichangia fedha nyingi za kigeni kwenye pato la Taifa. Katika miaka ya hivi karibuni mazao haya yamekuwa na uzalishaji usioridhisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufanisi mdogo wa vyama vya ushirika, matumizi duni ya teknolojia na pembejeo, masoko machache ya ndani na utegemezi wa soko la nje, kuendelea kupungua na kukosekana kwa ruzuku ya Serikali na mipango thabiti ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huu Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali kuainisha Mipango na utekelezaji wake ili kuinua uzalishaji wa mazao tajwa kwa lengo la kuongeza mchango wa mazao hayo katika pato la Taifa na uchumi wa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya pembejeo kwa Msimu wa 2016/2017; Ili kuwa na uhakika wa chakula na kilimo cha biashara matumizi ya pembejeo ni muhimu. Kwa kuzingatia umuhimu huu, Kamati ilitaka kupata taarifa kuhusu mpango wa ruzuku ya pembejeo kwa msimu wa 2016/2017 ikiwa ni pamoja na hatua iliyofikiwa ya ulipaji madeni ya Mawakala wa pembejeo kwa msimu wa 2014/15 na 2015/16 kiasi cha sh.64,571,263,837.50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kuwepo kwa taarifa za Mawakala wa pembejeo kuchelewa kulipwa madai yao kiasi cha sh. 64,571,263,837.50 kutokana na kusambaza pembejeo kwa wakulima kwa msimu wa mwaka 2014/2015 na 2015/2016 na hivyo kutishia kutosambaza pembejeo kwa msimu wa 2016/2017. Kamati ilitaka kupata Taarifa ya hatua zilizochukuliwa na Serikali kulipa deni hilo ili deni hilo lisiathiri msimu wa mwaka 2016/2017.

Maelezo ya Serikali yalifafanua kuwa Wizara imeshahakiki na kuandaa kiasi cha sh. 6,322,112,906.30 kama malipo ya awali na kwamba zoezi la uhakiki linaendelea kwa sehemu ya deni iliyosalia. Kufuatia ufanuzi huo, Kamati ilitaka Serikali kuongeza kasi ya uhakiki wa madeni yaliyosalia na kuwalipa Mawakala wa pembejeo stahiki zao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa ruzuku za pembejeo kwa msimu wa mwaka 2016/2017; taarifa ya Wizara ilieleza kuwa Selikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 20 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku za pembejeo za kilimo, kiasi ambacho kingetosheleza kutoa ruzuku kwa kaya 378,900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kwamba kiasi kilichotengwa kwa msimu wa mwaka 2016/2017 ni pungufu ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa

kwa msimu wa mwaka 2014/2015, ambapo idadi ya kaya zilizopata ruzuku ziliwa kaya 999,900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilishangazwa na Serikali kuendelea kupunguza fedha za ruzuku ya pembejeo kinyume na mipango ya Serikali ya kukuza uzalishaji katika kilimo kama njia ya kupata malighafi kwa ajili ya viwanda. Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti itakayotosheleza mahitaji ya ruzuku za pembejeo za kilimo. Aidha, uratibu na usimamizi wa mpango mpya wa utoaji ruzuku ya pembejeo za kilimo uzingatie kuepuka dosari zilizokuwepo katika mfumo wa vocha. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa uzalishaji mbegu nchini; ili kuwa na uhakika wa usalama wa chakula pamoja na mambo mengine, upatikanaji na matumizi ya mbegu bora ni jambo la msingi. Hapa nchini mahitaji halisi ya mbegu bora ni tani 60,000 kwa mwaka. Hata hivyo kiasi kinachopatikana ni tani 36,410 ambapo asilimia 60 ya mbegu hizo zinazalishwa nje ya nchi. Hali hii ya kutegemea mbegu kutoka nje ya nchi inahatarisha usalama wa chakula. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali ilianzisha Wakala wa mbegu za kilimo yaani ASA ili mbegu zinazohitajika na wakulima zizalishwe hapa nchini. Hata hivyo, tangu kuanzishwa kwake mwaka 2006, ASA haijaweza kumudu jukumu hilo kutokana na ufinyu wa bajeti. Aidha, kukosekana kwa mazingira rafiki ya kuvutia wawekezaji katika sekta ya mbegu. Kwa mfano, mbegu zinazozalishwa nchini zimekuwa zikitozwa kodi wakati mbegu zinazoagizwa toka nje ya nchi hazitozwi kodi. Kamati inalitaka Bunge liishauri Serikali kuona mbegu za ndani hazitozwi kodi. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilipokea taarifa kuhusu uratibu wa shughuli za uvuvi nchini. Kamati ilitaka kupata taarifa hii ili kuweza kufahamu mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la Taifa na mipango mikakati iliyopo ya kuwezesha sekta ya uvuvi kuchangia pato la Taifa kwa kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchambua Taarifa hiyo, Kamati ilibaini kuwa Sekta ya Uvuvi haijalinufaisha Taifa kwa kiwango kinachostahili. Aidha, mipango iliyopo imeshindwa kutekelezeka kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa mfano, Kamati za Bunge zinazosimamia sekta ya uvuvi, katika nyakati mbalimbali zimekuwa zikishauri juu ya Serikali kuwekeza katika bandari ya uvuvi kama njia ya kuliwezesha Taifa kunufaika ipasavyo na rasilimali za uvuvi hususani katika bahari kuu. Hata hivyo, utekelezaji wa ushauri huu umekuwa ni wa kusuasua kwa maelezo kwamba fedha zikipatikana bandari ya uvuvi itajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti. mpango mkakati ya Serikali kukabiliana na uvuvi haramu; kutokana na kukithiri kwa vitendo vya uvuvi haramu vinavyotishia ustawi wa sekta ya uvuvi, Kamati ilitaka kufahamu hatua zinazochukuliwa na

Serikali ili kukabiliana na uvuvi haramu na kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kwamba zana za kukabiliana na uvuvi haramu zinagharimu fedha nyngi na kwamba bajeti ndogo inayotengwa katika sekta ya uvuvi inakwamisha utekelezaji wa mipango inayolenga kudhibiti uvuvi haramu. Ili kuwa na matumizi endelevu ya mazao ya uvuvi Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha kugharamia udhibiti wa vitendo vya uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa tafiti kwenye Sekta za Uvvi na Kilimo; maendeleo katika sekta yoyote yanatokana na tafiti ambazo hufanywa katika sekta husika. Kwa kutambua umuhimu wa utafiti kwenye sekta ya kilimo na uvuvi, Kamati ilichambua Miswada ya Sheria ya kuanzishwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Mwaka 2016 na Taasisi ya Utafiti wa Uvvi ya Mwaka 2016 na kuwasilisha taarifa yake Bungeni tarehe 14 Septemba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika ranch za Taifa. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilikutana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvvi na kupokea na kujadili Taarifa kuhusu uendeshaji wa Ranch za Taifa pamoja na kutembelea Ranch ya Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vikao hivyo, Kamati ilibaini kuna uwekezaji mdogo usiowezesha ranch za Taifa kuijendesa kibashara na hivyo kuzifanya kutokuwa na tija. Kwa mfano: katika ranch ya Ruvu, Kamati ilibaini mifugo mingi kufa kutokana na ukame na kukosekana kwa uangalizi stahiki, na ranch zingine kuhodhi maeneo makubwa ambayo hayatumiki ipasavyo na hivyo kupelekea wananchi kuvamia maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na uwekezaji wenye tija kwenye ranch za Taifa, Kamati inaishauri Serikali kufanya uwekezaji wa kisasa katika ranch za Taifa ambao utasaidia wafugaji wengi kujifunza mbinu za ufugaji bora kutoka kwenye ranch za Taifa lakini pia bidhaa zitakazozalishwa kwenye ranch hizo zitauzwa kwa bei nzuri ndani na nje ya nchi na hivyo kuongeza pato la Taifa. Aidha, ni vyema Serikali ikaandaa mkakati wa makusudi wa kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao ya mifugo kwa kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo, ili kuwa na soko la uhakika ndani na nje ya nchi. Ikiwezekana, Serikali iruhusu wafugaji kutumia ranch hizo kwa utaratibu maalum. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi; Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo ilitungwa ili kuwezesha mifugo kuwa na alama, kufahamu idadi ya mifugo, mahali ilipo pamoja na kufahamu wamiliki wa mifugo hiyo. Madhumuni ya utambuzi na usajili wa

mifugo ni kuwezesha udhibiti wa magonjwa, wizi wa mifugo, ustawi wa mifugo na kuhakikisha usalama wa mifugo kwa ajili ya walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti,pamoja na nia nzuri ya Sheria hii, utekelezaji wake katika baadhi ya maeneo umekuwa ukilalamikiwa na hivyo kupelekea wafugaji walio wengi kuukataa. Kufuatia hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sheria hii ili kuweza kubaini maeneo yanayolalamikiwa na kisha kurekebisha kasoro zitakazobainika ili kuwezesha sheria hii kutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya maendeleo ya maji vijijiini. Kamati ilikutana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Umwagiliaji na kupokea taarifa kuhusu programu ya maendeleo ya maji vijijiini ili kufahamu utekelezaji wa malengo yaliyoanishwa katika Sera ya Maji ya mwaka 2002. Aidha, Kamati ilitaka kufahamu Mpango Mkakati uliopo na hatua zinazochukuliwa ili kuongeza kasi ya utoaji huduma ya maji safi na salama vijijiini.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ili kufanikisha azma ya upatikanaji wa maji ya uhakika na salama vijijiini, Serikali imeanzisha mfuko wa maji kwa ajili ya kugharamia miradi hiyo. Kamati inasisitiza fedha zinazokusanywa zitolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa maji ya uhakika, safi na salama mijini.Kamati ilipata nafasi ya kukutana na Mamlaka za Maji za Jiji la Dar es salaam (DAWASCO) na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma (DUWASA) ili kufahamu mikakati ya Serikali katika kuhakikisha maeneo ya mijini nayo yanakuwa na uhakika wa upatikanaji wa maji ya uhakika na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Kamati ilianza na maeneo ya Dar es Salaam na Dodoma kwa kuzingatia kuwa Dar es Salaam ni Jiji Kuu la biashara Tanzania ambalo lina changamoto kubwa ya ongezeko la idadi ya watu. Aidha, Dodoma ilichaguliwa kutohana na uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Tano kuhamia Dodoma uamuzi ambaa utapelekea Mji wa Dodoma kuwa na ongezeko la watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,napenda kuliarifu Bunge lako kuwa kwa upande wa Jiji la Dar es SalaamKamati iliridhishwa na kupongeza mafanikio yaliyopatikana kwa Serikali kukamilisha mradi wa maji kutoka Bagamoyo mpaka Dar es saaam (Ruvu chini). Kamati ina maoni kuwa, katika bajeti ya Mwaka 2017/2018, Serikali itenye fedha kwa ajili ya kuimarishe na kukarabati mitandao ya kusambazia maji, ambayo miundombinu yake imechakaa na haikidihi mahitaji makubwa yaliyoko hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa upande wa Mji wa Dodoma Kamati iliridhishwa na mkakati ulioandaliwa na ambao umeanza kutekelezwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma (*DUWASA*), ambapo wakazi wa mji huu watapata huduma ya maji kutoka chanzo cha maji cha bwawa la Farkwa linalotarajiwa kujengwa Chemba - Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa kutambua mahitaji makubwa ya maji yatakayotokana na Serikali kuhamia Dodoma, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati wa makusudi kuiwezesha kifedha na kitaalam Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma (*DUWASA*) ili iweze kutekeleza jukumu hilo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya mabwawa nchini. Kamati ilipokea taarifa kuhusu uratibu wa miradi ya mabwawa nchini hususan miradi ya mabwawa iliyochukua muda mrefu. Kamati ilitaka kupata taarifa zinazohusu mabwawa kufuatia mabadiliko ya tabianchi yanayopelekea maeneo mengi kuwa kame hivyo kufanya mabwawa hayo kuwa muhimu katika kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, umwagiliaji/ kilimo, uzalishaji umeme na kwa ajili ya mifugo. Kwa ujumla Kamati ilibaini miradi mingi ya mabwawa haijatekelezwa kutoka na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kutokamilika kwa ujenzi wa mabwawa kwa muda uliopangwa kunaisababishia Serikali hasara kutoptaka na miundombinu ya miradi hiyo kuchakaa kabla ya kuanza kutumika, lakini pia kuongezeka kwa gharama za ujenzi tofauti na ilivyokadiriwa na hivyo kuwakosesha wananchi huduma iliyokusudiwa. Kwa msingi huu, Kamati inalishauri Bunge liitake Serikali kuchukua hatua madhubuti za kuwezesha kukamilika kwa miradi ya mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kuinua Sekta ya Kilimo kuitia kilimo cha umwagiliaji. Kamati ilipokea taarifa kuhusu mikakati ya Serikali katika kuinua Sekta ya Kilimo kuitia kilimo cha Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Kamati ilitaka kufahamu mikakati iliyopo ili iweze kuishauri Serikali hatua muafaka za kuchukua na hasa ikizingatiwa kwamba kilimo cha Tanzania kwa kiasi kikubwa hutegemea mvua ambayo inaathiriwa na mabadiliko ya tabia ya nchi na kuathiri uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti,takwimu zinaonesha Tanzania ina eneo lenye ukubwa wahekta 29.4 milionizinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, hata hivyo eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji hadi sasa nihekta 461,326sawa na asilimia 1.6 ya eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa asilimia ndogo ya eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji imetokana na sababu mbalimbali zinazojumuisha ufinyu wa bajeti na mtiririko wa fedha usioridhisha, ushiriki mdogo wa sekta binafsi kwenye kilimo cha umwagiliaji na kutotumika ipasavyo kwa maji ya maziwa kutokana na sura ya nchi inayozunguka maziwa.

Kamati imesikitishwa na taarifa ya Serikali kuwa kati ya hekta 29.4 milioni za eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, ni asilimia 1.6 tu ya eneo hilo ndilo linalotumika kwa sasa.Kamati inaitahadharisha Serikali kuwa sekta ya kilimo haiwezi kuwa na tija kwa kuendelea kutegeMEA misimu ya mvua katika kilimo kutokana na hali halisi ya mabadiliko ya tabianchi ambapo mvua zimekuwa si za uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchambua utekelezaji wa Bajeti za Wizara. Bajeti za Wizara zilizochambuliwa ni Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuuvi na Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Mwenyekiti,sehemu hii inahu su Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha husika pamoja na kuchambua utekelezaji za Wizara kwa mwaka wa fedha unaomalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti,wakati wa uchambuzi wa bajeti, Kamati ilichambua fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, miradi ya maendeleo na makisio ya fedha zitokanazo na ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida Kamati ilibaini kuwa matumizi mengi yasiyo ya lazima hayakutengewa fedha na hivyo kusaidia Serikali kuelekeza fedha hizo kwenye miradi ya maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii kwani kwa kutenga fedha za ndani kunadhihirisha utayari wa Serikali katika kujitegemea na kuwa letea wananchi wake maendeleo ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa upande wa miradi ya maendeleoKamati ilibaini kwamba kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Serikali imetenga kiasi kikubwa cha fedha za ndani ukilinganisha na fedha za nje, lakini fedha hizo zimekuwa hazitolewi kama zilivoidhinishwa na Bunge na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa. Hili siyo jambo dogo katika utekelezaji wa Mipango ya Serikali, linahitaji ufumbuzi la sivyo Bajeti ya Serikali katika miradi ya maendeleo itaendelea kuwa kiinimacho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati. Baada ya kueleza shughuli zilizotekelawa na Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja, naomba kutoa maoni na mapendekezo Kumi na Moja (11) ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kutotolewa kwa wakati:-

KWA KUWA, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba upo udhaifu mkubwa katika kutoa fedha za maendeleo zinazotengwa na Serikali na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Sekta za, Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji na Umwagiliaji;

NA KWA KUWA udhaifu huu umekuwa ukiathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi hiyo na kuifanya Serikali na wananchi kwa ujumla kutokopata matokeo yaliyotarajiwa.

KWA HIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba; Serikali itoe fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuwa na uhakika wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa kutekelezwa. Pendelezo hili likitekelezwa litasaidia kuondokana na kero za muda mrefu za ukosefu wa huduma ya maji ambayo ni huduma muhimu katika ustawi wa binadamu, wanyama, mazingira na uzalishaji mali, kupungua kwa migogoro ya wakulima na wafugaji na kuondokana na tatizo la uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili ni; mabadiliko ya tabia nchi na athari zake kwenye Sekta ya Kilimo:-

KWA KUWA, kilimo cha Tanzania hutegemea mvua za msimu;

NA KWA KUWA, mvua hizi zimeathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi hivyo kuathiri shughuli za uzalishaji, ni dhahiri kuwa, kilimo cha umwagiliaji ni moja ya njia muhimu ya kuongeza na kuimarisha uzalishaji wenye tija;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kwamba; Serikali ihuishe katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/2018, mpango utakaobainisha namna nchi itakavyotumia rasilimali maji zilizopo kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tatu ni; Umuhimu wa mnyororo wa thamani kwenye mazao:-

KWA KUWA, mazao mengi ya wakulima yamekuwa yakipotea kabla ya kufika kwa mlaji kutohana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa soko la uhakika na teknolojia bora ya uhifadhi;

NA KWA KUWA kupotea kwa mazao hayo kumekuwa kukisababisha hasara kwa wakulima na kuwafanya kutonufaika kikamilifu na kazi zao;

KWA HIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba; Serikali katika Mpango wa Maendelo wa Taifa wa Mwaka 2017/2018 iwasilishe mikakati ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao ya kilimo na itekeleze kikamilifu mipango hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba nne ni; mazao yatokanayo na kilimo na umuhimu wake kwenye Uchumi wa Viwanda:-

KWA KUWA, Serikali ya Awamu ya Tano inasisitiza umuhimu wa uchumi wa kujitegemea kupitia Sekta ya Viwanda;

NA KWA KUWA, ili kufikia malengo hayo, Serikali haina budi kuimarisha Sekta ya Kilimo ambayo sio tu itatoa malighafi kwa ajili ya viwanda lakini pia itawezesha Taifa kuwa na utoshelezi wa chakula...

**MWENYEKITI:** Bado sekunde 20.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mapendekezo hayo niliyoyatoa, hitimisho, shukurani.

**MWENYEKITI:** Wewe malizia tu! Toa hoja uende!

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyoitoa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, toa hoja tu uende!

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge waweze kuipokea taarifa hii, na kuijadili na kuipokea. Ahsante sana. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja!

**MWENYEKITI:** Ameshatoa.

## **TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KWA MWAKA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

[Inatolewa chini ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za  
Kudumu za Bune, Toleo la Januari, 2016] –

### **SEHEMU YA KWANZA**

#### **1.0. MAELEZO YA JUMLA**

##### **1.1. Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15), Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017, ili iweze kujadiliwa na kuungwa mkono na Bunge lako Tukufu.

##### **1.2. Majukumu**

**Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji yameainishwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Nyongeza ya Nane kifungu cha 7, Toleo la Januari, 2016 kuwa ni kusimamia shughuli za Wizara za Maji na Maendeleo ya Umwagiliaji pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi. Aidha, kifungu cha 7(1) kinafafanua majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge za Sekta, ambapo Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ni moja kati ya Kamati hizo na ina majukumu yafuatayo:-

###### **1.2.1. Kushughulikia bajeti za Wizara.**

Bajeti za Wizara zilizojadiliwa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ni Maji na Maendeleo ya Umwagiliaji na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi;

###### **1.2.2. Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba.**

Mikataba iliyojadiliwa na Kamati ni ile inayohitaji kuridhiwa na Bunge kwa mujibu wa Katiba;

1.2.3. Kushughulikia taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

1.2.4. Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

### **1.3. Njia/Mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitumia mbinu mbalimbali zilizosaidia kazi Kamati kufanyika kwa ufanisi. Mbinu hizo ni pamoja na:-

- 1.3.1. Kufanya vikao vya kupitia, kujadili na kuchambua TRaarifa mbalimbali kuhusu utendaji katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na maji;
- 1.3.2. Kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kujiridhisha na thamani ya fedha (value for money) ziligharamia miradi hiyo;
- 1.3.3. Kukutana na wadau na kupokea maoni yaliyotumika kuboresha Miswada ya Taasisi za Utafiti za Kilimo na Uvuvu; na
- 1.3.4. Kufanya mapitio ya machapisho mbalimbali kuhusu dhana ya uanzishaji wa Taasisi za Utafiti katika Sekta za Kilimo na Uvuvu kisheria ili kufanya ulinganisho na uzoefu wa nchi zingine katika masuala hayo.

### **1.4. Shughuli zilizotekelzwa**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Januari 2016 hadi Januari 2017, Kamati imeweza kutekeleza shughuli mbalimbali zifuatazo:-

- 1.4.1. Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati;
- 1.4.2. Mafunzo kuhusu Uendeshaji wa shughuli za Kamati.
  - a) Bunge na Kamati zinavyofanya kazi na muundo na majukumu ya Kamati za Bunge;
  - b) Muundo na Majukumu ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvu na Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na Sera na Sheria zinazotumika kushughulikia maswala yote yanayohusu Kilimo, Mifugo na Uvuvu;

- c) Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa miswada na uchambuzi wa bajeti;
- 1.4.3. Kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2015/2016;
- 1.4.4. Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016;
- 1.4.5. Kuchambua Miswada ya Sheria Mbalimbali.
  - a) Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ya Mwaka, 2016 (*The Tanzania Fisheries Research Institute Bill, 2016*); na
  - b) Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Mwaka, 2016 (*The Tanzania Agricultural Research Institute Bill, 2016*)
- 1.4.6. Kushughulikia Taarifa za Utendaji za Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2015/2016;
- 1.4.7. Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara za Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Umwagiliaji kwa mwaka 2015/2016;
- 1.4.8. Kukagua Utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016; na
- 1.4.9. Kufanya ziara kwenye baadhi ya maeneo kame nchini kwa lengo la kubaini athari za ukame katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi ili kuweza kuishauri Serikali hatua madhubuti za kuchukua.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0. UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU

#### 2.1. Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Taarifa inahusu uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Uchambuzi huu utahusu masuala kumi na nane (18) amabayo yalitokana na Kamati kutekeleza majukumu ya msingi yaliyoanishwa Kikanuni kupitia vikao, ziara na ufuatiliaji utendaji wa Wizara na Taasisi inazozisimamia kisha kutoa maoni, ushauri na mapendekezo.

**Mheshimiwa Spika**, ufuatao ni uchambuzi washughuli zilizotekelezwa na Kamati tangu kuundwa kwake.

### **2.1.1. Taarifa za Serikali kuhusu hali ya hewa na ukame nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Serikali kuhusu hali ya hewa na ukame nchini. Kutohama na Taarifa hiyo, ilionekana hatari ya kujitokeza kwa upungufu wa chakula nchini. Hata hivyo, Taarifa za Serikali zilibainisha kuwa Taifa lina utoshelezi wa chakula kwa kiwango cha ziada kwa **asilimia 123** katika msimu wa mwaka 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, hali halisi kutoka Majimboni inaonyesha kuna upungufu wa chakula katika Halmashauri 55, bei ya chakula nchini imeendelea kupanda kutohama na athari za ukame zilizopelekea uzalishaji kidogo hivyo kusababisha upungufu wa mazao sokoni.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia hali ya ukame, upungufu wa chakula na kuendelea kupanda kwa bei za mazao, Kamati inalishauri Bunge liitaki Serikali kuchukua hatua za dharura zifuatazo:-

- (a) Sehemu ya akiba ya chakula kilichohifadhiwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NRFA) kitolewe na kuuzwa kwa bei elekezi iliyowekwa na Serikali katika Halimashauri 55 zilizobainika kuwa na upungufu mkubwa wa chakula;
- (b) Serikali ihakikishe kuwa, mbegu bora zinazostahimili ukame na zenyet kukomaa kwa muda mfupi zinapatikana na kuwafikia wakulima mapema kabla ya mvua za msimu wa mwezi Machi;
- (c) Serikali iongeze kasi ya kuhamasisha, kuratibu na kusimamia Wakulima kulima mazao ya muda mfupi na yanayostahimili ukame;
- (d) Serikali iratibu na kusimamia ipasavyo udhibiti wa usafirishaji wa mazao ya chakula nje ya nchi, na
- (e) Wananchi wahimizwe kuweka akiba ya chakula cha kutosha hasa kwenye maeneo yaliyopata mvua chini ya wastani.

### **2.1.2. Ziara ya ukaguzi kwenye baadhi ya maeneo kame nchini**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Taarifa ya Serikali kuhusu hali ya ukame na athari zake na hatua ambazo Serikali imekuwa ikichukua, Kamati ilifanya ziara katika baadhi ya maeneo kame (Case Study) katika Wilaya za Kiteto na Simanjiro mkoani Manyara kwa lengo la kubaini hali halisi ili iweze kuishauri vema Serikali kuhusiana na matokeo ya ziara.

**Mheshimiwa Spika**, shabaha kubwa ya ziara hiyo ilikuwa ni kutambua athari za ukame, upatikanaji chakula, hali ya mifugo na maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa ukosefu wa mvua umeleta madhara yafuatayo nchini:-

- (a) Uhaba mkubwa wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo hali iliyosababisha wafugaji kuhama kwa ajili ya kutafuta maeneo yenye maji na malisho. Kamati inatahadharisha kuwa mwenendo huu unaweza kupelekea kuongezeka kwa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi endapo hatua sahiki hazitachukuliwa;
- (b) Kukauka kwa visima na mabwawa. Kwa mfano katika Wilaya ya Simanjiro visima virefu 32 kati ya 92 havitoi maji na visima vifupi 33 kati ya 51 havitoi maji. Aidha, mabwawa makubwa 6 kati ya 15 yamekauka na mabwawa madogo 25 yamekauka kabisa na kupelekea mifugo na binadamu kukosa uhakika wa maji safi na salama na hivyo kuweza kusababisha milipuko ya magonjwa;
- (c) Upungufu wa uzalishaji wa mazao mbalimbali, hali iliyopelekea usalama wa chakula kutoridhisha. Aidha, hali hiyo imesababisha kupanda kwa bei za mazao kwa kiasi ambacho wananchi wanashindwa kumudu ongezeko la bei na kusababisha hali ngumu ya maisha;
- (d) Mabadiliko ya tabianchi na shughuli za binadamu kwa kiasi kikubwa vimeathiri vyanzo vya maji vya asili. Ili kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali maji, Kamati inashauri Serikali iongoze kasi ya usimamizi na udhibiti wa shughuli za binadamu kwenye vyanzo vya maji;
- (e) Kutokana na visima vingi kukosa maji na mabwawa kukauka, Kamati inaishauri Serikali kuwa na Mpango Mkakati wa makusudi kwa ajili ya kuchimba mabwawa makubwa katika kila Kata ili kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi mbalimbali;

- (f) Ili kukabiliana na upungufu wa chakula, Kamati inashauri Serikali za Mikoa na Halmashauri zisimamie na kimarisha mifumo ya kuhifadhi
- (g) chakula baada ya mavuno ili kupunguza upotevu wa chakula na kuhakikisha upatikanaji wa chakula wakati wote.

#### **2.1.3. Mkakati wa kuongeza Mnyororo wa Thamani katika mazao ya bustani**

**Mheshimiwa Spika**, takwimuzinaonyesha tangu mwaka 2013/2014 kumekuwepo na ongezeko kubwa la uzalishaji wa mazao ya bustani ambayo ni mboga na matunda, ongezeko lilidochangiwa na juhudzi za Serikali katika kuhamasisha kilimo cha mazao ya bustani kwa kutumia skimu za umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile kuimarika kwa ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ndogo ya mazao ya bustani kumesaidia kuongezeka kwa mazao ya bustani na hivyo kutoa ajira kwa wananchi na hasa vijana na kinamama. Hata hivyo, mazao ya bustani yanakabiliwa na changamoto mbalimbali, Changamoto hizo ni pamoja na:-

- (a) Upotevu wa mazao tangu yanapovunwa hadi kumfikia mlaji;
- (b) Ubora duni wa mazao;
- (c) Ukosefu wa mikopo kwa wakulima wa mazao ya bustani, mikopo ambayo ingeweza wakulima hao kuwekeza katika teknolojia zinazotumika baada ya kuvuna;
- (d) Upatikanaji wa nishati ya umeme isiyominika;
- (e) Ukosefu wa usafiri mbadala na
- (f) Vifaa vya kuhifadhi na au vifungashio.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto hizo kuongezeka kwa mahitaji ya matunda na mboga kunatoa fursa ya upatikanaji wa soko kwa wakulima wadogo na wauzaji. Hivyo ni jukumu la Serikali kuwaelimisha wakulima na kuhakikisha inaweka mazingira ya kilimo kuwa cha kibiashara kwa kutunga sera, sheria, kanuni na miundombini bora.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini mfumo huu ukitekelezwa kwa ufasaha utawawezesha wakulima wa kati kutokulabali kuuza mazao yao yakiwa shambani au yakiwa kama malighafi na hivyo kunufaika kwa kuwa na soko la uhakika.

#### **2.1.4. Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilianzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa madhumuni ya kusaidia upatikanaji utoshelezi na usalama wa chakula pamoja na kuchagiza mapinduzi ya kilimo kutoka kilimo cha kujikimu kuwa kilimo cha biashara ili kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali ili kuchagiza sekta ya kilimo, kilimo cha Tanzania bado kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kiwango kidogo cha uzalishaji, kutokana na ukosefu wa mbinu na teknolojia za kisasa, ukosefu wa mitaji na upatikanaji wa mikopo kwa wakulima, ukosefu wa masoko ya uhakika wa mazao pamoja na kutokuwepo kwa ongezeko la thamani kwa mazao ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, pamoja na sababu nyingine, changamoto za sekta ya kilimo kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo kukosa mtaji wa kutosha kuwezesha benki hiyo kuketeleza majukumu yake. Hivyo, Serikali itekeleze kusudio lake la kutoa mtaji kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili benki hiyo iweze kutoa mikopo mingi zaidi kwa wakulima.

#### **2.1.5. Migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya Wakulima, Wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.**

**Mheshimiwa Spika**, migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya Wakulima, Wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi pamoja na sababu nyingine migogoro hii huchangiwa kwa kiasi kikubwa na kutotekelezwa ipasavyo mpango wa matumizi bora ya ardhi na hivyo kusababisha muingiliano wa shughuli za kilimo na ufugaji.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na migogoro hiyo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa pamoja na hatua zinazoendelea kuchukuliwa, migogoro baina ya wakulima na wafugaji imeendelea kuongezeka na kusababisha uvunjifu wa amani, vifo na uharibifu wa mazingira. Aidha, Kamati ina taarifa kuwa Tume iliyoundwa na Serikali kushughulikia migogoro baina ya Wakulima, Wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi haishirikishi ipasavyo wadau muhimu kama Wafugaji. Kamati inalishauri Bunge liitake Serikali kushirikisha ipasavyo makundi yote yanayohusika na migogoro ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Bunge kuitaka Serikali kushirikisha ipasavyo makundi yote yanayohusika na migogoro ya ardhi, Kamati pia inashauri Serikali kuongeza kasi ya kutekeleza kwa vitendo Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi kwa kupima na kutenga maeneo kwa ajili ya

shughuli za kilimo, mifugo, uhifadhi na shughuli nyingine. Lakini pia kupata uzoefu wa namna nchi zenyet mifugo mingi zilivyoweza kuondokana na migogoro. Nchi hizo ni pamoja na **Ethiopia** ambayo takwimu zinaonyesha kuwa ina ng'ombe **million 55, Sudan** yenye ng'ombe **million 32** na hakuna migogoro ikilinganishwa na **Tanzania** ambayo ina ng'ombe **million 25.8.**

#### **2.1.6. Mipango iliyopo katika kuendeleza mazao ya biashara (Korosho Pamba,Tumbaku na Kahawa)**

**Mheshimiwa Spika**, mazao ya Korosho, Pamba, Tumbaku na Kahawa ni mazao ya biashara ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakichangia fedha nyingi za kigeni kwenye pato la Taifa. Katika miaka ya hivi karibuni mazao haya yamekuwa na uzalishaji usioridhisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufanisi mdogo wa vyama vya ushirika, matumizi duni ya teknologia na pembejeo, masoko machache ya ndani na utegemezi wa soko la nje, kuendelea kupungua / na kukosekana kwa ruzuku ya Serikali na mipango thabiti ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao hayo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huu Kamati inaliomba Bunge liitaka Serikali kuainisha Mipango na utekelezaji wake ili kuinua uzalishaji wa mazao tajwa kwa lengo la kuongeza mchango wa mazao hayo katika pato la Taifa na uchumi wa mtu mmoja mmoja.

#### **2.1.7. Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Pembejeo kwa Msimu wa 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuwa na uhakika wa chakula na kilimo cha biashara matumizi ya pembejeo ni muhimu. Kwa kuzingatia umuhimu huu, Kamati ilitaka kupata Taarifa kuhusu Mpango wa Ruzuku ya Pembejeo kwa msimu wa 2016/2017 ikiwa ni pamoja na hatua iliyofikiwa ya ulipaji madeni ya Mawakala wa Pembejeo kwa msimu wa 2014/15 na 2015/16 kiasi cha shillingi **64,571,263,837.50.**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia kuwepo kwa taarifa za Mawakala wa Pembejeo kuchelewa kulipwa madai yao kiasi cha shillingi **64,571,263,837.50** kutokana na kusambaza pembejeo kwa wakulima kwa msimu wa 2014/15 na 2015/16 na hivyo kutishia kutosambaza pembejeo kwa msimu wa 2016/17. Kamati ilitaka kupata Taarifa ya hatua zilizochukuliwa na Serikali kulipa deni hilo ili deni hilo lisiasili msimu wa mwaka 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, maeleo ya Serikali yalifafanua kuwa Wizara imeshahakiki na kuandaa kiasi cha shillingi. **6,322,112,906.30** kama malipo

ya awali na kwamba zoezi la uhakiki linaendelea kwa sehemu ya deni iliyosalia kufuatia ufanuzi huo, Kamati iliitaka Serikali kuongeza kasi ya uhakiki wa madeni yaliyosalia na kuwalipa Mawakala wa Pembejeo stahiki zao.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu mpango wa ruzuku za pembejeo kwa msimu wa mwaka 2016/2017, Taarifa ya Wizara ilieleza kuwa Selikali imetenga kiasi cha shilingi **bilioni20** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku za pembejeo za kilimo, kiasi ambacho kingetosheleza kutoa ruzuku kwa kaya **378,900**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kwamba kiasi kilichotengwa kwa msimu wa mwaka 2016/2017 ni pungufu ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa kwa msimu wa 2014/2015, ambapo idadi ya kaya zilizopata ruzuku zilikuwa kaya **999,900**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishangazwa na Serikali kuendelea kupunguza fedha za ruzuku ya pembejeo kinyume na mipango ya Serikali ya kukuza uzalishaji katika kilimo kama njia ya kupata malighafi kwa ajili ya viwanda. Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti itakayotosheleza mahitaji ya ruzuku za pembejeo za kilimo. Aidha, uratibu na usimamizi wa mpango mpya wa utoaji ruzuku ya pembejeo za kilimo uzingatie kuepuka dosari zilizokuwepo katika mfumo wa vocha.

#### 2.1.8. Umuhimu wa uzalishaji mbegu nchini

**Mheshimiwa Spika**, ili kuwa na uhakika wa usalama wa chakula pamoja na mambo mengine, upatikanaji na matumizi ya mbegu bora ni jambo la msingi. Hapa nchini mahitaji halisi ya mbegu bora ni tani **60,000** kwa mwaka, hata hivyo kiasi kinachopatikana ni tani **36,410** ambapo **asilimia 60%** ya mbegu hizo zinazalishwa nje ya nchi. Hali hii ya kutegemea mbegu kutoka nje ya nchi inahatarisha usalama wa chakula.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kukabiliana Na changamoto hiyo, Serikali ilianzisha Wakala wa Mbegu za Kilimo (Agricultural Seed Agency- ASA) ili mbegu zinazohitajika na wakulima zizalishwe hapa nchini. Hata hivyo, tangu kuanzishwa kwake mwaka 2006, ASA haijaweza kumudu jukumu hilo kutokana na ufinyu wa bajeti. Aidha, kukosekana kwa mazingira rafiki ya kuvutia wawekezaji katika sekta ya mbegu. Kwa mfano mbegu zinazozalishwa nchini zimekuwa zikitozwa kodi wakati mbegu zinazoagizwa toka nje ya nchi hazitozwi kodi.

#### 2.1.9. Mipango Mikakati ya Serikali kuinua Sekta ya Uvuvi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi ili kupokea Taarifa kuhusu uratibu wa shughuli za uvuvi nchini. Kamati ilitaka kupata taarifa ili kuweza kufamu mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la Taifa na mipango mikakati iliyopo ya kuwezesha sekta ya uvuvi kuchangia pato la Taifa kwa kiwango kinacho staili pamoja na kuinua kipato cha wavuvi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuchambua Taarifa hiyo, Kamati ilibaini kuwa Sekta ya Uvuvi haijalinufaisha Taifa kwa kiwango kinachostahili. Aidha, mipango iliyopo imeshindwa kutekelezeka kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa mfano Kamati za Bunge zinazosimamia sekta ya uvuvi, katika nyakati mbalimbali zimekuwa zikishauri juu ya Serikali kuwekeza katiika bandari ya uvuvi kama njia ya kuliwezesha Taifa kunufaika ipasavyo na rasilimali za uvuvi hususan katika bahari kuu, hata hivyo utekelezaji wa ushauri huu umekuwa ni wa kusuasua kwa maelezo kwamba fedha zikipatika bandari ya uvuvi itajengwa.

#### **2.1.10. Mipango Mikakati ya Serikali kukabiliana na uvuvi haramu**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na kukithiri kwa vitendo vya uvuvi haramu vinavyotishia ustawi wa sekta ya uvuvi, Kamati ilitaka kufamu hatua zinazochukuliwa na Serikali ili kukabiliana na uvuvi haramu na kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kwamba zana za kukabiliana na uvuvi haramu zinagharimu fedha nyingi, na kwamba bajeti ndogo inayotengwa katika sekta ya uvuvi inakwamisha utekelezaji wa mipango inayolenga kudhibiti uvuvi haramu. Ili kuwa na matumizi endelevu ya mazao ya uvuvi Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha kugharamia udhibiti wa vitendo vya uvuvi haramu.

#### **2.1.11. Umuhimu wa Tafiti kwenye Sekta za Uvuvi na Kilimo**

**Mheshimiwa Spika**, maendeleo katika sekta yoyote yanatokana na tafiti ambazo hufanywa katika sekta husika. Kwa kutambua umuhimu wa utafiti kwenye sekta ya kilimo na uvuvi, Kamati ilichambua Miswada ya Sheria ya kuanzishwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Mwaka 2016, na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ya Mwaka 2016 na kuwasilisha taarifa yake Bungeni tarehe 14 Septemba, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa hiyo ya Kamati miiongoni mwa mambo muhimu ambayo Kamati ilibaini ni ushiriki mdogo wa wadau wakati wa utungaji sheria kutokana na utaratibu wa wadau kutakiwa kujigharamia wenyewe gharama za usafiri na malazi wakati wa kutoa maoni. Hali hii

imekuwa ikizikoseshaa Kamati za Bunge kupata maoni muhimu kutoka kwa wadau ambao kimsingi ndio watekelezaji wa sheria na hivyo kupelekea wakati mwingine Bunge kutunga sheria mbaya au isiyotekelozeka.

#### **2.1.12. Uwekezaji katika Ranchi za Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilikutana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvubi na kupokea na kujadili Taarifa kuhusu uendeshaji wa Ranchi za Taifa pamoja na kutembelea Ranchi ya Ruvu.

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao hivyo, Kamati ilibaini kuna uwekezaji mdogo usiowezesha Ranchi za Taifa kuijendesha kibiashara na hivyo kuzifanya kutokuwa na tija. Kwa mfano: katika Ranchi ya Ruvu, Kamati ilibaini mifugo mingi kufa kutokana na ukame na kukosekana kwa uangalizi stahiki, na Ranchi zingine kuhodhi maeneo makubwa ambayo hayatumiki ipasavyo na hivyo kupelekea wananchi kuvamia maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuwa na uwekezaji wenye tija kwenye Ranchi za Taifa, Kamati inaishauri Serikali kufanya uwekezaji wa kisasa katika Ranchi za Taifa ambao utasaidia wafugaji wengi kujifunza mbinu za ufugaji bora kutoka kwenye Ranchi za Taifa lakini pia bidhaa zitakazozalishwa kwenye ranchi hizi zitauzwa kwa bei nzuri ndani na nje ya nchi na hivyo kuongeza pato la Taifa. Aidha, ni vyema Serikali ikaandaa mkakati wa makusudi wa kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao ya mifugo kwa kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo, ili kuwa na soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

#### **2.1.13. Malalamiko kuhusu Utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo. (Sheria Namba 12 ya Mwaka 2010)**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo ilitungwa ili kuwezesha mifugo kuwa na alama, kufahamu idadi ya mifugo, mahali ilipo pamoja na kufahamu wamiliki wa mifugo hiyo. Madhumuni ya utambuzi na usajili wa mifugo ni kuwezesha udhibiti wa magonjwa, wizi wa mifugo, ustawi wa mifugo na kuhakikisha usalama wa mifugo kwa ajili ya walaji.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia nzuri ya sheria hii, utekelezaji wake katika baadhi ya maeneo umekuwa ukilalamikiwa na hivyo kupelekea wafugaji walio wengi kuukataa. Kufuatia hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathimini ya utekelezaji wa Sheria hii ili kuweza kubaini maeneo

yanayolalamikiwa na kisha kurekebisha kasoro zitakazobainika ili kuwezesha sheria hii kutekelezwa ipasavyo.

#### **2.1.14. Program ya Maendeleo ya Maji Vijijini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Umwagiliaji na kupokea Taarifa kuhusu Programu ya Maendeleo ya Maji vijijini ili kufahamu utekelezaji wa malengo yaliyoanishwa katika Sera ya Maji ya mwaka 2002. Aidha, Kamati ilitaka kufahamu Mpango Mkakati uliopo na hatua zinazochukuliwa ili kuongeza kasi ya utoaji huduma ya maji safi na salama vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kufanikisha adhma ya upatikanaji wa maji ya uhakika na salama vijijini, Serikali imeanzisha Mfuko wa Maji kwa ajili ya kugharamia miradi hiyo. Kamati inasisitiza fedha zinazokusanywa zitolewe kwa wakati.

#### **2.1.15. Upatikanaji wa maji ya uhakika, safi na salama mijini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata nafasi ya kukutana na Mamlaka za Maji za Jiji la Dar es salaam (DAWASCO) na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma (DUWASA) ili kufahamu mikakati ya Serikali katika kuhakikisha maeneo ya mijini nayo yanakuwa na uhakika wa upatikanaji wa maji ya uhakika na salama.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilianza na maeneo ya Dar es salaam na Dodoma kwa kuzingatia kuwa Dar es salaam ni jiji kuu la biashara Tanzania ambalo lina changamoto kubwa ya ongezeko la idadi ya watu. Aidha, Dodoma ilichaguliwa kutokana na uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Tano kuhamia Dodoma uamuzi ambao utapelekea mji wa Dodoma kuwa na ongezeko la watu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa kwa upande wa jiji la Dar es salaam Kamati iliridhishwa na kupongeza mafanikio yaliyopatikana kwa Serikali kukamilisha mradi wa maji kutoka Bagamoyo mpaka Dar es salaam (Ruvu chini) - Dar es salaam Water Supply and Sanitation Project. Hata hivyo, Kamati ina maoni kuwa, katika bajeti ya Mwaka 2017/2018, Serikali itenye fedha kwa ajili ya kuimarisha na kukarabati mitandao ya kusambazia maji, ambayo miundombinu yake imechakaa na haikidhi mahitaji makubwa yaliyoko hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mji wa Dodoma Kamati iliridhishwa na mkakati ulioandaliwa na ambao umeanza kutekelezwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma (DUWASA), ambapo wakazi wa mji huu watapata huduma ya maji kutoka chanzo cha maji cha Bwawa la Farkwa linalotarajiwa kujengwa Chemba - Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua mahitaji makubwa ya maji yatakayotokana na Serikali kuhamia Dodoma, Kamati inaishauri Serikali kuwa na Mkakati wa makusudi kuiwezesha kifedha na kitaalamu Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma (DUWASA)ili iweze kutekeleza jukumu hilo kwa wakati.

#### 2.1.16. Uratibu wa Miradi ya Mabwawa Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Umwagiliaji na kupokea Taarifa kuhusu uratibu wa miradi ya mabwawa nchini hususan miradi ya mabwawa iliyochukua muda mrefu. Aidha, kufahamu mipango iliyopo katika kuongeza kasi ya utekelezaji miradi hiyo. Kamati ilitaka kupata Taarifa zinazohusu mabwawa kufuatia mabadiliko ya tabia nchi yanayopelekea maeneo mengi kuwa kame hivyo kufanya mabwawa hayo kuwa muhimu katika kuhakikisha upatikanaji maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, umwagiliaji/ kilimo, uzalishaji umeme na kwa ajili ya mifugo. Kwa ujumla Kamati ilibaini miradi mingi ya mabwawa haijatekelezwa kutoka na ukosefu wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kutokamilika kwa ujenzi wa mabwawa kwa muda uliopangwa kunaisababishia Serikali hasara kutokana na miundombinu ya miradi hiyo kuchakaa kabla ya kuanza kutumika, lakini pia kuongezeka kwa gharama za ujenzi tofauti na ilivyo kadiriwa na hivyo kuwakosesha wananchi huduma iliyokusudiwa. Kwa msingi huu, Kamati inalishauri Bunge liitake Serikali kuchukua hatua madhubuti za kuwezesha kukamilika kwa miradi ya mabwawa.

#### 2.1.17. Mikakati ya kuinua Sekta ya Kilimo kupitia kilimo cha umwagiliaji

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Umwagiliaji na kupokea Taarifa kuhusu Mikakati ya Serikali katika kuinua Sekta ya Kilimo kupitia kilimo cha Umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kufahamu mikakati iliyopo ili iweze kuishauri Serikali hatua muafaka za kuchukua na hasa ikizingatiwa kwamba kilimo cha Tanzania kwa kiasi kikubwa hutegemea mvua ambayo inaathiriwa na mabadiliko ya tabia ya nchi na kuathiri uzalishaji

wa mazao mbalimbali. Kwa muktadha huu, kilimo cha umwagiliaji ni moja ya njia muhimu za kuongeza tija katika uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonyesha Tanzania ina eneo lenye ukubwa wa **hekta 29.4 milioni** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, hata hivyo eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji hadi sasa ni **hekta 461,326** sawa na **asilimia 1.6** ya eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa asilimia ndogo ya eneo linalotumika kwa kilimo cha umwagiliaji imetokana na sababu mbalimbali zinazojumuisha ufinyu wa bajeti na mtiririko wa fedha usioridhisha, ushiriki mdogo wa sekta binafsi kwenye kilimo cha umwagiliaji na kutotumika ipasavyo kwa maji ya maziwa kutokana na sura ya nchi inayozunguka maziwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeskitishwa na Taarifa ya Serikali kuwa kati ya hekta **29.4 milioni** za eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, ni **asilimia 1.6** tu ya eneo hilo ndilo linalotumika kwa sasa. Kamati inaitaadharisha Serikali kuwa sekta ya kilimo haiwezi kuwa na tija kwa kuendelea kutegemea misimu ya mvua katika kilimo kutokana na hali halisi ya mabadiliko ya tabia nchi ambapo mvua zimekuwa si za uhakika.

#### **2.1.18. Kuchambua Utekelezaji wa Bajeti za Wizara.**

Bajeti za Wizara zilizochambuliwa ni Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maendeleo ya Uvuuvi na Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inahusu Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti iliyoindhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha husika pamoja na kuchambua utekelezaji za Wizara kwa Mwaka wa Fedha unaomalizika.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa bajeti, Kamati ilichambua fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, miradi ya maendeleo na makisio ya fedha zitokanazo na ukusanyaji wa maduhuli.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida Kamati ilibaini kuwa matumizi mengi yasiyo ya lazima hayakutengewa fedha na hivyo kusaidia Serikali kuelekeza fedha hizo kwenye miradi ya maendeleo. Kamati inapongeza Serikali kwa hatua hii kwanikwa

kutenga fedha za ndani kunadhihirisha utayari wa Serikali katika kujitegemea na kuwaletea wananchi wake maendeleo ya kweli.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa miradi ya maendeleo Kamati ilibaini kwamba kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Serikali imetenga kiasi kikubwa cha fedha za ndani ukilinganisha na fedha za nje, lakini fedha hizo zimekuwa hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na Bunge na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa. Hili siyo jambo dogo katika utekelezaji wa Mipango ya Serikali, linahitaji ufumbuzi la sivyo Bajeti ya Serikali katika miradi ya maendeleo itaendelea kuwa kiinimacho.

**Jedwali:** Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za ndani za miradi ya maendeleo kwa kipindi cha nusu mwaka (2016/2017) katika Sekta Kilimo, Mifugo, Maji na Umwagiliaji

FUNGU NAMBA	FEDHA ZILIZOIDHINISHWA	FEDHA ZILIZOTOLEWA	ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA
<b>FUNGU 43 (KILIMO)</b>	22,000,000,000	0	0%
<b>FUNGU 24 (TUME YA USHIRIKA)</b>	0	0	0%
<b>FUNGU 99 (MIFUGO NA UVUVI)</b>	8,000,000,000	280,000,000	4%
<b>FUNGU 49 (MAJI)</b>	690,155,000,000	134,695,298,877	20%
<b>FUNGU 5 (TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI)</b>	6,000,000,000	767,480,000	13%

Chanzo: Taarifa za Wizara katika Vikao vya Kamati.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0. MAONI NA MAPENDEKEZO

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelawa na Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja, naomba kutoa maoni na mapendekezo Kumi na Moja (11) ya Kamati kama ifuatavyo:-

### **3.1. Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kutotolewa kwa wakati**

**KWA KUWA**, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba upo udhaifu mkubwa katika kutoa fedha za maendeleo zinazotengwa na Serikali na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za, Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Maji na Umwagiliaji **NA KWA KUWA** udhaifu huu umekuwa ukiathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi hiyo na kuifanya Serikali na wananchi kwa ujumla kutokupata matokeo yaliyotarajiwa, **KWA HIYOBASI**, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba; Serikali itoe fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuwa na uhakika wa utekelezaji wa miradi iliyopangwa kutekelezwa. Pendekezo hili likitekelezwa litasaidia kuondokana na kero za muda mrefu za ukosefu wa huduma ya maji ambayo ni huduma muhimu katika ustawi wa binadamu, wanyama, mazingira na uzalishaji mali, kupungua kwa migogoro ya wakulima na wafugaji na kuondokana na tatizo la uvuvi haramu.

### **3.2. Mabadiliko ya Tabianchi na Athari zake kwenye Sekta ya Kilimo**

**KWA KUWA** kilimo cha Tanzania hutegemea mvua za msimu **NA KWA KUWA**, mvua hizi zimeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi hivyo kuathiri shughuli za uzalishaji, ni dhahiri kuwa, kilimo cha umwagiliaji ni moja ya njia muhimu ya kuongeza na kuimarisha uzalishaji wenye tija, **KWA HIYO BASI**, Kamati inapendekeza Bunge liazimie kwamba; Serikali ihuishe katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/2018, mpango utakaobainisha namna nchi itakavyotumia rasilimali maji zilizopo kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

### **3.3. Umuhimu wa Mnyororo wa Thamani kwenye Mazao**

**KWA KUWA**, mazao mengi ya wakulima yamekuwa yakipotea kabla ya kufika kwa mlaji kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa soko la uhakika na teknolojia bora ya uhifadhi, **NA KWA KUWA** kupotea kwa mazao hayo kumekuwa kukisababisha hasara kwa wakulima na kuwafanya kutonufaika kikamilifu na kazi zao **KWAHIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba; Serikali katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/2018 iwasilisha mikakati ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao ya kilimo na itekeleze kikamilifu mipango hiyo

### **3.4. Mazao yatokanayo na kilimo na umuhimu wake kwenye Uchumi wa Viwanda**

**KWA KUWA**, Serikali ya Awamu ya Tano inasisitiza umuhimu wa uchumi wa kujitegemea kupitia sekta ya viwanda, **NA KWA KUWA**, ili kufikia malengo hayo, Serikali haina budi kuimarisha sekta ya kilimo ambayo sio tu itatoa malighafi kwa ajili ya viwanda lakini pia itawezesha Taifa kuwa na utoshelezi wa chakula **KWA HIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba; Serikali itenga fedha za kutosha zitakazowezesha kukuza, kuimarisha na kuendeleza sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

### **3.5. Kuongezea mtaji Benki ya Maendeleo ya Wakulima**

**KWA KUWA**, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilianzishwa kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa mikopo kwa wakulima **NA KWA KUWA**, Serikali iliahidi kuongezea mtaji wa shilingi **100,000,000,000** kila mwaka ili kuwakopesha wakulima **KWA HIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba; Serikali itimiza azma yake ya kuongeza mtaji wa shilingi **100,000,000,000** kila mwaka katika benki ya wakulima ili kuongeza upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wakulima wengi.

### **3.6. Kuongeza Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo kwa Wakulima**

**KWA KUWA** mpango wa ugawaji waruzuku ya pembejeo kwa utaratibu wa vocha umeonyesha kushindwa kufanya kazi vizuri na kulalamikiwa katika maeneo mengi nchini **NA KWA KUWA**, Serikkali tayari imeanza kutekeleza mfumo mpya wa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa bei nafuu kwa wakulima **KWAHIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba; Serikali iongeza usimamizi na uratibu wa mfumo mpya wa utoajiRuzuku ya Pembejeo za Kilimo kwa Wakulima ili kuepukana na changamoto zilizojitokeza kwenye mfumo wa kutoa pembejeo kwa utaratibu wa vocha sanjali na kuongeza kiasi cha pembejeo kitakachotosheleza mahitaji halisi ya wakulima nchini.

### **3.7. Umuhimu wa uzalishaji wa mbegu bora nchini**

**KWA KUWA** mahitaji halisi ya mbegu ni makubwa kuliko uzalishaji wake nchini na hivyo kuhatarisha usalama wa chakula kutoptana na wakulima kuendelea kutumia mbegu za asili ambazo hazina tija, **NA KWA KUWA** Azma ya Serikali ya kuanzisha Wakala wa Mbegu za Kilimo ni kuongeza uzalishaji, upatikanaji na utumiaji wa mbegu bora kwa gharama nafuu. Azma hii imeshindwa kutekelezeka kutoptana Wakala kutengewa bajeti isiyotosheleza. **HIVYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba; Serikali itenga bajeti itakayotosheleza Wakala wa Mbegu kuwa na mtaji wa kuzalisha mbegu za kutosha. Lakini pia kuandaa mazingira rafiki yatakayowezesha sekta binafsi kushiriki katika uwekezaji wa kuzalisha mbegu.

### 3.8. Kutenga Fedha za Kutosha kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula

**KWA KUWA**, Taarifa ya Serikali imebainisha upungufu wa chakula kwenye Halmashauri 55 **NA KWA KUWA**, bei za vyakula nchini imeendelea kupanda kutokana na athari za ukame zilizopelekea uzalishaji kidogo hivyo kusababisha upungufu wa mazao sokoni **HIVYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba; Serikali itenga fedha za kutosha na kuzitoa kwa wakati ili kuiwezesha Mamlaka ya Taifa ya Hifadhi ya Chakula (NFRA) kununua na kuhifadhi mazao kadri ya tathimini ya uhitaji wa Taifa kuhakikisha usalama wa chakula nchini.

### 3.9. Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi

**KWA KUWA**, migogoro baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi imeendelea kuongezeka na kusababisha uvunjifu wa amani, vifo na uharibifu wa mazingira. **NA KWA KUWA**, Taarifa za mamlaka mbalimbali za Serikali zimeeleza suluhisho la migogoro hiyo ni kutekeleza Mpango wa Matumizi bora ya ardhi nchini, **HIVYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba; Serikali iongeza kasi ya kutekeleza kwa vitendo Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi kama ulivyoainishwa kwenye Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999.

### 3.10. Kushirikisha vyombo vya Ulinzi na Usalama kudhibiti uvuvi haramu

**KWA KUWA** Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu **NA KWA KUWA** vitendo hivyo vimeendelea kushamiri na kusababisha athari kubwa katika ekolojia ya maeneo ya uvuvi **KWA HIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba; Serikali iandae utaratibu maalumu utakaowezesha ushirikishwaji wa Jeshi la Wananchi katika kufanya doria kwa ajiri ya kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu.

### 3.11. Kuongeza Tozo ya Mafuta kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maji

**KWA KUWA** Sheria ya fedha ya mwaka 2015 ilianzisha tozo ya shilingi hamsini (50) kwa kila lita ya mafuta ya diseli na petroli kama chanzo cha mapato kwa Mfuko wa Taifa wa Maji **NA KWA KUWA** Mfuko wa Taifa wa Maji umeonyesha mafanikio makubwa katika kuwezesha upatikanaji fedha za kugharamia miradi ya maji, na kwamba fedha zinazopatikana zimeonyesha kutokidhi mahitaji ya miradi ya maji iliyopo **KWA HIYO BASI**, Kamati inaliomba Bunge liazimie kwamba; wakati wa utungaji wa Sheria ya fedha ya mwaka 2017 kuongeza tozo kwa kila lita ya mafuta ya diseli na petroli kutoka shilingi hamsini (50) hadi kufikia tozo ya shilingi mia moja (100) kwa kila lita ya mafuta ya diseli na petroli.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0. HITIMISHO

#### 4.1. Shukurani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa umuhimu wa pekee napenda kuishukuru Serikali kuitia Mawazairi wa Maji, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa sekta hizi kwa ushirikiano wao wakati wote Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake. Aidha, napenda pia kuwashukuru wadau wote wa sekta za Maji, Kilimo, Mifugo na Uvuvi ambao kwa namna moja au nyingine walishirikiana na Kamati wakati wa kuchambua Miswada, kutoa semina na mafunzo kwa Wajumbe kwa lengo la kuongeza uelewa na hata wakati wa uchambuzi wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyoitoa wakati wa Kamati kutekeleza majukumu yake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine G.Ishengoma,Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb Mjumbe
4. Mhe. Mahmoud H. Mgimwa, Mb "
5. Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb "
6. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb "
7. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb "
8. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb "
9. Mhe. Matta Ali Salum, Mb "
10. Mhe. John John Mnyika, Mb "
11. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb "
12. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb "
13. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb "
14. Mhe. Pascal Yohana Haonga, Mb "
15. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb "

- |                                       |   |
|---------------------------------------|---|
| 16. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb     | " |
| 17. Mhe. Abdallah Hamis Ulega, Mb     | " |
| 18. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb          | " |
| 19. Mhe. Daniel N. Nsanzugwanko, Mb   | " |
| 20. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb | " |
| 21. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb     | " |
| 22. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb     | " |
| 23. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb      | " |
| 24. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb | " |

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt, Thomas Kashililah pamoja na Sekreterieti ya Kamati amba ni Ndg. Rachel Nyega, Ndg. Virgil Mtui na Ndg. Martha Chassama na msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati hadi kukamilika Taarifa hii.

#### 4.2. Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza Shughuli zilizotekelozwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Dkt. Mary M. Nagu, (Mb)

**MWENYEKITI,**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**  
**9 FEBRUARI, 2017**

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge Ardhi, Maliasili na Utalii.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba taarifa ya Kamati iingie kwenye Hansard kama ilivyowasilishwa na kwamba maelezo ya kina yanapatikana katika taarifa iliyogawiwa kwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu

ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017, ili iweze kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ina Sehemu kuu nne. Sehemu ya Kwanza inaelezea utangulizi, Sehemu ya pili inaelezea utekelezaji wa majukumu ya Kamati, kwa kipindi cha Mwaka 2016/2017 na matokeo yaliyobainishwa. Sehemu ya tatu inaelezea maoni na mapendekezo ya Kamati, na Sehemu ya Nne ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati – ziara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara iliyofanyika katika miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) iliyopo katika eneo la Mwongozo, Kigamboni na eneo la Hananasifu Kinondoni, Kamati iliona kuwa nyumba zilizojengwa eneo la Mwongozo zina vyumba vidogo na nyingine zimejengwa chini ya kiwango ikilinganishwa na gharama ya nyumba hizo.

Vilevile, Kamati iligundua kuwa nyumba zinazojengwa na shirika sio za gharama nafuu kwa sababu shirika hulazimika kununua ardhi na kugharamia uwekaji wa miundombinu ya maji, barabara na umeme vitu ambavyo huchangia kuongezeka kwa gharama za ujenzi wa nyumba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapendekeza kuwa ili kupunguza gharama za nyumba za National Housing na kunufaisha watu wa kipato cha kati na cha chini, ni vema taasisi zinazohusika na ujenzi wa miundombinu zishirikishwe kujenga miundombinu kwenye maeneo yenye miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa ili kupunguza gharama ya nyumba hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara katika Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni. Kamati ilifanya ziara kwenye ofisi za Wakala wa Uendelezaji wa Mji mpya wa Kigamboni tarehe 18 Machi, 2016 na kupokea taarifa kuhusu maendeleo ya mradi. Kamati haikuridhishwa na hatua za Serikali katika utekelezaji wa mradi huu kwa kuwa hadi wakati Kamati inapokea taarifa za utekelezaji wa mradi hakukuwa na fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya uendeshaji wa mradi ikiwa ni pamoja na kulipa fidia katika maeneo yatakayojengwa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hii hakukuwa na mradi ulioonekana kuanzhishwa na hivyo kupoteza maana halisi ya kuwepo kwa mradi na uanzishaji wa wakala. Hali hii imesababisha Serikali kupoteza fedha kwa kulipia pango la Ofisi za Wakala na kuwa na watendaji ambao hawana majukumu ya kutekeleza. Kamati inaishauri Serikali iachane na mradi huu kwa kuwa imechukua muda mrefu bila kuwa na utekelezaji wowote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Tarehe 30 Machi, 2016, Kamati ilitembelea Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika kitengo cha huduma kwa wateja. Kamati iliweza kuona maboresho yaliyofanyika kwa kuwepo mfumo bora wa kielektroniki wa kuhudumia wateja, mfumo ambao unarahisisha kazi na kupunguza msongamano wa wateja na kuokoa muda. Kamati inaipongeza Wizara ya ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ubunifu huu na kuishauri Serikali kuwa na mfumo kama huu katika Wizara nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara katika Wakala wa Utafiti wa Nyumba bora na Vifaa vya Ujenzi. Kamati ilipata fursa ya kutembelea Wakala wa Taifa wa Nyumba bora na vifaa vya ujenzi tarehe 20 Januari, 2017 na kujionea shughuli mbalimbali zilizofanywa na Wakala.

Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wamajukumu ya Wakala yenyekumu kuu la kufanya utafiti, kukuza na kushawishi ujenzi wa nyumba bora za kudumu na za gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijionea teknolojia mbalimbali ambapo teknolojia mojawapo ilikuwa inahusu utengenezaji wa vigae na teknolojia nyingine ilikuwa inahusu utengenezaji wa matofali yaani *interlocking blocks*. Hata hivyo, pamoja na tafiti mbalimbali zinazofanywa zipo changamoto za uhaba wa watumishi wenye uzoefu katika nyanja za utafiti, kuchakaa kwa karakana ya vyuma inayopelekea kuwa na uwezo mdogo wa kuzalisha mashine za kufyatua matofali ya kufungamana na kutokuwa na ofisi maeneo mengine nchini zaidi ya Dar es Salaam. Hali hii imesababisha wananchi walio wengi kutokujua teknolojia zinazobuniwa na wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuitengea wakala bajeti ya kutosha sambamba na kuajiri wataalam wa kutosha ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Saadan, tarehe 29 Machi, 2016, Kamati ilitembelea hifadhi ya Taifa ya Saadan hususan kwenye eneo lenye mgogoro wa mipaka kati ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan na Kampuni ya Eco-Energyya Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo Kamati ilibaini kuwa eneo la mgogoro lenye ukubwa wa hekta 3,441 ni eneo ambalo liko ndani ya Hifadhi ya Saadan ilioanzishwa kisheria kwa tangazo la Serikali namba 281 la mwaka 2005. Aidha, Kamati ilibaini kuwa katika eneo alilopewa mwekezaji lenye ukubwa wa hekta 22,069 linajumuisha hekta 3,441 za eneo la mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliona kuwa endapo eneo lenye mgogoro litaachiwa kampuni ya Eco-Energy, athari mbalimbali zitajitokeza ikiwa

ni pamoja na kupungua kwa maji katika mto Wami kutakakosababishwa na umwagiliaji wa miwa itakayolimwa na mwekezaji na kuathiri watumiaji wengine. Vilevile ukulima wa zao la miwa katika eneo hili litavutia wanyamapor i hasa tembo kuja kula miwa na kusababisha mgogoro kati ya hifadhi na mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari nyingine ni pamoja na madhara ya madawa na mbolea yatakayotumika kwenye kilimo ambayo yataleta athari kwenye mazalia ya samaki na kuathiri ikolojia katika eneo la mto wami linaloingia baharini jambo ambalo linaipunguzia hifadhi ya Taifa ya Saadan vigezo vilivyo sababisha kuipandisha hadhi kutoka pori la akiba kuwa hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kujadiliana naye kuhusu suala hili ambapo alieeleza Kamati kwamba tayari Serikali imechukua hatua za kubatilisha umiliki wa mwekezaji katika eneo hilo. Hata hivyo, kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa, umuhimu na upekee wa hifadhi hii, Kamati inashauri kuwa ni vema Serikali ikaliachaa eneo hilo litumiwe na Hifadhi ya Saadan na mwekezaji akitafutiwa sehemu nyingine kuepusha mgogoro. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziara katika Chuo cha Misitu Olmotonyi, tarehe 4 Aprili, 2016 Kamati ilifanya ziara katika mradi wa uendelezaji shirikishi wa Misitu nchini unaotekelizwa na Chuo cha Misitu cha Olmotonyi kilicho nje kidogo ya Jiji la Arusha. Katika Ziara hiyo Kamati ilipokea taarifa ya shughuli zilizotekelizwa na mradi ikiwa ni pamoja na mafunzo kwa wadau wa misitu, ukarabati wa nyumba za kuishi wafanyakazi, ununuzi wa vifaa vya kutolea mafunzo pamoja na magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haikuridhishwa na taarifa iliyohusu fedha zilivyonumika katika utekelezaji wa mradi hivyo iliagiza uchunguzi maalum ufanyike ili kuweza kubaini gharama halisi zilizotumika katika mradi na kuleta taarifa kwa Kamati. Hata hivyo Wizara hajatekeleza mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziara Katika Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania. Kamati ilitembelea Wakala wa Mbegu za miti Tanzania tarehe 17 Januari, 2017 na kupokea taarifa ya utendaji ya wakala. Kamati inatambua kazi nzuri ya uzalishaji wa mbegu za miti inayofanywa na wakala na kuzuza ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iligundua kuwepo kwa changamoto zinazoikabili wakala ikiwa ni pamoja na upungufu wa wataalam, ufinyu wa bajeti, uhaba wa vitendea kazi na chumba kidogo cha maabara. Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya wakala, kuajiri watumishi wa kutosha na kupanua maabara iliyopo kwa lengo la kuboresha ufanisi wa wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara kutembelea Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania tarehe 17 Januari, 2017 na kujionea shughuli mbalimbali zinazotekelawa na Taasisi hiyo. Kamati ilibaini kuwepo kwa tafiti za misitu na matokeo mbalimbali ya tafiti hizo ikiwa ni pamoja na kugundua aina za miti inayostawi na kuongezeka katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, taasisi imefanya tafiti juu ya njia mbalimbali zinazotumika kuza mazao ya misitu pamoja na njia za kupambana na majanga ya moto katika misitu hapa nchini kwa lengo la kukuza Sekta ya Misitu ili kusaidia kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi hii bado inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti, uhaba wa watumishi na uhaba wa vitendea kazi. Kamati inaishauri Serikali kuboresha maslahi ya watumishi katika taasisi zetu za utafiti sambamba na kuweka vitendea kazi vya kutosha ili taasisi hizi ziweze kupata wataalam watakoatekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziara katika Mamlaka ya Wanyapori Tanzania (TAWA). Kamati ilifanya ziara ya kutembelea Mamlaka ya Wanyamapor Tanzania tarehe 17 Januari, 2017 na kupokea taarifa ya utendaji wa Mamlaka hiyo. Kamati inatambua kazi inayofanywa na Mamlaka ya wanyamapor Tanzania ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa mapori ya akiba na mapori tengefu. Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazoikabili Mamlaka. Changamoto hizo kwa ufupi ni kama zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi hasa askari wa wanyamaporjambo ambalo linachangia ongezeko la ujangili na uvamizi wa mifugo katika hifadhi zetu. Kuwepo kwa tatizo sugu la uvamizi wa makundi makubwa ya mifugo katika maeneo yaliyohifadhiwa. Kuwepo kwa mbinu mpya za ujangili ambapo majangili sasa wanatumia sumu kuua wanyamapor.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbinu hii ni hatari sana kwani inaua wanyamapor wengi na wa aina mbalimbali hata wale ambao hawakuwa wamekusudiwa. Kamati inaishauri Serikali kuajiri watumishi wa kutosha wenye ujuzi na utaalam wa kisasa hasa askari wa wanyamapor na kutatua migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji vinavyopakana na hifadhi kwa kuwashirikisha wananchi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuwaondoa wafugaji wote walioko katika hifadhi zetu ili kunusuru hifadhi na mazingira kwa ujumla. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziara katika Ghala la Kuhifadhia Nyara za Taifa. Kamati ilitembelea ghala la kuhifadhia Nyara za Taifa makao makuu ya Wizara ya Maliasili na Utalii tarehe 18 Januari, 2017 na kupokea taarifa kuhusu uhifadhi wa meno ya tembo na nyara nyingine za Taifa. Kwa ujumla Kamati

imeridhishwa na namna uhifadhi wa meno ya Tembo na Nyara nyingine unavyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Kimataifa na kwa kuzingatia mikataba iliyopo kuhusu nyara hizo, ikiwezekana itafutwe suluhu ya kudumu kwa kuwa idadi ya meno na nyara inaongezeka siku hadi siku. Aidha, Kamati inashauri ghala la nyara za Taifa likarabatiwe, liwekewe vifaa vya kutambua na kupambana na moto na ulinzi uimarishwe zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziarakatika makumbusho ya Taifa. Kamati ilitembelea Makumbusho ya Taifa pamoja na Kijiji cha makumbusho kilichopo Kijitonyama Dar es Salaam na kuona vivutio mbali mbali vya utalii ikiwa ni pamoja na baadhi ya nyumba zilizojengwa kwa asili ya makabila ya Tanzania. Kamati imebaini kuwa pamoja na taasisi hii kuhifadhi urithi mkubwa wa Taifa letu, bado Watanzania wengi hawana hamasa ya kutembelea Makumbusho ya Taifa ikilinganishwa na wageni kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya taasisi hii miundombinu yake imechakaa na kupoteza uhalisia na maana halisi ya uwepo wa makumbusho ya Taifa ambayo ni muhimu kwa historia ya Taifa letu. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa mpango wa kujenga nyumba za makabila mbalimbali ya Tanzania kwa kutumia ramani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utelekelezaji wa mpango huo na ikiwezekana nyumba hizo zijengwe kwa malighafi kutoka katika maeneo yanakopatikana makabila hayo ili kuongeza uhalisia. Vile vile Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa Makumbusho ya Taifa kupewa gawio la fedha zitakazokusanywa na mfuko wa kuendeleza utalii. Sambamba na hilo Serikali itoe elimu kwa wananchi itakayowahamasisha kujenga utamaduni wa kutembelea makumbusho ya Taifa kwa lengo la kujua historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikutano. Kamati ilikutana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa nyakati tofauti kupokea na kujadili taarifa mbalimbali zilizotolewa mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

Kamati ilipokea taarifa ya Utendaji wa Tume ya Matumizi ya Ardhi. Katika taarifa hiyo Kamati ilibaini kuwepo kwa ufinyu wa bajeti na upungufu wa wataalam uliopelekea utendaji wa tume kuwa hafifu. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea bajeti Tume ya Matumizi ya Ardhi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kuhusu migogoro ya ardhi nchini. Kumekuwepo na ongezeko kubwa la migogoro ya ardhi inayotokana na sehemu kubwa ya ardhi ya nchi yetu kutokupimwa na kupangiwa matumizi na hivyo kusababisha migogoro baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Aidha, mashamba makubwa yaliyotelekezwa yamekuwa kichocheo cha migogoro kwa sababu wakulima na wafugaji wasio na ardhi wamekuwa wakiyavamia na kuyatumia bila kuwa na kibali maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuongeza nguvu ili kuhakikisha kuwa ardhi yote inapimwa na kupangiwa matumizi hali ambayo itachangia kupunguza migogoro ya ardhi nchini. Vilevile, Kamati inashauri Serikali kuziwezesha Manispaa, Majiji na Halmashauri zetu kwa kuzipa vifaa vya upimaji na wataalam wa kutosha ili kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi nchini. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu mashamba makubwa yaliyotelekezwa hapa nchini. Katika taarifa hiyo Kamati ilielezwa kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea na zoezi la uhakiki wa umiliki wa mashamba makubwa yaliyotelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Zoezi hili mpaka kufikia Oktoba 2016 jumla ya mashamba 1,912 yalihakikiwa na mashamba 271 kati ya hayo, yilibainika kuwa yametelekezwa. Hali hii imepelekea wananchi kuvamia baadhi ya mashamba hayo na kufanya shughuli zao binafsi bila ya kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mpango mzuri wa Serikali wa kuchukua hatua ya kuanza kubatilisha miliki za baadhi ya mashamba yaliyotelekezwa na kuyapangia matumizi ya ardhi, ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo kwa ajili ya hazina ya ardhi (*land bank*), lakini zipo changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara katika kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizo ni pamoja na upungufu mkubwa wa fedha za kuendesha zoezi la uhakiki wa ardhi, kukosekana kwa mpango bora wa matumizi ya ardhi vijiji na gharama kubwa za kuandaa mpango bora wa matumizi ya Ardhi nchini. Kamati inashauri Serikali kuongeza bajeti kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi sambamba na upangaji wa matumizi ya ardhi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kuhusu program ya upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini. Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Programu ya Upimaji na Umilikishaji wa ardhi nchini, (*Land Tenure Support Programme*). Kamati inaipongeza Wizara ya Ardhi kwa kuanzisha programu hii kwa kuwa imelenga

kuongeza faida kwenye mikataba ya uwekezaji katika mashamba makubwa, kwa kuweka utaratibu bora wa umiliki ardhi pamoja na matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, programu imeendelea kuratibu zoezi la upimaji na urasimishaji wa ardhi za kimila katika wilaya mbalimbali hapa nchini kwa kuanza na Wilaya ya Kilombero, Ulanga na Malinyi, ambapo takribani hakimiliki 300,000 na hati miliki za ardhi 25,000 zimetolewa kwa muda wa miaka mitatu ambazo zitatumika kama dhamana ya kuwawezesha wakulima na wafugaji kupata mikopo

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria ya ardhi vijiji ili kuwapa uelewa wananchi kwa lengo la kuwapunguzia migogoro ya ardhi nchini. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya upimaji na urasimishaji ardhi ili kuwawezesha wananchi kupata haki miliki watakazotumia kama dhamana ya kupata mikopo ili waweze kujikwamua kiuchumi. Vilevile Kamati inaishauri Serikali iandae mipango bora ya matumizi ya ardhi vijiji kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikutano na Wizara ya Maliasili na Utalii. Katika taarifa ya utendaji wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) Kamati ilibaini kuwa katika hifadhi 16 zinazosimamiwa na Shirika zipo hifadhi ambazo hazijaweza kuijendesha zenyewe na hutegemea mapato ya Hifadhi zingine. Zipo hifadhi ambazo hazijatangazwa vya kutosha na kusababisha watalii wengi kwenda katika Hifadhi zilizoko kaskazini mwa nchi hali inayopelekea Hifadhi zingine kukosa mapato kutohana na idadi ndogo ya watalii wanaozitembelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa zinazozikabili hifadhi zetu ikiwa ni pamoja na ujangili na migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji vinavyopakana na hifadhi. Kamati imefurahishwa na hatua zinazochukuliwa na Shirika la Hifadhi za Taifa kwa jinsi linavyowashirikisha wananchi hususan wanaoishi kuzunguka Hifadhi za Taifa katika kuzilinda maliasili zetu kuitia mpango wa ujirani mwema. Kamati inaishauri Serikali kuitia Shirika la Hifadhi za Taifa kuhakikisha kuwa linatatua migogoro ya mipaka kati ya Hifadhi na wananchi ili kuboresha uhusiano. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kuhusu hali ya ujangili nchini. Kamati ilitaarifiwa kuwepo kwa mbinu mpya ya ujangili ambapo majangili wanatumia sumu kuua wanyamapori. Mbinu hii mpya ni hatari sana kwa uhifadhi kwani siyo tu inaua wanyama wengi kwa wakati mmoja bali pia inaua wanyama wasiokusudiwa. Kamati inaishauri Serikali kubadili mbinu za kupambana na majangili kwa kuongeza vifaa vya mawasiliano, silaha za kisasa na kuunda kikosi maalum kwa ajili ya kupambana na ujangili na kutumia kikosi chake cha

Intelijensia kubaini mtandao wa ujangili wa tembo nchini ili kuokoa rasilimali hii muhimu iliyohatarini kutoweke. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kuhusu maendeleo ya misitu na nyuki nchini. Kamati ilipokea taarifa kuhusu maendeleo ya rasilimali ya Misitu na Nyuki inayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS). Katika taarifa hiyo faida mbalimbali za misitu ziliainishwa ikiwa ni pamoja na kuhifadhi mazingira, kutoa ajira, kupunguza umaskini, kuhifadhi bioanuai, kuhifadhi udongo, chanzo cha nishati na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, misitu ni muhimu katika kurekebisha mfumo wa hali ya hewa na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Kamati inatambua mchango mkubwa wa sekta ya misitu katika kukuza uchumi wa nchi kwani huchangia wastani wa asilimia tatu nukta mbili ya Pato la Taifa na asilimia tano nukta tisa ya mapato yatokanayo na biashara ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja mchango mkubwa unaofanywa na na sekta hii, bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na mahitaji makubwa ya mazao ya misitu ikilinganishwa na ongezeko la ujazo wa miti, upanuzi wa makazi usio na mipango endelevu ya ardhi na kuwa kichocheo kikubwa cha uvamizi wa misitu ya hifadhi, migogoro ya mipaka baina ya hifadhi za misitu na jamii inayoizunguka hifadhi, matukio ya moto katika misitu, kukosekana kwa nishati mbadala, pamoja na upungufu wa watumishi walioajiriwa kulingana na eneo la misitu wanadolismamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu katika usimamizi wa rasilimali misitu kwa kuajiri askari wa kutosha pamoja na kuwaelimisha wananchi umuhimu wa misitu katika maisha ya kila siku. Aidha, Serikali iongeze wataalam wa misitu ili waweze kufanya shughuli za ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kuhusu changamoto ya kuzibwa kwa shoroba katika hifadhi za Taifa. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na maeneo mengi yenye wanyamapori, yakiwemo mapori tengefu, Mapori ya Akiba, Hifadhi za Jamii (WMA) na Hifadhi za Taifa. Aidha, yapo maeneo mengine yasiyohifadhiwa yalitumika kama mapito ya wanyamapori toka enzi hizo kutoka hifadhi moja kwenda nyingine yaani shoroba. Kwa muda mrefu hapakuwa na sheria ya katazo la shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo, hali iliyosababisha shoroba nyingi kuvamiwa na sasa ni makazi na mashamba ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, upanuzi wa miundombinu ya barabara, umeme, simu na maji pamoja na kukosekana kwa mipango bora ya ardhi katika vijiji vinavyozunguka maeneo ya hifadhi kumesababisha shoroba nyingi

kuzibwa hali inayosababisha migogoro ya wanyama kuvamia maeneo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzibwa kwa shoroba hizi kumepelekea changamoto mbalimbali hususan kupungua kwa kiasi kikubwa cha uhamaji wa wanyamaporl kwa lengo la kujaza nafasi zinazotokana na upungufu wa wanyama katika hifadhi moja hadi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii vilevile, inachangia kwa kiasi kikubwa kushindwa kusafirisha vinasaba muhimu (*gene pool*) ambavyo vinafanya ukuaji mzuri na endelevu ambapo matokeo yake wanyama wanalazimika kuzaliana ndugu jambo linalodhoofisha ubora wa vinasaba na kupelekeea kupata vinasaba hafifu na kuwepo hatari ya kutoweka kabisa. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na wananchi wanaoishi maeneo hayo, kuzibaini shoroba zote zilizopo na zilizofungwa ili zifunguliwe na kutungiwa sheria ili ziweze kuheshimiwa na kutumiwa na wanyamaporl. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya utalii nchini. Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu maendeleo ya utalii nchini. Mbali na mafanikio katika sekta ya utalii bado Serikali haijawekeza vyta kutosha katika utalii wa aina nyingine kama vile utalii wa fukwe za bahari, uvuvi, utamaduni na maeneo mengine. Serikali imeelekeza nguvu nyingi katika utalii wa wanyamaporl hasa ukanda wa kaskazini. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati itakayohakikisha kuwa vivutio vyote vyta Utalii vilivyopo nchini vinaendelezwa na kutangazwa ipasavyo ili kuvutia watalii wengi kutembelea nchi yetu na hivyo kuongeza pato la Taifa litokanalo na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano na Chama cha Wasafirishaji Wanyama Hai Tanzania, Kamati ilikutana na Chama cha Wasafirishaji na Wauzaji wa Viumbe Hai Nje ya Nchi yaani *Tanzania Wildlife Exporters Association* na kupokea malalamiko yao ambapo Serikali ilisitisha ghafla biashara ya uuzaaji wa wanyama hai nje ya nchi huku wadau wakiwa wamepewa leseni kihalali na walikuwa wamekwisha kamata wanyama tayari kwa kuwasafirisha. Hali hii imezua sintofahamu baina ya Serikali na wadau. Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya mfumo mzima wa utoaji leseni za kusafirisha wanyama hai nje ya nchi ili wananchi nao waweze kufaidika nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vilevile ilifanya Semina mbalimbali ambapo semina mojawapo ilifanya na Haki Ardhi na vilevile ilifanya semina na Jumuiya ya Wadau wa Misitu Tanzania (MJUMITA). Katika semina hizo Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

Wananchi wengi hawazijui sheria za ardhi na hivyo kujikuta wakiingia katika migogoro ya ardhi bila kujua. Vilevile Kamati iligundua kwamba mkaa na

kuni ni vyanzo vikubwa vyatishi majumbani na kwa sababu hakuna Sera wala sheria inayoelekeza upandaji, utunzaji na uvunaji wa miti, Kamati inaishauri Serikali kurasimisha sekta ya mkaa kwa kuitungia sera na sheria ili kuinusuru misitu yetu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza jitihada za kuelimisha wananchi kuhusu sheria za ardhi na wajibu wao katika kuzitekeleza ili kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza kwa kukosa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu; Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Maoni:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti na fedha kutotolewa kwa wakati kumesababisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kushindwa kufanya ukaguzi wa mashamba na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa mashamba yaliyotelekezwa na maeneo mbalimbali hapa nchini. Kutokuzingatia matumizi ya Sheria za Ardhi kumesababisha wananchi kuvamia mashamba hasa yale yaliyotelekezwa na ambayo yapo kwenye hatua za ubatilisho na kupelekea ongezeko la migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutoweka mikakati madhubuti ya kulinda maeneo ya hifadhi hasa njia za mapitio ya wanyama kumesababisha baadhi ya shoroba kutoweka na nyingine zimo hatarini kutoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezeka kwa ujangili hasa wa kutumia sumu kumesababisha wanyama wengi kufa na kutishia kutoweka kwa baadhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza maoni ya Kamati, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Nyumba za Gharama Nafuu:-

NA KWA KUWA, Shirika la Nyumba la Taifa limekuwa likigharamia ujenzi wa miundombinu katika miradi yake ya ujenzi wa nyumba;

NA KWA KUWA, ujenzi huo wa miundombinu umesababisha kupanda kwa gharama za nyumba na kufanya nyumba hizo kuwa za bei ya juu kwa mwananchi wa kipato cha chini kushindwa kumudu;

HIVYO BASI, Kamati inashauri Serikali kupitia wadau husika wa maji, umeme, barabara na ardhi kuwa na mpango mkakati wa pamoja ili kupeleka huduma hizo kwenye maeneo ya ujenzi wa nyumba ili kupunguza gharama ya ujenzi na hivyo kuzifanya nyumba za Shirika kuwa za gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashamba Yaliyotelekezwa:-

KWA KUWA, kumekuWa na mashamba makubwa yaliyotelekezwa kwa muda mrefu hapa nchini;

NA KWA KUWA, utelekezaji wa mashamba hayo umesababisha kuongezeka kwa migogoro ya ardhi kutokana na wakulima na wafugaji kuvamia mashamba hayo;

HIVYO BASI, Kamati inashauri kuwa ni vyema Serikali ikabatilisha milki ya mashamba hayo, kuyapima na kuyapangia matumizi ya ardhi maeneo yote yaliyotelekezwa na kuyagawa kwa watumiaji mbalimbali kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uvamizi wa Mifugo Katika Maeneo ya Hifadhi:

KWA KUWA, kumekuwa na tatizo sugu la makundi makubwa ya mifugo kuvamia maeneo yaliyohifadhiwa;

NA KWA KUWA, uvamiizi huo umesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira ikiwemo kukauka kwa vyanzo vya maji na mito;

HIVYO BASI, Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali kuchukua hatua za haraka kuondoa mifugo yote iliyovamia maeneo ya hifadhi ili kulinda mazingira na hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujangili wa Wanyamapor:-

KWA KUWA, matukio ya ujangili bado yanaendelea tena kwa mbinu mpya za kutumia sumu;

NA KWA KUWA, ujangili umesababisha baadhi ya wanyamapor kuuawa kwa wingi na kutishia kutoweuka;

HIVYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuunda vikosi maalum vya kupambana na ujangili sambamba na kutumia vifaa na silaha za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Utalii:-

KWA KUWA, Serikali imewekeza zaidi katika utalii wa Wanyamapor;

NA KWA KUWA, Serikali haijaonesha kabisa nia ya kuviendeleza na kuvitangaza vivutio vingine vya utalii na hivyo kusababisha kushuka mapato yatokanayo na utalii;

HIVYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati wa kuvitambua, kuviedeleza na kuvitangaza vivutio vyote vya utalii vilivyopo nchini ili kuvutia watalii wengi kutembelea nchi yetu na hivyo kuongeza pato litokanalo na Utalii. Aidha, Serikali inashauriwa kuboresha miundombinu katika maeneo yenye vivutio vya utalii ili kuwavutia wawekezaji kuwekeza kwenye maeneo ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne ni hitimisho. Mafanikio ya Kamati ya Ardhi Maliasili na Utalii katika kutekeleza shughuli zake kwa Mwaka 2016 yametokana na ushirikiano wa karibu sana wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hizi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa pamoja na wadau wetu wote...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia! Muda wako umekwisha, malizia, toa hoja.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba kutoa hoja. *(Makofii)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa hoja imeungwa mkono.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALI KWA KIPINDI CHA JANUARI 2016 HADI JANUARI 2017  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]

**SEHEMU YA KWANZA**

- 1.0 MAELEZO YA JUMLA**
- 1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari 2016 hadi Januari 2017, ili iweze kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge.

Taarifa hii ina Sehemu Kuu Nne. Sehemu ya Kwanza inaelezea Utangulizi, Sehemu ya pili inaelezea utekelezaji wa majukumu ya Kamati, kwa kipindi cha Mwaka 2016/2017 na matokeo yaliyobainishwa. Sehemu ya Tatu inaelezea maoni na mapendekezo ya Kamati, na Sehemu ya Nne ni hitimisho.

## 1.2 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii yameainishwa katika Nyongeza ya Nane iliyoundwa chini ya kanuni ya 118, kifungu cha 6 (6) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo 2016, kuwa:-

*“...Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii itasimamia shughuli za Wizara mbili nazo ni*

*(a)Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na (b) Wizara ya Maliasili na Utalii”.*

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli za Wizara zinazosimamiwa na Kamati ni pamoja na Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ilio chini ya Wizara tajwa, Taarifa za utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo pamoja na utekelezaji unaofanywa na Wizara hizi kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (b) ya Katiba. Aidha, mbali na majukumu tajwa, Kamati ya Ardhi Maliasili na Utalii ina jukumu la kushughulikia jukumu lolote litakaloletwa katika Kamati na Mheshimiwa Spika kwa kuzingatia Kanuni 119 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

## 1.3 KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI KWA MWAKA 2016

### 1.3.1 ZIARA

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016 Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo:-

- Hifadhi ya Taifa ya Saadan,
- Chuo cha Misitu Olmotonyi,
- Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,
- miradi ya ujenzi wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa iliyopo Kigamboni na Kinondoni,
- Wakala wa Uendelezaji wa mji mpya wa Kigamboni,

- Wakala wa Taifa wa mbegu za miti,
- Taasisi ya Utafiti wa misitu Tanzania,
- Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania,
- Ghala la kuhifadhi Nyara za Taifa,
- Makumbusho ya Taifa na
- Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba bora na vifaa vya ujenzi.

### 1.3.2 Mikutano

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari 2016 mpaka Januari 2017

Kamati ilifanya mikutano na Wizara na taasisi zilizo chini ya wizara kwa kupokea na kuchambua taarifa mbali mbali zilizoletwa mbele ya Kamati. Kwa upande wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa zifuatazo:-

- Mradi wa Umilikishaji wa Ardhi Nchini,
- Utendaji wa Tume ya Matumizi ya Ardhi,
- Migogoro ya Ardhi Nchini,
- Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa,
- Utendaji wa Wakala wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi
- Hatima ya Mashamba makubwa yaliyotelekezwa,
- Utekelezaji wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu
- Taarifa kuhusu programu ya upimaji na umilikishaji wa Ardhi nchini
- Utendaji wa wakala wa mji mpya wa kigamboni, na
- Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2015/2016 pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Kamati ilipokea na kuchambua taarifa zifuatazo:-

- utendaji wa Shirika la Hifadhi la Taifa
- Hali ya Ujangili Nchini.
- Maendeleo ya Misitu nchini,
- Utendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu nchini,
- Changamoto ya kuzibwa kwa shoroba katika hifadhi za Taifa.
- Maendeleo ya Utalii Nchini,
- Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2015/2016 pamoja na mapendekezo ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
- Utendaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania.

Aidha, Kamati ilikutana na chama cha wasafirishaji wa wanyama hai (Tanzania Wildlife Exporters Association) na kupokea malalamiko yao juu ya uamuzi wa Serikali kusitisha biashara ya kuuza wanyama hai nje ya Nchi.

### 1.3.3 Uchambuzi wa Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Kamati, ililetewa Muswada wa sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa Mwaka 2016 [The Valuation and Valuers Registration Act 2016], uliokuwa na dhumuni la kutunga sheria moja itakayosimamia taaluma na shughuli za Uthamini Tanzania Bara kwa lengo la kupunguza changamoto na kuboresha sekta ya ardhi nchini. Kamati ilipata muda wa kuujadili na kuuchambua muswada na kuufanya marekebisho yaliyolenga kuboresha na hatimaye kuwasilisha Bungeni kwa lengo la kuridhiwa na Bunge.

### 1.3.4 Semina

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilifanya semina na mikutano mbalimbali katika nyakati tofauti, kwa lengo la kuongeza uelewa wa wajumbe katika maeneo yanayohusu Sekta wanazozisimamia. Semina hizo ni kama zifuatazo:-

- Muundo na Majukumu ya wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
- Muundo na majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii
- Haki, Sheria na taratibu za umilikishaji wa Ardhi
- Urasimishaji wa Sekta ya Mkaa nchini.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

**2.1** Mheshimiwa Spika, sehemu hii inahusu matokeo yaliyopatikana kutokana na kazi zilizoteklezwa na Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2016.

### 2.2 ZIARA

#### 2.2.1 Ziara katika Miradi ya Ujenzi ya Shirika la Nyumba la Taifa

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara iliyofanyika katika miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) iliyopo katika eneo la Muongozo, Kigamboni na eneo la Hananasifu Kinondoni, Kamati iliona kuwa nyumba zilizojengwa eneo la Muongozo zina vyumba vidogo na nyingine zimejengwa chini ya kiwango ikilinganishwa na gharama ya nyumba hizo. Vilevile, Kamati imegundua kuwa nyumba zinazojengwa na shirika sio za

gharama nafuu kwa sababu shirika hununua ardhi na kugharamia uwekaji wa miundombinu ya maji, barabara na umeme vitu ambavyo huchangia kuongezeka kwa gharama za ujenzi wa nyumba.

Kamati inapendekeza kuwa ili kupunguza gharama za nyumba za (NHC) na kunufaisha watu wa kipato cha kati na chini, ni vema taasisi zinazohusika na ujenzi wa miundombinu zishirikishwe kujenga miundombinu kwenye maeneo yenye miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa ili kupunguza gharama ya nyumba hizo.

### **2.2.2 Ziara Katika Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara kwenye ofisi za Wakala wa Uendelezaji wa Mji mpya wa Kigamboni tarehe 18 Machi, 2016 na kupokea taarifa kuhusu maendeleo ya mradi. Kamati haikuridhishwa na hatua za Serikali katika utekelezaji wa mradi huu kwa kuwa hadi wakati Kamati inapokea taarifa za utekelezaji wa mradi hakukuwa na fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya uendeshaji wa mradi ikiwa ni pamoja na kulipa fidia katika maeneo yatakayojengwa miundombinu. Kutokana na hali hii hakukuwa na mradi wowote ulioonekana kuanzishwa na hivyo kupoteza maana halisi ya kuwepo kwa mradi, na uanzishaji wa Wakala. Hali hii imesababisha serikali kupoteza fedha kwa kulipia pango la Ofisi za Wakala na kuwa na watendaji ambao hawana majukumu ya kutekeleza. Kamati inaishauri serikali iachane na mradi huu kwa kuwa imechukua muda mrefu bila kuwa na utekelezaji wowote.

### **2.2.3 Ziara katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 30 Machi, 2016, Kamati ilitembelea Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika kitengo cha Huduma kwa Mteja. Kamati iliweza kuona maboresho yaliyofanyika kwa kuwepo mfumo bora wa kielektroniki wa kuhudumia wateja, mfumo ambao unarahisisha kazi na kupunguza msongamano wa wateja na kuokoa muda. Kamati inaipongeza Wizara ya ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ubunifu huu na kuishauri serikali kuwa na mfumo kama huu katika Wizara nyingine.

### **2.2.4 Ziara katika Wakala wa Utafiti wa Nyumba bora na Vifaa vya Ujenzi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Wakala wa Taifa wa Nyumba bora na vifaa vya ujenzi tarehe 20 Januari, 2017 na kujiona shughuli mbali mbali zinazofanywa na Wakala.

Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wakala yenyeye jukumu kuu la kufanya utafiti, kukuza na kushawishi ujenzi wa nyumba bora za kudumu na za gharama nafuu, kwa lengo la kuinua na kuboresha viwango vya nyumba, pamoja na kuongeza ubora wa maisha mijini na vijiji. Kamati ilielezwa uwepo wa teknolojia mbili madhubuti ambazo zimegundulika kutokana na tafiti zilizofanywa na wakala. Teknolojia hizo ni teknolojia ya utengenezaji wa matofali ya kufungamana (Interlocking blocks) yasiyohitaji udongo mwashi wa kujengea, yasiyotumia saruji nyingi na yenyeye kupunguza gharama za ujenzi hadi kufikia asilimia 40.

Teknolojia nyingine ni ya utengenezaji wa vigae vya kuezekeea ambavyo hutengenezwa kwa kutumia saruji, mchanga na nyuzi za mkonge. Teknolojia hii hurahisisha kazi na hupunguza gharama za ujenzi kwa kutumia saruji kidogo na kurahisisha kupatikana kwa vifaa imara vya kuezekeea. Hata hivyo pamoja na tafiti mbali mbali zinazofanywa zipo changamoto za uhaba wa watumishi wenye uzoefu katika Nyanja za utafiti, kuchakaa kwa karakana ya chuma inayopelekea kuwa na uwezo mdogo wa kuzalisha mashine za kufyatua matofali ya kufungamana na kutokuwa na ofisi maeneo mengine nchini zaidi ya Dar Es Salaam. Hali hii imesababisha wananchi walio wengi kutokujua teknolojia zilizobuniwa na wakala.

**Kamati inaishauri Serikali kuitengea wakala bajeti ya kutosha sambamba na kuajiri wataalam wa kutosha ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.**

#### **2.2.5 Ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Saadan**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 29 Machi, 2016, Kamati ilitembelea hifadhi ya Taifa ya Saadan hususan katika eneo lenye mgogoro wa mipaka kati ya Hifadhi ya Taifa ya Saadan na Kampuni ya **Eco-Energy** ya Bagamoyo. Katika ziara hiyo Kamati ilibaini kuwa eneo la mgogoro lenye ukubwa wa **hekta 3441** ni eneo ambalo liko ndani ya Hifadhi ya Saadan iliyoanzishwa kisheria kwa tangazo la Serikali namba **281** la mwaka 2005. Aidha, kamati ilibaini kuwa katika eneo alilopewa mwekezaji Kampuni ya **Eco-Energy ya Bagamoyo** lenye ukubwa wa hekta **22, 069** linajumuisha **hekta 3441** za eneo la mgogoro.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliona kuwa endapo eneo lenye mgogoro litaachiwa kampuni ya **Eco-Energy**, athari mbalimbali zitajitokeza ikiwa ni pamoja na kupungua kwa maji katika mto Wami kutakakosababishwa na umwagiliaji wa miwa itakayolimwa na mwekezaji (**Eco-energy**) na kuathiri watumiaji wengine. Vilevile ukulima wa zao la miwa katika eneo hili litavutia wanyamapori hasa tembo kuja kula miwa na kusababisha mgogoro kati ya hifadhi na mwekezaji. Athari nyingine ni pamoja na madhara ya madawa na mbolea yatakayotumika kwenye kilimo yataleta athari kwenye mazalia ya

samaki na kuathiri ikolojia katika eneo la mto wami linaloingia baharini jambo ambalo linaipungizia hifadhi ya Taifa ya Saadan vigezo vilivyo sababisha kipandisha hadhi saadan kutoka pori la akiba kuwa hifadhi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kujadiliana naye kuhusu suala hili ambapo alieeleza Kamati kwamba tayari serikali imechukua hatua za kubatilisha umilki wa mwekezaji katika eneo hilo. Hata hivyo, kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa, umuhimu na upekee wa hifadhi hii, **Kamati inashauri kuwa ni vema Serikali ikaliacha eneo hilo litumiwe na Hifadhi na mwekezaji akapewa eneo jingine ili kupusha migogoro.**

#### **2.2.6 Ziara katika chuo cha Misitu Olmotonyi**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 4 Aprili, 2016 Kamati ilifanya ziara katika mradi wa uendelezaji shirikishi wa Misitu nchini unaotekelizwa na Chuo cha Misitu cha Olmotonyi kilicho nje kidogo ya jiji la Arusha. Katika Ziara hiyo Kamati ilipokea taarifa ya shughuli zilizotekelizwa na mradi ikiwa ni pamoja na mafunzo kwa wadau wa misitu, ukarabati wa nyumba za kuishi wafanyakazi, ununuvi wa vifaa vya kutolea mafunzo pamoja na magari. Kamati haikuridhishwa na taarifa iliyohusu fedha zilivyotumika katika utekelezaji wa mradi hivyo iliagiza uchunguzi maalum ufanyike ili kuweza kubaini gharama halisi zilizotumika katika mradi na kuleta taarifa kwa Kamati. Hata hivyo wizara haijatekeleza mpaka sasa.

#### **2.2.7 Ziara Katika Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Wakala wa Mbegu za miti Tanzania tarehe 17 Januari, 2017 na kupokea taarifa ya utendaji ya wakala. Kamati inatambua kazi nzuri ya uzalishaji wa mbegu za miti inayofanywa na wakala na kuziwa ndani na nje ya nchi. Kamati iligundua kuwepo kwa changamoto zinazoikabili wakala ikiwa ni pamoja na upungufu wa wataalam, ufinyu wa bajeti, uhaba wa vitendea kazi, na chumba kidogo cha Maabara. **Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti ya wakala, kuajiri watumishi wa kutosha na kupanua maabara iliyopo kwa lengo la kuboresha ufanisi wa wakala.**

#### **2.2.8 Ziara katika Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania tarehe 17 Januari, 2017 na kujionea shughuli mbalimbali zinazotekelizwa na Taasisi hiyo. Kamati ilibaini kuwepo kwa tafiti za Misitu na matokeo mbalimbali ya tafiti hizo ikiwa ni pamoja na kugundua aina za miti inayostawi na kuongezeka katika maeneo mbali mbali nchini, umri sahihi wa kupanda na kuvuna miti, magonjwa na wadudu waharibifu wa miti na njia za kuyazuia, namna bora ya utunzaji wa misitu, pamoja na kusambaza matokeo

ya utafiti kwa wadau mbalimbali. Aidha, taasisi imefanya tafiti juu ya njia mbalimbali zinazotumika kuuza mazao ya misitu pamoja na njia za kupambana na majanga ya moto katika Misitu hapa nchini kwa lengo la kukuza Sekta ya Misitu ili kusaidia kuinua uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi hii bado inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti, uhaba wa watumishi na uhaba wa vitendea kazi. **Kamati inaishauri Serikali kuboresha maslahi ya watumishi katika taasisi zetu za utafiti sambamba na kuweka vitendea kazi vya kutosha ili taasisi hizi ziweze kupata wataalamu watakaotekeleza majukumu yao kwa ufanisi.**

### 2.2.9 Ziara katika Mamlaka ya Wanyama pori Tanzania (TAWA)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea Mamlaka ya Wanyamapor Tanzania tarehe 17 Januari, 2017 na kupokea taarifa ya utendaji wa Mamlaka hiyo. Kamati inatambua kazi inayofanywa na Mamlaka ya wanyamapor Tanzania ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu. Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbali mbali zinazoikabili Mamlaka. Changamoto hizo ni pamoja na:-

- Upungufu mkubwa wa watumishi hasa askari wa Wanyamaporjambo ambalo linachangia ongezeko la ujangili na uvamizi wa mifugo katika hifadhi zetu,
- Kuwepo kwa migogoro ya mipaka kati ya mapori ya Akiba na wananchi wanaishi kuzunguka maeneo hayo.
- Kuwepo kwa tatizo sugu la uvamizi wa makundi makubwa ya mifugo katika maeneo yaliyohifadhiwa.
- Kuwepo kwa vitendo vya ujangili vinavyotishia kutoweka kwa baadhi ya wanyamaporhususan Tembo na faru.
- Kuwepo kwa mbinu mpya za ujangili ambapo majangili wanatumia sumu kuua wanyamapor. Mbinu hii ni hatari kwani inaua wanyamapor wengi na wa aina mbali mbali hata wale ambao hawakuwa wamekusudiwa.

**Kamati inaishauri Serikali kuajiri watumishi wa kutosha wenye ujuzi na utaalamu wa kisasa hasa askari wa wanyamapor na kutatua migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji vinavyopakana na hifadhi kwa kuwashirikisha wananchi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuwaondoa wafugaji wote walioko katika hifadhi zetu ili kunusuru hifadhi na mazingira kwa ujumla.**

### 2.2.10 Ziara katika Ghala la Kuhifadhia Nyara za Taifa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea ghala la kuhifadhi Nyara za Taifa makao makuu ya Wizara ya Maliasili na Utalii tarehe 18 Januari, 2017 na kupokea taarifa kuhusu uhifadhi wa meno ya tembo na nyara nyingine za Taifa. Kwa ujumla Kamati imeridhishwa na namna uhifadhi wa meno ya Tembo na Nyara nyingine unavyofanyika. **Kamati inashauri Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Kimataifa na kwa kuzingatia mikataba iliyopo kuhusu nyara hizo, ikiwezekana itafutwe suluhu ya kudumu kwa kuwa idadi ya meno na nyara inaongezeka siku hadi siku.** Aidha Kamati inashauri ghala la Nyara za taifa likarabatiwe, liwekewe vifaa vya kutambua na kupambana na moto na ulinzi uimarishwe zaidi.

### 2.2.11 Ziara katika Makumbusho ya Taifa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Makumbusho ya Taifa pamoja na Kijiji cha makumbusho kilichopo Kijitonyama Dar Es Salaam na kuona vivutio mbali mbali vya utalii ikiwa ni pamoja na baadhi ya nyumba zilizojengwa kwa asili ya makabila ya Tanzania. Kamati imebaini kuwa pamoja na taasisi hii kuhifadhi urithi mkubwa wa taifa letu, bado Watanzania wengi hawana hamasa ya kutembelea Makumbusho ya taifa ikilinganishwa na wageni kutoka nje ya nchi.

Kutokana na bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya taasisi hii miundombini yake imechakaa na kupoteza uhalisia na maana halisi ya uwepo wa makumbusho ya Taifa ambayo ni muhimu kwa historia ya Taifa letu. Kamati inapongeza Serikali kwa kuandaa mpango wa kujenga nyumba za makabila mbalimbali ya Tanzania kwa kutumia ramani ya nchi yetu. **Kamati inaishauri Serikali kuharakisha utelekelezaji wa mpango huo na ikiwezekana nyumba hizo zijengwe kwa malighafi kutoka katika maeneo yanakopatikana makabila hayo ili kuongeza uhalisia.** Vile vile Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa Makumbusho ya Taifa kupewa gawio la fedha zinazokusanywa na mfuko wa kuendeleza utalii kupitia Tourism Development Levy. Sambamba na hilo Serikali itoe elimu kwa wananchi itakayowahamasisha kujenga utamaduni wa kutembelea makumbusho ya Taifa kwa lengo la kujua historia ya nchi yetu.

## 2.3 MIKUTANO

**Mheshimiwa Spika** Kamati ilikutana kupokea na kuchambua taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zilizo chini ya wizara hizi. Aidha, Kamati ilikutana na Chama cha Wauzaji wa viumbe hai yaani (*Tanzania Wildlife Exporters Association*)

### **2.3.1 Mkutano na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kamati ilikutana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa nyakati tofauti, kupokea na kujadili taarifa mbalimbali zilioletwa mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

### **2.3.2 Taarifa kuhusu utendaji wa Tume ya Matumizi ya Ardhi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa ya Utendaji wa Tume ya Matumizi ya Ardhi. Katika taarifa hiyo Kamati ilibaini kuwepo kwa ufinyu wa bajeti na upungufu wa wataalam uliopelekea utendaji wa tume kuwa hafifu. **Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti Tume ya Matumizi ya Ardhi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.**

### **2.3.3 Taarifa kuhusu Migogoro ya Ardhi nchini**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na ongezeko kubwa la migogoro ya ardhi inayotokana na sehemu kubwa ya ardhi ya nchi yetu kutokupimwa na kupangiwa matumizi na hivyo kusababisha mgongano baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Aidha mashamba makubwa yaliyotelekezwa yamekuwa kichocheo cha migogoro kwa sababu wakulima na wafugaji wasio na ardhi wamekuwa wakiyavamia na kuyatumia bila kuwa na kibali maalum.

**Kamati inashauri Serikali kuongeza nguvu ili kuhakikisha kuwa ardhi yote inapimwa na kupangiwa matumizi hali ambayo itachangia kupunguza migogoro ya ardhi nchini. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuziwezesha manispaa, Majiji na Halmashauri zetu kwa kuzipatia vifaa vyta upimaji na wataalam wa kutosha ili kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi nchini.**

#### **2.3.3.1 Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2015/2016 pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo kwa Mwaka 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa Fedha 2015/16, pamoja na mapendekezo ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2016/17 na kuiwasilisha Bungeni mnamo tarehe 28 Mei, 2016

#### **2.3.3.2 Taarifa kuhusu Mashamba Makubwa Yaliyotelekezwa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu mashamba makubwa yaliyotelekezwa hapa nchini. Katika taarifa hiyo kamati ilielezwa kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI inaendelea na zoezi la uhakiki wa milki za mashamba makubwa yaliyotelekezwa. Katika Zoezi hili mpaka kufikia Oktoba 2016 jumla ya mashamba **1,912** yalihakikiwa na mashamba **271** kati ya hayo, yalibainika kuwa yametelekezwa. Hali hii imepelekea wananchi kuvamia baadhi ya mashamba hayo na kufanya shughuli zao binafsi bila ya kibali.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mpango mzuri wa Serikali wa kuchukua hatua ya kuanza kubatilisha miliki za baadhi ya mashamba yaliyotelekezwa na kuyapangia matumizi ya ardhi, ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo kwa ajili ya hazina ya ardhi (*land bank*), lakini zipo changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara katika kutekeleza jukumu hili. Changamoto hizo ni pamoja na upungufu mkubwa wa fedha za kuendesha zoezi la uhakiki ardhi, kukosekana kwa mpango bora wa matumizi ya ardhi vijijini, na gharama kubwa za kuandaa mpango bora wa matumizi ya Ardhi nchini. **Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti kwa wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi sambamba na upangaji wa matumizi ya ardhi.**

### **2.3.3.3 Taarifa Kuhusu Programu ya Upimaji na Umilikishaji wa Ardhi Nchini.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Programu ya Upimaji na Umilikishaji wa ardhi nchini, (*Land Tenure Support Programme*). Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha programu hii kwa kuwa imelenga kuongeza faida kwenye mikataba ya uwekezaji katika mashamba makubwa, kwa kuweka utaratibu bora wa umiliki ardhi pamoja na matumizi yake. Aidha, programu imeendelea kuratibu zoezi la upimaji na urasimishaji wa ardhi za kimila katika wilaya mbalimbali hapa nchini kwa kuanza na wilaya ya Kilombero, Ulanga na Malinyi, ambapo takribani hakimiliki 300,000 na hati miliki za ardhi 25,000 zimetolewa kwa muda wa miaka 3, ambazo zitatumika kama dhamana ya kuwawezesha wakulima na wafugaji kupata mikopo. **Kamati inaishauri Serikali kutoa Elimu kwa umma kuhusu sheria ya ardhi vijijini ili kuwapa uelewa wananchi kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi nchini.** Aidha, **Kamati inaishauri Serikali kuongeza Kasi ya upimaji na urasimishaji ardhi ili kuwawezesha wananchi kupata haki miliki watakazotumia kama dhamana ya kupata mikopo ili waweze kujikwamua kiuchumi.** Vilevile **Kamati inaishauri Serikali iandae mipango bora ya matumizi ya ardhi vijijini kwa lengo la kupunguza migogoro ya ardhi hapa nchini.**

### **2.3.4 Mikutano na Wizara ya Maliasili na Utalii**

**Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya mikutano mbalimbali na** Wizara ya Maliasili na Utalii. Katika mikutano hiyo, taarifa zifuatazo zilijadiliwa:-

#### **2.3.4.1 Taarifa kuhusu Utendaji wa Shirika la Hifadhi la Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, Katika taarifa ya utendaji ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) Kamati ilibaini kuwa katika hifadhi 16 zinazosimamiwa na Shirika zipo hifadhi ambazo hazijaweza kuijendesha zenyewe na hutegemea mapato ya Hifadhi zingine. Zipo hifadhi ambazo hazijatangazwa vya kutosha na kusababisha watalii wengi kwenda katika Hifadhi zilizoko kaskazini mwa nchi hali inayopelekea Hifadhi zingine kukosa mapato kutokana na idadi ndogo ya watalii wanaozitembelea. Vile vile Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa zinazozikabili hifadhi zetu ikiwa ni pamoja na ujangili na migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji vinavyopakana na hifadhi. Kamati imefurahishwa na hatua zinazochukuliwa na Shirika la Hifadhi za Taifa kwa jinsi linavyowashirikisha wananchi hususan wanaoishi kuzunguka Hifadhi za Taifa katika kuzilinda Maliasili zetu kupitia mpango wa ujirani mwema. **Kamati inaishauri Serikali kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa kuhakikisha kuwa linatatua migogoro ya mipaka kati ya Hifadhi na wananchi ili kuboresha uhusiano.**

#### **2.3.4.2 Taarifa kuhusu hali ya Ujangili nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kuwepo kwa mbinu mpya ya ujangili ambapo majangili wanatumia sumu kuua wanyamapori. Mbinu hii mpya ni hatari sana kwa uhifadhi kwani siyo tu inaua wanyama wengi kwa wakati mmoja bali pia inaua wanyama wasiokusudiwa. **Kamati inaishauri Serikali kubadili mbinu za kupambana na majangili kwa kuongeza vifaa vya mawasiliano, silaha za kisasa na kuunda kikosi maalumu kwa ajili ya kupambana na ujangili na kutumia kikosi chake cha Intelijensia kubaini mtandao wa ujangili wa Tembo nchini ili kuokoa rasilimali hii muhimu iliyo hatarini kutoweke.**

#### **2.3.4.3 Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2015/2016 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/16, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa Fedha 2016/17 na kuiwasilisha Bungeni mnamo tarehe 23 Mei, 2016.

#### **2.3.4.4 Taarifa kuhusu Maendeleo ya Misitu na Nyuki Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa kuhusu maendeleo ya rasilimali ya Misitu na Nyuki inayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

(TFS). Katika taarifa hiyo faida mbali mbali za misitu ziliainishwa ikiwa ni pamoja na kuhifadhi mazingira, kutoa ajira, kupunguza umaskini, kuhifadhi bioanuia, kuhifadhi udongo, chanzo cha nishati na maji. Aidha, misitu ni muhimu katika kurekebisha mfumo wa hali ya hewa na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Kamati inatambua mchango mkubwa wa sekta ya misitu katika kukuza uchumi wa nchi kwani huchangia wastani wa aslimia 3.2 ya Pato la Taifa, na aslimia 5.9 ya mapato yatokanayo na biashara ya nje.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja mchango mkubwa unaofanywa na na sekta hii, bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na mahitaji makubwa ya mazao ya misitu ikilinganishwa na ongezeko la ujazo wa miti, upanuzi wa makazi usio na mipango endelevu ya ardhi na kuwa kichocheo kikubwa cha uvamizi wa misitu ya hifadhi, migogoro ya mipaka baina ya hifadhi za misitu na jamii inayoizunguka hifadhi, matukio ya moto katika misitu, kukosekana kwa nishati mbadala, pamoja na upungufu wa watumishi walioajiriwa kulingana na eneo la misitu wanadolismamia. **Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu katika usimamizi wa rasilimali misitu kwa kuajiri askari wa kutosha pamoja na kuwaelimisha wananchi umuhimu wa misitu katika maisha ya kila siku. Aidha, serikali iongeze wataalam wa misitu ili waweze kufanya shughuli za ugani.**

#### **2.3.4.5      Taarifa Kuhusu Changamoto ya Kuzibwa kwa Shoroba Katika Hifadhi za Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu imebarikiwa kuwa na maeneo mengi yenye wanyamapori, yakiwemo mapori tengefu, Mapori ya Akiba, Hifadhi za Jamii (WMA) na Hifadhi za Taifa. Aidha, yapo maeneo mengine yasiyohifadhiwa yalitumika kama mapito ya wanyamapori toka enzi hizo kutoka hifadhi moja kwenda nyingine yaani shoroba. Kwa muda mrefu hapakuwa na sheria ya katazo la shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo, hali iliyosababisha shoroba nyingi kuvamiwa na sasa ni makazi na mashamba ya watu. Vile vile, upanuzi wa miundo mbinu ya barabara, umeme, simu na maji pamoja na kukosekana kwa mipango bora ya ardhi katika vijiji vinavyozunguka maeneo ya hifadhi kumesababisha shoroba nyingi kuzibwa hali inayosababisha migogoro ya wanyama kuvamia maeneo ya watu. kuzibwa kwa shoroba hizi kumepelekea changamoto mbalimbali hususan kupungua kwa kiasi kikubwa cha uhamaji wa wanyamapori kwa lengo la kujaza nafasi zinazotokana na upungufu wa wanyama katika hifadhi moja hadi nyingine. Hali hii vilevile, inachangia kwa kiasi kikubwa kushindwa kusafirisha vinasaba muhimu (gene pool) ambavyo vinafanya ukuaji mzuri na endelevu ambapo matokeo yake wanyama wanazimika kuzaliana ndugu jambo linalodhoofisha ubora wa vinasaba na kupelekea kupata vinasaba hafifu na kuwepo hatari ya kutoweke kabisa. **Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na wananchi wanaoishi maeneo**

**hayo, kuzibaini shoroba zote zilizopo na zilizofungwa ili zifunguliwe na kutungiwa sheria ili ziweze kuheshimiwa na kutumiwa na wanyamapori.**

#### **2.3.4.6 Taarifa kuhusu Maendeleo ya Utalii Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu maendeleo ya utalii nchini. Mbali na mafanikio katika sekta ya utalii bado Serikali haijawekeza vya kutosha katika utalii wa aina nyingine kama vile utalii wa fukwe za bahari, uvuvi, utamaduni na maeneo mengine. Serikali imeelekeza nguvu nyingi katika utalii wa wanyamapori hasa ukanda wa kaskazini. **Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati itakayohakikisha kuwa vivutio vyote vya Utalii vilivyopo nchini vinaendelezwa na kutangazwa ipasavyo ili kuvutia watalii wengi kutembelea nchi yetu na hivyo kuongeza pato la Taifa litokanalo na utalii.**

#### **2.3.5 Mkuano na Chama cha wasafirishaji wanyama hai Tanzania (Tanzania Wildlife Exporters Association)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Chama cha wasafirishaji na wauzaji wa viumbi hai nje ya nchi yaani Tanzania Wildlife Exporters Association na kupokea malalamiko yao ambapo serikali ilisitisha ghafla biashara ya uuzaji wa wanyama hai nje ya nchi huku wadau wakiwa wamepewa leseni kihalali na walikuwa wamekwisha kamata wanyama tayari kwa kuwasafirisha. Hali hii imezua sintofahamu baina ya serikali na wadau. **Kamati inaishauri serikali kuangalia upya mfumo mzima wa utoaji leseni za kusafirisha wanyama hai nje ya nchi ili wananchi nao wawezekufaidika nazo.**

### **2.4 SEMINA**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata Semina mbili kutoka shirika lisilo la kiserikali la **HakiArdhi** kuhusu mchango wa Asasi za kiraia katika kuwaelimisha wananchi juu ya sheria mbalimbali za ardhi na Mtandao wa Jumuiya ya Wadau wa Misitu Tanzania ( **MJUMITA**) kuhusu umuhimu wa nishati itokanayo na Tungamotaka ( Kuni na Mkaa) kutungiwa sera na sheria. Katika semina hizo Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

- Wananchi wengi hawazijui sheria za ardhi na hivyo kujikuta wakiingia katika migogoro ya ardhi bila kujua
- Mkaa na Kuni ni vyanzo vikubwa vya nishati majumbani na kwa sababu hakuna Sera wala sheria inayoelekeza upandaji, utunzaji na uvunaji wa miti, vimekuwa chanzo kikubwa cha uharibifu wa Misitu kutoptana na ukataji

holela wa miti na uchomaji wa mkaa na hivyo kutishia nchi yetu kugeuka jangwa.

**Kamati inaishauri serikali kurasimisha sekta ya mkaa kwa kuitungia sera na sheria ili kuinusuru misitu yetu. Aidha Kamati inaishauri serikali kuongeza jitihada za kuuelimisha wananchi kuhusu sheria za ardhi na wajibu wao katika kuzitekeleza ili kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza kwa kukosa elimu.**

## 2.5 Miswada

**Mheshimiwa Spika**, katika muswada wa sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini, (**The valuation and Valuers Registration Bill, 2016**) Kamati ilitoa taarifa, maoni na mapendeleko yaliyopelekea kuboresha muswada na baadaye kuwasilisha bungeni. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Msawaada huu kwa wakati jambo ambalo limewezesha kutungwa kwa Sheria inayosimamia taaluma ya Uthamini na kuunda Bodi ya wathamini nchini.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

#### 3.1 Maoni

- i) Ufinyu wa bajeti na fedha kutotolewa kwa wakati kumesababisha wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kushindwa kufanya ukaguzi wa mashamba na uandaaji wa mipango ya matumizi ardhi kwa mashamba yaliyotelekezwa na maeneo mbali mbali ya ardhi vijiji;
- ii) Kutokuzingatia matumizi ya sheria za ardhi kumesababisha wananchi kuvamia mashamba hasa yale yaliyotelekezwa na ambayo yapo kwenye hatua za ubatilisho na kupelekea ongezeko la migogoro ya ardhi;
- iii) Kutokuwepo kwa miundombinu ya maji, umeme, barabara, katika maeneo yanayoengwa nyumba za gharama nafuu kunapelekea kuongezeka kwa gharama za nyumba na hivyo kuzifanya nyumba zinazojengwa na shirika la nyumba la Taifa kuwa za gharama ya juu na sio za gharama nafuu;
- iv) Serikali kutoweka mikakati madhubuti ya kulinda maeneo ya hifdhii hasa njia na mapitio ya wanyama (Wildlife corridors) kumesababisha baadhi ya shoroba kutoweka na nyingine zimo hatarini kutoweka.
- v) Uvamizi unaofanywa na Wafugaji katika Hifadhi za Taifa , mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Misitu ya Hifadhi ni jambo linasababisha kuharibika kwa mazingira katika maeneo hayo na kuchangia kukauka kwa vyanzo vya maji na ukame na mabadiliko ya Tabianchi;

vi) Uvamizi wa misitu kwa shughuli za binadamu ikiwemo kilimo, ufugaji, makazi na uchimbaji wa madini kumesababisha uharibifu mkubwa wa misitu na hivyo kutishia kuenea kwa jangwa nchini;

vii) Kuongezeka kwa ujangili na hasa wa kutumia sumu kumesababisha wanyama wengi kufa na kutishia kutoweke kwa baadhi yao;

### **3.2 Mapendeleko**

Mheshimiwa Spika, **baada ya kueleza maoni ya Kamati, naomba kutoa mapendeleko ya Kamati kama ifuatavyo:-**

#### **3.2.1 Ujenzi wa Nyumba za Gharama Nafuu**

Kwa kuwa, Shirika la Nyumba la Taifa limekuwa likigharamia ujenzi wa miundombinu katika miradi yake ya ujenzi wa nyumba; Na kwa kuwa ujenzi huo wa miundombinu umesababisha kupanda kwa gharama za nyumba na kufanya nyumba hizo kuwa za bei ya juu na mwananchi wa kipato cha chini kushindwa kumudu, Hivyo basi, **Kamati inashauri, Serikali kupitia wadau husika wa maji, umeme, barabara na ardhi kuwa na mpango mkakati wa pamoja ili kupeleka huduma hizo kwenye maeneo ya ujenzi wa nyumba ili kupunguza gharama za ujenzi na hivyokuzifanya nyumba za Shirika kuwa za gharama nafuu.**

#### **3.2.2 Mashamba yaliyotelekezwa**

Kwa kuwa kumekua na mashamba makubwa yaliyotelekezwa kwa muda mrefu hapa nchini, Na kwa kuwa utelekezaji wa mashamba hayo umesababisha kuongezeka kwa migogoro ya ardhi kutokana na wakulima na wafugaji kuvamia mashamba hayo, hivyo **basi Kamati inashauri kuwa ni vyema serikali ikabatilisha milki ya mashamba hayo, kuyapima na kuyapangia matumizi ya ardhi maeneo yote yaliyotelekezwa na kuyagawa kwa watumiaji mbali mbali kwa lengo la kupunguza migogoro ya Ardhi hapa nchini.**

#### **3.2.3 Kuzibwa kwa Shoroba Katika Hifadhi za Taifa**

Kwa kuwa, shoroba nyingi nchini zimezibwa kutokana na shughuli za kibinadamu ambazo zinaongezeka siku hadi siku, Na kwa kuwa, kuzibwa kwa shoroba kunaleta hatari ya kutoweke kwa baadhi ya vinasaba vya wanyama na baadae wanyama wenyewe kutoweke hali inayozorotesha sekta ya utalii na kuathiriri pato la taifa litokanalo na utalii, hivyo basi, **Kamati inapendeleko kuwa, Serikali ibainishe maeneo yote ya shoroba za wanyama na kuandaa kanuni za kuzitambua kisheria shoroba ili kuweka utaratibu na njia bora za**

**kulinda shoroba ili wanyamapor waendelee kupita bila kusababisha madhara kwa binadamu na mali zao.**

### **3.2.4 Uvamizi wa mifugo katika maeneo ya Hifadhi**

Kwa kuwa kumekuwa na tatizo sugu la makundi makubwa ya mifugo kuvamia maeneo yaliyohifadhiwa, Na kwa kuwa uvamiizi huo umesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira ikiwemo kukauka kwa vyanzo vya maji na mito, hivyo basi **Kamati inaliomba Bunge kuitaka Serikali kuchukua hatua za haraka kuondoa mifugo yote iliyovamia maeneo ya hifadhi ili kulinda mazingira na hifadhi zetu.**

### **3.2.5 Ujangili wa Wanyamapor**

Kwa kuwa matukio ya ujangili bado yanaendelea tena kwa mbinu mpya za kutumia sumu, Na kwa kuwa ujangili umesababisha baadhi ya wanyamapor kuuawa kwa wingi na kutishiwa kutoweka, Hivyo basi **Kamati inaishauri serikali kuuunda vikosi maalum vya kupambana na ujangili sambamba na kutumia vifaa na silaha za kisasa.**

### **3.2.6 Maendeleo ya Utalii**

Kwa kuwa Serikali imewekeza zaidi katika utalii wa Wanyamapor, Na kwa kuwa Serikali haijaonyesha kabisa nia ya kuviendeleza na kuvitangaza vivutio vingine vya Utalii na hivyo kusababisha kushuka mapato yatokanayo na Utalii, hivyo basi **Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati wa kuvitambua, kuviendeleza na kuvitangaza vivutio vyote vya Utalii vilivyopo nchini ili kuvutia Watalii wengi kutembelea nchi yetu na hivyo kuongeza pato litokalo na Utalii. Aidha, serikali inashauriwa kuboresha miundombinu katika maeneo yenye vivutio vya utalii ili kuwawutia wawekezaji kuwekeza kwenye maeneo ya utalii**

## **SEHEMU YA NNE**

### **4.0 HITIMISHO**

### **4.1 SHUKURANI**

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio ya Kamati ya Ardhi Maliasili na Utalii katika kutekeleza shughuli zake kwa Mwaka 2016, yametokana na ushirikiano wa karibu sana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hizi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa pamoja na wadau wetu wote, napenda kuwashukuru wote kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kukushukuru kwa ushirikiano tulioopata kwa mwaka mzima wakati Kamati inatekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah pamoja na makatibu wa Kamati hii Ndugu Gerald Magili, Haika Mtui na Elieka Saanya kwa kuratibu shughuli zote za Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Kipekee niwashukuru waheshimiwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kutoa maoni, ushauri pamoja na ushirikiano wao kwenye Kamati, halii iliyowezesha kufanikisha kazi zote za Kamati yetu. Naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

- |  |                |
|--|----------------|
| 1. Mhe. Atashasta J. Nditiye, Mb,      | - Mwenyekiti   |
| 2. Mhe. Kemilembe J. Lwota, Mb,        | - M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Fredy Atupele Mwakibete, Mb,   | - Mjumbe       |
| 4. Mhe. Devotha Mathew. Minja, Mb,     | -Mjumbe        |
| 5. Mhe. Dkt Godwin Oloyce. Mollel, Mb, | -Mjumbe        |
| 6. Mhe. Grace Sindato Kiwelu, Mb       | - Mjumbe       |
| 7. Mhe. Jaffar Sanya Jussa, Mb,        | - Mjumbe       |
| 8. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb,    | - Mjumbe       |
| 9. Mhe. Khalifa Salim Sulemain, Mb,    | - Mjumbe       |
| 10. Mhe. Lucy Fidels Owenya, Mb,       | - Mjumbe       |
| 11. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya, Mb   | - Mjumbe       |
| 12. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb        | - Mjumbe       |
| 13. Mhe. Musukuma Joseph Kasheku, Mb   | - Mjumbe       |
| 14. Mhe. Omari Abdallah Kigoda, Mb     | - Mjumbe       |
| 15. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb     | - Mjumbe       |
| 16. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb     | - Mjumbe       |
| 17. Mhe. Risala Kabongo, Mb            | - Mjumbe       |
| 18. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb  | - Mjumbe       |
| 19. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb        | - Mjumbe       |
| 20. Mhe. Sebastian Simoni Kapufi, Mb   | - Mjumbe       |
| 21. Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb      | - Mjumbe       |
| 22. Mhe. Zainabu Nuhu Mwamwindi, Mb    | - Mjumbe       |
| 23. Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb        | - Mjumbe       |
| 24. Mhe. Neema William Mgaya, Mb       | - Mjumbe       |
| 25. Mhe. Salma Mohamed Mwassa, Mb      | - Mjumbe       |

#### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza Shughuli zilizotekelizwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na Mapendelekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii pamoja na maoni na mapendelekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Mhe.Eng. Atashasta Nditiye, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,**

**MALIASILI NA UTALII**

09 Februari, 2017

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati nitaomba, kuna michango mingine inakuja kwa maandishi, mnapoijibia huwa hamuipeleki Hansard! Naomba michango yote ya maandishi ipelekwe Hansard, ili iwe kumbukumbu sahihi ya michango ya Wabunge. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, tuna wachangiaji saba asubuhi hii. Tutaanza na Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Edwin Sannda, Mheshimiwa Mohamed Mahmud Msigwa, Mheshimiwa Manase Nyenza na Dkt. Ndugulile.

Mheshimiwa Sakaya!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Taarifa zilizoko mbele yetu. Awali niwashukuru sana watoa hoja wote, Kamati zote mbili kwa taarifa zao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nitakwenda *straight* kwenye hoja. Naomba nianze kwa kusema kwamba, tunayo hifadhi moja tu Tanzania yenye urithi wa kipekee, hifadhi ambayo ina vivutio ambavyo haviko sehemu nyingine Tanzania, Afrika na hata Dunia nzima na ni Hifadhi yetu ya Ngorongoro. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ambayo imekuwa inatuingizia kipato kikubwa sana kwa Taifa hili, lakini kwa karibu miaka 10 sasa, hifadhi hii isipoangaliwa kwa makini inakwenda kupotea ndani ya Tanzania. Hifadhi hii imewekwa ndani ya Urithi wa Dunia, imeingia kwenye Maajabu saba ya Dunia na imewekwa chini ya UNESCO, Shirika la Uhifadhi la Dunia, lakini Watanzania ambao tumepewaa hadhi ya kuwa na hifadhi hii tumeshindwa kuitunza na sasa hivi hali ya hifadhi hii inakwenda kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Ngorongoro inakabiliwa na tatizo kubwa la watu kulima ndani ya hifadhi, Ngorongoro inakabiliwa na watumishi kutafuna fedha za hifadhi, inakabiliwa pia na kuongezeka kwa mifugo. Jana nilikuwa nasoma vyombo vya habari, tayari Ngorongoro hata watumishi wanahamishwa

wanakataa wanakwenda Mahakamani kushtaki. Najaribu kuelewa kwamba, miaka mitano ijayo tunayo Ngorongoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, hadhi ya Hifadhi ya Ngorongoro iendelee kubaki kama Uriithi wa Dunia kwa vizazi vya leo na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeunda Tume hapa Tanzania kwa ajili ya kupitia migogoro ya wakulima na wafugaji na kuweza kuondoa mauaji yanayotokea ndani ya nchi yetu. Hata hivyo napenda kujua, Tume hii imeshaanza kazi, itamaliza lini? Tume hii ambayo inahusu Wizara nne na wataalam kutoka Wizara nne wakati bado inaendelea na kazi bado kuna wataalam na watendaji wanaopita kwenye maeneo ya hifadhi na kuweka alama katikati ya nyumba za watu bila kushirikisha Ofisi za Wilaya, Wakurugenzi hata Wabunge kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tujue, Serikali imeamua kuunda Tume, itekeleze kwanza jukumu la Tume. Tume ije na mpango kamili utakaoweza kutoa suluhi ya kutosha kuondoa migogoro ya wafugaji, kuondoa migogoro ya wakulima na migogoro ambayo watu wanapoteza maisha yao hapa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba, Wizara ya Ardhi wamefanya kazi nzuri; wamefungua kanda nne ndani ya Tanzania kuweza kurahisisha huduma za ardhi. Pamoja na kufungua Kanda nne ndani ya nchi yetu bado kuna tatizo kubwa katika Halmashauri zetu, manispaa zetu pamoja na majiji la kutokuwa na fedha za kutosha kuweza kupima maeneo. Tunayo shida kubwa sana Waheshimiwa Wabunge, nchi yetu haijapimwa, maeneo mengi hayajapimwa, migogoro inaongezeka kwa sababu pamoja na kwamba Wizara inajitahidi; na namshukuru Mheshimiwa Lukuvi anafanya kazi nzuri, lakini bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie namna ya kuweza kutoa fedha kama *revolving fund* kwenye manispaa zetu, kwenye halmashauri zetu pamoja na kwenye majiji, wapewe fedha wapime maeneo, wakishayapima wayauze wapate fedha, warejeshe fedha. Hiyo kazi ilianza kama miaka mitano iliyopita kwenye Manispaa za Dar-es-Salaam; Temeke, Ilala na Kinondoni, sikujua ule mpango uliishia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba, ule ulikuwa ni mpango mzuri, tuliusapoti lakini umeishia katikati. Ni mpango mzuri, Serikali iwezeshe, ipeleke watalaam wa kutosha kwenye halmashauri, ipeleke vifaa kwenye manispaa, kwenye majiji na halmashauri, lakini pia, itoe fedha waweze kupima

kuhakikisha kwamba, nchi yetu inapimwa. Kutegemea Wizara peke yake tutachukua miaka mingi sana kuweza kupima maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo kubwa sana la makazi holela. Mimi kila nikiongea juu ya ardhi nazungumzia makazi holela. Tumekuwa kama Serikali hatujipangi. Leo kila ukienda watu wanaanzisha miji miwili, mitatu, baada ya miezi mitano, baada ya mwaka ni mji tayari. Tayari wanahitaji huduma za maji, barabara, na umeme. Serikali kwa nini isiwe na mpango? Watu waambiwe kajengeni pale? Kwa nini inasubiri wananchi wajiamulie wenyewe wakakae wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukianza kutembea kuanzia Dodoma, elekea Morogoro unaenda Dar-es-Salaam, vijiji vinaanzishwa kidogo, kama utani. Serikali ipo, viongozi wapo, wataalam, lakini wanaona wananyamaza kimya. Leo tumekuwa na nchi ambayo haijapimwa maeneo mengi, miji yake ni ya kiholela na bado inazidi kuanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ifike mwisho kuwa na mji usiopimwa, usiopangwa, miji ambayo ni ya kiholela. Nchi nzima tunakuwa na vichuguu, hatutaki kuwa na nchi yenye vichuguu. Kwa hiyo tunaomba, Wizara inafanya kazi nzuri lakini haijaweza kudhibiti ujenzi holela kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala pia, la *National Housing*. Nishukuru kwamba, wanafanya kazi nzuri, tatizo kubwa ni jukumu la Serikali kuhakikisha wananchi wake wanapata makazi bora. *National Housing* inafanya kazi kwa niaba ya Serikali, ni kwa nini Serikali haiwezi ku-subsidize nyumba za *National Housing* ili wananchi wa hali ya chini waweze kukaa na kuishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini *National Housing* inunue simenti bei ileile, mchanga bei ileile, vifaa vya ujenzi bei ileile utegemee wakauze nyumba rahisi? Haiwezekani! Pia, wanapeleka huduma za maji wenyewe, umeme wenyewe, miundombinu wenyewe. Serikali inatakiwa iweze kutoa baadhi ya vitu kupunguza gharama, nyumba za *National Housing* zinufaishe wananchi wote wenyе hali ya kawaida na wenyе hali ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasahivi nyumba za *National Housing* zinakaliwa na kununuliwa na watu wa hali ya juu, watu wa chini hawanufaiki kabisa. Kwa hiyo, hata ile maana ya kuwepo kwa *National Housing* yenyewe inakuwa haina tija kwa wananchi wa hali ya chini. Ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba *National Housing* inakuwa na nyumba nzuri, lakini za standard ambazo mwananchi ye yote yule anayetaka kumudu anaweza kumiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo, TANAPA inajitahidi inafanya kazi nzuri. Naomba Serikali ihakikishe inafungua, inaweka miundombinu kwenye maeneo ya hifadhi za Kusini, tuweze kufungua hifadhi za Kusini. Leo ukiangalia *Tanzania National Park* inajitahidi lakini ni upande mmoja wa Kaskazini. Huku maeneo ya Iringa kuna vivutio vizuri, Kitulo, Mbeya, maeneo mengi. Serikali ni wajibu wake iweke miundombinu kwenye *National Parks* nydingine zilizoko nje na Kaskazini ili tuweze kuwa na utalii nchi nzima. Vivutio viro, tatizo ni kwamba, maeneo hayo hayawezi kufikika kwa sababu hakuna miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo tatizo lingine. Tumekuwa tunazungumzia suala la concession fees kwenye *National Park*. *National Park* wame-introduce concession fees kwa maana ya tozo ya vitanda kwa hoteli ambazo ziko ndani ya hifadhi kwa miaka zaidi ya 10 sasa. Wanatumia zilezile za miaka 20 iliyopita, Dola tano mpaka Dola saba, wakati huo imewekwa hii tozo Dola tano mpaka Dola saba tulikuwa tunalipa kitanda Dola 150 mpaka Dola 200, leo kitanda kimoja *National Parks* ni Dola 500 mpaka Dola 1,000 lakini tozo iko palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba, Bodi haikuwepo, sasa Bodi imeshateuliwa tayari, naiomba Serikali mapema iwezekanavyo tozo mpya za *National Parks* ziweze kuwa introduced ili *National Park* ipate fedha za kutosha kuboresha miundombinu, lakini pia kuweza kusimamia utalii ndani ya hifadhi zetu za TANAPA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la Loliondo. Tumeona migogoro mingi ndani ya Loliondo. Naiomba Serikali; kwa taarifa ambazo tumezipata ni kwamba, sehemu ambayo inagombaniwa mpaka Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Mrisho Gambo wametofautiana yeye na Mheshimiwa Waziri ni eneo la chanzo cha maji. Katika eneo lile wanaokuja kufuga kule ni watu wa kutoka nje ya nchi, wameleta mifugo kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba kwenye masuala ya uhifadhi na hasa kulinda vyanzo vya maji tusiweke siasa.

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe tu taarifa anayezungumza kwamba, eneo linalozungumzwa Loliondo ni eneo la Vijiji vya Loliondo na si eneo la hifadhi na wala hakuna kilimo Ngorongoro kinachoendelea. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya, Taarifa hiyo!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia juu ya vyanzo vya maji. Nimesema eneo linalogombaniwa ni eneo ambalo linaonekana lina chanzo cha maji. Suala la kuwepo kwa chanzo cha maji haliangalii hifadhi au si hifadhi, ni chanzo cha maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mingi tumeshuhudia mifugo Loliondo inakufa wakati wa ukame kwa sababu maji yanakosekana. Leo hata wale wa Loliondo wenyewe wakishindwa kutunza vyanzo vyao vya maji wakati wa ukame mifugo itakufa tu. Kwa hiyo, nasema kwamba, tuangalie *interest* ya Taifa lakini pia, *interest* ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni chanzo cha maji kilindwe...

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** ...iwe nje ya hifadhi iwe ndani ya hifadhi!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hebu kaa chini, *please!*

Endelea Mheshimiwa Sakaya. Na muda wako Mheshimiwa Sakaya, umekwisha.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha?

**MWENYEKITI:** Mda wako umekwisha eeh!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Kiwelu, halafu ajiandae Mheshimiwa Lucy Owenya dakika tano na Mheshimiwa Haonga, dakika tano.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa niunge mkono taarifa zote mbili zilizowasilishwa na Wenyeviti wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kutoa mchango wangu ningependa kuiambia Serikali, Bunge huwa linakutana hapa kuitisha bajeti ya Wizara na huwa wanatuambia wameweka *cealing* kwa hiyo, tunafuata *cealing* waliyotupa, lakini toka taarifa hizi zimeanza kuwasilishwa hapa ndani ya Bunge, hakuna Kamati hata moja ambayo imesema kuna Wizara ambayo imepata fedha zote walizozihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niiombe Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba, Bunge likishapitisha bajeti ihakikishe bajeti inafika kwa wakati kwenye zile Wizara, ili ile mipango iliyopangwa kwa ajili ya hizo Wizara iweze kutekelezeka, bila hivyo tutakuwa tunapiga kelele tu na kazi hazifanyiki. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la migogoro ya wakulima na wafugaji. Tumekuwa tukiona katika vyombo vya habari kwamba wakulima na wafugaji wamekuwa wakigombana kila siku. Ningependa kujua ile Kamati iliyoundwa ya pamoja ya kutatua migogoro imefikia wapi? Amesema msemajii aliyejita, tungetaka kujua wamefikia wapi ili kupunguza mauaji ya wakulima na wafugaji ambayo yanaendelea kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni ya wakulima, wafugaji na wafanyakazi, haipendezi kuona wakulima wetu au wafugaji wakiendelea kuuana kila siku. Ifike wakati sasa Serikali ije na mpango madhubuti wa kutuonesha kwamba wanamalizaje tatizo hili la wafugaji na wakulima. Ili liishe ni lazima tuwe na matumizi bora ya ardhi na ndiyo maana nimeanza kwa kusema kwamba, ni lazima Wizara hii ya ardhi iweze kupatiwa pesa kwa wakati, iweze kupima na kuondoa migogoro hii. Tukiweza kupima na kuwapa wakulima maeneo yao na wafugaji, naamini kabisa tutakwenda kuondoa vifo vya wakulima na wafugaji kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisemee TANAPA. Niipongeze TANAPA imekuwa ikifanya kazi nzuri sana, lakini yapo matatizo yanayoendelea kujitokeza kwa maaskari wa TANAPA. Ni juzi tu hapa Mbunge alinyanyuka na kusema kwamba kuna mwananchi amepigwa risasi ya jicho na ikatokea kisogoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuwaomba ndugu zetu wa TANAPA na Wizara kwa ujumla wawe wanafanya utafiti ambao unaweza kujua kwamba askari wanaowaa jiri wanao uzalendo wa kweli; kwa sababu kila siku Wizara imekuwa tukikaa nao na wanasema wanatoa mafunzo lakini mafunzo haya naona bado hayasaidii. Ndugu zetu, watoto wetu wameendelea kuuawa na sisi hatupendi kuleta migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana TANAPA ichukulie suala hili kwa umakini sana na kufuatilia ili kuondoa tatizo la vifo kwenye mbuga zetu, mapori ya akiba na hifadhi. Naamini tukifanya hivyo tutakwenda kupunguza suala la vifo kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la njaa. Juzi tulikuwa tumekwenda Karatu kwenye msiba, kwa bahati nzuri tuliona mizoga ya ng'ombe, mbuzi katika makundi makubwa imetapakaa, imekufa. Sasa ningependa kujua Wizara husika inachukua tahadhari gani kunusuru mifugo hii?

Pia si kwa mifugo tu, hata kwa wananchi. Wameanza kufa ng'ombe, lakini itakuwa ni aibu kubwa sana Watanzania wakifa kwa njaa. Ilitolewa taarifa hapa na siamini kama iko sahihi kwa sababu, ma-DC na Wakuu wa Mikoa wamekuwa waoga sana kutoa taarifa sahihi. Ningependa Serikali ihakikishe kwamba, hakuna Mtanzania yejote atakayekufa kwa njaa katika kipindi hiki cha ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuzungumzia suala lililosemwa kwenye taarifa yetu; tulikutana na wasafirishaji wa nyama, wafanyabiashara wanaosafirisha wanyama-hai. Walitueleza matatizo yaliyowakumba, walipewa leseni lakini walisitishiwa biashara hiyo; na kibaya zaidi walipositishiwa tayari walikuwa wameshakamata wanyama kwa ajili ya kuwasafirisha. Sasa ningependa kujua ni sababu gani za msingi zilizosababisha watu hawa kusitishiwa biashara yao? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna taarifa zinazodai kwamba wako watu amba si Watanzania wamepewa vibali kwa ajili ya kusafirisha wanyama hawa. Ningependa kujua ni sababu gani za msingi zilizosababisha Watanzania hawa amba rasilimali hizi ziko ndani ya nchi yao, wao wananyimwa, lakini wanapewa wengine. Tungependa waziri anapokuja kujibu atuambie. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile suala nililokwa nalisemea la kuhusu migogoro ya mipaka; Serikali inachangia sana na hii inaonesha kwamba Wizara zile husika huwa hazitoi ushirikiano, hazishirikishani na hii ndiyo inayoleta shida, kwa sababu unakuta kimeanzishwa Kijiji, Kata, Wilaya au Mkoa lakini hawashirikishi hata haya Mashirika ya TANAPA pale wanapoweka ile mipaka kujua kwamba hili ni eneo la hifadhi. Kwa hiyo, ningeomba sana Wizara zile husika waweze kushirikisha mashirika yetu haya pale wanapokwenda kuanzisha either ni Kijiji au Kata kwenye yale maeneo ambayo yanazunguka hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini tukifanya hivi tutaendelea kuondoa malalamiko ya wananchi na nchi yetu itakuwa na amani. Hatuwezi kuona Watanzania wanaendelea kufa kila siku kwa sababu ya sisi tuliopewa nafasi tumeshindwa kuzitumia nafasi zetu kuwaweka waweze kuishi vizuri katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema Mwenyekiti katika taarifa yetu, utalii wetu bado hatujaweza kuutangaza vizuri. Tulibahatika sisi Kamati Bunge lililopita kutembelea Afrika Kusini tuliona wenzetu wanavyotumia utalii wa fukwe, lakini nchi yetu tumeshindwa kutumia fukwe tulizonazo na tunazo fukwe nzuri sana; lakini za kwetu ukipita ni harufu tu, utasikia harufu zinazonuka huko tumeshindwa kuzitumia vizuri. Niiombe sasa Wizara itumie utalii wa fukwe lakini pia na yale maeneo ambayo kwenye kamati tumeonesha tuweze kuyatangaza vizuri na kupata watalii wa kutosha. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo maeneo mengi sana ya utalii, lakini kama nchi tumeshindwa kutumia na wale wenzetu wa kusini wanayo maeneo na tumeomba kabisa kwamba ile Bodi ya Utalii iweze kupata fedha za kutosha kuweza kutangaza maeneo yale ili tuweze kupata pato kubwa sana la fedha za kigeni kutoka nje kama mataifa mengine ambayo wameweza kupata kupitia maeneo ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Owenya dakika tano ukimaliza Mheshimiwa Haonga dakika tano.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba ku-declare kwamba mimi ni mdau wa utalii na nitaanza na suala zima la hali ya utalii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyotambua, utalii ni kati ya sekta ambayo inachangia katika pato la Taifa kwa asilimia 17.5, lakini nasikitika na naona kwamba asilimia hizi zitapungua. Mheshimiwa Waziri wakati akijibu hoja tulivyokuwa tunachangia Kamati ya Bajeti alisema ongezeko la VAT halikuathiri wageni kuja nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mdau; wageni wengi waliokuja mwaka jana; VAT tulipitisha hapa Bungeni mwezi wa Sita na Sheria ikaanza kutumika mwezi wa Saba; watalii wanatoka nchi mbalimbali wengi walikuwa wameshaanza kusafiri kuja nchini Tanzania, kwa hiyo walikuwa wamesha-book package zao. Kwa vyovvye vile mgeni anakuja mpaka hapa Tanzania amefika unamwambia kwenye package yako na kuongeza eighteen percent hawakubali. Sasa badala yake wale local tour operators ndio waliolipia zile fedha za zaidi na badala ya kuwasaidia Watanzania mmezidi kuwaumiza. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa ili tuweze kupata figure halisia baada ya mwaka huu tujue ni watalii wangapi wamekuja. Kwa mfano compare Januari mwaka jana na Januari mwaka huu tuone ni watalii wangapi wamefika. Mimi nipo kwenye sekta hii na Januari mwaka huu sasa hivi mahotelii ni matupu hakuna wageni, tuijilize ni kwa nini hakuna wageni? Kule kilimanjaro huwa tuna-run Kilimanjaro marathon; Kilimanjaro marathon ni international inaleta wageni wengi sana hapa Tanzania. Baada ya kukimbia huwa wanapanda mlima, wanaenda safari na wanaenda kwenye beach tours; lakini mwaka huu wageni ni wachache, mahotelii bado hayajajaa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba muangalie ni kwa nini wageni hawa hawaji tena Tanzania wanaenda nchi jirani, wanaenda Mombasa. Tuna wanafunzi huwa wanakuja Tanzania kama volunteers wale wanafunzi *they are about sixteen to eighteen years old*, wanakuja, wazazi wao wanajitolea, wanakuja kwa *three weeks holiday*; wazazi wanajitolea, wanachangisha fedha wanakuja wanasadida kwenye kujenga mashule kupaka rangi na kadhalika, lakini hapa Tanzania tumekuwa tukiwachaji work permit ya dola mia tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke wale wanafunzi wakija wanalipa visa fee ya Dola hamsini, bado wakikaa hapa kwa wiki mbili wanapanda mlima, wanaenda safari na wanaenda mpaka Zanzibar. Sasa wazazi wao wamejitolea kuja kutusaidia Watanzania lakini wanachajiwa dola mia mia tano kwa kuja kujitolea. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali mliangalie hili kwa sababu tunapoteza wageni wetu. Mwaka huu nilikuwa na wageni zaidi ya mia saba lakini wote wame-cancel wanaenda Mombasa, tutapata wageni karibu hamsini tu. Naomba Serikali iliangularie hili tujaribu kuondoa ile permit visa ya dola 500 *atleast mchaji reasonable price*, labda hata kama dola mia moja hivi itakuwa ni *fair*, lakini dola mia tano ni nyingi sana tukumbuke na wale ni wanafunzi na wale wazazi wanakuja kutusaidia sisi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunaamini michezo ni afya na kama Bunge la Tanzania ningefurahi sana tarehe 26 mwezi wa Pili kuwaalika Wabunge na nyie mje mkashiriki kwenye Kili Marathon; mnaweza mkakimbia zile kilomita tano kama sapoti kwa sababu zile ni *fun run* mnaweza mkatembea ama mkakimbia, lakini itakuwa na sisi kama Watanzania tumeonesha moyo katika haya mashindano ya Kimataifa ambayo watu wanatoka *all over the world* lakini sisi kama Watanzania na kama Bunge la Tanzania bado wengi wetu hatujaweza kwenda katika mashindano yale. (Makofii)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nichangie Kamati hii ya Kilimo, Mifugo na Maji na ninaomba ku-declare *interest* kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba kwa bahati mbaya sana tunadhani kwamba tunaweza kuwasaidia Watanzania angalau kuondokana na umaskini kupitia kilimo; jambo ambalo kwa kusema ule ukweli kwa haya yanayofanyika imekuwa ni vigumu sana na sidhani kama kweli *tupo serious*. Unaona leo kwenye ruzuku ya pembejeo za kilimo wamepeleka bilioni

20 kwenye bajeti, na bilioni 20 yenye hii, hizi fedha bado inaonekana hali ni mbaya na hizi fedha bilioni 20 haziwezi kuwatoshia wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti tulishapendekeza siku za nyuma kwamba ikiwezekana huu mfumo wa kuweka ruzuku kwenye pembejeo za kilimo, Serikali iachane nao kabisa kwa sababu hauwasaidii wakulima wetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukitaka kumsaidia mkulima ni mara mia ukapunguza kodi kwenye mbolea, kwa sababu kinachopandisha bei ya mbolea tunajua kabisa ni kodi; hii kodi ambayo ipo kwenye mbolea. Bahati nzuri hata Waziri amewahi kuzungumza kwamba kwenye mbolea kule kuna tatizo moja, kuna kitu kinaitwa udalali. Tukitaka kuwasaidia wakulima twendeni tukapunguze kodi kwenye mbolea na kwenye pembejeo nyingine ili wakulima wetu waipate dukani kwa bei ndogo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ajabu sana leo nchi kama Malawi inatumia Bandari ya Dar es Salaam na inapofikisha mbolea nchini kwake bei ni ndogo sana mfuko hata shilingi elfu 20 haufiki; unapokwenda Zambia vivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu tumewachezea vya kutosha na Mheshimiwa Waziri, naomba niwe muwazi kabisa, msema mkweli ni mpenzi wa Mungu, tutakapokuwa tunaenda kwenye Bunge la Bajeti kabisa kama mchezo tunaoenda nao ndio huu, nitashika Shilingi ya Mheshimiwa Waziri na nitaomba huko mbele ikiwezekana uweze kuachia Wizara hiyo kwa sababu naona kama ina changamoto nyingi sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ule ukweli kabisa hali jinsi ilivyo hata kwa wafugaji wetu; leo mifugo inakufa. Ukimuuliza Waziri hapa ndugu yangu mifugo iliyokufa; karibu nchi nzima mifugo inakufa kwa sababu ya ukame; hata takwimu hana. Hajui mifugo mingapi, ng'ombe wangapi wamekufa na mbuzi wangapi wamekufa. Sasa kwa hali kama hii, huu ni uzembe na udhaifu mkubwa sana kwa Wizara hii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wamekuwa wakijipendekeza wanazungumza na uongo hadi wanadanganya wanasema kwamba njaa hakuna kwa sababu Mtukufu Rais amesema njaa hakuna na wao wanafuata hivyo hivyo. Kwa hiyo, inapofika mahali Rais akisema hii ni nyekundu si nyeupe, Waziri nae anasema hii ni nyekundu kwa sababu Rais kazungumza, huko sio kuwasaidia Watanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwe muwazi kabisa nchi nyingine, kwa mfano nchi kama Kenya mifugo ikifa Serikali inaanua kwenda kufidia, inawapa wananchi angalau mifugo kidogo kwa ajili ya kufidia kidogo wananchi wasiingie hasara. Sasa nashauri ikiwezekana na sisi Serikali yetu tuweze kuiga

kwa majirani wa zetu hapa Kenya na nchi nyingine tuweze kuiga mfumo wanaoutumia. Mifugo inapokufa angalau tuweze kuwafidia kidogo wafugaji wetu, maana leo katika Taifa letu mifugo imekufa hatujui sasa ukame huu ukiendelea itakuwaje, maeneo mengine; hali ni mbaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya ziara maeneo mbalimbali, Kamati yetu tumekwenda Simanjiro na Kiteto, hali ni mbaya kweli kweli tunakutana na mifugo mingi, mizoga ng'ombe wamekufa njiani. Leo Serikali yetu kama haitachukua hatua za kuwafidia wale wafugaji hakika hali itakuwa ni mbaya zaidi kuliko wakati mwingine wowote ule katika Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme; kusema ule ukweli kabisa yapo maeneo mengine mengi tu ambayo bado Wizara hii ina matatizo. Alikuwa anaongea Mwigulu Nchemba hapa akiwa Waziri. Kuna matumaini fulani fulani hivi ambayo kidogo alitaka kuonesha. Anasema mbolea itapatikana madukani kama coca cola; Mheshimiwa Waziri amewasiliana na Mwigulu hiyo mbolea kama coca cola madukani ime... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante unachukua muda wa mtu mwingine. Mheshimiwa Edwin Sannda.

(Hapa Mheshimiwa Pascal H. Haonga alisika akiendelea kuongea licha ya muda wake kwisha)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kaa chini. Mheshimiwa Edwin Sannda, ajiandae Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mheshimiwa Manase Njeza, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile na tunaweza tukam-chipin Mheshimiwa Zitto.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Kwanza kabisa nipende kuchukua fursa hii kuzipongeza Kamati zote mbili kwa taarifa na mapendekezo yao na pia nianze kwa kusema naunga maoni na mapendekezo yote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nichukue fursa kuzungumzia machache. Kwa upande wa Kamati ya Maliasili napenda kwanza kushauri kutolewe na zitengwe fedha kwa ajili ya kutoa elimu ili watu wafahamu umuhimu na faida za uhifadhi kati ya mipaka ya mapori ya akiba, mapori tengefu na maeneo ya makazi. Watu wamekuwa hawaelewi umuhimu wa hili jambo; ndio maana unakuta watu wanavamia, mifugo mara nyingine inakwenda inaingia ndani ya hifadhi, kunakuwa na vurumai sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufuatalia hakuna fedha hata kidogo zinazotengwa za kutoa elimu kuitia Wizara na hizi Mamlaka za Uhifadhi; sasa wanawezaje kuendesha hiyo kampeni ya kuelimisha wananchi? Matokeo yake wanakwenda na nguvu tu, wakati mwingi wanatumia nguvu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kwenye Jimbo langu Kondoa kufanya zoezi hili na likafanikiwa kwa kiwango kikubwa, watu wameanza kuelewa kutii sheria bila shuruti, kwa maana ya kutokuingia kule ndani, lakini pia taasisi hizi zinazohusika na uhifadhi ni lazima ziwe na fungu la kufanya zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwetu kuna pori la akiba la Swagaswaga na lipo Mkungunero na watu lazima waelewe namna ya ku-co-exist, tusipo co-exist na wananchi wakajua kuna faida gani ya haya mapori, wakazona na wakanufaika nayo ina maana itakuwa vurumai inaendelea tu. Kwa hiyo, nataka kusisitiza Wizara lazima kutengwe fungu hawa watu waweze kuelimishwa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hiyo hiyo namba mbili, askari wa wanyamapori; kweli wana jukumu la uhifadhi, lakini ndugu zetu hawa kwa kuwa wamekuwa wanahifadhi wanyamapori wamekuwa na wenyewe kama wanyama, wanaua hovyo. Wakati mwingine hata hakuna sababu ya kutumia nguvu kubwa hiyo, lakini wanakutana na mtu labda tena wakati mwingine; mimi nina kesi mwezi wa 12 hapa, alikuwa ameonekana kijana ana pikipiki amebeba kifurushi cha sukari guru, kinavuja vuja hivi wao wakadhani ni nyama ya pori labda ni swala. Walimfuatalia wao wana gari lao *land cruiser* yule kijana ana pikipiki wamekwenda kumuua kwenye kijiji wala si kwenye hifadhi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana mmoja, hana silaha hana lolote, anaendesha pikipiki yake of course na yeye alikimbia maana wale askari wa hifadhi wakionekana watu wanapata hofu; akawa anakimbia na pikipiki yake wale jamaa wamemkimbiza wamefika hatua kijana asiye na silaha anapigwa risasi sita. Sasa hata kama angekuwa ni Thomson Gazelle ameuwawa pale si furushi la sukari guru kweli hukumu yake ilistahili kupigwa risasi zote zile? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na mamlaka, hizi taasisi hebu tuwafundishe hawa askari wetu wawe na ubinadamu kidogo. Halafu baada ya kumuua wamemchukua wakamkimbizia porini ili waje kudai kwamba mtu huyu ameuwawa ndani ya hifadhi; mtu kauwawa kijijini. Wakachukua na furushi lake la sukari guru na pikipiki wakaingia nayo ndani kwenda kupotosha ushahidi. Kumekuwa na taratibu hiyo mara nyingi sana kwa sababu askari kwa askari taarifa ikiripotiwa wanalindana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuona dalili zile, bahati nzuri nilifika kwenye tukio mapema sana, nimshukuru sana Mheshimiwa Mwigulu nilizungumza naye nikamwambia nina wasiwasi hapa kuna dalili za kupotosha

ushahidi, watu wameingiza maiti ndani. Wewe umeua mtu si unamuacha kwenye *crime scene*? Tena ni askari una ujuzi, unaondoa kwenye *crime scene* unapeleka porini ili ukamsingizie. Basi akaweka jitihada ule utaratibu ukafuatwa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuwa ni askari saba mpaka sasa hivi wamekamatwa askari watatu tu wako ndani *including* wawili waliopiga risasi; mmoja ali-shoot risasi mbili na mwagine risasi nne. Imeenda kupasua mapafu na moyo mpaka kijana wa watu akapoteza maisha namna hiyo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuwafundishe askari wetu; Mheshimiwa Waziri na viongozi wote huko; hawa jamaa wawe na ubinadamu. Kuwa wahifadhi wa wanyampori haina maana nao ni wanyama. Nataka kupendelekeza, tukio lile lilitangazwa na likawa kubwa sana kwenye vyombo vyahabari, basi hata hawa maaskari watakapohukumiwa nalo lijulikane ili wananchi wapate imani na Serikali yao kwa sababu wanaona watu wanawekwa ndani kwa muda tu halafu wanapotea. Mtu aliyeua namna hii stahili yake ni hukumu ya kunyongwa mpaka kufa, umeua makusudi, si bahati mbaya. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nisisitze sana Wizara iliangalie hili kwa kina sana na limetokea, Mkungunero; miaka ya nyuma wakati wa tokomeza tuliona haya yamekuwa kwa wingi sana. Kwa hiyo, nisisitze Wizara ilililie mkazo na kuwafunda wale askari, si wanyama wale. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kuzungumzia uimarishwaji wa ile mipaka kati ya mapori tengefu, mapori ya akiba, hifadhi na maeneo ya wananchi. Ndugu zangu siku vile vikosi kazi vinapokwenda kuweka ile mipaka ishirikishe wananchi. Kwa sababu unaweza ukasema ushirikishe wananchi baadaye migogoro inaendelea miaka nenda rudi. Wawe sehemu ya uwekaji wa mipaka ile. Idara za ardhi katika Halmashauri zetu zishiriki, wanakwenda na GPS wanaona mipaka na wanajiridhisha hii ndio iliyoandikwa na ndio tunayoijua. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu vinginevyo malalamiko yanaendelea, aaa, mpaka ulikuwa hapa, sasa wameusogeza mbele. Sasa tutaendekeza malalamiko ya namna hii kwa muda gani? Kuna ugumu gani Wizara na hizi mamlaka za hifadhi kuwashirikisha wananchi na idara za Halmashauri zikaenda na vifaa; na document zao wanazo basi utaratibu unakuwa *clear*. Hilo nalisitisiza sana ili tuweze kupunguza hii migogoro isyokwisha kati ya hifadhi na maeneo ya makazi na kilimo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kwa ufupi sana kuhusu kilimo; jamani tutazungumza sana kilimo na uchumi wa viwanda. Hiki kilimo kama

hatutakiwekea bajeti kubwa kabisa ya kutosha kwenye upande wa umwagiliaji tutakuwa tunapiga story tu. (Makof)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mgimwa, Mheshimiwa Njeza ajiandae.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote napenda kuwapongeza Wenyeviti wote waliowasilisha leo mada zao hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa majukumu makubwa ya Bunge letu Tukufu ni kuishauri na kuisimamia Serikali, lakini kumekuwa kuna tatizo hapa. Tutazungumza, tutasema, lakini hayo tutakayokuwa tumeyazungumza na kuyasema na kuwashauri wenzetu wa Serikali watakuwa hawayafanyii kazi kama siku za nyuma. Kwa mfano, katika bajeti iliyopita sisi Waheshimiwa Wabunge wote kwa kauli moja tulishauri tuongeze tozo ya maji kutoka sh. 50 kwenda kwenye sh.100 na Wabunge wanajua matatizo yaliyopo kwenye majimbo yao. Cha kusikitisha kabisa Serikali iilikataa hili jambo na hela ambayo inafanya kazi sasa hivi ni hela ya Mfuko wa Maji, hela iliyokuwa kwenye bajeti kuu haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu ili hoja ambayo tulikuja nayo kwenye bajeti tuendelee nayo na yawe ndio maazimio ya Bunge ili hiyo sh. 50 iongezwe ili kwenye bajeti ya safari hii tusiime maneno; kwamba tozo ya maji imetoka kwenye sh.50 kwenda kwenye sh.100 ili tuendelee kupata maji katika maeneo yetu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninalopenda kushauri katika Wizara hii ya Maji ni suala la mita; tuwe na mfumo wa prepaid kama ilivyokuwa umeme, kwa sababu mionganoni mwa watu wanashindwa kulipa maji kwa wakati matokeo yake Sekta hii ya Maji inashindwa kuijendesha. Kwa masikitiko makubwa taasisi nyingi za Serikali zimeshindwa kulipa na ndizo zilizoweka mzigo mkubwa sana kwenye taasisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sekta hii kutengeneza hifadhi, kuchimba mabwawa ya kutosha ili maji yawe ya uhakika kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la kilimo. Asilimia 67 mpaka 72 ya Watanzania ni wakulima na Serikali imesema kwamba inataka kwenda kwenye uchumi wa viwanda, tutaendaje kwenye uchumi wa viwanda kama hatujawekeza vya kutosha kwenye eneo la kilimo? Tuna matatizo kwenye eneo

la pembejeo, naiomba Serikali katika eneo la pembejeo tuangalie kwa nafasi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma tulikuwa tuna eneo kubwa la kutoa ruzuku katika eneo hili, lakini cha kusikitisha ruzuku inayotoka safari hii ni ndogo kuliko iliyokuwa siku za nyuma, mfuko wa ruzuku katika eneo hili umepungua. Kwa hiyo, waongeze mfuko wa ruzuku tofauti na uliokuwepo miaka iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, Serikali imekuwa hailipis pesa za mawakala, kwa hiyo wametengeneza gap kubwa kati ya mawakala na wakulima wetu waliokuwa kijijini. Serikali inadaiwa zaidi ya bilioni 64, huu mwaka wa tatu na baadhi ya mawakala wameuziwa nyumba zao na baadhi ya mawakala wamekufa kutohata na shock walizokuwa nazohatika maeneo. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ijiangalie na iwalipe hawa mawakala kusudi waweze kufanya kazi zao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye eneo la ukame. Hapa kwenye eneo la ukame kuna tatizo. Naishauri Serikali ipeleke mbegu ambazo zinahimili ukame katika maeneo husika, lakini vilevile katika yale maeneo ambayo kwenye ripoti yetu tumeyasoma leo, zile halmasauri 55 ambazo zina matatizo ya chakula tunaiomba Serikali ipeleke chakula haraka iwezekanavyo. Kwa sababu tunaweza tukashindwa kupeleka chakula kwa wakati tukasababisha *inflation*, chakula kitakuwa kiko juu kwa sababu ya *demand pull inflation* katika maeneo yale, kwa hiyo hata ule mfumuko wa bei tunaouzungumzia kwamba tunaweza tukau-control, tatizo la chakula likiendelea kuwepo katika maeneo husika automatically *inflation* itaongezeka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa tunaiomba Serikali iondoe kodi kwenye mbegu zinazozalishwa hapa nchini. Unakuta mbegu zinazotoka nje ya nchi hazina kodi lakini mbegu zinazozalishwa na Watanzania zina kodi. Haya ni masikitiko makubwa sana, waziondoe hizo kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaombwa Serikali iongeze mtaji kwenye Benki ya Kilimo, mtaji uliopo sasa hivi hautoshi. Kwa hiyo, wakulima wetu hata kama wanataka kufanya kazi kwa ajili ya kuisaidia hiyo sekta ya viwanda ambayo inataka kuja hatuwezi kupata kwa sababu benki katika sekta hii haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kidogo kuhusu ranchi. Tuna tatizo, kuna baadhi ya ranchi zilichukuliwa na watu binafsi na zinaendelea kumilikiwa na watu binafsi. Hatuna sababu ya zile ranchi kuendelea kumilikiwa na watu binafsi ikiwa hawazitumii kwa yale makusudi tuliyoyakusudia; matokeo yake mifugo mingi inazurura kwenye hifadhi za Taifa na kuleta kero ambazo

hazina sababu. Kwa hiyo wale watu ambao wanatumia ranchi zile ambazo hazina sababu ya kutumiwa wanyang'anywe zirudishwe Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ninalotaka kuzungumzia kidogo ni suala la maliasili. Nataka kuzungumzia suala la VAT kwenye maliasili. VAT inapokuwepo automatically unaongeza gharama za utalii, kwa hiyo Serikali yetu badala ya kupata mapato tunayostahili kupata, hatuwezi kupata mapato yale kwa wakati, kwa hiyo Serikali iliangularie upya suala la VAT. Wenzetu wa Kenya tulikwenda nao kwa kauli moja, lakini ilipofika wakati wa utekelezaji Wakenya wakaji-withdraw kwenye hili jambo wakatuacha tukakaa peke yetu, kwa hiyo utalii wa hapa nchini ukawa gharama zaidi kuliko wa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu. Miundobinu ya utalii katika nchi yetu ni dhaifu, kwa hiyo tunatakiwa tuijangalie kwenye hili eneo, tuboreshe miundombinu katika maeneo ya utalii na tujenge nyumba za bei rahisi kwenye hifadhi zetu ili watu wa kawaida waweze kwenda kutalii. Kwa hiyo kuna haja ya kutunza utalii wa ndani katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi. Maafisa wengi wa ardhi, hasa maafisa wa mipango miji wamekuwa wana matatizo makubwa sana katika maeneo yao, hawafanyi kazi zao ipasavyo matokeo yake watu wanaendelea katika ujenzi holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. Naomba yale maazimio yote ambayo yametolewa na Kamati zilizohusika tuyapigie kura na yaweze kutekelezwa na Serikali. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Manase Njeza, ajiandae Dkt. Ndugulile na Mheshimiwa Zitto.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adimu ya kuchangia hizi Kamati mbili muhimu; Kamati ya Ardhi na Kamati ya Kilimo. Kamati zote mbili zimewasilisha ripoti nzuri sana na maoni yao ni mazuri sana na naiomba sana Serikali ichukue haya maoni na mapendekezo kwa uzito kulingana na umuhimu wa ardhi ya nchi yetu pamoja na kilimo kwa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na suala la mipango miji. Sheria ya Ardhi ya Mipangomiji na Vijiji ni nzuri sana, lakini ukiangalia mipangilio yetu ya miji toka 2007 ilipotoka hiyo sheria kwa kweli inasikitisha sana. Napendekeza; kwa uzito wake wa mipangomiji sasa hivi hakuna miundombinu kwenye miji yetu, hakuna barabara, hakuna sehemu ya kuitisha mabomba; hilo lingezingatiwa na kuhakikisha namna ya kuzishirikisha taasisi binafsi na National Housing wakafanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kuwa tunakuwa na mipangomiji mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri nilionao ni kwenye Mji Mdogo wa Mbalizi. Pale Mji mdogo wa Mbalizi kulikuwa na watu 2,000 miaka 10 iliyopita lakini sasa hivi kuna watu wanaokaribia 150,000; lakini ukienda pale ni squatters tu hakuna mitaa. Kwa watu hao 150,000 hata miundombinu ya maji ni ile iliyokuwepo kwa ajili ya watu 2,000. Sasa hii inatuonesha ni namna gani tuko nyuma katika kupanga miji yetu. Wananchi wetu wanataka hizi huduma na sisi tunaiomba Serikali iangalie jinsi ya kuwasaidia wananchi. Sasa hivi vijiji vingi vinageuga kuwa miji, badala ya watu kujenga kiholela Serikali iwe ya kwanza kuhakikisha kuwa inapanga hayo maeneo na yanapimwa kwanza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mbalizi kuna ekari zaidi ya 6,000 za iliyokuwa *Tanganyika Peckers* miaka zaidi ya 50 iliyopita, kile kiwanda hakikuanza kufanya kazi, hizo ekari 6,000 zote hazijafanyiwa chochote na halmashauri na wananchi wote wa Mbeya DC waliamua kuwa waombe hili eneo ili liweze kupimwa liwe makazi ya watu, wautengeneze mji bora ambao utaonesha kioo cha Mbeya kwa sababu hilo eneo ndilo eneo ambalo liko karibu na uwanja wa ndege, ndilo eneo ambalo unatoka katika nchi jirani za Zambia mpaka Afrika Kusini unapoingia Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wananchi wameomba hilo eneo ili wapewe kuwe na mpangomji na Sheria Namba Nane kama sijakosea inasema uwekezaji wa mashamba kwa mijini usizidi eka tatu. Kwa hiyo hiyo eka 6,000 kwa kuwekwa mjini kwa ajili ya malisho ya ng'ombe nafikiri tutakuwa tunachechesha. Uzuri wake halmashauri imetenga eneo mbadala kwa sababu nao wanahitaji hiki kiwanda cha nyama na vilevile wanahitaji maboresho kuhakikisha kuwa tunafuga mifugo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walichokifanya halmashauri, wamejenga wao machinjio ya kisasa kwa ajili ya soko la ndani na soko la nje. Kwa hiyo, eneo mbadala limepatikana na Serikali itakapopata mwekezaji eneo tunalo tayari. Sisi tunachoomba, hili eneo ambalo liko mjini iachiwe Halmashauri ya Mji wa Mbalizi ili tutengeneze makazi ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi shule zetu za msingi na sekondari zina idadi ya wanafunzi kubwa mno na hatuwezi kupanua shule, wanafunzi wakifaulu darasa la saba wanakwenda sekondari za mbali ambazo wanatembea zaidi ya kilometra 10, sidhani katika hali ya sasa hivi kama hayo yanakubalika. Kwa hiyo, tunaomba sana huu ushauri Serikali iuchukue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeona kwamba ardhi yetu pamoja na kuwa tajiri wanaofaidi ni wageni. Nilipotembelea *National Housing* na kamati yangu pale *Tanganyika Peckers*, Kawe, tuliambiwa kuwa ile ardhi mwekezaji alinunua kwa bilioni sita kwa ajili ya kiwanda, hakujenga, hakuendeleza.

National Housing walipokwenda pale kutaka wapate lile eneo mwekezaji akakataa, alipotaka kununua kakataa, akakubali kwamba waingie joint venture, kwa bilioni sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Investment* iliyoko pale sasa hivi ni mabilioni kama sio trillioni. Sasa jaribu kufikiria mtu mgeni unampa utajiri wa namna hii kwa mali yetu, hajafanya chochote. Sasa hilo lisijirudie katika maeneo mengine ya iliyokuwa Tanganyika Peckers. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo; mimi ni mkulima. Ili umsaidie mkulima unahitaji uwekezaji kwanza, unahitaji umpe mtaji, unahitaji utaalami, unahitaji masoko. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wamelichangia hili kwa umakini mkubwa sana, lakini angalia, mtaji utapata wapi? Benki ya wakulima leo hii haina mtaji, bilioni 60 ilizokuwa nazo imewekeza karibu bilioni tatu tu, sasa wakulima nani atawasaidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye wataalam wataalam wenye hatuwaoni wakija kwenye mashamba yetu. Mimi nikiwa kama mkulima sanasana wageni wangu wanaonitembelea kutoka Serikalini ni OSHA na...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, jiandae Mheshimiwa Zitto.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia, na kama itakupendeza ntaomba dakika zangu mbili nimpatie Mheshimiwa Zitto Kabwe aweze kuendelea nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa uwasilishaji wa taarifa nzuri ambayo imesheheni mambo makubwa ya msingi. Nitajielekeza moja kwa moja katika suala la Mji mpya wa Kigamboni. Katika ukurasa wa sita wa taarifa hii Kamati hii ya Bunge ilitembelea Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni na naomba ninukuu walichokisema:-

“Kamati ilifanya ziara katika Ofisi ya Wakala wa Uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni tarehe 18 Machi, 2016 na kupokea taarifa kuhusu maendeleo ya mradi. Kamati haikuridhishwa na hatua ya Serikali katika utekelezaji wa mradi huu na hadi wakati Kamati inapokea taarifa za utekelezaji wa miradi hakukuwa na fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya uendelezaji wa mradi ikiwa ni pamoja na kulipa fidia katika maeneo yatakayojengwa miundombinu.

Kutokana na hali hii hakukuwa na mradi wowote ulioonekana kuanzishwa na hivyo kupoteza maana halisi ya kuwa na mradi na uanzishwaji wa Wakala. Hali hii imesababisha Serikali kupoteza fedha za kulipia pango za wakala na kuwa na watendaji ambao hawana majukumu ya kutekeleza. Kamati inashauri Serikali iachane na mradi huu kwa kuwa umechukua muda mrefu bila kuwa na utekelezaji wowote.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono hoja hii, ni mwaka wa tisa tangu Serikali itoe azimio la kujenga Mji wa Kigamboni. Hadi hivi sasa wananchi wa Kigamboni hawawezi wakajenga wala wakauza ardhi yao wala kuiendeleza, inawaleta umaskini mkubwa sana. Nami naunga mkono ripoti ya Kamati. Katika mwaka wa jana wa fedha Serikali haikutoa hata senti tano na wala hivi tunavyoongea hakuna hata senti tano ya fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa jana niliitisha mikutano ya wadau wa Kigamboni, Wenyeviti wangu wote wa Serikali za Mtaa, Madiwani na Baraza la Madiwani wa Manispaa ya Temeke kabla halijavunjwa na tukatoka na azimio kwamba moja, KDA ivunjwe na mamlaka yake yakabidhiwe katika Halmashauri mpya ya Kigamboni.

Pili, suala zima la uendelezaji wa Kigamboni sasa kwa kuwa Kigamboni sasa hivi ni wilaya inayojitegemea, ni halmashauri inayojitegemea, ina Idara ya Mipango Miji ambayo ina sifa na vigezo vyta kusimamia uendelezaji wa Kigamboni; muda wa miaka tisa umetosha sasa tunaomba sisi kama Wanakigamboni tuivunje KDA na shughuli zote zikabidhiwe katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaliomba sasa Waheshimiwa Wabunge hili nalo, pamoja na kwamba mmelitoa kwenye preamble, naomba liingie kama azimio ili sasa Serikali itoe msukumo zaidi, pamoja na mapendekozo ambayo tumeyaleta sisi kama Wanakigamboni hili sasa liwe ni azimio la Bunge ili sasa baada ya hapo Serikali iweze kutekeleza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi ya kusema, naomba niishie hapo. Nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Zitto, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dokta Ndugulile asisahau amendment ili tuweze kufanya hiyo amendment jioni kwa ajili ya kusaidia watu wa Kigamboni. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina mambo matatu tu, mawili ni ya jimboni kwangu na moja ni la Kitaifa. Jambo la kwanza ni kuhusiana na mradi wa maji Kigoma. Tulikuwa tuna mradi wa maji ambao una thamani ya Dola za Kimarekani milioni 16 ambao ungeweza kutatua tatizo la maji la Manispaa ya Kigoma-Ujiji kwa asilimia mia moja na mradi ule ulikuwa uishe mwezi Machi, 2015. Bahati mbaya mpaka sasa mradi ule bado haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la mwezi Februari, 2016 niliuliza swali hapa Bungeni na Wizara kupitia kwa Naibu Waziri wakasema kwamba mradi huu utakwisha mwezi Oktoba, 2016. Baadaye Mheshimiwa Waziri akafanya ziara katika Mkoa wa Kigoma na akatembelea mradi huu na akawa ametuahidi kwamba mradi huu utakamilika mwezi Desemba, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu Bungeni mwezi Mei mwaka jana niliitahadharisha Serikali kwamba, mkandarasi aliyepewa kazi hii ya ujenzi wa mradi huu tayari amefilisika na anatumia fedha ambazo tunamlipa kulipia madeni yake katika maeneo mengine ambako anadaiwa; kwenye miradi mbalimbali duniani, lakini Serikali ikasema kwamba italishughulikia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana, mwezi Januari mwaka huu Mkuu wa Mkoa wa Kigoma ametangaza rasmi kwamba mkandarasi huyu amefilisika. Imeleta taharuki kubwa kwa wananchi wa Manispaa ya Kigoma-Ujiji na hawaelewi sasa nini hatma ya mradi huu tena. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kutoa maelezo ya kina katika majibu yake kuhusiana na suala hili, kwa sababu ni mradi muhimu sana ni mradi ambao tumeuhangaikia, ni mradi ambao fedha za wafadhili zimetoka zaidi ya Shilingi bilioni 32 na tunashindwa kuelewa ni kwa nini Serikali haijachukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia mkandarasi huyu hana mradi Kigoma peke yake, ana mradi pia Musoma na mradi huo pia na wenyewe unasuasua. Kwa hiyo, Waziri atakapokuwa analieleza hili, si kwa maslahi ya Kigoma peke yake, pia aangalie namna gani ambavyo tunaweza tukapambana na wakandarasi wa namna hii ambao wanachukua miradi hawaimalizi na kusababishia wananchi kero nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la umwagiliaji. Mwaka jana nilizungumza kwenye Bajeti ya Wizara ya Kilimo na vile vile nilizungumza kwa maandishi kwenye Bajeti ya Wizara ya Maji na pia nilizungumza na Waziri mwenyewe na Waziri alikuja Kigoma na akatembelea Mradi wa Umwagiliaji wa mto Rwigwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 5 Juni, 2015, Katibu Mkoo wa Wizara ya Mambo ya Nje alimuandikia barua Katibu Mkoo wa Wizara ya Kilimo na Chakula wakati ule kuhusiana na mradi wa umwagiliaji wa mpunga katika bonde la Mto Rwigwe. Barua ile ilikuwa na kumbukumbu namba CHC.325/395/01/42 ambapo Katibu Mkoo aliisaini na kuagiza jambo hili liweze kufanyiwa kazi. Katika barua ile Katibu Mkoo wa Wizara wa Mambo ya Nje aliambatisha barua kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Quwait (Quwait Development Fund), barua ile ilikuwa ni ya tarehe 24 Mei, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichopaswa kufanywa upande wetu sisi ni kufanya *detailed feasibility study* ya mradi huu ili mradi huu uweze kufadhiliwa na Quwait Development Fund na hivyo tuweze kuwa na mradi mkubwa sana wa umwagiliaji na kuzalisha zao la mpunga katika Manispaa ya Kigoma katika bonde la mto Rwigwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa na nilikuwa naangalia bajeti hapa ya Tume ya Umwagiliaji nimeona kwamba pamoja na kwamba tulipitisha bajeti ya Shilingi bilioni sita katika bajeti ya mwaka huu, fedha ambazo zimeshapelekwa Tume ya umwagiliaji ni asilimia 13 tu ya fedha ambazo zilitakiwa na sasa hivi tumeshafikia nusu ya mwaka wa fedha wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo ya Serikali na jambo hili linahusu Wizara tatu. Linahusu Wizara ya umwagiliaji, Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara ya Fedha, kwa sababu Quwait Fund wana-desk pale Wizara ya Fedha. Tuweze kupata suluhisho la jambo hili kwa sababu mradi huu ni mradi mkubwa sana na ni mradi ambao unaweza ukatatua tatizo la chakula katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu sasa hivi nchi yetu inakabiliwa na baa la njaa, chakula ni kichache hakitoshi, kwa hiyo, ni muhimu sana kuwa na miradi mingi ya umwagiliaji na mradi mmoja muhimu sana ni huu mradi wa bonde la Mto Rwigwe. Nitakachokifanya kwa mara nyingine nitampatia Waziri barua zote hizi ili aweze kushauriana na Mawaziri wenzake; Waziri wa Fedha na Waziri wa Mambo ya Nje tuweze kupata suluhisho la jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni la Kitaifa. Kamati ya Kilimo imependekeza kwamba tuongeze Sh. 100 kwenye bei ya mafuta ili tuweze kupata fedha za kutosha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Maji. Sipishani kabisa wala sibishani na Kamati juu ya suala zima la kuongeza uwezo wa Mfuko wa Maendeleo ya Maji ili kuweza kutatua tatizo la maji kwa sabaabu ndilo tatizo kubwa ambalo wananchi wetu wanalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu tu ni kwamba lazima tuwe aware kwamba kwa wiki tatu zilizopita bei ya mafuta kwenye soko la dunia imeongezeka kwa asimia 30. Kwa hiyo maamuzi yoyote ambayo tunayafanya, tuangalie namna gani ambayo tusipeleke mzigo kwa wananchi wa kawaida. Hata hivyo, tunalo suluhisho katika jambo hili, miaka takribani 10 iliyopita tulipitisha Sheria kwa ajili ya kutoa fedha kwenda REA, fedha kwenye mafuta ya taa, mafuta ya diesel na mafuta ya petrol.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiwango kikubwa sasa hivi, REA imefanikisha malengo yake ya kuweza kufikisha umeme vijiji. Kwa hiyo tunachoweza kukifanya kwenye Sheria ya Fedha; na ningeomba tufanye marekebisho kidogo kwenye mapendekezo haya; ni kupunguza Sh. 50 kutoka kwenye fedha ambazo zinakwenda REA kutoka Sh. 100 mpaka Sh. 50 na tupunguze Sh. 100 kwenye fedha za mafuta ya taa zinazokwenda REA, fedha hizi sasa tuzipeleke kwenye maji. Kwa maana hiyo ni kwamba tutakuwa tumebakiza gharama za mafuta zitakuwa ni vile vile na sekta ya maji itakuwa imepata fedha za kutosha kwa ajili ya kuweza kutatua tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kuweza kufanya hivi kwa sababu baadaye tunaweza tukajikuta tumesababisha mfumuko mkubwa wa bei bila kufanya mambo haya kwa uangalifu ambao unatakiwa. Kwa hiyo, naomba tu watu wa Kamati ya Maji, sipingi hoja yao, naiunga mkono lakini tuirekebishe kwa namna ambayo itaweza kuondoa mzigo wa....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto muda wako umekwisha. Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa, japokuwa nilidhani kwamba ningeweza kuchangia mchana lakini nakushukuru sana inawezekana mchana kutakuwa na wachangiaji walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia katika Taarifa zote za Kamati kama ambavyo zimewasilishwa na Wenyeviti. Kwa masikitiko makubwa sana, taarifa hii ya Kamati ya Mifugo na Maji iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu, ukurasa wa 12 unazungumzia mgogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitishwa sana na taarifa hii ya Kamati ambayo kwa namna moja au nyingine wameshindwa kabisa kuona kwamba mgogoro kati ya wakulima na wafugaji ni mgogoro mkubwa ambao unahitaji Serikali kuingilia kati kwa haraka. Nimesikitishwa sana kwa sababu ukisoma

taarifa hii, mgogoro kati ya wakulima na wafugaji umeandikwa nusu page, kwa kweli ni masikitiko yangu makubwa na hiki ni kilio cha wakulima wote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina maana kwamba hatuwapendi wafugaji, tunawapenda sana wafugaji, lakini kwa namna ambavyo Serikali imeshindwa kutatua migogoro kati ya wakulima na wafugaji na ndiyo maana nasimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu na mara zote ambapo nasimama tunaona kabisa hatari kubwa; ile amani tuliyoachiwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere inakwenda kupotea kwa sababu tu ya mgogoro huu kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelisema hili kwa muda mrefu sana na hata Waheshimiwa Mawaziri wanafahamu hilo. Mgogoro huu kati yetu, sisi Rufiji kule, hatuna mgogoro wa ardhi naomba Bunge lako Tukufu litambue, Rufiji hatuna mgogoro wa ardhi; tulichonacho ni *criminal trespass*, mwingiliano wa jinai ambaao unafanywa na wafugaji katika maeneo ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili ni kubwa na mwezi wa 11 watu wawili wameuawa, mkulima alichinjwa na mfugaji alichomwa moto akiwa hai katika maeneo ya Kilimani. Cha kushangaza sana hakuna kiongozi yeote wa Serikali au Wizara aliyefika katika maeneo husika ili kuweza kutoa pole na kuweza kuongea ili kuondoa mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni masikitiko yangu makubwa sana na Wanarufiji wote leo hii wananiangalia kwenye TV, nimesimama mbele hapa; si Tanzania tu, dunia nzima Wandengereko wote dunia nzima na Warufiji wote wanajua; mgogoro kati ya wakulima na wafugaji unapaswa utatuliwe haraka sana vinginevyo unakwenda kuligawa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mambo mazuri ambayo alituachia Rais wetu wa Awamu ya Kwanza, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ya kupendana Watanzania tunaona kabisa kwamba tunaanza kubaguana. Mimi nasema wazi mbele ya Bunge lako Tukufu, mgogoro huu unakuwa mgumu kwa sababu viongozi wa Wizara hii wengi ni wafugaji na wanashindwa kutatua matatizo ya wakulima. Naomba niihie hapo, *message sent and delivered* kama ambavyo Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni tatizo kubwa la RUBADA. Tunayo hii Mamlaka ya RUBADA, Mamlaka ya kuendeleza Bonde la Mto Rufiji. RUBADA ilianzishwa mwaka 1978. Dhamira ya uanzishwaji wa RUBADA ilikuwa ni kuendeleza bonde pamoja na Mto Rufiji, lakini tunasikitika sana Warufiji baada ya Mamlaka hii kukabidhiwa Bonde la Mto Rufiji basi wananchi wa Rufiji wamekuwa maskini wa hali ya juu. RUBADA imeshindwa kuwasaidia Warufiji

Iakini pia RUBADA imeshindwa kuwasaidia wananchi wote wanaoishi na wanaopitiwa katika Bonde la Mto Rufiji kuanzia Morogoro na maeneo mengine yote ya Tanzania yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge liazimie sasa kuivunja RUBADA mara moja na Mamlaka yote ambayo inamiliikiwa na RUBADA ibaki chini ya Halmashauri husika ikiwa ni pamoja na vijiji. Tunaamini kabisa Warufiji tukikabidhiwa bonde letu la Mto Rufiji tutaweza kuwatafuta wawekezaji watakaosaidia kilimo cha umwagiliaji. Naomba katika maazimio liingie azimio la kuifuta RUBADA, haina maslahi yoyote na hawana uwezo wa kuwasaidia Watanzania wanaoishi maeneo ya Rufiji zaidi ya kufanya udalali ambao hata sisi wenyewe tunaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikumbushie jambo lingine la mwisho, ni kuhusu ujenzi wa nyumba zinazojengwa na *National housing*. Tukiangalia dhamira ya Mwalimu Nyerere, mimi ni mjamaa kweli kweli! Tukiangalia azimio la Mheshimiwa Rais wetu wa kwanza, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, uanzishwaji wa *National Housing* ulilenga kuwasaidia Watanzania wanyonge, Watanzania wadogo wasio na uwezo, wafanyakazi wa Serikali, Iakini leo hii *National Housing* ipo kwa ajili ya matajiri tu. Hakuna Mtumishi wa Serikali wala Mtanzania mnyonge mwenye uwezo wa kwenda kupanga kwenye nyumba za *National Housing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliombe Bunge lako Tukufu, ile dhamira ya uanzishwaji wa *National Housing* kama ambavyo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Kwanza alivyoanzisha, kuchukua nyumba za Mabepari na kumilikiwa na Serikali. Dhamira ile ilikuwa ni kwenda kuwasaidia Watanzania wanyonge pamoja na Watumishi wa Serikali, naomba Bunge lako pia liazimie, *National Housing* iweze kuchunguzwa na kuangaliwa sasa ni namna gani itaweza kuwasaidia Watanzania walio wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe maazimio haya yaingie na niombe Mwenyekiti wa Kamati atakaposimama hapa aweze kujibu hoja hizi kama ambavyo nimeweza kuzieleza. Mgogoro wa wakulima na wafugaji unahitaji kuingiliwa kwa haraka sana na Serikali ili uweze kutatuliwa. Ni jambo la aibu sana kwa Kamati kuandika nusu page mogogoro wa wakulima na wafugaji. Watanzania wanauawa, Watanzania wanauana, wamepoteza dhamira ya kupendana wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ile miiko ya Mwalimu Nyerere aliyoianzisha wakati ule wa kupigania uhuru na hata baada ya uhuru. Tunaomba Kamati iweze kujuliza ni kwa nini wamefikia hatua hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma vizuri ukurasa wa 13 unasema kwamba viongozi wa Serikali ambao wanashiriki katika kutatua migogoro hii hawakuwashirikisha wafugaji. Hili ni jambo la aibu kabisa. Ni wakulima wangapi wameshirikishwa katika mgogoro huu? Hili ni jambo la aibu, lakini tunafahamu kwamba kwa sababu wakulima hawana pa kusemea, lakini sisi kama viongozi wao tunasimama hapa kwa ajili ya kuwatetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wapiga kura walio wengi; lakini tunatambua kwamba katika pato la Taifa, kilimo kinachangia asilimia zaidi ya 70. Tuiombe Serikali itambue hilo. Pia hata Wizara ukiiangalia namna ambavyo inatupuuza wakulima. Ukiangalia katika bajeti iliyopita, Wilaya yetu ya Rufiji ambayo tuna ekari zaidi ya 13,000 ambapo kuna bonde zuri kwa ajili ya kilimo tungeweza kuuza Tanzania, Afrika Mashariki na Afrika ya Kati, lakini Wizara ya Kilimo imetenga sifuri kwenye bajeti yake ya kilimo kusaidia wananchi wa Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusaidia kilimo tunaamini kwamba hata hiyo Tanzania ya viwanda hatutafikia huko. Naomba kuwasilisha lakini naomba; katika maazimio niliyoyaomba ni pamoja na kuifuta RUBADA kwa sababu haina faida yoyote kwa Watanzania. RUBADA wamekuwa madalali na sisi hawatusaidii lolote. Tunaomba bonde libaki chini ya wananchi wanaomiliki bonde hilo na maeneo ya mto ili tuweze kuwatafuta watu watakaoweza kutusaidia katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha mchana, nina tangazo moja. Ratiba ya semina ya leo; tukitoka hapa tunaanza na ratiba ya chakula kwa Wabunge wote na semina itaanza saa 7.30.

Wachangiaji wetu wa jioni tutaanza na Mheshimiwa Katani, Mheshimiwa Shekilindi, Mheshimiwa Bilakwate, Mheshimiwa Boniface Mwita, Mheshimiwa Jackline Msongozi.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

(Saa 6.56 Mchana Bunge *lilisitishwa hadi saa 10.00 Jioni*)

(Saa 10.00 Jioni Bunge *lilirudia*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

**NDG. ASIA P. MINJA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji na

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii

(Majadiliano yanaendelea)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Katani asubuhi, yeye ndiyo mchangiaji wetu wa mwanzo.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana lakini pia niombe nitumie dakika saba ili dakika tatu atumie ndugu yangu Hamidu Hassan Bobali. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Wizara hii ya Kilimo, kwanza nianze na suala la mfumo wa stakabadhi ghalani ambao umetumika kwenye korosho. Kwa namna moja au nyingine tumeona kabisa kwamba kwa wakulima wa korosho mfumo huu umewasaidia sana. Naishauri Serikali na Wizara kwamba mfumo huu usiwe kwenye korosho tu, kwa sababu Mikoa ya Kusini tunalima ufuta, mbaazi na mazao mengine. Sasa kwa sababu mfumo huu kwenye korosho umekuwa bora sana ingependeza sasa mfumo huu uelekezwe pia kwenye mazao mengine kama ufuta, mbaazi na mazao mengine kama tumbaku ili uweze kuwanufaisha na Watanzania wengine. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na jambo kwenye korosho linaitwa *export levy*, ushuru huu ni ushuru mkubwa sana. Kwenye korosho Serikali inachukua asilimia 15 ya *market price*, lakini kwenye maelekezo wakati wanaunda mfuko ule wa kuendeleza zao la korosho katika mambo ambayo wameyasahau sana sikuona pesa zinatengwa kwa ajili ya kuwanufaisha wakulima wa korosho kwenye suala la elimu. Leo kama kungekuwa na mkakati mzuri kwenye suala la elimu, ilivyotokea wanafunzi wa vyuo vikuu wamekosa mikopo na kwenye korosho kuna pesa asilimia 15 za *export levy* zingeweza kusaidia Mikoa ya Lindi na Mtwara kuongeza wadahiliwa wale wanaokwenda vyuo vikuu kwa kupata pesa za kutosha zinazotokana na hii *export levy*. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto nyingine kwenye Vyama vya Msingi vya Ushirika ambavyo vinachukua shilingi 60 kwa kila kilo moja kama ushuru wao. Pesa zile hazina maelekezo. Sasa ningemuomba Waziri kwa sababu jamii zetu zina matatizo mengi sana, wakati anatoa maelekezo yake aweke mkakati kwenye pesa za Vyama vya Msingi tuone zinaweza kusaidia jamii kwenye mambo ya msingi, leo tunakaa kuhangaika kutafuta pesa

shilingi 10,000 kwa ajili ya CHF, wakati kwa mfano Mkoa wa Mtwara tuna Vyama vya Msingi ambavyo vinakusanya mamilioni ya pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano chama kimoja cha kwangu KITAMA kina uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi milioni 80,000 pesa ambazo ukienda kwenye mkutano mkuu wa chama cha msingi watu wanagawana shilingi 5,000 au 10,000 ambazo hazimsaidii chochote mkulima wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mapendekezo yangu kwa Wizara na kwa Waziri mwenye dhamana, aone ni namna gani pesa zile za Vyama vya Msingi za ushuru, inachukuliwa angalau kiasi fulani cha pesa zinawekezwa kwenye mambo ambayo yanaweza kusaidia jamii mfano hiyo CHF au la, hata wale watoto wanaofaulu kidato cha tano na kwenda cha sita kama wanakosa ada basi ielekezwe kwamba kila Chama cha Msingi cha Ushirika angalau kisomeshe watoto watano kuwapeleka *form five* na *six*. Ingesaidia sana, badala ya pesa hizi kuendelea kutumika kwa malengo ambayo siyo ya msingi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulikaa hapa tukawa tumezungumza jambo la stock exchange, jambo hili Mheshimiwa Waziri nilidhani kwenye majaribio haya tusiyafanye kwenye korosho tu kwanza. Mfumo wenyewe wa stakabadhi ghalani Mheshimiwa Waziri kama utakumbuka umeanza mwaka 2007 tumekuja kutekeleza mfumo wa stakabadhi ghalani 2016/2017 mwaka huu ambao wewe ndiyo Waziri! Maana yake miaka iliyopita yote mfumo wa stakabadhi ghalani haujatekelezwa Mkoa wa Lindi na Mtwara na maeneo mengine yote. Wakulima walikuwa wanaendelea kwa kutumia Vyama vya Msingi, kukopa pesa benki wakawa wanalipa pesa nyingi ambazo mpaka leo ukienda Tandahimba kule kuna vyama vinadai pesa nyingi kwa sababu ya mfumo ule mbovu ambao hatukuutekeleza kama tunavyoenda sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu tumeanza mwaka huu kuutekeleza mfumo wa stakabadhi ghalani hii stock exchange naomba Mheshimiwa Waziri tuendelee kwanza na mfumo huu, tuwe tumejifunza vya kutosha angalau miaka mitatu, minne, tukijiridhisha kwamba tunakwenda vizuri ndiyo twende kwenye mifumo hii ya kisasa ambayo inahitaji capacity kubwa ya uelewa mkubwa, tofauti na watu wetu wa Mtwara. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie sasa kwenye Wizara ya Ardhi. Alizungumzia Kaka yangu Mchengerwa pale. Nilipata fursa kukaa na wakulima pamoja na wafugaji. Suala linalozungumzwa na Mheshimiwa Mchengerwa pale lile la Rufiji ni jambo zito sana. Waziri wa Ardhi aangalie namna ya pekee sana na Wizara nyingine muone namna gani jambo hili la migogoro ya wafugaji na wakulima mnawenza mkalimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwigulu akiwa Waziri wa Kilimo kipindi kifupi kile alianza michakato ya kuona migogoro hii inaishaje. Sasa siyo vibaya Mheshimiwa Waziri ukamfuata Mheshimiwa Mwigulu ukaangalia mikakati ambayo alikuwa anaiweka badala ya kila Waziri anaekuja anakuja na mkakati mpya, na mambo mapya mkayasahau hata yale mazuri ambayo wengine walanza kuyafikiria. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuomba Mheshimiwa Waziri kwenye jambo hili la Vyama vya Ushirika ambalo nilizungumza mwanzo uliangalie kwa mapana sana. Tuna madeni ya wakulima ambao wanadai pesa za korosho za mwaka 2012/2013 na mwaka 2013/2014 na hii kwa Wabunge ambao ni wawakilishi wa wanachi hatuna neno jema kwao ambalo tunaweza tukawaijibu. Tumeshadanganya sana na ikiwezekana urudi mwenyewe uje Jimboni kwangu Tandahimba kuna wakulima wanadai pesa zao za mwaka 2012/2013, mwaka 2014/2015 mpaka leo hawajui hatma ya pesa zao zinapatikana namna gani. Kwa hiyo, niombe sana wakati wa majumuisho uone jambo hili unaliwekaje ili tuwe na majibu hata tunaporudi majimboni tuseme tulifikisha kwa Serikali na Serikali imetujibu moja, mbili, tatu, nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Katani. Tunaendelea na Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze mambo mawili tu kwa kuwa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji nataka nichangie kwenye maeneo mawili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la Mfuko wa Maji, nashukuru Waziri wa Fedha yupo, fedha pekee ambazo Wizara hii inapata ni fedha za Mfuko wa Maji peke yake. Ukiacha fedha za Mfuko wa Maji, Wizara ya Maji haipati fedha za maendeleo ya miradi ya maji kutoka Serikalini. Kwa hiyo, tunaomba ufanuzi na tunaomba suala hili Waziri wa Fedha alieleze Bunge hili kwa nini fedha za maendeleo ambazo tulizipitisha kwenye Bunge hili la Bajeti haziendi kwenye Wizara ya Maji ukiacha na fedha za Mfuko wa Maji ambazo ni shilingi 50, tunachangia huko tunaponunua mafuta.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; suala la Bandari ya Uvuvi. Tangu Bunge la Kumi, Wabunge hapa walikuwa wanapiga kelele suala la Bandari ya Uvuvi, tunapoteza fedha nyingi sana katika nchi hii kwa kukosa Bandari ya Uvuvi, nimesikitika sana. Nimestaajabu kuona Wajapani wametoa fedha kujenga Bandari ya Uvuvi eti inakwenda kujengwa Chato!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Uvubi ikajengwe Chato wakati tuna maeneo kwenye Bahari Kuu tunapoteza fedha nyingi wavuvi wanakuja kuvua wanashindwa kutua Tanzania kwa sababu hatuna Bandari ya Uvubi. Kwa nini Bandari ya Uvubi msifikirie kuipeleka Mtwara, kwa nini msifikirie kuipeleka Tanga, kwa nini msifikirie Bagamoyo, Bandari ya Uvubi ukaweke Chato kwa samaki gani walioko Chato ili tukajenge bandari kubwa ya uvubi na kwa kiwango gani cha fedha ambazo tunapoteza kwenye Ziwa Victoria? Kwa nini tusifikirie kujenga Bandari ya Uvubi kwenye Bahari ya Hindi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu hili suala kwa kweli linatia doa Serikali yenu. Bandari ya Uvubi imekuwa ikidaiwa sana humu ndani na tunapoteza fedha nyingi kwenye Bahari Kuu, kwa sababu ya kukosa Bandari ya Uvubi, leo Bandari ya Uvubi inaenda kujengwa Chato, fedha waliyotoa Wajapani ni jambo la hatari na ni jambo ambalo kwa kweli linafedhehesha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nataka nizungumzie ni suala la migogoro ya wakulima na wafugaji. Mheshimiwa Mchengerwa amezungumza hapa na mimi ni Mjumbe wa Kamati. Kwa kweli mwenyewe pia sikufurahishwa sana na taarifa tulioiandika kuileta hapa juu ya migogoro ya wakulima na wafugaji. Migogoro hii haipungui, inaongezeka. Mheshimiwa Waziri, tunahitaji migogoro ya wakulima na wafugaji ipungue, badala ya kila siku inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina makakati gani wa kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji ili suala hili liwe historia? Vifo vinaongezeka, migogoro inaongezeka, hata maeneo yale ambayo kulikuwa hakuna migogoro ya wakulima na wafugaji kama Lindi hivi sasa na kwenyewe kumeshaanza kuwa plotted ni maeneo ya migogoro. Tunaomba Wizara iwe serious, mnapoamua kumaliza changamoto za wakulima na wafugaji...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bobali. Tunaendelea na Mheshimiwa Shabani Shekilindi. Waheshimiwa, wachangiaji ni wengi sana kutohana na umuhimu na uzito wa hoja ambayo tunayo mbele yetu. Sasa hatuwezi kusema mchangie dakika tano itabidi kutengua Kanuni. Isipokuwa kwa vile upendo ni pamoa, muambizane kila anayechangia amuombe mwenzie dakika tano ili na yeye aweze kuchangia, mkikubaliana wenyewe. Kila mtu amwombe mwenzie atampa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita Mheshimiwa Shekilindi, ajiandae Mheshimiwa Bilakwate, Mheshimiwa Boniphace Getere na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ajiandae. Sasa katika hawa wanaochangia wale ambao wanaomba kudandia basi mmalizane huko huko. (Kicheko)

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati wote wawili kwa kuwasilisha hoja zao vizuri. Pia ni-declare *interest* kwamba na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu tulitembelea mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Mji Mpya Kigamboni, lakini mradi ule haujatengewa hata shilingi tano. Sasa basi niishauri Serikali ili jengo lile lisiendelee kulipa kodi wala wafanyakazi basi nadhani mradi ule urudishwe sasa kwenye Halmashauri ya Kigamboni. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulitembelea mradi wa utafiti wa nyumba bora na vifaa vya ujenzi. Kwa kweli kama tuna nia ya dhati tuwezeshe wakala wale wa nyumba na vifaa vya ujenzi. Tulifika pale wataalam walikuwa hata sita hawafiki, lakini vitu wanavyofanya ni vitu vikubwa sana. Sasa niishauri Serikali yangu kwamba wataalam wale wapewe uwezo ili waongezeka, waende mpaka Wilayani, naamini kabisa kwamba wataalam wale wakiongezeka na wakifika Wilayani vijana wetu watapata ajira. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefika pale wanatengeneza vigae na tofali. Vigae vile wanatengeneza kwa nyuzi za katani, huoni sasa wataalam wale wakiwa wengi wataenda Wilayani mpaka vijiji na kwenda kufundisha vijana wetu wale na hao vijana wakishapata taaluma ile basi waende kwenye Halmashauri wajisajili ili kazi za Halmashauri zikitokea waanze kupewa kazi na kuanzakujenga majengo kama ya zahanati, maabara, shule na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mradi nimeuona ni mradi mzuri sana. Naamini kama kweli Serikali yetu tukufu ina nia ya dhati basi iwekeze kwenye mradi ule. Wakala wale ni wa kweli wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la migogoro ya ardhi. Migogoro ya ardhi ni kitu ambacho kimekithiri hapa nchini kwetu Tanzania. Sina imani kabisa kwamba migogoro hii inaweza kuisha kwa jinsi tunavyoenda sasa. Niishauri tu Serikali yangu kwamba kama tunataka migogoro hii iishe basi tuhakikishe kwamba tunaandaa utaratibu mzima wa maeneo yote ya hapa nchini yanapimwa na watu wanapata hati zao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuhakikishe kwamba watu wetu wa Wilayani hususan Maafisa Ardhi wanapewa zana na vifaa vya kutosha kuweza kupima ardhi hii kwa haraka. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Dada yangu Naibu Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Angeline Mabula wanafanya kazi moja nzuri sana kiasi

kwamba hatia Watanzania walio wengi wanaimani kubwa sana nao. Walitutangazia kwamba wameshafuta mashamba zaidi ya 200 lakini kuna shamba la mwekezaji mmoja kule Mnazi anaitwa *Renash Enterprises Plot No. 292, title deed 11,247 ekari 2,442; na title deed 1746 ekari 1,188; title deed 4144 yenye ekari 562.* (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza mwekezaji yule analima tu eneo hili tena eneo kidogo sana ambalo ni ekari 562. Eneo lote lililobaki amelitelekeza, ni vichaka, kuna mapori makubwa ambayo kwa kweli hayastahili kuwa pale wakati watu wana shida ya ardhi. Nimuombe Waziri wangu na Naibu Waziri wa Ardhi, *title* hizi zifutwe na mpaka sasa taratibu zilishafuatiliwa lakini naambiwa kwamba Ofisi ya Ardhi Kanda ya Kaskazini bado hati ile haijafutwa. Sasa nimuombe Waziri wangu atakapoamka ku-wind up basi aniambie kwamba hati ile itapatikana lini ili Halmashauri yangu iendele kupata mapato yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye kilimo, naishauri tu moja kwa moja Serikali ijenge mabwawa mengi ya kutosha hapa nchini kwa ajili ya wakulima waweze kulima kilimo cha kisasa na cha umwagiliaji. Pamoja na hayo, wapeleke pembejeo kwa wakati pia hakuna asiyefahamu kwamba Lushoto ni ya wakulima wa matunda na mboga mboga, wakulima wale wanachangia sana kwa kutoa ushuru mwangi Halmashauri, lakini Serikali sijawahi kusikia Serikali inatenga ruzuku za pembejeo kuwapa wakulima wale wa matunda na mboga mboga. Ninaishauri Serikali yangu kwamba iwatengenee wakulima wale wa mboga mboga na matunda nao waweze kupata ruzuku ya pembejeo.(Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la maji. Kama inavyofahamika maji ni janga la Kitaifa basi nashauri kwa kuwa *EWURA* wanatoza pesa kuitia nishati hii ya mafuta, niiombe sasa *EWURA* itenye asilimia 50 kwa ajili ya kupeleka maji vijijini.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Shaban Shekilindi. Tunaendelea na Mheshimiwa Bilakwate ajiandae Mheshimiwa Boniphace.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza napongeza Kamati zote kwa taarifa ambazo wamezileta. Kabla sijaanza kuchangia naiomba Serikali, tunakuja hapa tunachangia maeneo mengi, tunashauri lakini unakuta vitu vingi tunavyoshauri mara nydingi havichukuliwi maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tunakuja hapa tunatumia kodi ya wananchi ambao tunawawakilisha, naiomba sana

Serikali muwe wasikivu tunapotoa ushauri muuzingatie, haiwezekani tunapiga kelele hapa halafu mwisho wa siku hakuna kinachofanyiwa kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mazao ya biashara. Ukisoma kwenye taarifa ya Kamati katika ukurasa wa 13 inaeleza katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni mazao haya yamekuwa na uzalishaji usioridhisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo pamoja na ufanisi mdogo wa vyama vyaa ushirika na matumizi duni ya teknolojia ya pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesahau haya mazao yamekuwa yanaendelea kupotea na wakulima wamekata tamaa. Wakulima wanakata tamaa kwa sababu Mheshimiwa Rais mwenyewe wakati wa kampeni na baada ya kupata nafasi ya Urais amekuwa akizungumzia sana hizi tozo na kodi ambazo mmeweka. Wakulima wamefika sehemu wanakata tamaa. Mimi nitoe mfano Mkoa wa Kagera, haya mazao kwa mfano zao kuu la kahawa siyo Mkoa wa Kagera tu, zao kwa kweli watu hawaoni faida yoyote ya kuliendeleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali na nimuombe Waziri wa Fedha na Waziri wa Kilimo, kabla hatujaingia kwenye bajeti na sisi Mkao wa Kagera tumetoa azimio na ninaomba Mikoa mingine mtuunge mkono hatutakuwa tayari kuunga mkono bajeti kama hamtaondoa hizi tozo na kodi ambazo zimebekwa. Tunataka wakulima hawa wafaidi. Hili ninaomba Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono. Haiwezekani mkulima analima hapati faida yoyote, ni lazima tujenge mazingira mazuri hata mkulima anapolima aweze kupata faida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni maji. Kama wengine walivyochangia kwa kweli suala la maji ni tatizo na janga kubwa la Kitaifa. Tuliishauri hapa Serikali tukasema iongeze tozo lakini Serikali ikakataa ikaja na sababu, leo hakuna Mbunge ambaye anaweza akasimama akasema kwenye Jimbo lake kuna pesa ya maji ambayo imipelekwa angalau hata asilimia 30. Mimi ninaomba Serikali tunaposhauri muwe mnazingatia. Ninajua mna nia njema lakini kuna mambo mengine lazima muwe mnatusikiliza na sisi tunaposhauri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tukasimama tukaitetea Serikali wakati Serikali hampeleki pesa, kwenye Majimbo yetu wananchi wanateseka hali ni ngumu. Tunahitaji maji, Mheshimiwa Waziri wa Maji, Kyerwa wananchi wamenituma maji sitakutetea hapa usiponiletea maji, na kuna miradi ambayo tayari tumeshaibuni iko kwenye usanifu, hiyo miradi inahitaji pesa. Kuna miradi mingine ambayo ipo ya miaka ya mingi, hii miradi ipo tu wananchi wanakuuliza tunakosa hata majibu. Kwa hiyo, niombe Serikali izingatie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niongelee migogoro ya ardhi. Kuna migogoro ya ardhi maeneo mengi. Kwa kweli kwa hapa nimpongeze Waziri kwa kazi wanayoifanya, lakini bado kazi ni kubwa na migogoro hii ni mikubwa, isije ikatokea sasa mauaji yanatokea kila kona. Mimi niwaombe kwa mfano kule Kyerwa kuna eneo ambalo lilishatengwa na Serikali ikatangaza kuwa hili eneo ni la wafugaji. Lakini eneo hili linaloitwa Sina limevamiwa na watu, wengine hawakufuata hata taratibu wameingia wameweka fence ni kama Serikali haioni. Haiwezekani wanaweka hivi vitu Serikali inaona na inajua hili eneo ilishalitenga kwa ajili ya shughuli fulani. Mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri wa Ardhi uje Kyerwa utatue huu mgogoro uishe, tujue nani ana haki ya kuwa kwenye hili eneo kihalali. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niiombe sana Serikali, mje hapa mtueleze Waheshimiwa Wabunge kwa nini mpaka sasa hamjapeleka pesa kwenye miradi ya maendeleo. Mlete sababu ambazo tutawaelewa kuliko kukaa kimya pesa haiendi na sisi hatujui kinachoendelea, hata wananchi wanapotuuliza, tunakosa jibu. Ni afadhali mkatueleza kama pesa haipo tujue pesa haipo hilo tukawaambie wananchi, kuliko tunakaa hapa tu kila mtu anazungumzia pesa ya maendeleo na hakuna kitu kinachoendelea. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali, ninajua nia ya Rais wetu na dhamira yake, kwa kweli tunamuunga mkono, lakini tunataka pesa. Hatuwezi tukaunga mkono tu kitu kinasemwa, kinasemwa halafu hatuoni kinachoendelea. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine niongelee uharibu wa mazingira. Mazingira yetu kwa kweli yameharibiwa sana. Na niombe sana Waheshimiwa Wabunge katika hili, tushirikiane wote kwa pamoja ili tuweze kunusuru mazingira yetu ambayo yameharibiwa. Vyanzo vya maji vimeingiliwa, wakulima wanaingia humo humo, milima na misitu yetu leo haipo tena, leo tunaongelea janga la kitaifa tunasema kuna njaa, kuna ukame. Ukame umesababishwa na sisi viongozi tukiwepo ni hatua zifi ambazo tumechukua ili kunusuru mazingira yetu yawe salama? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tufike wakati sasa siyo kulinda tena kura, wakati mwagine Waheshimiwa wanasiwa mnalinda nafasi zenu hamtaki kuingilia kwenye mambo ambayo ni ya msingi. Watu wanapoharibu mazingira unasema nikisema hapa nitajiharibia kura, unajiharibia wewe. Mwisho wa siku tunakuja kuomba chakula cha njaa, tuhakikishe tunaenda kwa wananchi wetu tuyalinde mazingira yetu ili mazingira yawe salama. Haya mambo ya kusema tunalinda kura wakati nchi inaharibika, tunakoelekeea ni kubaya. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge hili tupambane nalo kwa nguvu zetu zote kuhakikisha mazingira yetu tunayarudisha kwenye hali ambayo ni sawa, ili tupate mvua. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la mwisho watu wanatangaza janga la njaa, kweli njaa ipo lakini siyo kama...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bilakwate. Mheshimiwa Boniphace, ajiandae Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma message hapa samahani, inasema Mkuu wa Mkoa Maalum wa Bunge anajianda kutangaza majina ya watu wote ambao hawajawahi kufanyiwa tohara, samahani Mwenyekiti.

**WABUNGE FULANI:** Rudia.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kuna message inasema anajiandaa kutangaza watu wote ambao hawajawahi kufanyiwa tohara ambapo ujumbe ulikuwa umefika hapa wiki iliyopita... (Kicheko)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hoja iko mbele yako jaribu kujadili.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na hoja. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia uhaba wa chakula. Kwanza niwashukuru watoa hoja wote, Kamati ya Ardhi na Kamati ya Kilimo, wamezungumza vizuri kwenye vitabu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua tu kwa Mawaziri wanaohusika na Wizara hizi au wa Serikali sijawahi kuona kwamba kwa nini kila siku tunazungumza hivi vitu vinavyohusu mifugo, vinavyohusu ardhi kutopimwa na sina hakika kwamba hivi muda huu toka Wabunge wamekuja toka mwaka 1961, haya mambo ya kupima ardhi yalikuwa hayajzungumzwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba kwa Wabunge wenzangu mkitaka Bunge hili tulitendee haki tuondoeni maneno yanayohusu U-CHADEMA na U-CCM. Mkiondoa haya maneno haya mtajenga Bunge ambalo ni imara na litasimamia Serikali. Tukifika humu tumebakil kubishana tu, tunabishana upande huu mara mwingine azushie Magufuli maneno, mara sijui Rais amefanya nini hatutafika hiyo. Tuzungumze mambo yanayohusu wananchi tuwaaulize Serikali

kwa nini kila siku tunazungumza migogoro ya mifugo na haitatuliki. Kama hakuna majibu tuseme sasa itakuaje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kila siku tunakuja hapa maneno tu kama ngonjera tu, tukubaliane kwamba kama sisi ni wasimamizi wa Serikali, tuiulize Serikali kwa nini sasa mipango hii ya ardhi ambayo wakulima na wafugaji wanauana, kwa nini haifiki mwisho? Tutapata majibu siku hiyo. Kama haifiki mwisho hatuendi kwenye bajeti, tutapata majibu haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kwenye eneo langu la Bunda. Amekuja Waziri Mhagama, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Ndugu yangu hapa Ramo Makani, amekuja Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Ole-Nasha wamejionea hali halisi ya uharibufu ya wanyama tembo katika maeneo yangu, kata saba na Bunda Mjini. Wameona hali ilivyo, ikaahidiwa kwamba watapeleka chakula hakijaenda. Sasa nimeona humu wanaandika tupeleke mbegu bora, unaipanda wapi? Unapanda mbegu bora lakini tembo anaishi pale kila siku, wale Wazanzibar wanaita ndovu, anaishi pale pale kwenye shamba, tunapeleka mbegu bora ya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hao tembo au ndovu hawawezi kutoka kwenye Jimbo lile watu watalima lini? Nawashukuru siku hizi wanajitahidi wapeleke na magari, lakini tembo au ndovu zimewashinda kutoa. Wanaishi pale pale kila siku, wamepeleka tochi imeshindikana. Kwa hiyo, nafikiri kwamba ni vizuri Serikali ituambie kama mpango wa eneo langu, vijiji vya Unyali, Maliwanda, Kihumbu, Nyamang'unta, Tingirima, Mgeta na kule kwa neighbour wangu Mheshimiwa Ester Bulaya, vijiji vya Nyamatoke na Mihale, watuambie kama maeneo haya hayawezi kulimwa basi Serikali ijiandae kwenda kuwapa chakula cha bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo sasa hivi wamefika wakati sasa wanavunja maghala, wanachukua chakula wanakula, hawana uwezo sasa wakulima pale, ngombe hawaendi porini wanakamatwa, sasa tunafanyaje? Kwa hiyo, tunaiomba Serikali katika hili kuwa wepesi wa kupeleka chakula cha msaada au chakula cha bei nafuu wapeleke katika Kata Saba za Jimbo langu. Hali ni mbaya na Kata Tatu za Jimbo la Bunda Mjini. Hali ni mbaya sana kwenye maeneo haya, njaa ni shida.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimpa rafiki yangu, jirani yangu anaitwa Ryoba dakika tano uwe unanichunga kama zikizidi itakuwa mbaya zaidi. Kwa hiyo, niseme tu kitu kimoja...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace ulikuwa unampa nani dakika tano.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimempa Ryoba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa zimekwisha dakika tano zako, kaa chini please. Mheshimiwa Ryoba.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimshukuru jirani yangu Mwita Gatere, Mbunge wa Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la tembo. Tembo ni tatizo Mkoa wa Mara. Tembo ni tatizo Serengeti ni tatizo Bunda, ni tatizo Tarime. Nichukue nafasi hii kutangaza janga la tembo Serengeti, Tarime na Bunda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika sehemu tembo anaenda kutafuta chakula kwenye ghala, anabomoa ghala, juzi hapa, ameenda kwenye Kijiji cha Nyichoka, wakabomoa ghala wakala chakula isitoshe wananchi wakahamishia chakula ndani ya nyumba akaenda akabomoa nyumba akala chakula chote, wananchi wamebaki hawana chakula. Bahati nzuri amekuja Naibu Waziri, tumempeleka mpaka maeneo hayo amekuta nyumba zimebomolewa.(Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo anauwa wananchi kwa wingi sana sasa hivi, tembo amekuwa ni hatari sana kwenye ukanda wetu huo. Kama Serikali isipochukua hatua ni hatari kubwa mtasikia huko. Sasa hivi majambazi wanauwa tembo hawaendi kuwatafuta hifadhini wanakuja kuwavizia kwenye viji vya Serengeti nje kabisa. Juzi hapa nilimwambia Mheshimiwa Waziri wamekuja wakaua tembo sita katika kijiji cha Merenga, wakawapiga wakaua wakang'oa meno wakaenda. Kwa hiyo, sasa hivi majambazi hawasumbuki kwenda kutafuta tembo hifadhini maana tembo wanakuja huku kusambua wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Wizara ya Maliasili na Utalii chukua hatua ya ku-protect wananchi wa Serengeti, Bunda na Tarime dhidi ya tembo. Kama hamtafanya hivyo tembo wanaenda kuisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni WMA.WMA ni chombo cha wananchi, wananchi wameji-organize wakatoa maeneo ya wakaunda WMA. Leo Wizara ndiyo inakusanya mapato yanayotokana na WMA kwa nini? Kwa mfano, tumeenda Babati kwenye ile WMA ya Burunge Wizara inakusanya mapato, imekusanya shilingi bilioni sita inawapelekea milioni 800 for what? Unakusanya bilioni sita unarudisha milioni 800 itafanya nini? Kwa hiyo, mimi niiombe Serikali, suala la WMA ukusanyaji wa mapato, uendeshaji wa WMA waacie WMA wenyewe, waendeshe wenyewe, wakusanye mapato yao, wajileetee maendeleo wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linalotesa WMA ni *single entry*. Tunaomba Serikali ifanye utaratibu wa kurekebisha bila kurekebisha issue ya *single entry* WMA zitakufa. Kule kwangu Serengeti WMA ya Ikona sasa hivi mahoteli yaliyokuwa ndani ya hifadhi wawekezaji wameanza kuondoka, kwa sababu hakuna wageni. Serikali naomba mrekebishe hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mauaji, kwangu Serengeti wameuwawa watu 50 na askari wa wanyamapori, ninayo taarifa ambayo nimeandikiwa na Serikali za Vijiji, Watendaji wa Vijiji ambavyo viko kandokando mwa hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba orodha hii nitakuletea uone askari wa wanyamapori wanauwa Watanzania wenzao kisa amekanya ndani ya hifadhi anapigwa risasi anauawa. Mimi binafsi Ryoba nimeshuhudia wameuwa, hivi huu ndiyo utaratibu au ndiyo maana Magufuli ameweka Katibu Mkuu mwanajeshi, Mwenyekiti wa Bodi Waitara mwanajeshi ili kuwaa Watanzania wanaoingia hifadhini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu wameuwawa vijana 50, huu ndiyo utaratibu wa Tanzania kuua vijana wake? Ndiyo utaratibu wa Serikali ya CCM? Hebu ninaomba Serikali chukua hatua, kama hamtachukua hatua nitawashughulikia mwenyewe. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ryoba dakika zako zimeisha. Waheshimiwa Wabunge ninaomba mijielekeze kwenye hoja na wale Wabunge mnaoamua kupeana dakika tano mnieleze mapema. Mheshimiwa Msongozi, ajiandae Mheshimiwa Laizer.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi kukushuru kwanza kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Kamati ya Huduma ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, pamoja na Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kupongeza uchaguzi uliopita tarehe 22 Januari, 2017 ambapo Chama cha Mapinduzi kiliwafunga wapinzani wetu wana UKAWA goli 22 kwa moja.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline hebu kaa kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, hebu tuwe na ustaarabu. Ninyi ni wastaarabu na tunaomba muwe wastaarabu. Mbunge ana dakika zake naomba uvumilivi ndani ya Bunge, akienda nje ya hoja nitasema mimi siyo wewe, hiyo ndiyo kazi yangu hapa siyo wewe. Mheshimiwa Jacqueline endelea.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana unajua tunajuana humu ndani wapo wanaokula msupa asubuhi, mchana na jioni kwa hiyo hainipi shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye suala la kilimo kwa maana ya ubora.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Selasini kaeni chini, Mheshimiwa Jacqueline nenda kwenye hoja iliyoko mbele yako.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Afute kauli yake, msupa ndiyo nini?

**MWENYEKITI:** Nenda kwenye hoja iliopo mbele yako.

**MBUNGE FULANI:** Atuthibitishie wanaokula msupa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Afute....

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Halima unajua msupa wewe.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Msupa tuje tule wote.

**MBUNGE FULANI:** Eeh, athibitishe.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Afute kauli.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Halima msupa si unajua?

**MBUNGE FULANI:** Msupa si unaeleweka.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Atuambie maana ya msupa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima zima *microphone* yako please. Tutaanza kutajana majina sasa!

Waheshimiwa tutaanza kutajana na siyo jambo jema. Tuna hoja muhimu mbele yetu, kuna suala la ardhi, kuna suala la mifugo, suala la kilimo ambayo wote mnahitaji kurudi Majimboni na majibu ya Serikali!

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nawaomba kaeni kimya. Mheshimiwa Jacqueline, nenda kwenye hoja ambayo iko mbele yako.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatupo kwa ajili ya kutishana, kila mtu amekuja kivyake hapa.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba hiyo kazi wanayoifanya ndiyo iliyowaleta humu ndani na hawana kazi nyingine kama wangkuwa na kazi wangkuwa watulivu wasikilize nini kinachochangiwa sasa hivi.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline kaa chini.

Waheshimiwa Wabunge, *respect starts within*, msikilazimishe kiti kichukue hatua za kudharau mamlaka ya kiti, na mkianza kudharau mamlaka ya kiti ambako mnaelekeea huko adhabu yake ni mbaya. Mheshimiwa Jacqueline na wewe nakuambia jielekeze kwenye hoja iliyopo mbele yako. (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, afute kauli.

**MWENYEKITI:** Sitaruhusu kuanzishwa mjadala wowote zaidi ya hoja ambayo iko mbele yako, tulieni! Endelea Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Sindano zenyewe sijazitoa kelele zinaanza. Sasa niende kwenye suala la ubora wa mbegu...

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline kaa chini, Katibu andika jina la Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Halima Mdee na hawa Waheshimiwa wawili halafu nipe mimi majina hayo. Mheshimiwa Jacqueline endelea.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Kilimo wawe makini sana kwenye suala la ubora wa mbegu. Mbegu

zinazopelekwa kwa wakulima siyo mbegu sahihi, wakati mwingine mbegu zile huwa zinakuwa zina shida, hata kama ni mbegu ambazo zinatolewa kwa mtindo wa ruzuku lakini bado hazimsaidii mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukisema kwamba kunai le hali ya mimba za utotoni, kwenye mbegu hizi nyingine nazo ni staili ya mimba za utotoni. Kuhusu hizi mbegu unakuta wakati mwingine mbegu zinakuwa ni fupi haziwezi kuzalisha kadiri ambavyo inastahili, kwa hiyo Wizara ya Kilimo tunaomba muwe makini. Pia niseme endapo mbegu hizo zisizokuwa na ubora zinaletwa, mwisho wa siku mwananchi anapokuwa amepata hasara, hasara hii inafidiwa na nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee suala la mawakala wa pembejeo. Mawakala wa pembejeo hili ni jambo ambalo tumekuwa tukiliimba kila siku. Mawakala wa pembejeo ambao kimsingi walikopesha Serikali, walifanya kazi ya kusambaza mbolea na mbegu mbalimbali kwa ajili ya kuikopesha Serikali mwisho wa siku mawakala hawa mpaka leo hawajalipwa. Toka mwaka 2014, mwaka 2015, mwaka 2016, ni lini Serikali hii itawalipa hawa mawakala? Wamekuwa na shida na wengine mpaka sasahivi wameshapoteza maisha na wengine wanadaiwa na mabenki, walikuwa wazima wakati wanakopesha mbolea hizi kwa wananchi, sasa hivi unakuta tayari wameshanunua magonjwa kama pressure. Naiomba Serikali iwe serious ili kuwasaidia hawa wananchi wajasiriamali ambao waliweza kuikopesha Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende pia kwenye Benki ya Kilimo. Wakati tunapitisha bajeti hapa mwaka jana mwezi wa sita, bajeti ya kilimo, Waziri alikuwa amesema kwamba angeweza kufikisha Benki ya Kilimo katika Mkao wetu wa Ruvuma, lakini nashangaa mpaka sasa hivi bado haijafika, sijui ndiyo bado upembuzi yakinifu au ni nini? Mpaka sasa hivi hakuna dalili zozote zile za kufikisha benki hii ya kilimo! Niombe Waziri wa Kilimo tafadhali kwa kuwa mkao wa Ruvuma ni mkoa ambao wananchi wake wanashugulika na kilimo kwa asilimia 92, naomba sasa benki hii iende ili iweze kuwasaidia wananchi hawa waweze kukopa na kuweza kufanya uzalishaji wenyе tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uvuvi; tunalo Ziwa Nyasa katika Mkao wetu wa Ruvuma. Mimi naomba nishauri jambo hapa, uvuvi katika Ziwa Nyasa samaki walioko pale wangeweza kuwa wengi zaidi na uvuvi ule ukawa na tija endapo kama Serikali ingeweza kufanya kama wanavyofanya wenzetu wa Malawi, kwa sababu ziwa hilo moja liko upande Malawi na upande mwingine wa ziwa upo upande wa Wilaya ya Nyasa kwa maana ya Tanzania. Kwa hiyo, wenzetu wa Malawi wanachokifanya wanalisha chakula kwenye lile ziwa, samaki wanakwenda kwenye upande wa Malawi kwa sababu kuna chakula. Wenzetu wa Malawi sasa wanapata mavuno mengi kutokana na hili

Ziwa Nyasa. Sisi tunaambulia patupu, ziwa lipo tunaambulia kuangalia tu mandhari ya ziwa lilivyo lakini hatuna faida nalo yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ione umuhimu kama tuko serious na suala hili la uvuvi, basi walao tufanye huo utaratibu wa kuwa tunalisha chakula ili tuweze kupata samaki wazuri ambao tutawauza na watatupatia pato...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Jacqueline. Tunaendelea na Mheshimiwa Laizer.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu na nianze na migogoro kati ya watumiaji wengine pamoja na hifadhi zetu. Inawezekana tutapiga kelele kuhusu jambo hili, lakini tukubaliane tu kama Bunge kwamba Serikali inalea na inachangia sana mauaji na mapigano ya wananchi pamoja na wanajeshi wetu katika maeneo ya hifadhi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pasipo shaka Serikali ina tathmini ya watu waliouawa katika hifadhi. Juzi waliuawa watu wanne kule Arumeru, hakuna kauli ya Serikali wala ziara yoyote ya Serikali iliyotembelea eneo hilo. Ikitokea ugomvi kati ya mkulima na mfugaji Serikali itapeleka polisi, Serikali itapeleka kila kitu, lakini akiuawa mwananchi katika eneo la hifadhi wala Serikali haijali na ndiyo maana Serikali inatoza watu wakiua tembo dola 15,000 lakini mwananchi analipwa shilingi milioni moja akiuawa. Kwa nini tuseme Serikali ina ajenda ya kuua watu wake kwa kisingizio cha uhifadhi wa wanyamapor? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi ya hifadhi, zile buffer zone ambazo Serikali inasema mita 500, maeneo mengine kuna maji, lakini mwananchi anaambiwa buffer zone zile zinaanza mita 500 katika eneo la mto ambalo kuna maji. Mwananchi atapataje nafasi ya kwenda kuyatumia yale maji? Ndiyo chanzo cha migogoro mingi. Maeneo mengine ukienda kama Ngorongoro, ukienda kule Sikonge, tumepeata taarifa wananchi wameuawa wanapigwa risasi ya kisogo na askari, lakini Serikali imaficha. Jana tumepeata taarifa ya kule Morogoro Serikali ya Mkoo chini ya Mkoo wa Mkoo waliwanyima Civil Society na Waandishi wa Habari kuingia kwenda kukusanya taarifa ya hali ya migogoro kati ya wakulima na wafugaji. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nalionna ni kwamba Serikali haijawa tayari kushughulikia matatizo haya. Kwa mfano, zimekuja ripoti mbalimbali, Operation Tokomeza, Ripoti ya akina Mheshimiwa Jenista Mhagama, wakati ule ilikwenda kutafuta tatizo la wafugaji na wakulima, Serikali

imekalia ripoti, hakuna taarifa yoyote ambayo so far Serikali imeyafanyia kazi mapendekezo ya Wabunge! Hivi tutaendeea kukaa kwenye Bunge mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Bunge hili litoe Azimio, Serikali itoe commitment leo kwamba matatizo ya wafugaji na wakulima yataisha lini nchi hii? Vinginevyo tutagawa Taifa hili, vinginevyo tutawagawa wananchi wetu hawa, vinginevyo tutatengeneza uadui amba ni mbaya kuliko uadui ulioko nje ya nchi yetu, kama Serikali haitoi commitment. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imesababisha haya kwa sababu Wizara hizi hawashirikiani, Waziri wa Kilimo anaenda peke yake, Waziri wa Ardhi anaenda peke yake, Waziri wa Maliasili anaenda peke yake. Naomba wakati naendelea hivi, tunaomba Kauli ya Serikali. Hivi kauli kubwa kuliko yote ni ipi? Rais amesema wafugaji wasisumbuliwe kwenye hifadhi mpaka Serikali itakapopata maeneo ya kuwapeleka, ananyanya Waziri wa Maliasili anasema ondokeni leo, bila kutuambia tunaenda wapi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani yule ambaye anaweza akatengua kauli ya Rais aliyesema tutengewe maeneo ya kwenda kwenye mifugo kabla ya kutuondoa katika maeneo yale? Waziri ananyanya anasema wafugaji waondoke, twende wapi? Mazingira ambayo tunayaonesha kama Serikali haitatengeneza utaratibu wa matumizi bora ya ardhi kwenye nchi yetu, migogoro hii haitakaa iishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitisha sheria hapa ya kuweka chapa mifugo, tumepitisha sheria ya kutenga maeneo ya mifugo, lakini mpaka sasa hakuna hata sehemu moja ambayo Serikali ime-declare kwamba eneo hili ni la wafugaji. Matokeo yake wafugaji wanaondoka wanaenda kwenye mashamba ya watu na hakuna mkulima yuko tayari kuona mfugaji akilisha ng'ombe kwenye shamba lake. Hicho ni chanzo cha migogoro na hatuna kauli thabitii ya Serikali ya kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kusikia wakisema tunalaani, tutaendelea kusema watu wakipelekwa mahakamani, lakini watu wanahonga na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa. Hatuwezi kama Bunge kuona wananchi wetu wanaauawa kwa sababu ya uzembe wa Mawaziri na uzembe wa Serikali yenye. Tunataka commitment ya Serikali tunamalizaje tatizo la wafugaji na wakulima nchini mwetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini miaka ya nyuma tulikuwa hatugombani? Ni kwa sababu ardhi ilikuwa inatosha, sasa ardhi imekuwa ndogo, Serikali haina mikakati. Mnasema Idara ya Ardhi watenge maeneo lakini hamuwapi bajeti. Kama kweli Bunge hili tunatamani kuwaunganisha Watanzania ni muhimu kuibana Serikali itoe commitment na schedule program

ya kuhakikisha inamaliza tatizo hili ambalo la wakulima na wafugaji ambalo limekuwa kubwa kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaomba nilichangie ni suala la Wizara ya Ardhi. Wengine wamechangia na Kamati imeona kwamba tatizo kubwa ni kwamba kuna mashamba makubwa ambayo yamehodhiwa na watu ambao hawajayaendeleza. Nitasema mashamba manne tu Monduli, ambayo watu wanne wanamiliki zaidi ya ekari 32,000 na mpaka sasa hawajalima hata nusu ekari, lakini mpaka leo Serikali haitoi kauli kwamba mashamba hayo yanarudi lini kwa wananchi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo shamba la Sluiz, tunalo shamba la Tan Farm, tunalo shamba la Stein ambalo lina ekari 16,000 peke yake hajaendelezwa na Serikali imeendelea! Kwa nini migogoro isitokee? Kwa hiyo, tunafikiri kama Serikali imedhamiria kweli kuyarejesha mashamba haya kwa wananchi ni muhimu ikafanya haraka. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu lingine ni kuhusu ukame ambalo limekuwa kubwa. Mmesema tuiseme kuna njaa, tukisema hivyo tunafunguliwa mashtaka. Mimi nafikiri mtalifungia Bunge lote hili, hakuna Mbunge asiyejua kwamba wananchi wanaenda kwenye maeneo wakilalamika njaa na tunaona. Tunaona mifugo yetu ambayo ni rasilimali yetu ikiteketea, tunaona mashamba yakikauka. Ni kweli Serikali haijaleta ukame, lakini tusikatae kwamba kuna taizo la njaa linalotokana na ukame ili tuende tukajadiliane kama Taifa tunafanya je kuwaokoa watu wetu wasife, kuliko kuendelea kusema kwamba hatuna tatizo, lakini tatizo hili linatumaliza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu asiyeona kwamba mvua zimechelewa kunyesha, lakini Serikali inakataa hakuna njaa ili Watanzania hawa wafe, tunaogopa nini wakati ninyi hamjaleta ukame au labda ninyi ndiyo mmeleta ukame? Kama siyo ninyi msizue watu kusema kuna tatizo. Anayeopata neema ya mvua ni ya Mungu tu. Sasa msiwacheke wale ambao neema hiyo haijawafikia, tukifanya hivyo tutasaidia Taifa letu kutafuta namna ambavyo tutapambana na majanga haya yaliyopo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho, tunalo tatizo la hifadhi zetu na wafugaji. Tunataka Serikali ituambie kwa nini Serikali isishirikiane na wananchi wa vijiji katika maeneo yao katika kutafuta suluhi ya kukubaliana mipaka mipy ya hifadhi zetu na wananchi wetu? Katika eneo la Ngorongoro peke yake mnataka kuchukua square metre 15,000 kilometra 1,500 ya wananchi kwa kisingizio kwamba kuna wahamiaji haramu, naitaka Serikali wakati inafanya majumuisho ituambie...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Laizer. Mheshimiwa Gekul anafuata na Mheshimiwa Nsanzugwanko ajiandae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nina mambo machache, naomba dakika zangu tano nimgawie Mheshimiwa Selasini, Mbunge wa Rombo, tembo wanamsumbua Jimboni kwake. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni suala la chakula. Wakati Waziri wa Kilimo akieleza hali ya chakula nchini alisema kuna Wilaya zaidi ya 56 kama sikosei zina upungufu mkubwa, lakini Wilaya hizo hatujapewa *list*, ninaitake Serikali watupe majina ya Wilaya hizo tuzifahamu na ni lini sasa chakula kitaenda, kwa sababu wananchi wetu wana hali mbaya sana.(Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea wananchi wangu wa Jimbo la Babati Mjini debe moja la mahindi wanunua kwa shilingi 20,000. Naomba nifahamu mnaapeleka lini hicho chakula kwa wananchi wetu kwa sababu hali ni mbaya na mliwambia kwamba wauze ng'ombe hata watatu wanunue debe moja, hao ng'ombe watatu hata bei haifiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumeenda Karatu tumeona ng'ombe wamedondoka barabarani wamekufa, sasa hata ng'ombe kumi hawatoshi kupata shilingi 20,000. Mtuambie mnaapeleka chakula lini hasa kwa wananchi wangu wa Babati wana hali ngumu kweli na mvua hazijanyesha. Wakati mwingine viongozi wa juu tuangalie kauli zetu, huenda hata Mungu anatuadhibu kwa ajili ya kauli zetu, mlisema hamtoi chakula, mvua ikaacha kunyesha, saa hizi hali mbaya. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu Kamati iliyoundwa. Hii Kamati ya Migogoro ya Ardhi ya Wakulima na Wafugaji ni Kamati ambayo inahusisha Wizara zaidi ya tano, mpaka leo hamtuambii hiyo Kamati imefika Wilaya ipi? Hamtuhusishi Wabunge na Madiwani huko chini tufahamu hiyo Kamati, tuliuliza. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maliasili, Ardhi na Mazingira, lakini huko kila tukizungumzia migogoro ya ardhi, wakulima na wafugaji mnatuambia Kamati iko site, mtuambie iko wapi? Imeanzia wapi? Imefikia wapi? Hiyo schedule mtupatие Wabunge ili tufuatilie, mkitujibu tu humu ndani mkatuambia Kamati iko site, watu wanauana haina maana yoyote Waheshimiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtuambie iko wapi, mje na Babati huku, anzieni huko pia. Morogoro kule watu wanauana, Wabunge tushirikishwe hiyo Kamati tuipe ushirikiano mgogoro huo wa wananchi wetu kuuana uishe. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni suala la kodi ya ardhi. Katika bajeti iliyopita Waheshimiwa Wabunge kodi ya ardhi tukasema TRA ikusanye, sasa hivi Halmashauri zetu hawakusanyi tena lakini TRA hawana manpower, haya maduhuli ya Serikali hayakusanywi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri tu Wizara ya Ardhi, mlikuwa mnatuletea asilimia 30 retention ya premium, sasa hivi hizo pesa zingetusaidia hata kununua vifaa, Halmashauri zetu hatuna vifaa vya upimaji ndiyo maana ardhi kubwa ya Tanzania haijapimwa. Leo badala ya kuwezesha Halmashauri zetu wabaki na hizo retention za 30 percent mlipitisha kwenye bajeti mwaka jana, wakati mmetufukuza mkapitisha, mkasema TRA wakusanye. TRA hawakusanyi, hawana manpower. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kwamba rudisheni sasa kazi hiyo kwa Halmashauri zetu ili kazi ya upimaji ardhi katika Halmashauri zetu iende sambamba na suala zima la upatikanaji wa fedha. Kwa sababu ile 30 per cent ilikuwa inatusaidia. Kama TRA hawakusanyi mwaka mzima kwa nini msifanye maamuzi? Kazi kwenu, wakati wa bajeti kaeni chini mfikirie siyo kodi tu ya ardhi, lakini pia hata kodi ya majengo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni suala la fedha za maji, fedha za maji kuna mlango wa Wizara ya Maji, mna bajeti yenu huko haiko wazi sana, lakini kuna TAMISEMI na kuna Halmashauri zetu. Kwenye Halmashauri mnatupa ceiling ndogo sana Mheshimiwa Waziri. Kaeni chini muweze kureconcile pamoja vyanzo vyote vya fedha za maji ili Wabunge tujue kwamba miradi mikubwa tupitishie milango ipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri ulikuja Babati katika Jimbo langu, pale Kata ya Sigino, uliona Kata nzima hawana maji kabisa vijiji vyote vine. Tukiwafuata mnasema kuna fedha upande wa Wizara ya Maji, kuna TAMISEMI, wakati huo huo ceiling hazitoki mapema saa hizi Mabaraza wameshaanza kukaa kwenye bajeti, ceiling hazijulikani. Toeni ceiling mapema, lakini onesheni mapema kwamba Wizara ya Maji tunaweza tuka-access fedha hizo kwa kiasi gani? Kama tutaendelea kutokuweka mambo haya wazi, tutaendelea kuimba wimbo wa kwamba hakuna maji katika Taifa letu kwa miaka zaidi ya 50 na akina mama wanaendelea kuchota katika makorongo na ndoo hazijashuka katika vichwa vyao. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Gekul. Tunaendelea na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninamshkuru sana na Mheshimiwa Gekul kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya maji ni mbaya, jana nilikuwa nasikiliza vyombo vya habari vya Kimataifa, watabiri wanasema Vita ya Tatu ya Dunia itatokana na upungufu wa maji katika dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba pale Rombo Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu Waziri wa Maji mmekuwa maarufu sana kwa Warombo, sababu ni tamko lenu la kuifuta *Kili* water. Baada ya kutoa tamko la kuifuta *Kili* water iliyowanyanya Warombo kwa ajili ya maji kwa miaka mingi sana, walikuwa wana matumaini makubwa sana sasa kuna jambo litafanyika tuweze kuwa na mamlaka yetu ili tuweze kuratibu matumizi ya maji kidogo tuliyonayo pale Rombo. Mheshimiwa Waziri nawaombeni sana hili jambo liweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba shida ni kubwa kuliko miaka mingine yote. Hivi ninavyozungumza ukame umeleta athari kubwa sana, vyanzo vidogo vya maji ambavyo tulikuwa navyo sasa vinatoa maji asilimia ndogo kabisa. Mheshimiwa Waziri bahati mbaya sana visima ambavyo tulivipata kutokana na mradi ule wa visima kumi vya World Bank mpaka sasa hivi miundombinu yake bado haijakamilika kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisima kwa mfano cha Shimbi Mashariki, visima kwa mfano vya Leto na vinginevyo maji yamepatikana lakini usambazaji umekuwa shida kwa sababu fedha hazijapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna imani na nyinyi kama nilivyowaambia baada ya kuifinya *Kili* water tumejenga imani kubwa sana na ninyi tusaidieni, kwa sababu hata huu utaratibu wa Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya kusaidia maji, own source ndogo haiwezi kufanya Halmashauri ikapata fedha ya kutenga kwa ajili ya kusaidia miradi ya maji. Kwa hiyo, ni matumaini yangu Mheshimiwa Waziri hilo utalichukulia kwa uzito mkubwa na pale Rombo pana Ziwa Chala ambalo lina maji, maji yale yanatumika na wenzetu Kenya. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza swali hapa nikajibowi wakati huo Waziri Maghembe akiwa Waziri wa Maji kwamba maji ya Ziwa Chala ni maji ya Kimataifa, kwa hiyo, kuna mikataba ambayo lazima iangaliwe. Tunachoshangaa watu wa Rombo maji ya Ziwa Chala yanatumika Kenya, kwa nini yasitumike Rombo? Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri muangalie uwezekano haya maziwa yaweze kutumika pia kusaidia watu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa kulizungumza ni kwa Waziri wa Mifugo na bahati nzuri amekaa jirani na Waziri wa Viwanda.

Nimesikia sana huku Bungeni kwamba wafugaji wapunguze mifugo na kadhalika, waipunguzie wapi? Kwa sababu hakuna viwanda vya nyama hapa

nchini, ng'ombe jinsi alivyo nyama ni pesa, ngozi ni pesa, kwato ni pesa na mifupa ni pesa. Kwa nini tusianzie hapo? Mheshimiwa Waziri teta na mwenzako upo jirani naye hapo alete viwanda kwa ajili ya mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mwijage kama alivyotueleza jana pale yuko sharp, ng'ombe zikiwa na afya huwa zinavuka Ngorongoro zinaenda kiwanda cha nyama Thika Kenya, huu ni ukweli kabisa, lakini sisi tumekaa hapa tunapiga hadithi tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tulivyouna ile Kamati ya Migogoro ya Wakulima na Wafugaji tulipita vijijini, wafugaji wanatuambia kuna shamba darasa la kilimo mbona hatujawahi kuona shamba darasa la mifugo? Kwa hiyo, mimi pamoja na kwamba siyo mfugaji kwa ile maana ya ufugaji tunayoijua, lakini naona migogoro mingine ya wafugaji na wakulima inatokana na kutofanya maamuzi ya kusaidia haya makundi ili yakafanya mambo kitaalam. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu juzi nilikuwa natoka kumzika Kaka yake na Mheshimiwa Cecilia Pareso. Pori hilo kutoka Minjingu mpaka Makuyuni ni harufu ya uvundo ng'ombe wamekufa, Simanjiro yote ni harufu ya mizoga ya ng'ombe. Kwa hiyo ni vizuri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Selasini. Tunaendelea na Mheshimiwa Nsanzugwanko ajiandae Mheshimiwa Bashe dakika tano na Mheshimiwa Mgumba dakika tano.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru. Mimi nitakuwa na machache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja nataka tuweke angalizo kuhusu hifadhi zetu na mifugo. Waheshimiwa Wabunge tusipokuwa makini baada ya miaka michache tutakuwa hakuna *wildlife* nchi hii. Hii ya wafugaji kung'ang'ania kwenye hifadhi zetu eti tu kwa sababu bwana mkubwa alisema msitoke, hii siyo sahihi jamani. *This country tuta-wipe-up wildlife* yote ya nchi hii. Nadhani hoja ya msingi ambayo nafikiri Serikali ingekwenda kuifanya kazi ni ile Tume ya Waziri Mkuu ya zile Wizara tano ziharakishe kufanya zoezi lile ili yale maeneo ambayo yamekosa sifa ya uhifadhi ndiyo mifugo ihamishiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Ngorogoro hamjui mkakati uliopo wa Wakenya hapa, wanataka kui-suffocate Ngorongoro hatimaye tuiue Serengeti ili wabaki na advantage ya Masai Mara ya Kenya. Nilikuwa naweka tu angalizo ili tuweze kuelewana vizuri na watu wa maliasili nadhani jambo hili hatuwezi

kulifumbia macho, tusipokuwa makini baada ya miaka michache nchi hii itakuwa haina maliasili wala haitakuwa na wanyamaporu au watapungua sana. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la tozo. Ukiangalia taarifa ya Kamati yetu ya Bajeti inazungumzia kwamba tozo hizi kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 kwamba hizi tozo zimeondolewa. Mimi nipo kwenye Kamati ya Kilimo na Mifugo, hizi tozo hazijaondolewa na taarifa niliyonayo ni kwamba Waziri wa Biashara anahangaika kutafuta namna gani ya kuziondoa, sasa hizi taarifa zingine zinakuwa hazina uhalisia. Tozo za mazao, tozo ya Bodi ya Pamba, Bodi ya Kahawa, Bodi ya Korosho kidogo wameangalia, lakini Bodi ya Chai bado na mazao mengine. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri nikikubaliana na mapendekezo ya Kamati hii ya kilimo madam tunakwenda kwenye bajeti tunaomba tozo hizi Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hizi tozo futeni. Waziri Mramba alizifuta hizi sijui kwa nini zinarudishwa. Wale wenyewe kumbukumbu tozo hizi ziliitwa kodi za kero, kodi za mazao na zikaondolewa, sasa leo kwa nini zishiondolewe? Nafikiri hilo ni jambo muhimu kwa sababu tunajenga na tunakwenda kwenye bajeti ni vema tozo za mazao ya biashara zikaondolewa ili wakulima waweze kuuza mazao yao na hatimaye wapate kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalopenda kuzungumzia ni upatikanaji wa mbegu, Waziri wa Kilimo unajua kwamba nchi hii hatuna mbegu, hata mbegu za mazao ya chakula zinazozalishwa nchini ni asilimia 35 mpaka asilimia 40, mbegu nyingi zinatoka nje ya nchi yetu. Zinatoka Zimbabwe na Kenya. Ushauri wangu kwa Serikali kama tulivyo sema kwenye Kamati yetu ya Kilimo haiwezekani tuzungumzie uchumi wa viwanda wakati hatuna hata mbegu za mazao yetu wenyewe ambayo hatimaye ndiyo zitatengeneza hivi viwanda vya agro *industries*. Sasa suala la mbegu ni la msingi sana na nilikuwa naomba wenzetu wa Serikali mkaliangalie hasa kwa sababu tunajenga upya bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upatikanaji wa mbolea limezungumzwa. Labda niseme Waheshimiwa Wabunge wananchi wetu wengi wanaishi vijiji na wananchi wetu wengi ni wakulima. Hawa wananchi wetu bado kuna shida ya upatikanaji wa mbolea. Kwa mfano, takwimu za mwaka jana huu mwaka tunaoumaliza sasa, ni kaya 378 tu ambazo zimepata pembejeo nchi nzima ambayo ni sawa sawa na asilimia 0.06 ya wakulima, sasa huu kama siyo mchezo wa kuigiza ni kitu gani? Hatuna mbolea, hakuna mbegu halafu unakuja kuzungumzia uchumi wa viwanda, viwanda vipi hivyo? (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda tunavyovifikiria lazima viwe ni viwanda ambavyo vitaajiri watu wetu wengi vijiji na viwanda hivyo ni viwanda vya

mazao ya kilimo pamoja na michikichi. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la uzalishaji wa mbegu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Waziri wa Uwekezaji na Waziri wa Mambo ya Ndani jengeni mkakati wa kuzalisha mbegu kupitia Magereza yetu. Jeshi la Magereza Waziri wa Mambo ya Ndani jana umelisema vizuri tu, nina hakika wenzetu wa Magereza wana mashamba makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mkakati maalum ambao umejengwa kibajeti, nina hakika tunaweza tukazalisha mbegu zetu wenye na zikatosheleza. Maeneo kama Magereza, JKT na hata watu binafsi wanaweza wakafanya kazi hii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho ni hii *food for thought* wenzetu wa Serikali mkalitzame. Kwa maoni yangu na maoni ya watu wengi kwenye Kamati yetu ya Kilimo jamani hii Wizara ya Kilimo ni kubwa sana, hii Wizara ina vitu vingi sana. Ushauri wangu kwa Serikali muangalie namna nzuri ya kumshauri bwana mkubwa hii Wizara muundo wake utazamwe upya. Maana yake una mifugo una kilimo, uvuvi, ushirika, masoko na taasisi zaidi ya 60 chini ya Wizara moja.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri sincerely kabisa, wenzetu wa Serikali mkakae mliangalie hili mumshauri bwana mkubwa namna anavyoweza kuhuisha huu muundo ili uweze kuwa na tija kwa sababu Wizara hii kwa kweli ni Wizara mama. Wizara hii ndiyo roho ya Taifa letu kwa sababu ndiyo inaa jiri watu wengi na ni tegemeo la maisha ya Watanzania walio wengi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni huu Mfuko wa Maji ambao umesemwa sana na kwenye Kamati tulikwenda mbali zaidi tukasema ni vizuri hata hizo fedha zinazotolewa tuwe tunajua ni kiasi gani cha mafuta yameuzwa. Kwa sababu msingi wa Mfuko wa Maji ni hizi fedha zimezungushiwa wigo wake ili zikaondoe tatizo la maji katika maeneo yetu vijijini. Kumekuwa na kuchechemea kidogo kwa Serikali. Tunataka kujua exactly ni kiasi gani ambacho Mfuko wa Maji unapaswa kupata, siyo ku-remit kwenda Wizarani. Mapato halisi ya Mfuko wa Maji lazima yajulikane kwa sababu ni kauli ya Bunge hili, tuli-ring fence zile fedha kwa ajili ya kwenda kuondoa matatizo ya maji katika maeneo yetu ya vijijini. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine nimeyasema jana, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nsanzugwanko. Tunaendelea na Mheshimiwa Mgumba dakika tano, Mheshimiwa Hussein Bashe dakika tano, ajiandae Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani dakika tano na Mheshimiwa Joseph Kakunda dakika tano.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa dakika tano na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze moja kwa moja kwenye ukurasa wa 24 wa kitabu cha Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji hasa kwenye miradi mikubwa ya mabwawa nchini ambayo haijatekelezwa kwa muda mrefu. Kama kuna mradi ambao haujatekelezwa muda mrefu kuliko yote hapa nchini basi ni mradi wa Bwawa la Kidunda. Huu mradi wa Bwawa la Kidunda kabla ya uhuru mwaka 1955 ndiyo wazo hili lilianza na andiko lake la kwanza usanifu ulifanyika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uhuru chini ya Serikali ya Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1962 akaubeba mradi huu akasema huu ndio ukombozi wa uchumi imara kwa sababu nchi yetu inategemea uchumi wake kwa kiasi kikubwa kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua Bwawa hili la Kidunda lilikuwa ndio liwe mkombozi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji lakini kwa ajili ya maji ya uhakika kwa Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro, ujazo wa wakati ule ulikuwa ukubwa wake zaidi ya cubic meter milioni 450, Serikali zote zilizokuja ziliendelea kuubeba mradi huu lakini hakuweza kutekelezwa kwa sababu ya ukosefu wa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu kuanzia mwaka 1994 pamoja na mahitaji ya maji kuendelea kuongezeka mradi huu ulibadilishwa matumizi kutoka katika *multiple use* maana ya kwamba mahitaji ya binadamu, mifugo pamoja na umwagiliaji yakawekwa tu kwa ajili ya *single use* yaani matumizi ya binadamu na kupunguza ukubwa wa bwawa kutoka cubic meter milioni 450 mpaka 190, kwa kusikiliza tu wadau wa maendeleo wasiotutakia mema kwa ajili ya maendeleo yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua wakati mwengine wadau wa maendeleo wakitaka kukuzuia wanaweza kukusingizia tu wakakwambia bwana hapo Selous hapo kuna nyoka hayupo ulimwengu mzima yupo hapo tu, mkilijenga hilo bwawa huyo nyoka atakuwa amepotea, na sisi tumekubali hiyo akili tukapunguza bwawa kutoka cubic meter milioni 450 mpaka 190. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nchi ulimwenguni sasa hivi inatanguliza maslahi ya wananchi wake zaidi kuliko ya mtu yeyote. Wamarekani wanasesma

Marekani kwanza, Waingereza wanasema Uingereza kwanza na Wachina wanasema China kwanza ni lazima tufanye maamuzi magumu katika hili ili tukubaliane na changamoto zinazotukabili nchini kwetu hasa ya ukame. Lazima turudi kwenye usanifu wa awali wa ule ujazo wa 450 milioni badala ya huu wa 190 tu kwa ajili ya matumizi ya binadamu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali tuende na andiko lile la asili ambalo liliandikwa tangu mwaka 1955 wakati ule hata mahitaji ya maji yalikuwa machache sana kuliko sasa hivi mahitaji ya maji ni makubwa zaidi, hata Mto Ruvu unaanza kupungua maji hususan wakati wa kiangazi. Kwa hiyo, hili Bwawa la Kidunda utekelezaji wake ndiyo utakuwa ni uokozi kwa ajili ya uchumi wetu kama tunavyojuu Dar es Salaam tunaitegemea zaidi ya asilimia 75 kwa uchumi wa nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili kwa Serikali ni kwa sababu miaka yote 62 mradi huu haujatekelezwa shida kubwa ni fedha. Leo hii kule Mkulazi ndiyo kinajengwa kiwanda kikubwa kuliko chote cha sukari kupitia kampuni ya *Mkulazi Holding*, lakini kwa tatizo la maji huu mradi hautatekelezeka. Bwawa hili ni lazima lijengwe ndiyo huu mradi wa Mkulazi nao u-take-off.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mgumba. Tunaendelea na Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono taarifa za Kamati zote mbili. Nataka niseme mambo machache na jambo la kwanza ni suala la maji, ninaiomba Wizara ya Maji mchakato wa maji wa Ziwa Victoria na utekelezaji wake tunatarajia sana watu wa Mikoa ya Tabora na Singida utekelezaji wa mradi huu, tumeusubiri kwa muda mrefu ingawa kuna matumaini madogo, tunaomba, tulitarajia mwezi huu wa pili mkandarasi angekuwa site, tungeomba jambo hili litekelezwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye maji fedha zinazoenda kwenye Mfuko wa Maji chanzo chake ni mafuta. Amesema Mheshimiwa Nsanzugwanko ni muhimu sana base ambayo Kamati ya Bunge inayosimamia section hii i-demand kutoka Serikali mahitaji halali ambayo yalitakiwa yaende kwenye mfuko ili siku nyingine wakija kwenye Bunge hapa watuambie matarajio yalikuwa ‘X’ kilichopatikana ni ‘Y’ ili Bunge liwe na picha halisi ya nini kinaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, narejea nilisema mwezi wa tisa nasema na leo; hakuna dhamira ya Serikali kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji. Nilitahadharishe Bunge kwamba tusiingizwe kwenye mkenge tukadhani hili ni tatizo la Mheshimiwa Tibeza, siyo tatizo la Mheshimiwa Tizeba tu wala siyo tatizo la Waziri wa Ardhi tu na wala siyo tatizo la Waziri wa Maliasili, hili ni tatizo linalotakiwa kuchukuliwa na Serikali collectively. Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji, Wizara ya Mifugo na Wizara ya Ardhi waje kwenye Bunge la Bajeti watuletee mpango wa Serikali juu ya kumaliza mgogoro wa wakulima na wafugaji. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu na la mwisho ni hii *dream* tuliyonayo, *dream* hii imekuwepo toka Serikali ya Awamu ya Kwanza kujenga Taifa la kujitegemea la viwanda, Serikali ya Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne na Serikali ya Awamu ya Tano. Ninachokiona makosa yale ya toka enzi za Mwalimu Nyerere yanafanyika leo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kosa la kwanza tuna-focus kuwekeza kwenye viwanda ambavyo ukitazama objective yake ni *import substitution industry*, ni wrong. Lazima tufike mahali Serikali ielewé hakuna *industrialization* kama hatujaamua kuwekeza kwenye sekta ya kilimo. Hakuna *industrialization* kama Wizara ya Viwanda, Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Wizara ya Miundombinu hawatokuja collectively na kuwa na *master plan* ya kutujengea viwanda katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwijage atakuwa anakuja hapa anatuambia njoo nikupe kiwanda. Mimi nimempa eneo hekta 200 Nzega, mpaka leo nataka niwaruhusu wananchi walime hakuna hata *hope*. Nataka nitoe mfano mwingine, leo hii tumbaku ina tozo na ushuru almost 16 lakini ukizitazama pamoja na silent ziko 19, Mheshimiwa Tizeba anajua.

Mheshimiwa Rais wakati anaomba kura alisema ataondoa tozo kwa wakulima, leo Nzega mkulima wa Idudumo akilima mpunga anaanza kutozwa kuanzia anavyotoka njiani nyumbani kwake na mageti mpaka anafika mashineni kuuza gunia lake moja, tunaongeza umaskini kwa watu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii hatujaweka bajeti ya pembejeo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, hasa wa Chama chetu cha Mapinduzi, tusiwe tayari ku-fall into the pressure ya Serikali. Tumepitisha bajeti ya ajabu sana ya Kilimo mwaka huu hapa sisi, ambayo haina fedha ya bwawa, Mheshimiwa Dkt. Tizeba Waziri wa Kilimo wala Wizara ya Maji hawana uwemo wa kutujengea mabwawa ya wafugaji, hana fedha za pembejeo, tunasema mawakala walipwe tutaambishi tu bado wanachunguza, Mheshimiwa Dkt. Tizeba hana lugha nyingine, kaapa yule, lakini hakuna fedha za kuwalipa, *this is the bitter truth...* (Makofii)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salum Rehani, ajiandae Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii kwa uchache nizungumze yale ambayo nilikuwa nimepanga niweze kutoa kama ushauri kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mbali saa nyingine kwa baadhi ya maelezo ambayo wenzangu wameyatoa, moja hasa likugusa kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka huu. Ni lazima tukubali ukweli kwamba tumepitisha bajeti ambayo siyo *practicable*, haifanyi kazi ile bajeti ni ndogo na hasa tukizingatia kwamba kwa kiwango kikubwa tumepunguza pembejeo kutoka kuwashudumia wakulima 999 mpaka kuwashudumia wakulima 300, hapa hatujawatendea haki wakulima wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zimeelekezwa katika maeneo mengine lakini pembejeo zimeshuka sana, sasa tuna ukame ambao umekabili nchi yetu, tulichokuwa tunatakiwa ni kuongeza nguvu kwa yale maeneo ambayo yamepata mvua ili wananchi wale waweze kuzalisha kwa wingi kuweza kufidia maeneo ambayo yalikuwa yamekosa mvua kwa kipindi hiki, ingeweza kuiweka nchi yetu kuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ya ukosefu wa mvua bado katika Ukanda wetu wote wa SADC unazikabili nchi zote hizi na ukosefu wa mvua.

Kwa hiyo, ukame utaendelea na ukosefu wa chakula utaendelea. Nchi pekee wanayoitegemea ni Tanzania, Tanzania yenyewe uzalishaji wake umekuwa wa kusuasua, tunakimbilia wapi, hapo ndipo pa kujiuliza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba bajeti ijayo tukubaliane Waheshimiwa Wabunge tuhakikishe kuna maeneo lazima yawe ya kipaumbele na tuhakikishe Serikali inasikiliza kilio chetu. Tulipendekeza kwa nguvu zote kwamba bajeti ya pembejeo ipande tukapendekeza fedha wapewe NFRA waweze kununua chakula kwa msimu uliokuwepo, NFRA hawanunui chakula wanangoja bajeti ya Serikali, chakula wanunua walanguzi na watu wengine wakianza kununua wao bei zimeshapanda.

Kwa hiyo, tuwatake NFRA wanunue chakula mwezi wa tano kwa yale maeneo yenye uzalishaji ili kuwepo na chakula cha akiba kujihami kwa hali ambayo inaweza kujitokeza huko mbele tunapokwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kusisitiza ni kwamba nchi hii hakuna kitu ambacho kimeonesha mwelekeo mzuri kama Mfuko wa Maji na tozo ya shilingi 50, tuliishauri Serikali msimu uliopita kwenye bajeti ipandishwe iwe shilingi 100, leo hii miradi yote iliyofanyika inaonekana katika Majimbo yetu ni kwa shilingi 50 ambayo imeweza kutengeneza zaidi ya bilioni 75 ambazo zimekwenda katika maeneo yetu mbalimbali. Kwa hiyo, nitoe wito wa Waheshimiwa Wabunge, bajeti ijayo tuiombe Serikali hiki kilio itusikie, ipandishe hadi shilingi 100 ambapo tutakuwa na uhakika kwa mwaka zaidi ya shilingi bilioni 300 na miradi yote ya maji itaweza kufanya kazi au itaweza kumalizika kwa wakati pasi na kutegemea tu pesa kutoka Serikalini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba fedha zaidi ziangaliwe maeneo ya utafiti, Tanzania tuna matatizo ya kupata mbegu ambazo zinatumika katika maeneo yetu, asilimia 70 sasa hivi ya mbegu tunaagiza nchi za nje. Tatizo kubwa ni zile tozo za wale watafiti au wale wazalishaji mbegu wa hapa nchini, lakini ukizalisha mbegu nchi za nje au nje ya Tanzania unakuwa na duty free. Hivyo, makampuni ya uzalishaji mbegu yamekimbia Zambia, Malawi, Zimbabwe, yanazalisha halafu yanaleta Tanzania kwa sababu kuingiza Tanzania ni bure. Kwa hiyo, kitendo hiki kinawavunja moyo watafiti, kinavunja moyo makampuni ya uzalishaji mbegu, hivyo basi kila mmoja anaona bora akazalishe nje au aende akanunue mbegu Belgium na afunge Tanzania halafu auze ndani ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kinacholeta athari zaidi ni baadhi ya mbegu zinazotoka katika nchi hizo hazifanyiwi uchunguzi, matokeo yake zinaleta athari za maradhi kwa watu mbalimbali na hasa kwenye ugonjwa wa kansa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linaloleta athari hapa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Rehani. Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Kubenea dakika tano ajiandae. Mheshimiwa Kakunda hayupo, Mheshimiwa Kubenea dakika tano na Mheshimiwa Bulaya ni dakika tano.

**MHE. SAED A. KUBNEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii.

Kwa ufupi sana, kwanza naunga mkono hoja ya Kamati iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu na pili, naunga mkono pia hoja iliyolewa kwenye Bunge hili ya kuvunja RUBADA na kuleta shughuli zote za RUBADA katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, katika ripoti imeelezwa kwamba Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) limekuwa linajenga nyumba na kuweka miundombinu ya umeme, maji na barabara na matokeo yake nyumba hizo zinazojengwa zimekuwa za ghamama kubwa. Pamoja na wito wa Kamati wa kutaka Serikali na wadau wengine wachukue hatua za kuweka miundombinu ya maji na barabara katika maeneo ambayo miradi ya *National Housing inapelekwa*, lakini kuna jambo moja muhimu sana ni muhimu Bunge lako Tukufu hili likaazimia kwamba Shirika la Nyumba la Taifa linajenga nyumba mpya za kisasa ambazo zinazwa kwa watu binafsi, lakini zipo nyumba katika nchi hii ambazo zimejengwa tokea wakati wa ukoloni na nyingine zimejengwa mwanzoni mwa uhuru zipo katika maeneo ambayo siyo ya biashara, lakini Shirikala Nyumba la Taifa halitaki kuuza kwa wapangaji walioishi katika nyumba zile kwa zaidi ya miaka 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba hizo nyingine ziko llala Sharif Shamba kwenye Jimbo lako la uchaguzi, nyingine ziko Temeke, nyingine ziko Ubungo na maeneo mengine mengi katika nchi hii. Kama Serikali inauza nyumba kwa wananchi wa kawaida, kwa wafanyabiashara wakubwa, kama shirika linaingia mikataba ni muhimu shirika hili likauza hizo nyumba kwa wakazi ambao wameishi katika hizo nyumba kwa zaidi ya miaka 20 au 30. Hili ni jambo muhimu sana kwa sababu litawasaidia wananchi wetu kupata nyumba za makazi. Tayari Serikali ilishakiri Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete akifungua nyumba mpya Iringa mwaka 2008 alikubali kwamba Serikali yake itauza nyumba zote hizo ambazo zinakaliwa na wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti hii kuna suala zima la utalii, lakini Bodi ya Utalii haikutengewa fedha katika bajeti, Bodi ya Utalii haina fedha, Serikali imefunga kituo cha biashara, kituo cha utalii cha uwekezaji kilichopo London na imefunga kituo cha biashara kilichopo Dubai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo hivi vilikuwa vinafanya kazi ya kuutangaza utalii wa Tanzania nje ya nchi, lakini sasa vituo vimefungwa na utalii hauwezi kutangazwa tena. Vituo hivi vilikuwa vinatangaza mambo ya *TANAPA*, mambo ya Ngorongoro, Zanzibar Island, Mafia na maeneo mengine ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Leo Bodi ya Utalii haina fedha, utalii hautangazwi matokeo yake Mlima Kilimanjaro unaambiwa uko Kenya wakati uko Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila uwekezaji, bila Serikali kuwekeza katika maeneo haya haiwezi ikapata faida, utalii unazalisha asilimia 17.5 ya bajeti ya Taifa, lakini Serikali imetupa utalii inasubiri Mwenyezi Mungu awaletee neema wakati neema haiwezi kuja bila kuwekeza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kwamba Bodi ya Utalii lazima ipewe fedha, ni lazima utalii utangazwe ili Taifa hili liweze kupata mapato mazuri kwenye utalii wetu. Bila kuweka fedha kwenye utalii wakati Serikali inafunga taasisi za utalii nje ya nchi hatuwezi kufika mbele, ni muhimu sana kwamba Bodi ya Utalii, Shirika la Utalii, Ngorongoro na kodi ya VAT kwa watalii iondolewe ili kuweza kuvutia watalii nchini, watalii waweze kuja wengi nchini na utalii uweze kutoa ajira. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wengi kabisa wametumbukia katika utalii lakini utalii katika...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nijikite katika masuala ya Jimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake najua wanansikiliza. Moja, kama ambavyo nilimsaidia Waziri wa Viwanda na Biashara babu yangu kwa wezi wale wa EPZ nawaambieni mkashughulike na wezi wa miradi ya maji, mmoja ni mtoto wa aliyekuwa kada wenu na Waziri mwenzenu wa zamani.

**MBUNGE FULANI:** Nani?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo kama wale wanaotajataja wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa zaidi ya shilingi milioni 800 Kata ya Kabasa, shilingi milioni 800 pesa za walipakodi, huyu mtoto, maji hakuna, kashughulikieni hilo tatizo. Nyamswa kwa Boni niliwaambia, ameharibu Mtware ameharibu na maeneo mengine, huu mradi mkubwa ndiyo usiseme kabisa ilikuwa kila Serikali ikiweka hela wanakata benki moja kwa moja kwa huu utapeli. Ranya kule walimfukuza, wananchi wangu wa Bunda wanataka maji, nimeshassafisha Baba yao nasafisha na uchafu wote, sitaki nataka wananchi wa Bunda wapate maendeleo, hilo limeshaisha, nadhani mmeshanielewa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunda kuna njaa, Baba wa Taifa alisema anayeficha maradhi kilio humuumbua, tuna njaa. Narudia, Bunda tuna njaa au niseme tu lugha laini, tuna upungufu wa chakula kwa kata zaidi ya sita. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, njaa hii siyo ya kujitakia, tatizo la tembo kuharibu mazao ya wananchi, dada yangu Mheshimiwa Jenista alishakuja kutembelea tukampeleka katika mashamba na moja ya shamba aliloenda kwenye Jimbo langu na akaahidi ataitisha kikao pamoja na Waziri wa Maliasili mpaka leo

hicho kikao hatujafanya, dada yangu sijui kikao tutafanya lini, utanijibu uniambie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Bunda wamesema hawataki kuomba chakula, wana uwezo wa kulima msiwatengenezee njaa wasiyoihitaji. Tembo wenu wanatoka wanakula mazao kule sijui ndovu, sijui tembo, sijui mazagazaga gani mtajjua wenyewe, halafu tena tukiwaambia tuna njaa hamtaki tuseme tuna njaa. Naomba wananchi wangu biashara ya kuombaomba hawataki na ninyi mmesema Serikali yenu hamtaki kuombwa sisi hatutaki kuomba, mnatuchokoza wenyewe, tembo wenu wanakuja kula mazao yetu, marufuku. Nimeshasema hivyo na mtuelewe, tunaomba mlele chakula kwa sababu tembo wenu ndiyo wamesababisha matatizo yote haya. Hayo ndiyo yaliyonifanya nisimame nizungumze. Wananchi wangu wanataka chakula, kwa sababu kuna njaa iliosababishwa na Serikali kwa tembo wao kuja kula katika mazao ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Kiwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Kuchauka, ajiandae Mheshimiwa Yussuf Hussein. (Makofi)

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa busara na hekima kwa kunipatia angalau hizi dakika tano na mimi nipate kuzungumzia masuala kadhaa ambayo yanankera katika maisha ya Watanzania, hususan Jimbo la Mlimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia kwa makini hiki kitabu cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, muda hautoshi, lakini kuna mambo mengi ambayo yanaizingira nchi yetu. Kwa mfano, ukurasa huu wa 33 wanasema umuhimu wa uzalishaji wa mbegu bora nchini, sasa katika Wilaya ya Kilombero pale Ifakara tangu mimi sijazaliwa kuna kituo cha utafiti Katrin pale Ifakara, lakini mimi sijawahi kuona katika maisha yangu matokeo ya Kituo hiki cha Katrin kwenda angalau katika Wilaya ya Kilombero tu siyo Tanzania, kwenda kuwaelimisha wakulima ni mbegu gani sahihi wanatakiwa watumie na kuna magonjwa yanayokabili mpunga na kile kituo kinasema kinafanya utafiti pamoja na mpunga, lakini wananchi wa Wilaya tu ya Kilombero hawajafaidika. Sasa sielewi, Serikali naomba mtupe maelezo kwa nini kituo hiki hakina matokeo chanya? Ama hamuwapi hela au kuna kitu gani, yaani tunasikia tu lakini hatuoni faida yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu manunuzi ya mpunga; wakati nakuja Bungeni nikapishana na Waziri tena nikasikia na wananchi Waziri anakuja wapi Mngeta, KPL, anakuja kufanya nini huyu kwa wawekezaji, amekwenda kule usiku kwa usiku, nikampigia simu akasema hata saa moja nitafika. Kaenda usiku

wa manane, kaenda kuangalia KPL, kaenda kuangalia ghala la chakula, sijui ndiyo uliambiwa ufanye utafiti wa chakula kiko wapi, watu wanasema mna njaa ninyi hamna, lakini usiku kwa usiku mnaingia pale mnaenda kuangalia ghala la chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, KPLni eneo ambalo linazalisha mpunga na mahindi, sasa nauliza hivi, hivi akiba ya chakula ni kwa mahindi tu, je mpunga sisi tunaolima mpunga hiyo siyo akiba ya chakula, kwa nini Serikali hamuweki katika mpango kununua mazao mbalimbali ya chakula kama mpunga. Mmedharau sana lakini ndiyo kilimo ambacho kipo katika nchi hii. Kwa hiyo hata kwenye upungufu wa chakula mnawenza mkapeleka mpunga watu wapate kula. Sasa nataka majibu ya Serikali, je mpunga lini mtauingiza katika bajeti upate kununuliwa kwa ujumla? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya maji, maji Kilombero na Jimbo la Mlimba yanatokea wakati wa mafuriko, lakini mafuriko yakiisha na maji yanaondoka, lakini kuna mito ya ajabu. Sasa Wizara ya Maji hebu chukueni angalau kuwe na Wilaya moja ya mfano, maana kila Mbunge hapa akisimama maji, hebu chukueni hata Wilaya moja ya mfano muoneshe kwamba mmefanya kwa asilimia fulani na angalau Mbunge mmoja akifika hapa awapongeze, basi muende kwa awamu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali njooni Kilombero ambako ni ghala la chakula, kuna mito karibu 39 lakini wananchi wa Kilombero hawana maji, wananchi wa Mlimba hawana maji, naomba mje. Naibu Waziri wa Maji ameahidi akihamia Dodoma baada ya Bunge hili atakuja kutembelea Jimbo la Mlimba, tumuoneshe miradi mbalimbali ya umwagiliaji na maji ya kunywa, miaka na miaka hela zinaingia lakini miradi haiishi, naomba mje mtagundua ufisadi wa kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa wenyekiti, kuhusu wafugaji na wakulima. Wafugaji na wakulima ni kero ndani ya nchi hii, lakini hawa wote wanategemeana, mfugaji anafuga mkulima analima. Hawa watu wanaowagombanisha ni Serikali kwa kutokupanga mipango bora ya ardhi ili kuwatengea maeneo wafugaji wafuge na wakulima walime, hawa wote wanategemeana, lakini katikakati kuna Serikali ndiyo inayoleta uchonganishi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Kilombero...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kiwanga. Mheshimiwa Kuchauka ajiandae Mheshimia Hussein.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kwenye hotuba hizi mbili. Awali ya yote nichukue fursa hii kuwashukuru sana Wenyeviti wa Kamati kwa hotuba nzuri walizotuletea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mchango wangu niuelekeze kwanza kwenye upande wa maji. Asubuhi nimeuliza swalii la nyongeza hapa jibu nililipata ni tofauti na matarajio. Mimi nimeongelea Mradi wa Ngongowele nimejibowi mradi wa kijiji kingine tofauti kabisa na mtaa wangu. Mradi wa Ngongowele umegharimu shilingi bilioni nne mpaka sasa hivi hauna maendelezo yoyote yale na hautegemei kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Mji wa Liwale kuna mradi wa *World Bank* pale kutafuta chanzo mbadala cha maji umegharimu shilingi milioni 200 nao mpaka leo hii unasuasua mradi huo haujaendelea. Kwa hiyo, kwa ujumla wake katika Halmashauri ile kuna shilingi 4,200,000,000, naomba Kamati inayohusika hebu nendeni mkaangalie ili muweze kuishauri Serikali nini cha kufanya. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika ule mradi wa maji wa vijiji kumi, Liwale nimepata vijiji vitatu tu, kijiji cha Barikiwa, Namiu na Mpigamiti lakini kuna miradi ambayo mpaka sasa hivi imesimama na hakuna kinachoendelea ambayo ni miradi ya kijiji cha Kipule, Kiangara, Mikunya, Mpengele, Kimambi, Nangorongopa, Nahoro na Kitogoro. Kwa hiyo, naiomba Kamati hii kama itapata wasaa hebu iweze kutembelea Jimbo lile la Liwale muone pesa za nchi hii zinavyoharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda Idara ya Maliasili. Nimeshasimama hapa mara nyingi na nimeshaongea sana, lakini nataka niongelee mgao wa asilimia 25. Kwenye Jimbo langu la Liwale hatujapata huu mgao wa asilimia 25 pamoja na kwamba hatujui asilimia 25 inatokana na mauzo gani lakini walituambia kwamba Halmashauri zote zinazozunguka Hifadhi tutapata mgao wa asilimia 25 kutoka kwenye Serikali Kuu kama ruzuku inayotokana na mauzo ya maliasili ya misitu lakini mpaka leo hii jambo hili halijatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye upande wa Maliasili nikiongelea upande wa malikale. Sisi pale tuna jengo lile la Wajerumani ambalo ni kumbukumbu ya Vita ya Majimaji mpaka leo hii yapo majina kwenye zile kuta, lakini Mheshimiwa Waziri nilisikitika sana nilipouliza hili swalii akaniambia kwamba Halmashauri ndiyo tuifanye hiyo kazi ya kuendeleza lile jengo ili kuweka kumbukumbu. Sijui ana maana kwamba sisi tufungue website yetu, tuutangaze utalii wa Liwale kwa kutangaza maliasili ile, mimi sijaelewa. Kwa hiyo, naomba

Waziri mwenye dhamana hebu atueleze ile malikale inayopotea pale mpango wake kwa Serikali hii ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye upande wa kilimo ambapo tuna tatizo la pembejeo, wengi wameshaliongea kwanza haziji kwa wakati. Mkao wa Lindi na Wilaya ya Liwale kwa ujumla wake safari hii tumepeata viatilifu fake ambavyo vimetupelekea kupata mazao hafifu ya korosho. Ukienda kwa mawakala wale wanaouza pembejeo za kilimo, utakuta ana stock mbili; maana kule kiatilifu kikubwa ni sulphur, anakwambia hii ni sulphur ya ruzuku na hii hapaya kununua. Ukichukua ile sulphur ya ruzuku ni kwamba umeumia, lakini ukichukua ile sulphur ambayo inauzwa cash ndiyo inaweza ikakuletea mazao mazuri.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yussuf Hussein jiandae Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Dakika kumi zimeisha?

**WABUNGE FULANI:** Tano.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Bismillah Rahman Rahim.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na kwa sababu ya dakika kumi ulizonipa basi niende haraka.

**MWENYEKITI:** Dakika tano. (Kicheko)

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Toba!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya kwanza ni kuhusiana na ufinyu wa bajeti. Kamati yetu sisi imeshindwa kutembelea maeneo ambayo hasa yana migogoro na kuweza kuishauri vizuri Serikali. Mgogoro wa Ngorongoro kila Mtanzania anaufahamu, Loliondo, lakini uvamizi katika mapori ya akiba ya Kigosi, Moyowosi, Burigi, Kimisi na kadhalika, kote huko tumeshindwa kufanya kazi kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, Wizara yenyewe hadi hapa tunazungumza bado robo moja kumalizia ina chini ya asilimia 30 ya bajeti ambayo imetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliombe Bunge hili, mtu anaonyeshwa njia wakati wa kwenda siyo wakati wa kurudi, bajeti ijayo tuhakikishe tunaweka fedha ya kutosha katika Kamati zetu na katika Wizara zetu ili tuweze kufanya kazi vizuri na kuishauri Serikali. (Makofii)

Mheshimiwa Mweyekiti, suala la pili, tuna tatizo kubwa sana katika nchi yetu lakini tunalidharau na tukiendelea kulidharau kwa mujibu wa tafiti zinazofanywa na wataalam baada ya miaka 20 nchi hii tutalia kilio cha kusaga meno. Waheshimiwa misitu yetu inapotea kwa kasi kubwa. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana ndugu yangu Mheshimiwa Kiwanga alilia machozi kama mtoto mdogo alivyokuwa anatembea katika Kamati akaona misitu inavyoathirika. Labda nitoe mfano, uchomaji wa mkaa ni chanzo kikubwa sana cha nishati na asilimia 90 ya Watanzania wanategemea nishati ya mkaa na kuni kwa ajili ya matumizi yao ya nyumbani, lakini vitu hivyo havina sheria, kanuni na hakuna sera ya uchomaji wa mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, kuna vijiji kumi Kilosa vimefanyiwa utafiti, wamepanga matumizi ya ardhi pamoja na matumizi ya misitu, wamegawa vile vijiji katika block 24 na kila mwaka wanatumia block moja kwa kuni, mkaa na matumizi yao. Kwa hiyo, miaka 23 wanaacha zile block zina-regenerate zenyewe. Kwa hiyo, pale tatizo lile limeondoka, faida yake nini? Hakuna uvamizi katika yale maeneo mengine, kijiji kinapata faida zaidi kutokana na mapato yanayopatikana, lakini pia kuna na ile teknolojia iliyowekwa pale ya uchomaji mkaa ile miti inatumwa vizuri pamoja na majiko yale bunifu waliyonayo. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusijidanganye, tuijulize, hivi ni miti mingapi inayokatwa kwa mwaka mmoja ndani ya nchi yetu na ni miti mingapi inayopandwa kwa mwaka ndani ya nchi yetu, inawiana? Huo mti utakaopandwa utakaa miaka mingapi ili tuje tukate tena? Kwa hiyo, tusijidanganye mtu anaweza akasema yeye hatumii mbao kwa sababu sasa hivi kuna teknolojia atatumia vioo kutengeneza milango, meza na kadhalika lakini akifa, nani ambaye haendi na ubao?

Kwa hiyo, tusijidanganye hii ni kwa wote Mkristo utaenda na sanduku, Muislam utawekewa ubao, kila mtu siku ya mwisho utaondoka na ubao. Kwa hiyo, miti ina faida kubwa ukiondoa zile *tangible* na *intangible benefit* kutoka kwenye miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, hili ni janga, ni kubwa lakini bado Watanzania tunalifumbia macho. Hivi hatuumii kila siku kusikia ndugu zetu wanauana kwa sababu ya tatizo la wafugaji na wakulima?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Deo Sanga ajiandae Mheshimiwa Chikota.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Kwanza nizungumzie suala linalohusiana na maji. Kwenye bajeti ya kipindi kilichopita kuna miradi mikubwa ambayo tulipitisha hapa. Kwa mfano, kuna miradi mikubwa ya maji ya miji ya Makambako, Njombe na Wanging'ombe ambapo ilionyesha fedha zinatoka Serikali ya India. Kwa hiyo, ni vizuri Waziri atakapokuwa anasimama atuambie Serikali imejipangaje juu ya kutatua tatizo la maji kwa mradi mkubwa huu wa Makambako, Njombe na Wanging'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la pembejeo hizi za ruzuku ambapo Mkoani kwetu Njombe zinachelewa sana. Sisi tunaanza kupanda kuanzia mwezi wa 11 na kuendelea. Kwa hiyo, Serikali ijipange vizuri msimu huu tunaokwenda sasa kuona kwamba pembejeo hizi zinafika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu, kuna hawa wasambazaji ambao mpaka sasa wanaidai Serikali na mpaka sasa wako watu ambao wamefilisika, wako watu wanauziwa nyumba zao. Ni lini Serikali italipa deni hili ambalo wananchi hawa walismambaza pembejeo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, ni suala la lumbesa kwa wakulima, nadhani Serikali ijipange vizuri suala hili lipigwe marufuku kwa nchi nzima ili kusudi isiwaumize wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano ni mifugo. Suala la mifugo limekuwa ni tatizo kubwa sana kwa wafugaji na wakulima na watu wanapoteza maisha. Aidha, Kamati au ninyi Serikali muone namna ambavyo nchi ya Sudan wana mifugo mingi kuliko sisi lakini hakuna tatizo la wakulima na wafugaji, waende kule wakajifunze wenzetu kule wanafanyeje mpaka hakuna migogoro ambayo ipo kama huku kwetu kila wakati mara watu wameuawa na kadhalika. Kwa hiyo, nadhani Serikali ijipange kuona namna ya kuondoa tatizo hili la mifugo na wakulima kwa sababu limekuwa ni kubwa sana, siyo kitu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sita, hapa kuna watu wamezungumzia Wizara hii ya Kilimo. Mimi niseme ndugu zangu, Waziri huyu Tizeba na Naibu wake wakati fulani tunawalaumu bure tu, sasa watachukua wapi fedha kama hawana fedha? Nadhani sisi tuungane kwa pamoja kuona namna ambavyo tunaiambia Serikali ili bajeti ya msimu huu tunaokwenda iwe nzuri kuliko bajeti iliokwisha ambapo ilitengwa shilingi bilioni 20 tu ambazo hazijatosha kitu chochote.

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani sasa badala ya kumlaumu Waziri na Naibu wake na Wizara kwa ujumla, tuone namna ambavyo sasa Serikali inajipanga kuona msimu huu tunakuwa na bajeti ya kutosha kwa sababu ndiyo uti wa

mgongo kwa wakulima wetu. Nadhani tukifanya hivyo, Serikali ikiongeza bajeti tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengi lakini kwa sababu na mimi nipo kwenye Kamati hii nirudie tena kuzungumzia hili suala la maji, Waziri utakaposimama uwaambie wananchi wa Makambako wataondokana lini na tatizo kubwa hili la maji na uwaambie fedha za kutoka nje wananchi wale wa Njombe, Wanging'ombe wanazipataje na mpango huu sasa unaendeleaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chikota ajiandae Mheshimiwa Malocha na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Na mimi nianze kwa kuunga mkono hoja zote mbili ile ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji na ile ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajielekeza kwenye masuala mawili, suala la kwanza ni la korosho. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Tizeba na Naibu wake Mheshimiwa Ole-Nasha kwa hatua walizochukua kwa tasnia ya korosho katika msimu huu wa korosho. Kuna mambo matano muhimu wametufanyia sisi wakulima wa korosho. Kwanza, walikuja Mtewa kushughulikia wezi waliohusika na ubadhirifu wa msimu wa mwaka 2014/2015 na walianza na Wilaya ya Masasi kukawa na changamoto kwamba hawakupewa support lakini hawakukata tamaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili baada ya kupata malalamiko yetu, Mheshimiwa Tizeba na timu yake waliamua kumuondoa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika. Kiongozi huyu alikuwa ana viongozi wa AMCOS ambao walihuksika na wizi na ubadhirifu wa msimu uliopita. Kwa hiyo, kwa ujasiri wake aliweza kumuondoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara hii katika kipindi kifupi cha msimu baada ya kuonekana kuna dosari ilithubutu kuvunja Bodi ya Korosho na kuisuka upya. Bodi hiyo mpya imeanza kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa na matunda yake tumeona msimu huu kwamba korosho imeuzwa hadi shilingi 4,000 kwa kilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu baada ya kuona mabilioni mengi ya fedha yanapelekwa kwenye Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho na hakuna kinachofanyika, Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Tizeba waliamua kusitisha shughuli zote za mfuko ule na shughuli zake zote kufanywa

na Bodi ya Korosho. Hii sasa itasaidia kujipanga upya na kutekeleza majukumu ambayo kimsingi kwa muda wa miaka mingi walikuwa wanapata fedha nyingi lakini hawatekelezi chochote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu, Wizara sasa imethubutu kuendesha mchakato wa kuhakikisha kiuatilifu muhimu au pembejeo muhimu kwenye zao la korosho sulphur dust kuagizwa moja kwa moja viwandani badala ya kuchukua kwa mawakala. Huu ni ujasiri mkubwa, kuna maneno mengi yamesemwa kwamba Waziri ana-interest na makampuni fulani lakini mti wenye matunda lazima upigwe mawe na kwenye vita ya mawe ya usiku ukiona mtu analalamika basi amegongwa jiwe. Kwa hiyo, hawa wanaolalamika kuna kitu walikuwa wanakipata kwenye mfumo wa ubadhirifu wa ununuzi wa hizo pembejeo, Mheshimiwa Waziri endelea na sisi wana Mtwara tunakuombea usiku na mchanana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Wizara ina kazi kubwa tatu sasa hivi. Kazi ya kwanza wasimamie ujenzi wa viwanda vya korosho kwa sababu huu Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho unapata zaidi ya shilingi bilioni 36 au 37 za export levy kwenye zao la korosho, lakini kwa miaka mingi hakuna kilichofanywa. Kwa hiyo, matarajio yangu sasa baada ya kazi hii kusimamiwa na Bodi ya Korosho tunaona sasa ujenzi wa viwanda vya korosho unaanza mkoani Mtwara na fedha ipo kwenye mfuko huu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kuna kiporo ambacho kimebaki. Tulikuwa tunasubiri taarifa ya ukaguzi ya COASCO. COASCO amekuja na taarifa kwamba msimu wa mwaka 2014/2015 kuna fedha zaidi ya shilingi bilioni sita hazikufika kwa wakulima. Taarifa ya TAKUKURU inaonyesha shilingi bilioni 30, taarifa ya Bodi ilionyesha shilingi bilioni 16; lakini juzi COASCO wamewasilisha taarifa kwamba kuna fedha shilingi bilioni sita zilitakiwa ziende kwa wakulima wa korosho lakini hazikwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu sasa Wizara itaendelea na moto ule ule isimamie haki ya wakulima ili waliohusika na ubadhirifu huu hata kama mkubwa wa ngazi yoyote awajibishwe ili fedha hizi ziende kwa wakulima. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna AMCOS 34 kwenye taarifa ile ya COASCO inasema hazikukaguliwa, kwamba hakuna kitu kilichoandikwa kwa msimu mzima. Uzembe huu hapa unalindwa na Maafisa Ushirika. Kwa hiyo, ni matarajio yangu kwamba Mheshimiwa Waziri chini ya usimamizi wako na Mrajisi mpya aliyeuleuliwa ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Malocha ajiandae Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kuweza kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuungana na wenzangu katika kuchangia taarifa za Kamati mbalimbali, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Uvubi na Kamati ya Maliasili. Kwanza naunga mkono taarifa za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza nizungumzie mgogoro kati ya wakulima, wafugaji na hifadhi za akiba za ardhi. Tulishazungumza mara kadhaa hapa kwamba zipo baadhi ya akiba za hifadhi ambazo hazina faida zaidi ya miaka 50 na ukimuuliza Waziri hii akiba ya hifadhi hii imeleta faida gani kwa Taifa hili au kwa wananchi hawa zaidi ya askari wa wanyamapori au askari wa misitu kuitumia kwa manufaa yao, kukamata wananchi na kuwatoza rushwa halafu kuwaruhusu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie hifadhi ya akiba ya Uwanda Game Reserve. Hifadhi hii ni zaidi ya miaka 50 na wakati hifadhi hii imetengwa idadi ya wananchi ilikuwa kidogo lakini sasa hivi hifadhi hii inazungukwa na vijiji zaidi ya 15, zaidi ya wananchi 26,000. Kwa hiyo, wananchi wanashindwa walime wapi, lakini hifadhi hii ukiiangalia faida yake haipo matokeo yake askari wanatumia hifadhi hii kwa manufaa yao binafsi. Mwananchi akisogelea hii hifadhi hata kwa kupita tu anakamatwa, anadaiwa pesa, asipokuwa na pesa anakamatwa anarundikwa ndani na wengine wamekuwa vilema, wengine wamepoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, tarehe 2 Januari, 2017, mwananchi mmoja anaitwa Luanda Salanganda Malele amepigwa risasi kwenye goti na askari anayeitwa Limomo baada ya kumkuta nje ya hifadhi. Akaambiwa kuna mtoto wako tumemkamata, akawaambia mimi sina mtoto aliyekamatwa, wakamdadisi kumdati pesa akakataa wakamwambia wewe una mazoea ya kujidai mjuaji tukikuomba pesa hutupati, wakaanza kumtishia kwa risasi. Katika kumtishia akakimbia akaenda kwenye nyumba ya jirani wakamtandika risasi kwenye goti, goti limechanikachanika sasa hivi yuko Muhimbili anasubiri kukatwa mguu.

**MBUNGE FULANI:** Looh!

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sisi kama binadamu Mwenyezi Mungu kweli anaweza akapenda maonevu ya namna hii? Hizi hifadhi zimewekwa kwa ajili ya binadamu tena tunaita hifadhi ya akiba,

tulishasema kwa nini Serikali isipite kufanya utafiti wa kina kuona hifadhi ambazo hazina faida, hata kama zina faida wanaangalia maslahi makubwa ya wananchi waweze aidha kurekebisha mipaka au kuziondoa kabisa. Kwa mfano, Uwanda Game Reserve haina manufaa kabisa kwa Taifa zaidi ya kusumbua wananchi kwa kuwakamata kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna Kamati inapita au Waziri aende kwenye hifadhi hii, akakutane na wananchi aweze kuzungumza nao wamueleze matatizo yao, vinginevyo yatatokea mapigano makubwa sana kwa hali iliyopo sasa hivi. Sisi tumebeba mzigo wa kila siku kutuliza hali hii ya hewa, kwa hiyo, tunaomba Serikali au Waziri afanye utaratibu wa kwenda kukutana na wananchi ili aweze kuwasikiliza na kutafuta muarobaini wa mgogoro huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni uhaba wa ardhi. Lazima tukubali ipo baadhi ya Mikoa au Wilaya zina uhaba wa ardhi na zina uhaba wa ardhi kwa sababu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Cecil kampa Mheshimiwa Ninja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba dakika tano na tano nitampa Mwalimu Bilago.

**MWENYEKITI:** Wewe umedandia, tano tu. (Kicheko)

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na nikiri kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii lakini katika taarifa ya Mwenyekiti aliyowasilisha utashangaa kwamba hakuna suala lolote linalozungumzia juu ya Faru John, hakuna suala lolote linalozungumzia juu ya Loliondo, ni burning issues kwa sasa hivi, Watanzania walitaka wapate majibu, lakini Kamati haikuweza kwenda ili kuweza kupata kielelezo ili kuleta Bungeni, ni jambo la kushangaza. Sijui ni Kamati ipi ambayo inaweza ikalifanya kazi zaidi ya Kamati ambayo ilikuwa maalum kwa ajili ya kuleta masuala haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa haraka, niongelee suala la kulinda corridors wanakopita wanyama, kama tulivyosikia kwenye taarifa ya Kamati ya Maliasili na Utalii, Wizara iliamua kuzuia maeneo ambayo ni mapito ya wanyama. Nazungumza hili kwa sababu wanyama ambao wanatoka Saadani kwenda Wamimbiki, Mvomero, Mikumi kuelekea mpaka Ruaha wananchi wamevunjiwa nyumba zao katika Wilaya ya Mvomero wakijumuisha pia

wananchi wa Manispaa ya Morogoro kutokana na kupisha hizi corridor za wanyama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kushangaza Serikali imewavunja wananchi nyumba hizi, haikuwalipa fidia lakini Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero imejengwa kwenye mapito hayo ya wanyama. Kama ni sheria ni lazima ikate pande zote mbili. Kuendelea kuwavunja wananchi nyumba zao bila kuwalipa fidia huku Serikali ikiendelea kuweka majengo ya Halmashauri na kujenga nyumba za wafanyakazi si kuwatendea haki wananchi. Naomba Wizara iangalie upya suala hili na kama kuna uwezekano walipe fidia kwa wananchi hawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mambo mengine ya migogoro ya wakulima na wafugaji Mkoani Morogoro. Ziko Kamati mbalimbali ambazo zimeundwa na Bunge hili lakini mpaka sasa hivi hakuna taarifa zozote ambazo zimefanyiwa kazi kusaidia kupunguza migogoro hii. Tunashuhudia watu wanapigwa mikuki ya midomoni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Rais akifuta hati mbalimbali za mashamba. Tatizo ni ardhi, kwa nini mashamba hayo yasirudi yakawasakiwananchi wa Wilaya za Mvomero na Kilosa ambako ndiko kwenye matatizo na migogoro ya kila siku? Hati hizi ambazo zimefutwa kwa nini ardhi hizi zisigawanywe kwa wananchi? Mpaka sasa ardhi zile zimeendelea kuwa mashamba pori pamoja na kufutwa huku wananchi wanaendelea kuwa na migogoro kutokana na uhaba wa ardhi. (Makofi)

Suala lingine ni kuhusu korongo lililojengwa la kuwatenga wakulima na wafugaji Wilayani Mvomero. Suluhu ya migogoro hii si kuendelea kuwatenga wakulima na wafugaji. Jamii hizi zinategemeana, hawa ni Watanzania, wanashirikiana lakini Serikali imeendelea na msimamo wake wa kuendelea kujenga korongo lile mbali na kwamba tulisema lisitishwe ili kutafuta suluhu katika ya makundi haya mawili ambayo yameendelea kuwa na migogoro ya siku hadi siku. Serikali imeendelea kutumia fedha zaidi ya shilingi milioni 17 kuendelea kuchimba korongo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mambo ambayo tunahitaji Wizara husika iyafanyie kazi ione. Kuna Kamati Maalum ya kutataua migogoro ya...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, huyu ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho. Sasa tunatoa nafasi kwa Serikali, tunaanza na Mheshimiwa Ole-Nasha dakika tano, atakuja Mheshimiwa Engineer Ramo dakika kumi, Mheshimiwa Angeline Mabula dakika kumi, Mheshimiwa Engineer Tizeba dakika

kumi na Mheshimiwa Engineer Lwenge dakika kumi. Tunaanza na Mheshimiwa Ole-Nasha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO A UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Kamati.

Kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na hatimaye kutuletea ripoti ambayo imesheheni ushauri amba ni mzuri. Kimsingi Kamati imekuwa karibu sana na sisi kama Wizara na tumeendelea kunufaika na ushauri wao, kwa kweli tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge amba kwa wingi wao wamechangia sana kuhusu masuala mbalimbali ya Wizara, masuala ya kilimo, mifugo na uvuvi. Inaendelea kuonesha namna gani Waheshimiwa Wabunge wanavyowajali wapiga kura wao amba wengi wao ni wakulima, wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, napenda kuchangia baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, kwa vyovypote vile na kwa sababu ya muda sitaweza kumaliza yote. Ya kwanza kabisa ni kuhusiana na suala la migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima na watumiaji wengine wa ardhi. Wizara inatambua fika kwamba hili ni tatizo kwa muda mrefu na imefika wakati kama wanavyoshauri Waheshimiwa Wabunge tatizo hili tukaondokana nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la migogoro ya ardhi ni suala mtambuka, linahusu Wizara zaidi ya moja. Ndiyo maana Serikali katika kuhakikisha kwamba tunalishughulikia tatizo hili imeunda Tume ambayo inashirikisha Wizara tano ikiwa inaratibiwa na Wizara ya Ardhi ili kwa pamoja tujaribu kuangalia migogoro hii ili hatimaye tuweze tukatafuta suluhu ya kudumu. Hivi tunavyozungumza, Tume hii ipo field na tayari imeshatembelea baadhi ya mikoa inawahoji wadau, inapitia ripoti mbalimbali za Kamati zingine za siku za nyuma kuangalia nini kilichosemwa na mwisho wake wataleta mapendekezo Serikalini ambapo na sisi tukishapata tutaleta mapendekezo kwa wadau mbalimbali mkiwepo ninyi Waheshimiwa Wabunge ili kwa pamoja tuangalie na tujadili namna gani ya kuweza kutokomeza hili tatizo ambalo kwa kweli limekuwa sugu kwa miaka mingi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge muwe na subira, ripoti itakuja, inawezekana ikaonekana kwamba imechelewa lakini tatizo la migogoro siyo tatizo dogo limekuwepo kwa miaka mingi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuzungumzia kuhusiana na hoja iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu madeni na ubadhirifu kwenye Vyama vya Ushirika hususan kwenye vyama vya korosho. Wizara yangu inatambua kwamba ubadhirifu katika Vyama vya Ushirika inachangia sana katika kudidimiza kilimo na ndiyo maana tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba tunakabiliana na wote wale wanaofanya ubadhirifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni COASCO imekamilisha kupitia mahesabu ya vyama 200 Mtwara na Lindi na imebaini kwamba kuna upungufu mkubwa na kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha za wananchi. Napenda kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Mikoa ya Lindi na Mtwara kwamba tupo njiani kwenda kuhakikisha kwamba tatizo hili linashughulikiwa na wale wote ambao wamehusika watachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuvunja Bodi za Vyama vya Ushirika hivyo 200. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa vilevile suala la Hifadhi ya Ngorongoro na Loliondo. Napenda kusema machache, Hifadhi ya Ngorongoro kama alivyosema Mheshimiwa Sakaya ni hifadhi ya kipekee sana duniani. Upekee huu pamoja na mambo mengine ni kwa sababu ni hifadhi ya pekee duniani ambayo binadamu anaishi kwa amani na wanyamapori. Hiyo ndiyo imeipatia Ngorongoro kuwa na sifa hiyo ya kipekee na Serikali inatambua hilo na inaendelea kushughulikia changamoto mbalimbali zilizopo ili tabia hii ya wananchi kukaa vizuri na wanyamapori iendelee kutokea.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Engineer Ramo dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii lakini nianze kwa kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa namna ambavyo tumekuwa tukishirikiana kufanya kazi na kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kusema kabisa mapema kwamba naunga mkono maoni na mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati, nasema mapema kwa sababu pengine muda hautatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ziko hoja ambazo nitazipitia haraka haraka katika muda huu mfupi uliopo. Hoja ya kwanza, naona wazi kabisa kwamba Wabunge wote wanakubaliana juu ya umuhimu wa utalii nchini hata michango yao na hoja zote walizozitoa zimejielekeza hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kukumbushana tu ni kwamba kwa sasa hivi Pato la Taifa linachangiwa na utalii kwa 17.2% wengine wanasema 17.5% lakini tuna kazi ya kuendelea kuboresha kwa sababu mwaka 2020 tunatakiwa tuwe tumefikia 18.3% na mwaka 2025 tunatakiwa tuwe tumefikia 19.5%. Yapo mambo ambayo tumekumbushwa na Kamati kwamba tuyafanye vizuri na Wizara imeyachukua kwa ajili ya kwenda kuyafanya kazi. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mambo hayo kuboresha miundombinu, lakini nataka nikumbushe tu kwamba upande wa miundombinu sio kila miundombinu ya utalii inatekelezwa na Serikali. Ipo inayotekelze na Serikali ambayo ni ile ya kuelekea kwenye vivutio na ile ya ndani ya vivutio tutaelekeza nguvu katika maeneo hayo kwa kushirikiana na Wizara nyingine kama Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa ajili ya kuboresha miundombinu lakini iko miundombinu kama ya hoteli ambayo haitekelezwi na Serikali. Kwa hiyo, kule tutashirikisha tu wadau na sekta binafsi ili waweze kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuboresha utalii wa ndani, tayari tumekwishaanza jitihada na jitihada zenyewe ziko katika kutangaza lakini pia katika kuweka mazingira ambayo yatawawezesha watalii wa ndani waweze kupata huduma ya usafiri kwenda haraka. Upande mwingine wa ku-facilitate utalii wa ndani ni upande wa malazi. Wapo Wabunge wametoa hoja hapa kwamba gharama za malazi ni ghali sana kule pengine Serikali ifanye utaratibu wa kupunguza gharama. Katika hifadhi karibu nane au tisa hivi tunazo tayari hostels ambazo zina gharama nafuu lakini pia tunazo nyumba za bei rahisi kwa ajili ya watalii wa ndani, lakini tutaendeleza jitihada hizi ili katika kila eneo ambapo kuna vivutio tuweze kuweka mazingira ambayo watalii wanaweza wakaenda wakiwemo watalii wa ndani na waweze kufanya utalii kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la kuboresha upande wa Ukanda wa Kusini. Upande wa Ukanda wa Kusini tayari tuna mradi unaitwa REGROW ambao unajielekeza katika kujenga circuit ya Kusini ya utalii na huku tunajielekeza katika hifadhi kama vile ya Kitulo lakini pia zile nyingine za Katavi lakini pia ukanda mzima ule. Hapa niishukuru Serikali kwa kufungua upande wa Kusini mwa nchi, baada ya kuwekwa barabara ya lami sasa unaweza ukatoka Makambako ukafika mpaka Mtwara kwa barabara ya lami. Barabara ile inaweza sasa ikatumiwa vizuri sana na watalii wanaotoka Kusini mwa Afrika wakitokea upande wa mpaka wetu wa Kusini mwa nchi wanaweza wakatumia barabara ile sasa na kuunganisha Kusini na Mashariki mwa nchi kwa ajili ya kuboresha utalii. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuboresha bidhaa za utalii kwamba tuna utalii wa aina moja, nataka niseme tu kwamba tayari tumeshapitia fukwe mbalimbali za bahari na maziwa lakini kwa upande wa fukwe za bahari tumeshapitia fukwe karibu 74 lakini hizi fukwe zina ownership mbalimbali. Wenye

hizo fukwe ni watu binafsi, mahali pengine ni Serikali, sasa bado tuko kwenye utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunaboresha mazingira ambayo yatawezesha uwekezaji katika maeneo hayo ili tuweze kujielekeza kwenye maeneo mengine ya utalii ukiwemo utalii wa kiutamaduni na utalii wa kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia utalii ingawaje ni kwa kifupi tu nizungumzie kuhusu uhifadhi. Hakuna utalii bila uhifadhi. Suala la uhifadhi limejadiliwa hapa kwa hisia mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamezungumzia kuhusu changamoto mbalimbali za uhifadhi. Kwa sababu ya muda, mimi niseme tu kwa kifupi, niseme maoni yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, *interest* zote za wadau mbalimbali nchi nzima, maslahi ya mtu mmoja mmoja, maslahi ya vikundi mbalimbali yote yatazingatiwa lakini mwisho wa siku tutazingatia maslahi ya Taifa. Ni vigumu sana kukidhi haja ya maslahi ya mtu mmoja au kikundi wakati maslahi ya Taifa yanaangamia. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kifupi nikisema hivyo nikienda kujielekeza sasa kwenye zile changamoto za uhifadhi niseme tu kwamba maeneo yote na hii nachukua kutoka kwenye hoja na maoni ya Kamati kwamba hakuna utata kuhusu suala la mifugo yote kuondoka ndani ya Hifadhi za Taifa. Tulisema kwamba yako maeneo ambayo mipaka ya baadhi ya vijiji inaingia ndani ya hifadhi na yako maeneo ambapo baadhi ya vijiji viko ndani kabisa ya hifadhi. Sasa huko kuna changamoto ambazo ni za kisheria zimo ndani ya Serikali, tunazifanya kazi, tutaweza kuja kupambanua kujua kwamba sasa vijiji vile ambavyo vina utata wa namna hiyo tupitie sheria kwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko vivutio vikubwa muhimu sana kama Ngorongoro kwa mfano kutaja vichache. Ngorongoro umuhimu umeelezwa, lakini mimi niongezee tu kwamba hapo mwanzoni tulikuwa na umuhimu wa Ngorongoro kwa sababu ya Crater zile tatu, Ngorongoro Crater yenyewe, Empakai Crater na Olmoti Crater. Hata hivyo, hivi karibuni utalii wa historia umejumuisha eneo la Olduvai Gorge pamoja na zile nyayo za Laetoli. Haya mawili yamefanya kupandisha hadhi ya Hifadhi ya Ngorongoro kuwa kubwa zaidi na kwa hiyo dunia nzima sasa hivi inakwenda kuona umuhimu wa Ngorongoro zaidi ya vile ambavyo tulikuwa tunaona hapo mwanzoni. Sasa zile changamoto za mifugo kuingia ndani, watu kujenga ndani majengo pamoja na watu kufanya huduma zingine za kijamii zote hizo sasa hivi ni changamoto ambazo tunatakiwa kwenda...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Angeline Mabula.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kwanza kwa kuishukuru sana Kamati na kuunga mkono pengine na kusema kwamba tunapokea ushauri ambao wameutoa ikiwa ni pamoja na ile addendum ambayo imeletwa kama Serikali tumeipokea na tutakwenda kuifanyia kazi. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi wamezungumzia masuala ya migogoro na kama mwenzangu wa kilimo alivyozungumza, suala hili la migogoro ni mtambuka. Nitapitia wachache ambao nimejaribu ku-note, ukiangalia suala la migogoro, zaidi ya Wabunge 15 wamezungumzia. Naomba nianze kwa kusema kwamba ushauri uliotolewa na Kamati tumeupokea kama ulivyo, wamezungumzia suala la National Housing kwamba nyumba ni za gharama nafuu, lakini ubora si mzuri sana. Hilo tumelipokea na tutakwenda kupitia tena kuona ni jinsi gani ambavyo watakwenda kuboresha. Sehemu kubwa pia hata ile size ya nyumba zinapoungwa mbili wengi wamesema hawazipendi sana katika kutembelea waliyazungumza hayo. Kwa hiyo, tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikija kwa hoja ya Mheshimiwa Sakaya ambayo alizungumzia habari ya Kamati iliyoundwa na Wizara tano ambazo hazijajulikana zinamaliza muda wake lini pamoja na Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Pauline Gekul wote walitaka kujua taarifa hizi zitakuja lini.

Mimi niseme tu kwamba tarehe 13 Februari, taarifa ya kwanza itatoka na wamepitia katika mikoa mitano, wamekwenda Tabora, Katavi, Morogoro, Geita na Kagera. Kwa hiyo, taarifa ya kwanza tutaipokea kutoka katika mikoa hiyo. Baada ya hapo awamu ya pili wanakwenda katika Mkoa wa Arusha, Manyara, Tanga na Pwani, kwa hiyo, tutawapa ratiba kamili watakapokuwa wanakwenda kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sakaya pia alitaka kujua namna ambavyo tunaweza tukasaiadia Halmashauri kuhakikisha kwamba viwanja vinapimwa na kuondoa hii migogoro. Niseme tulikuwa na ule mfuko na bado upo lakini haufanyi kazi vizuri sana kwa sababu Halmashauri zetu zinakopa na hazirudishi. Jumla ya Halmashauri 27 zilishakopeshwa kiasi cha shilingi 962,676,000 lakini kati ya hizo Halmashauri 11 hazijalipa, bado zinadaiwa. Kwa hiyo, pesa ambayo ilitakiwa irudi ni shilingi 1,155,211,224.

Kwa hiyo, niwaombe tu Halmashauri ambazo zinadaiwa mrejeshe ikiwemo Halmashauri ya Magu, Mji Mdogo wa Makambako, Kagera, Bunda kwa maana ya Chato lakini kuna Singida, Sengerema, Iringa, Tumalenga, Ruvuma, Songea na Tarime. Hizi ni Halmashauri zinazodaiwa, tuwaombe sana mrejeshe ile mikopo ili na wengine waweze kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala la kusaidia, tuseme tu kwamba kanda zetu tumejaribu kuziimarisha, lakini tatizo tulilonalo kwa nchi nzima tuna upungufu wa watumishi wa sekta ya ardhi kwa asilimia 64. Kwa hiyo, utaona kwamba kuna upungufu mkubwa ambapo kwa kweli kuweza kukidhi haja inakuwa ni ngumu. Pamoja na upungufu huo, tunazo Halmashauri kama saba ambazo hazina kabisa wataalam hao, kwa hiyo, unaweza ukaona changamoto jinsi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ambavyo tunajaribu kuimarisha kanda zetu, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge pale mnapokuwa na ratiba za upimaji shirkisheni ofisi zetu za kanda, kwa sababu tunatarajia watakuwa tayari warmekamilika na timu nzima za wataalam lakini pia na vifaa vya upimaji. Kwa sababu unakuta kanda moja pengine inasimamia Halmashauri zaidi ya 18 mpaka 36, basi niombe tu ile ratiba iweze kwenda vizuri ili hawa nao wasaidie katika kupima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sehemu kubwa ni jukumu letu katika Halmashauri zetu kuona ni jinsi gani tunapanga mikakati yetu vizuri kuweza kuweka utaratibu wa kupima kila mwaka na kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi, tukiweka angalau vijiji vitatuau vinne kila mwaka tutasogea. Gharama siyo kubwa ni kati ya shilingi milioni sita mpaka 7 na kuna vijiji vingine vina uwezo basi tuwashirikishe wale waweze kuona ni jinsi gani wanaweza wakahudumiwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ku-subsidized nyumba za National Housing hili tulichukue tu tulifanyie kazi, kwa sababu ni mashirika mengi yanayojenga, bado TBA, WatumishiHousing, NSSF kila mmoja atataka kunufaika na pungozo hilo. Kwa hiyo, niombe tulichukue tutaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la mashamba ambapo wamezungumzia kwamba kasi ni ndogo pengine na gharama ya kuweza kuyapima. Mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwenye maeneo yetu sisi ndiyo tuna mashamba hayo na tunatambua jinsi gani ambavyo hayajaendelezwa. Kazi ya Wizara ni kupokea kile ambacho mmeona hakifanyi kazi vizuri na kimekiuka taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwaombe wakati wanafanya kazi zao wale watumishi wa idara husika iwe ni sehemu ya kazi zao. Mmaana hapa mmesema hakuna pesa anahitaji pesa lakini akiweka kama ni sehemu ya kazi zake za kila siku, yule anayefanya kazi za uandani anapokwenda kufanya kazi kule basi afanye na kazi hii itasaidia sana katika kuona ni jinsi gani tunaweza tukapunguza au tukatoa taarifa za haya mashamba. Tusingubiri hela za kuja kupimiwa au kukaguliwa kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Njeza amezungumzia suala la mipango miji, naomba nikiri tu hili nalo ni kutokana na upungufu tulionao. Pia tunaomba sana kwa sababu wenzetu wa Mbeya wako katika mpango kabambe wa *master plan* basi hilo nalo liingie katika mpango huo, itasaidia sana katika kuona ni jinsi gani tunaweza tukaweka mpango mzuri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la ile project ya Kawe, imezunguziwa kwamba amepewa mtu binafsi kwa US dollar milioni 6.5.

Naomba niseme tu kwamba tungeweza hata kuishukuru Serikali kwa namna ilivyoweza kuokoa, kwa sababu lile lilikuwa imewekwa chini ya PSRC na ndipo hapo Wizara ikaomba kuitia *National Housing* ili kuweza kuchukua ile fifty, fifty angalau eneo lingine lirudi Serikalini. Isinge kuwa hivyo basi basi eneo lote lilikuwa limeshaondoka. Mimi nasema kwa kweli lile eneo na gharama yake ni kubwa kwa maana ya kwamba lina-appreciate kila siku. Kwa hiyo, kitendo cha kuchukua asilimia 50 ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Engineer Tizeba dakika kumi ajiandae Mheshimiwa Engineer Lwenge.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami kwa kuanzia niishukuru sana Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa taarifa nzuri ambayo kwa ukweli imegusa maeneo yote muhimu ambayo wao wana wajibu wa kuyasimamia na kutoa ushauri kwa Serikali. Nawashukuru sana tumefanya kazi vizuri na niseme tu mapema kwamba yote ambayo wamependekeza na kutolea ushauri tumeyachukua, mengine tutayafanya kazi mara moja na mengine ambayo yanahitaji muda tutaendelea kuyafanya kazi kadri muda utakavyokuwa unakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza mambo mengi na kwa hisia sana. Hisia hizo zinaonesha ni kwa kiasi gani wanaguswa wao na wananchi wanaowawakilisha na haya mambo ambayo wameyazungumzia. Kilimo katika tafsiri yake pana kinamgusa kila mtu na kwa hivyo haishangazi na kwa kweli lazima utegemee mjadala utakaokuwa unahu kilimo uwe na sura hii. Mimi mwenyewe ningeshangaa kama mjadala wa Kamati hii ungekuwa na sura tofauti na hii niliyoiona hapa ndani. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, niombe nizungumzie tu mambo machache ambayo mwenzangu Mheshimiwa Ole-Nasha hakuyagusa. Nianze na suala la tozo. Suala la tozo limekwishatolewa kauli na Mkuu wa nchi

kwamba zote zile ambazo ni za hovyo hovyo na zenyе usumbufu Serikali izifanyie kazi na iziondoe. Ziko tozo ambazo hazikuwa na madhara ya kibajeti katika mazao tumeziondoa, kwenye korosho, tumbaku, pamba tumezifuta. Ziko tozo ambazo zilikuwa na madhara ya kibajeti kama tungezifuta mara moja. Kwa hivyo, hizi zinafanyiwa kazi iko Kamati ya Serikali ya Makatibu Wakuu wanaendelea kufanya kazi na kwa kweli tutakapoingia katika bajeti hii ya mwaka huu tozo nyingi mtaona zitakuwa zimeondolewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo hizi haziathiri tu bei za mazao na mambo mengine lakini ziko tozo pia zinazoathiri kilimo ambazo haziko kwenye mazao. Waheshimiwa hapa wamezungumzia ghamama kubwa ya pembejeo, mbolea tu inazo tozo 14 mbalimbali. Kwa hiyo, tunavyozungumzia kushusha ghamama ya pembejeo pamoja na hatua zingine ambazo tumejipanga kuzichukua, lakini itabidi pia tuangalie katika hizi tozo zilizopo kwenye mbolea ili mjumuiko wa hatua hizo utuhakikishie kwamba mbolea itashuka bei kiasi kwamba wakulima na watumiaji wengine wa pembejeo wataweza kumudu bei bila wakati mwingine kulazimika kuweka ruzuku katika pembejeo hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Haonga analiona hilo, kwamba tunao uwezekano wa kufika mahali tukaondoa ruzuku kwenye pembejeo kama tutaweza kushusha bei zake katika *levels* ambazo mkulima wa kawaida anaweza kuzimudu. Hatua kadhaa zinachukuliwa, moja, ni kama alivyosema kununua moja kwa moja kwa wazalishaji wa hizi pembejeo. Tumefanya hivi mwaka huu na kwa kweli mbolea imeshuka bei kwa wastani wa asilimia karibu 28. Tutaendelea kuchukua hatua zingine za kupunguza kodi hizi, lakini pia kuna mazungumzo mazuri sasa hivi ya ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza sulphur hapa hapa nchini. Tukifanikiwa kufanya hivyo maana yake ni kwamba hata bei ya sulphur tunayoinunua sasa hivi kwa bei kubwa huko nje na yenyewe itashuka bei. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie haraka haraka suala la mbegu. Mbegu ni tatizo kweli, bado utoshelevu wetu wa mbegu bora uko kwenye asilimia 40 Kitaifa, kwa hivyo asilimia 60 bado tunaagiza nje. Mbegu inayozalishwa hapa ndani ina changamoto moja kubwa kwamba inatozwa kodi wakati mbegu zinazoagizwa nje ya nchi hazitozwi kodi. Hata mimi haiingii akilini, ni kwa sababu kwa kufanya hivyo, mbegu inayozalishwa Tanzania inakosa ushindani lakini inakuwa inakatisha tamaa kwa wazalishaji wa ndani kuzalisha zaidi kwa sababu hata wakizalisha mbegu inayotoka nje inakuwa na ushindani zaidi kuliko ya hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo totalitazama katika Serikali na kwa kweli nadhani ni jambo ambalo tunaweza tukaliondoa tu mara moja ili kuwapa motisha wazalishaji wa ndani wa mbegu tuweze kujitosheleza. Wakala wetu wa Mbegu wa Taifa nimekwishawapa maelekezo, mashamba yote ambayo

wameyatunza yamekuwa mapori, wawape watu wenye uwezo wa kutuzalishia mbegu waingie nao mikataba kwa masharti ambayo yatakuwa yanawawezesha wale watu kuzalisha bila kupata hasara. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la fedha katika Wizara ya Kilimo. Kamati imeona kweli kwamba bajeti iliyokwishatolewa mpaka sasa ni kidogo, labda nitoe taarifa kwamba kilimo kinapata fedha nyingi nje ya mfumo wa bajeti ya Serikali. Leo tunavyozungumza, fedha ilioingia katika kilimo kuitia vyanzo tofauti na bajeti ya Serikali iko kwenye tune ya shilingi trilioni 1.7, hii si hela kidogo katika kilimo cha nchi hii. Tunapata fedha nyingi kwenye kilimo nje ya mfumo wa bajeti kuitia mashirika mbalimbali kwenye SAGCOT na kadhalika. Bill & Melinda Gates Foundation peke yake imeingiza Tanzania dola milioni 700 ambazo zimeelekezwa kwenye kilimo, wacha World Bank, AGRA na wengine. Kwa hiyo, kilimo kwa maana ya bajeti ambayo inapita kwenye Wizara ni fedha inayoonekana si nyingi sana lakini fedha nyingine inakwenda kwenye Halmashauri lakini wafadhili wengi wanapeleka moja kwa moja kwenye programu na miradi mbalimbali ya kilimo inayotekelizwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza na taasisi za fedha, zimekubali pia sasa kuanza kukopesha, kutoa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kilimo. NMB peke yake wametenga mwaka huu wa fedha shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kukopesha miradi ya kilimo na shughuli zingine zinazohusiana na kilimo. Kwa hiyo, tukitumia hizi fursa vizuri kilimo chetu kitasonga mbele.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuna hoja hapa ilikuwa nzito sana na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amejaribu kuijibu, lakini na yeye atakuletea wewe. Kuna hoja hapa kuwa mbegu zinazotengenezwa na viwanda nchini Tanzania, za viwanda vya kizalendo kwa azma hii ya viwanda Tanzania inatozwa kodi. Mbegu zinatoka nchi za nje zinapita kwenye mipaka ya Tanzania kwa kibali cha Serikali bure. Je, mwaka huu tutapata unafuu kwa haya mambo ya kilimo? Kama huna majibu acha lakini ilimradi meseji nimeshakuletea, nakushukuru. Tunaendelea na Mheshimiwa Engineer Lwenge. (Makofij)

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi uliyonipa. Nianze kwanza kwa kuishukuru Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa uongozi wake mzuri ambao umesaidia sana Wizara yangu katika kutekeleza majukumu ya kuwapatia Watanzania maji safi pamoja na kilimo cha umwagiliaji. Pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, wamezungumzia kwa uchungu kabisa matatizo ya wananchi wetu wanaokosa huduma ya maji hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hatujafikia malengo, ukiangalia Azimio Namba Sita la Umoja wa Mataifa linasema kwamba nchi wanachama wote wahahakikishe wananchi wao wanapata maji kwa asilimia 100 ikifika mwaka 2030. Sasa Tanzania ni mwanachama lakini sisi kwa nchi za Afrika tuliamua kwamba jambo hili la kuhakikisha kwamba tunawapatia wananchi maji safi na salama kwa haraka zaidi kuunda Umoja wa Mawaziri wa Maji katika Afrika ambao unajulikana kwa jina la AMCOW na Tanzania imepewa heshima ya kuwa Mwenyekiti kwa miaka miwili kuanzia mwaka 2016 mpaka 2018. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba Rais wetu ndiyo atakayekuwa anazungumzia suala la maji kwenye vikao vya Umoja wa Nchi za Afrika kwamba mmefanya nini. Mnajua jambo hili la kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji ni lazima tuwe na nguvu ya pamoja. Kama tulivyobuni katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwamba haitawezekana Serikali peke yake kuweza kufikisha huduma ya maji kwa wananchi wote ni lazima tuwe na nguvu ya pamoja ya Serikali, wananchi pamoja na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mwaka 2007/2008 mpaka Juni 2016 tulianzisha Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ya awamu ya kwanza. Washirika wa maendeleo pamoja na Serikali waliweza kuweka fedha kwenye mfuko kiasi cha bilioni 1.6 ni karibu trilioni 3.2, hizi ni fedha nyingi na tumeweza kujenga miradi mingi zaidi ya miradi 1,800 ili kuondoa hali ilivyokuwa huko mwanzo na sasa tumefikia mahali ambapo angalau wastani wa maji vijiji, wananchi wanapata kwa asilimia 72. Hii haina maana kwamba kila kijiji kina asilimia 72, viko vijiji vingine vina asilimia 30 na vingine vina asilimia 80. Sasa ukichukua wastani kwa kuangalia idadi ya watu wanaopata maji kwenye vituo ambavyo vimejengwa imefikia asilimia 72.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo tunalipata ni kwamba Serikali imejenga miradi mingi lakini miradi mingi haifanyi kazi kama Waheshimiwa Wabunge mnavyosema. Serikali pia imeanza kubuni mradi mwagine wa kuhakikisha hii miradi iliyojengwa kwa fedha nyingi za Serikali iinakuwa endelevu na inafanya kazi. Tumefanya tathmini wastani wa asilimia 30 ya miradi mingi iliyojengwa haifanyi kazi. Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la DFID tumeanzisha mpango mwagine wa kuhakikisha miradi hii inakuwa endelevu, imetoa kama Euro milioni 80, bilioni 214 kwa kila kituo cha maji kitakachotengenezwa na Halmashauri wanapewa fedha zaidi ya paundi 1500. Mpango huu tumeshaupeleka nchi nzima kwa Halmashauri 185.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge tuzihamasishe Halmashauri zetu ziingie kwenye mfumo huu ili miradi yote ambayo tayari tulishajengwa na tumetumia fedha nyingi iweze kufanya kazi

na wananchi wetu waweze kupata maji. Ni Halmashauri 57 ndiyo zimeitikia wito huu, naomba Halmashauri zilizobaki pia ziingie kwenye mpango wa kujenga vituo vya maji. Ukishajenga kituo kimoja unaongezewa fedha na DFID ili kusudi uweze kujenga vituo vingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika programu ambayo tumeanza Julai, 2016 awamu ya pili ya programu tayari washirika wa maendeleo wameweza kupledge kiasi cha dola bilioni 1.6 ambazo zitaingia kwenye utekelezaji wa miradi, katika vile vijiji ambavyo vilikuwa havijapata miradi tutaviingiza kwenye hii program. Tayari nimetayarisha mwongozo toka mwezi wa Julai, nitawapa nakala Waheshimiwa Wabunge kabla hamjaondoka muondoke na huu mwongozo wa kuhakikisha kwamba Halmashauri zetu kwanza zinakamilisha miradi iliyokuwa inaendelea na pia zinaanzisha miradi mipya ili kusudi tufikie hii mipango ya Serikali. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepita kwenye Halmashauri unakuta wanasema kwamba tunasubiri fedha, fedha haziwezi kuja kwa sababu hata zikija huna kitu cha kufanya. Unatakiwa uanze maandalizi, uweze kufanya manunuzi baada ya pale hela itakuja kwa certificate. Mfumo huu umetusaidia toka Januari mpaka Desemba tumepeleka shilingi bilioni 177 kwenye Halmashauri zetu kwa ajili yamaji vijijini na miradi mingi imekamilika sasa hivi wananchi wanapata maji. Tumesafika zaidi ya asilimia 76 kwa sababu miradi inakamilika na wananchi wanaendelea kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana ndugu zangu tusibaki tunasema fedha haziji, fedha zinakuja kwa kazi maalum, haziwezi kuja zikakaa tu. Tumekuta baadhi ya Halmashauri wanazo fedha kwenye akaunti lakini hakuna wanachokifanya. Sasa nasema tuache ufanyaji kazi wa kimazoea, lazima kila wakati watu twende kwenye mfumo wa kutoa matokeo. Tukija kwenye mfumo wa kutoa matokeo nina hakika wananchi watapata maji kulingana na malengo ambayo Serikali imeweza kuweka. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema maji ni uhai, maji ni uchumi na maji pia ni utu. Hautaweza kujenga viwanda kama maji hakuna. Hivi vitu vyote lazima tufanye kwa pamoja. Najua kabisa Serikali inaweza bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuweza kuandaa miradi mikubwa. Kila mmoja alikuwa anasimama hapa anataka maji ya Ziwa Victoria, anataka maji ya mito mikubwa, tutakwenda kufanya vile jinsi tunavyojenga uwezo wa nchi. Hata hivyo, kwa kuanzia tulisema tuanze na miradi ambayo uendeshaji wake unaweza kufanywa na vijiji lakini jinsi tunavyoendelea...

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Taarifa.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Lazima Serikali tutaingia kwenye miradi mikubwa. Nitasema miradi michache ambayo kwa mwaka huu wa kwanza tumeweza kufanya.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, tulikuwa na mradi...

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo. Mheshimiwa Mbogo.

## TAARIFA

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, ameelezea kwamba sasa hivi miradi yote...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kaa.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** ...inabidi certificate ije Wizarani na ndiyo watoe fedha. Hata hivyo, Disemba, Ofisi yake kupitia Katibu Mkuu Msaidizi walitoa mwongozo unaolekeza kwamba miradi ya zamani ndiyo certificate itakuja na hii miradi mipyä fedha zitakuja kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda hiki anachokieleza hapa ndiyo inavyotakiwa lakini Watendaji wetu wa Halmashauri wanahitaji ku-act kwenye maandishi yaliyotoka Wizarani tofauti na maelekezo ambayo anayatoa hapa kwani hii itatusaidia miradi hii mipyä fedha zije na tuweze kutekeleza. Kama maagizo haya anayatoa ndiyo yanayotakiwa kufuatwa basi watoe waraka uende kwenye Halmashauri zetu ili waanze kutekeleza. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, angenipa nafasi ili kusudi niweze kumuelewesa aweze kuelewa. Nimesema tulishatoa mwongozo toka Julai tulivyoanza mwaka wa fedha ambao unaelezea kila kitu kuhusu miradi inayoendelea pamoja na miradi mipyä. Na mimi nitampa nakala ya mwongozo huo aangalie ili akasimamie Halmashauri yake nini cha kufanya. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge mnielewe na mnikubalie kwa sababu tukianza

kubishana hapa ndiyo maana miradi haiendi, naomba sana. Wabunge wote nitawapa mwongozo, nitawapa na taarifa ya utekelezaji wa programu ya awamu ya kwanza. Kwa hiyo, tumepeleka kwa maandishi na pia tumewafanyia semina hawa Wakurugenzi na Wahandisi wa Maji kuhusu jambo hili, lakini unafika mahali mtu bado anashangaa shangaa, haelewi cha kufanya. Sasa hayo ni majipu itabidi tuanze kuyatumbua. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niseme baadhi ya mafanikio ambayo tumeweza kupata. Mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Mto Ruvu, Ruvu Chini na Ruvu Juu umekamilika. Hivi sasa tunaweza kuzalisha maji lita milioni 502 kati ya milioni 544 zinazohitajika kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam. Tatizo letu tulilonalo lilikuwa ni mtandao na sasa hivi Serikali tunaendelea na kujenga mtandao maeneo yote ambayo hayana mtandao ili kusudi waweze kupata maji. Kwa mwaka huu wa fedha Serikali itaweka fedha zaidi katika kujenga mtandao katika maeneo ambayo hayana maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielezee mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Ziwa Viktoria kupeleka Tabora, Nzega na Igunga mpaka Sikonge. Tayari tumeshapata mkandarasi, tumepeleka Serikali ya India tupate no objection ili tusaini mkataba, mkadarasi yule aweze kuanza kufanya kazi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi pia wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Miji ya Magu, Misungwi, Lamadi na kupanua maeneo ya Illemela katika Jiji la Mwanza. Tarehe 16 tunasaini mkataba, Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo nawakaribisha tuje tusaini mkataba na kazi ile inaanza mara moja. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa kutoa maji ya Ziwa Victoria kupeleka miji ya Kagongwa, Tinde na Isaka, tayari mkandarasi tumeshampata tuko kwenye maandalizi ya kuweza kusaini mkataba na kazi ile itaanza mara moja. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umezungumziwa mradi wa milioni 500 wa Serikali ya India wa Mheshimiwa Deo Sanga, Mji wa Makambako, Muheza pamoja na ile Miji 17 ikiwa ni pamoja na Zanzibar. Hatua tuliyofikia mpaka sasa tuko kwenye hatua ya kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya usanifu wa kina na kutengeneza makabrasha ya zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu tunavyoanza mwaka wa fedha 2017/2018 tender zitatangazwa na kazi ile itakwenda kuanza kufanyika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Deo Sanga pamoja na wale wote wa miji ile 17 tunakwenda kuikamilisha kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa. (Makof)

**MWENYEKITI:** Sasa namwita mwenye hoja, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kufanya majumuisho ya hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Namshukuru Makamu Mwenyekiti kwa kuwasilisha taarifa vizuri asubuhi na nawashukuru Wajumbe kwa maandalizi mazuri ya taarifa yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvubi pamoja na Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa kutoa ufanuzi kwa hoja mbalimbali ambazo zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia kwa maandishi na kwa kuzungumza. Wingi wao umeonesha jinsi sekta hii ilivyo muhimu na nyeti sana kwa wananchi na kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge 60 wamechangia ambapo 25 walichangia kwa maandishi na 35 walichangia kwa kuzungumza. Kwa muda ulionipa, naomba nisipitie orodha hiyo lakini nimeihifadhi na Waheshimiwa wanaweza kuja kuona ili waone kwamba mchango wa kila mmoja umechukuliwa na unafanyiwa kazi kuboresha taarifa ya sekta hii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhitimisha hoja za Kamati kama ifuatavyo. Kwanza, nikiri kwamba hoja zile zilizotolewa kwa kweli zimeboresha taarifa yetu. Kuna Wabunge wawili walioleta ammendments ambazo tutaziongeza na nitapenda kusema ni kwa namna gani tutaziongeza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zote zilijadiliwa lakini naomba niongelee hoja chache tu kwa sababu ya muda na ninyi wote mnajua muda huu ni mfupi sana. Nitajitahidi kama muda utaniruhusu nitakwenda kwenye hoja kadri ambavyo zitakuja kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mgogoro wa wakulima na wafugaji. Mimi nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba si jambo dogo, ni kubwa. Wananchi wa Tanzania walio wengi ni wakulima na wafugaji na kama wao hawatakuwa wanapatana, ni migogoro kila wakati mfahamu ya kwamba na wao wenyewe wataathirika lakini maendeleo ya nchi yatakuwa yameathirika kwa kiasi kikubwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi inatokana na ardhi. Suala la mgogoro wa ardhi linahusisha wakulima na wafugaji kwa kiasi kikubwa. Nataka niseme kwamba kuna mgogoro wa wakulima au wafugaji na hifadhi, kuna mgogoro wa wakulima na wafugaji na wawekezaji, hakuna namna nyingine ya kumaliza migogoro hii bila ya Serikali kutekeleza kwa vitendo mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kupima na kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za kilimo, mifugo, uhifadhi na shughuli nyingine za binadamu kama Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999 inavyotaka. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mchengerwa ameleta hoja hapa, yeye ametaka tuondoe hoja ya Kamati. Mimi naomba hoja ya Kamati ibaki kwamba Bunge liazimie Serikali iongeze kasi ya kutekeleza kwa vitendo mpango wa matumizi bora ya ardhi kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999 na Bunge linaazimia kwamba mgogoro wa wakulima na wafugaji sasa ushughulikiwe katika ngazi ya Kitaifa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini kwa kuwashirikisha wadau wenyewe. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu nataka kusema kwamba Watanzania ni vizuri sana wafahamu kwamba ardhi ni mali ya asili na mali ya asili ambayo inatupa sisi maisha. Mifugo ni mali ya mtu mmoja-mmoja, lakini hata hivyo mifugo ni mali ya asili ya Taifa vilevile. Ni kweli kwamba kuna maeneo ambayo hayana utamaduni wa kuwa na mifugo, lakini kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, Watanzania wana uhuru wa kwenda kila mahali lakini kwa utaratibu uliowekwa. Na mimi naona suala hili ambalo linawapa taabu hasa Mikoa ya Kusini na ile ambayo haikuwa na utamaduni wa mifugo, Serikali na wadau wanaohusika tujaribu kuangalia matumizi bora ya ardhi yanatekelezwa na sio kusema kwa mdomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi ndugu zangu kwa sababu Ethiopia ina ng'ombe milioni 55, Sudan ina milioni 38, sisi tuna milioni 25.8, tuna ng'ombe wachache kuliko wenzetu na ukiangalia nchi zile zina jangwa kuliko hata Tanzania. Kwa hiyo, jambo kubwa ni kwamba sisi hatujajipanga na tukijipanga tutaondoa migogoro hii, wakulima walime kwa amani na wafugaji wafuge kwa amani kwa manufaa ya Taifa letu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nilisemee hapa ni kuhusu ruzuku ya pembejeo. Ndugu zangu kama tunataka tuwe na tija kwenye kilimo suala la pembejeo halina mjadala. Kwa kweli, Wabunge waliochangia hoja hii wameeleza jinsi pembejeo za kilimo zisivyowafikia wakulima kwa wakati na hivyo kukwamisha shughuli za kilimo. Wamependekeza pembejeo za kilimo ziuzwe madukani ili kuwapa wakulima fursa ya kununua pembejeo wakati wowote wanapohitaji na tozo yoyote iondolewe kwenye pembejeo ili waweze kumudu bei ya kununua na hivyo kuhakikisha kwamba tija ya kilimo inakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye pembejeo kuna suala la mawakala, naomba mmalize uhakiki Mheshimiwa Waziri. Hatuwezi kuendelea na uhakiki kwa mwaka mzima. Tukishahakiki tuwalipe mawakala wale ambao wanastahili kulipwa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni vyanzo vya mapato kwa Mfuko wa Taifa wa Maji. Waheshimiwa Wabunge wengi wamekubaliana na mapendekezo ya Kamati, lakini hapa Mheshimiwa Zitto alileta mabadiliko kidogo. Sisi tunacholilia ni kwamba Mfuko wa Maji uliopo hautoshelezi mahitaji na hasa ukizingatia kwamba mwaka huu fedha nyingi zilizoenda kwenye Wilaya zetu ni zile zinazotokana na mfuko na hela ya bajeti iliyotolewa ni kidogo sana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wabunge wengi kwanza wameitaka Serikali itoe fedha hizo kwa sababu suala la maji kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni uhai, ni uchumi na bila maji hakuna viwanda, hakuna uhai na hakuna kuishi kule nyumbani. Kwa kweli wanaoteseka ni akina mama na ambapo wanapotumia muda mrefu kutafuta maji watoto wanaanguka au wanaungua kwa moto na gharama za afya na usalama wa watoto unakuwa hatarini. Kwa hiyo, naiomba Serikali ilione hilo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndugu zangu naomba Kauli Mbiu hii ya maji tuipokee. Pia kama alivyoleta mapendekezo Mheshimiwa Zitto, niwaombe wataalam waliangalie na wakati wa bajeti tuli-effect. Kwa hiyo, tumepokea mpendekezo yake, lakini inatakiwa kufanyiwa kazi na nina hakika itapita. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea ni umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji katika kukabiliana na ukame na mabadiliko ya tabianchi. Waheshimiwa Wabunge sisi na Watanzania wote ni mashahidi kuhusu ukame wa mwaka huu ulivyoleta *frustration*, umeleta hofu na ndiyo maana bei ya vyakula mbalimbali imepanda. Najua kuna Wilaya ambazo zina chakula, kuna Wilaya ambazo hazina chakula na zimesemwa kwamba ni 55, lakini hata wale wenye chakula kidogo kutokana na hofu iliyoletwa na ukame huu, bei ya chakula imepanda na kwa kawaida itachangia kwenye mfumuko wa bei.

Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na wengine wote wanaohusika kwa kweli tutafute na tusambaze chakula ili tu-stabilise bei ya chakula na kuondoa hofu ya watu na watu waishi kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili miaka ijayo tuweze kuondokana na hofu hii ya ukame, hatuna njia nyingine, Kamati inasisitiza umuhimu wa Tume ya

Umwagiliaji kutegewa fedha za kutosha na kupelekewa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili iweze kutekeleza vyema miradi inayohusu kilimo cha umwagiliaji. Tunachoona ni kwamba Tume haijapelekewa fedha yoyote, tunamuomba Mheshimiwa Waziri wa Maji afuatilie kwa Waziri wa Fedha. Kilimo cha umwagiliaji kitasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa chakula na njaa na itaifanya nchi hii iishi kwa amani zaidi kuliko kama tunakuwa na hofu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi ambayo ningeweza kusema ila nawaaomba sana Waheshimiwa Wabunge mapendekezo yaliyomo kwenye Maazimio ambayo Kamati imeyaandaa ambayo yamechukua mambo yote muhimu myaunge mkono. Vilevile kama walivyosema Wenyeviti walionitangulia tutafute namna ya kuona kwamba Serikali inafanya kazi Maazimio haya. Inaonesha kwamba taarifa za Kamati zimeleta manufaa makubwa sana na utaona kwamba Wabunge wengi wamebakia hapa na Mawaziri wamechukua muda wao kutoa ufanuzi, lakini haitakuwa na manufaa kama kweli maazimio haya hayatafanyiwa kazi na Serikali na wale wote wanaohusika na tukiyafanya kazi kila mwaka, ndivyo tutakavyopiga hatua. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo niliyoyasema, narudia tena kutoa hoja kwamba muunge mkono Maazimio ya Kamati hii ya Kilimo, Mifugo na Maji na ahsanteni sana kwa usikivu wenu. (Makof)

**MWENYEKITI:** Toa hoja.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU – MWENYEKITI WA WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa hoja lakini naomba nirudie. Natoa hoja tupitishe Mapendekezo na Maazimio ya Kamati ya Bunge. (Makof)

**MHE. DKT. CHRISTINE G.ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, sasa nitalihoji Bunge kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hiyo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari 2017 ilipitishwa na Bunge)

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, sasa hii ni Taarifa Rasmi ya Bunge kwenda Serikalini. Nampongeza sana Mwenyekiti na pia napongeza majibu yote mazuri ya Serikali. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, toka tuanze Bunge leo mchana kuna wageni wetu hapa wanatoka Saint Peter Clever, Dodoma, nimeona ni muhimu niwatambulishé sababu wamekaa kwa umakini na wana haki ya kutambulishwa. Simameni Bunge liwapigie makofi. Karibuni Dodoma. (Makofi)

Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Utalii.

**MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGÉ YA ARDHÍ, MALIASILÍ NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami vilevile nianze kwanza kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mbalimbali kwenye taarifa yetu.

Nitoe shukrani vilevile kwa Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao tulifaya kazi bega kwa bega bila kuchoka. Vilevile nitoe shukrani kwa michango iliyotoka kwa Mawaziri kuhusu kuboresha taarifa yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ilishindwa kutekeleza baadhi ya majukumu kama ulivyosikia michango mbalimbali ya Wajumbe kutokana na ufinyu wa bajeti uliokuwepo. Kuna baadhi ya michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wameitoa lakini haimo ndani ya taarifa yetu mfano mdogo ni suala la RUBADA. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la RUBADA kwenye mipango ya Kamati yetu ya Utekelezaji ya mwaka 2016 tulitakiwa twende RUBADA kuangalia na kufanya kazi lakini pesa haikuwepo kwa hiyo tulishindwa kwenda kule na ndiyo maana hata kwenye taarifa yetu suala la RUBADA halikuwepo. Nipende tu kulitaarifu Bunge lako kwamba siku pesa itakapopatikana tutakwenda na tutakuwa kwenye nafasi nzuri sana ya kuweza kuishauri Serikali yetu nini cha kufanya kuhusu RUBADA. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea michango kwa maneno ya Waheshimiwa Wabunge 22 lakini nimepokea ya maandishi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge 16. Nashukuru sana kwa michango yao yote, michango ambayo ilijaa uzalendo wa hali ya juu na uchungu wa nchi yetu ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upimaji na urasimishaji wa ardhi lilizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana, ni kweli kwamba sehemu nydingi sana za miji yetu haijapimwa na hiyo ni changamoto ambayo Serikali

inatakiwa iangalie kwa makini. Kamati inaishauri Serikali itenye pesa za kutosha kuwezesha upimaji na urasimishaji wa ardhi kwa wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kitu cha ajabu, juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo kwamba Wizara ya Maliasili iende ikatambue mipaka ya baadhi ya hifadhi. Sisi kama Kamati tulishangaa, tuliamini kwamba ilitakiwa na Wizara ya Ardhi nayo ishirikishwe katika kutambua mipaka ya hifadhi za maliasili, lakini hatuoni kama hilo lilitendeka na tuna wasiwasi kama kweli hilo zoezi litaweza kufanyika kwa Wizara ya Maliasili peke yake bila kushirikisha Wizara ya Ardhi. Kama Kamati tunaishauri Serikali Wizara zishirikiane katika kufanya kazi ili kuleta tija katika mambo mbalimbali ambayo wanaelekezwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea mchango kutoka kwa baadhi ya Wabunge kuhusu ile Kamati ya Wizara Tano inayoshughulikia migogoro. Sisi kama Kamati tumeipokea na tunazidi kuisitiza Serikali ihakikishe kwamba ile Kamati inaleta ripoti yake kwa wakati ili tuweze kupunguza kama sio kuondoa kabisa migogoro kati ya hifadhi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Ngorongoro vilevile hatukuweza kuliingiza kwenye taarifa ya Kamati yetu kwa sababu tuliliweka kwenye ratiba ya kwenda kutembelea Ngorongoro ili tuweze kuishauri vizuri Serikali, lakini kama kawaida tuliambiwa bajeti haitoshi tukashindwa kwenda. Ni ngumu sana kutoa taarifa na kuzungumzia kitu ambacho hujawahi kukiona. Tunachelea kuzungumza taarifa ya sehemu muhimu kama Ngorongoro kwa kutegemea makaratasi tulioletewa mezani. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mjumbe mmoja wa Kamati yangu vilevile ameulizia kuhusu suala la Faru John. Nilitegemea suala hili lingeulizwa na Wajumbe wengi kweli, lakini nashukuru kwamba wengi walielewa kwamba hili suala lipo kwenye uchunguzi, liko chini ya Waziri Mkuu kuna tume imeundwa kulichunguza. Tunaamini tume hiyo itatuletea ripoti baada ya hapo tutaanza kulijadili. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la askari wa wanyamapori. Kwa ujumla kama Kamati hata sisi tunasikitishwa sana na baadhi ya askari wa wanyamapori ambao wanaamua kuchukua sheria mkononi na kuua Watanzania wenzetu. Kwa hiyo, kama Kamati tunashauri Wizara ya Maliasili na Utalii iongeze mafunzo kwa askari wetu, lakini vilevile tuishauri Serikali kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu hifadhi zetu kwa sababu bila wananchi kupata uelewa wa kutosha migogoro kati ya askari na wananchi itaendelea kuwepo na hatupendezwi na madhara yanayotokana na vifo vya Watanzania wanaoingia kwenye hifadhi zetu. Kuna njia rahisi zinaweza kutumika ambazo haziwezi kuleta madhara sana kwa wananchi wetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ongezeko la VAT kwenye suala letu la utalii. Wakati tunaandaa ripoti yetu tulikutana na Wizara nayo ikatuhidi kwamba mwisho wa mwaka wa fedha watakuwa na taarifa kamili ya hali ya utalii. Kwa hiyo, naomba kama Kamati na Bunge tuvumilie, tusubiri Wizara ituletee taarifa hiyo na kama kutakuwa na upungufu tutaangalia namna ya kuboresha zaidi ili hifadhi na utalii wa nchi yetu uendelee kukua na utuletee tija katika mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye suala la National Housing. Wabunge wengi sana wameongelea sana suala la National Housing. Kama mapendekezo ya Kamati yalivyojionyesha ni kweli kwamba maeneo mengi ambayo National Housing wanakwenda kujenga wanalazimika kununua ardhi, halafu wakishajenga wanalazimika kuleta miundombinu ya barabara, wanaleta umeme na maji. Wakati mwingine National Housing wanapata viwanja sehemu ya mbali na maeneo ambako hivyo vyanzo viro na wao wanalazimika kuchukua hizo gharama na kuzigawa kwa kila nyumba moja moja. Hali hiyo inasababisha nyumba za National Housing zisionekane ni za gharama nafuu kwa sababu ukishalipia vitu vyote hivyo huwezi kupata gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa natamani sasa Serikali ishirikiane, taasisi zote zinazohusika zishirikiane. Haiwezekani National Housing wagharamie suala la maji halafu Mamlaka za Maji ndiyo ziende zisome bili na kupata pesa kama zenyewe, hiyo ni kumbebesha mwananchi mzigo usikuwa na tija. Vilevile kwa masuala ya umeme, haiwezekani National Housing wasafirishe nguzo hamsini kupeleka kwenye destination ya site halafu TANESCO waje wachukue bili kwa sababu tu umeme ni wa kwao. Naamini TANESCO wakichukua jukumu lao na Mamlaka za Maji zikichukua jukumu lao pamoja na Halmashauri zetu zikichukua jukumu la kupeleka miundombinu ya barabara nyumba zetu za National Housing zitakuwa za gharama nafuu na sisi kama Kamati tunalitetea Shirika letu la National Housing liweze kuendelea kufanya kazi zake za kuwahudumia wananchi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea amendment kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kuhusu suala la Kigamboni Development Agency. Kamati inakubaliana nayo na tutaomba iingizwe kwenye taarifa yetu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na hifadhi zetu. Kwenye taarifa yetu tumeiweka wazi kwamba kuna mifugo ambayo ipo ndani ya hifadhi zetu. Bado tunasisitiza kwamba kikanuni na kisheria mifugo hairuhusiwi kuwemo ndani ya hifadhi. Tuwashauri Waheshimiwa Wabunge wawaeleweshe wananchi. Nilifurahishwa sana na Mheshimiwa Sannda ambaye alichukua jukumu la kuwaelimisha wananchi na wanahehimu hifadhi na hawaingilii hifadhi. Hizi hifadhi kama zikivurugika, nchi yetu itakuwa jangwa na hatutapona. Hiyo mifugo tunayoitetea leo na yenyewe itakufa. Kwa

hiyo, tujitahidi tushirikiane tuhifadhi misitu yetu ili kuhifadhi mazingira yetu yasiharibike. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nitaongelea suala la mashamba makubwa yaliyotelekezwa. Kamati yetu imependekiza Serikali ifanye uhakiki wa haraka mashamba yote makubwa yaliyotelekezwa yachukuliwe yapangwe na yagawiwe kwa wananchi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Vilevile kama itawezekana na Serikali tunatamani iwe na *land bank* ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya viwanda kwa sababu tunakwenda kwenye dunia ya viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la shoroba, siwezi nikazungumza moja kwa moja migogoro ya tembo na wananchi inayotokea sehemu mbalimbali hasa Mkoa wa Mara. Nachelea ku-*confirm* moja kwa moja kwamba inawezekana shoroba zimeingiliwa, inawezekana zimeingiliwa au hazijaingiliwa. Hata hivyo, natamani Serikali sasa iamke na iende kutambua shoroba zote ambazo zimeingiliwa kwa sababu baadhi ya shoroba Halmashauri imejenga, baadhi ya shoroba kuna shule zimejengwa na hizo zote ni za Serikali. Kwa hiyo, ushirikiano kati ya Wizara mbalimbali ni muhimu sana kuhakikisha tunalinda shoroba zetu na zile ambazo kweli kabisa taasisi za Serikali zimejenga basi Serikali iangalie namna ya kufidia ziondolewe ili wanyama wapate mahali pa kupita. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo sehemu aliyopita miaka hamsini iliyopita habadilishi anapita palepale. Kwa hiyo, ukijenga aki-escape lazima atadhuru mifugo na mazao ya wananchi kwa sababu sehemu anakopita ni palepale hata miaka mia inayokuja. Kwa hiyo, tulinde shoroba zetu ili kuепusha migogoro kati ya wakulima na mifugo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata changamoto kidogo kutoka kwa Mheshimiwa Kanyasu kuhusu pori la Geita kuvamiwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Kanyasu kwa kuonesha uchungu wa kutaka kuhifadhi pori letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati pamoja na maoni na maendeleko yalimo katika taarifa hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja! (Makofi)

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia na nimpongeze sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati na Kamati yake pamoja na majibu mazuri ya Serikali ambayo wameyatoa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilileta schedule of amendment kwa maana jedwali la marekebisho ili hoja ambayo walikuwa wameindika kwenye ripoti yao katika ukurasa wa sita na saba iweze kupata maoni lakini vilevile kuweza kupata Azimio la Kamati ya Bunge. Nashukuru sana kwamba Kamati ya Bunge imeipokea lakini nashukuru vilevile kwamba Serikali nayo imeipokea na imeahidi kwenda kulifanya kazi. Hata hivyo, kwa malengo ya kuweka kumbukumbu sahihi naomba niwasilishe rasmi hoja hii ili iwe ni kumbukumbu sahihi na Azimio la Kamati ya Bunge. Naomba kutoa hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Aah, aah, ngoja. Wewe umeleta amendment na imeshakubaliwa na Kamati na Serikali na mimi nitalihoji Bunge pamoja na amendment yako, nakutaja jina lako, haitoshi hiyo, dogo hilo? (Kicheko)

**WABUNGE FULANI:** Inatosha.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Adhi, Maliasili na Utalii pamoja na Maoni na Mapendekezo yalimo kwenye taarifa hiyo pamoja na Marekebisho ya Mheshimiwa Dkt. Ndugulile ambaye kwa kweli na mimi nasema amefanya kazi nzuri sana, wana Kigamboni wamepata Mbunge mzuri na amewatetea vizuri sana. (Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari 2017 pamoja na Marekebisho ya Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile yalipitishwa na Bunge)

**MWEYEKITI:** Sasa hii ni taarifa rasmi kwa Serikali kutoka Bungeni. Nimpongeze Mwenyekiti na Kamati yake na niipongeze Serikali kwa majibu mazuri sana. (Makofi)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Kaa chini Halima, namwita Mheshimiwa Kubenea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ndiyo Mheshimiwa Waziri.

### KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(1) na Kanuni ya 50...

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni 28(8) ambayo Mheshimiwa Mbunge ameiweka kama enabling provision kwa ajili ya kuwasilisha Maelezo Binafsi siyo Kanuni sahihi, alipaswa kutoa maelezo yake hayo kupitia Kanuni ya 50(1) na (2). Kanuni ya 28(8) siyo Kanuni ambayo inamu-enable yeye kuwasilisha Maelezo Binafsi, ni kanuni ambayo inampa mwongozo Mheshimiwa anaye-preside kwenye kitu ni utaratibu gani utafuatwa baada ya kuwa wamepokea Maelezo Binafsi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile ukiangalia Kanuni ya 64(1)(c)...

**MWENYEKITI:** Ngoja, unasema Kanuni ipi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 28(8) ambayo ndio ameitumia kuwasilishia Maelezo yake Binafsi, tunasema siyo Kanuni sahihi ya ku-enable kuwasilishia Maelezo hayo Binafsi ilitakiwa itumike Kanuni ya 50(1) na siyo mara ya kwanza na iko wazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hayo ukiangalia Kanuni ya 64(1)(c) pale mwisho...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Amejuaje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Ukiangalia mwishoni...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Katika maelekezo ambayo analiomba Bunge litoe kwa Waziri wa TAMISEMI ...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Halima, subiri kwanza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** ...ni jambo ambalo tayari jana lilishatolewa uamuzi na maelekezo ni masuala gani ambayo Kamati ya Maadili itayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nipende tu kusema kwamba kisheria sisi kama Bunge hili ambao tunatakiwa tuwe walinzi na wahifadhi wa Katiba, sheria pamoja na kanuni, haya maelezo hayapo proper mbele ya Bunge hili na hayapaswi kuwasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo maelezo yangu. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Umejuaje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima ulikuwa unasemaje?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Kanuni ya Kuhusu Utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1) inatakiwa itolewe wakati Mbunge anazungumza. Sasa huyu bibie hapa anakurupuka tu, hoja ikituhusu na Katibu wa Bunge subiri anayesimamia Kiti ndiyo atatoa mwongozo. Sasa unatumia Kanuni ambayo kwanza siyo proper, hakuna mtu ambaye amesimama anazungumza, wewe ulikuwa peke yako unasimama unajzungumisha mwenyewe, tumwachie Mwenyekiti ndiyo ana Kiti yeye ndiyo atajua kama maelezo...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**(Hapa hakutumia kipaza sauti).

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sikiliza, tulia bwana...

**MBUNGE FULANI:** Wewe umejuaje?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hatujibu maswali hapa, siyo kipindi cha maswali na majibu kwa hiyo tulizana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, hebu Mheshimiwa Angella mwachenii aseme.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka kusema ni hivi, mosi, Kanuni aliyotumia sio proper. Kanuni ya Kuhusu Utaratibu kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1) inatakiwa kutolewa pale mtu anapozungumza. Hiyo ni *ruling* ambayo aliitoa Naibu Spika wakati amekaa kwenye Kiti, akasema Kuhusu Utaratibu inatakiwa itolewe wakati mtu anazungumza. Kanuni imesema lakini vilevile *ruling* ya Mheshimiwa Naibu Spika ilisema hivyo na hakuna kitu kingine chochote ambacho kilitolewa kupingana na ile *ruling* kwa hiyo as far as we are concerned ndiyo inayosimama. Hilo la kwanza. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili Mheshimiwa Kubenea hajaanza kuzungumza. Kwa hiyo, ungesubiri aanze kuzungumza ndiyo wewe usimame useme ya kwako wewe...

**MBUNGE FULANI:** Kwani amejuaje?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Halafu ukishayasema ya kwako wewe Kiti ndiyo kiamue. Kwa hiyo, usituwahishe kwenye shughuli, wewe tulizana, anze kushusha hoja halafu Mwenyekiti ataangalia kama hoja yako ina mashiko, nashukuru. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Maelezo Binafsi wala yasiwape taabu...

**WABUNGE FULANI:** Yes.

**MWENYEKITI:** Subirini nimalize basi. Kanuni ya 68(10) inasema uamuzi wa Spika kuhusu suala lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho.

**WABUNGE FULANI:** Sawa. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Sasa baadaye nikisema mtanipiga? Naahirisha hoja hii mpaka hapo nitakapowasiliana na Ofisi ya Spika. (Makofij/Kicheko)

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Naahirisha shughuli za Bunge ....

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwongozo tu.

**MWENYEKITI:** Mpaka kesho saa tatu asubuhi. (Makofi)

*(Saa 1.19 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 10 Februari, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*